NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

### Kikao cha Kumi na Mbili - Tarehe 30 Machi, 2015

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

### MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali leo tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza, atauliza swali la kwanza.

Na. 117

### Mwakilishi wa Wazee katika Vyombo vya Maamuzi

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA** aliuliza:-

Kwa muda mrefu wazee wa nchi hii wamekuwa wakililia uwakilishi katika vyombo mbalimbali vya maamuzi kama vile Bunge, Halmashauri, Vijiji na kadhalika kama ilivyo kwa vijana, wanawake na watu wenye ulemavu ili sauti zao zisikike:-

Je, ni lini Serikali itasikia kilio cha wazee hawa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Conchesta Leonce Rwamlaza, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Utaratibu wa kupata wawakilishi katika vyombo vya maamuzi kama vile Bunge, umeelezwa katika Ibara ya 66 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Ibara hii imefafanua aina za Wabunge na namna ya kuwapata. Utaratibu wa kuwapata wawakilishi katika Halmashauri umeelezwa

katika Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Sura ya 292 yaani *The Local Authority Election Act, Cap. 292*. Aidha, utaratibu wa kuwapata wawakilishi katika vijiji hutawaliwa na Sheria ya Serikali za Mitaa, Sura ya 287 na Sheria ya Serikali za Mitaa, Sura ya 288.

Mheshimiwa Spika, wawakilishi wanaowakilisha makundi mbalimbali katika Bunge, Halmashauri na Vijiji, kwa mfano, wanawake, vijana, watu wenye ulemavu na kadhalika, wamekuwa wakipatikana kupitia mapendekezo yanayowasilishwa na vyama vya siasa kwenye vyombo vinavyosimamia uchaguzi katika ngazi hizo.

Mheshimiwa Spika, ili kuongeza uwakilishi wa makundi mbalimbali wakiwemo wazee, vyama vya siasa vinahimizwa kuhakikisha mapendekezo yanayopelekwa kwenye vyombo vinavyosimamia uchaguzi, yanahusisha makundi mbalimbali likiwemo kundi la wazee.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, ukiyatazama majibu haya ni kwamba ni kama wazee wametupwa katika vyama vya siasa. Kilio cha wazee kwa muda mrefu ni kupata uwakilishi katika vyombo hivi ili waweze kusema mambo yao kama ilivyo kwa watu wenye ulemavu, wanawake na vijana.

(i) Mimi ninachohitaji kujua ni lini Serikali itaweza kuweka ndani ya sheria moja kwa moja ili itambulike kwamba wazee nao wanapaswa kupata viti vyao kupitia vyama vya siasa?

(ii) Kwa muda mrefu tumekuwa tukilia ndani ya Bunge hili wazee wapewe pensheni yao; wale walioko katika mfumo rasmi na ambao hawako katika mfumo rasmi; je, ni lini Serikali itaweza kulipa pensheni hiyo kwa wazee ili waweze kujikwamua katika maisha yao?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika, ninaomba nimjibu Mheshimiwa Mbunge, maswali yake ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwanza, nimpongeze sana dada yangu Conchesta kwa sababu kwa kweli amekuwa akipigania sana haki za wazee. Waheshimiwa Wabunge wengine pia wamekuwa wakifanya hivyo mara nyingi katika Bunge lako Tukufu, kwa hiyo, nawashukuru sana Wabunge kwa kuwatambua wazee.

Swali lake la kwanza anachotaka kujua ni lini Sheria hizi zitabadilika. Hata sheria tulizonazo sasa hazisemi uwakilishi wa makundi hayo maalum uwatenge

wazee. Wanapoteuliwa walemavu, watakapoteuliwa wanawake, wanapoteuliwa makundi haya yote, wanaweza kuwemo wanawake vijana ama wanawake wazee.

Mheshimiwa Spika, katika Bunge lako hili Tukufu, takribani asilimia 20 ya Wabunge waliopo humu ndani kwa sasa ni wazee ambao wanakadiriwa kuanzia miaka 60 kwenda mbele. Kwa hiyo, unaona hata Wabunge tulioketi humu ndani ya Bunge, takribani asilimia 20 ya Wabunge walioko humu ndani ni wazee na tunawaona wazee wetu wanatusaidia sana humu ndani.

Kwa hiyo, nirudie kusisitiza, vyama vya siasa kwa mujibu wa sheria tulizonazo sasa hivi na kwa mujibu wa Katiba, wanayo madaraka ya kufanya uteuzi wa makundi hayo mbalimbali. Ninaendelea kusisitiza vyama hivyo viendelee kuzingatia kama ni walemavu wazee wawemo, kama ni wanawake wazee, vijana, rika zote wawemo. Kwa hiyo asilimia hiyo 20 inaonesha uwakilishi wa kutosha, lakini kama tutabadilisha Katiba, tutabadilisha Sheria hizo, tunaweza kuangalia tunafanya nini.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Conchesta pia amezungumzia suala la pensheni kwa wazee, Serikali inalitambua suala hili na kwa muda mrefu imekuwa ikifanya kazi ya kuhakikisha tunaweza kufanya nini kuwasaidia wazee. Niwaarifu Waheshimiwa Wabunge, kwa hivi sasa Mfuko wetu wa *TASAF* katika Awamu ya Tatu, umekuwa ukishughulika na kaya maskini, wakiwemo wazee katika nchi yetu ya Tanzania, kuhakikisha maisha yao yanaboreshwa.

Na.118

**Barabara ya Nangaru**

**MHE. SAID M. MTANDA** aliuliza:-

Je ni lini barabara ya Nangaru itatengenezwa kwa changarawe na ni kiasi gani cha fedha kitatumika?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Said Mtanda, Mbunge wa Mchinga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Nangaru hadi Milola ni barabara ya udongo *(earth road)* yenye urefu wa kilomita 24.2. Bajeti ya mwaka wa fedha 2014/2015, Serikali imetenga fedha jumla ya shilingi 117,470,000/= kwa ajili ya kuchonga kilomita 24.2 na kuweka changarawe kilomita 5. Hadi sasa fedha

ambazo zimepokelewa ni shilingi milioni 40. Kazi zilizofanyika ni kuandaa *site,* kuchonga barabara, kujenga kalvati moja na kujenga mifereji ya maji. Aidha, kazi inayoendelea ni kumwaga changarawe kilomita tano na kushindilia.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka 2015/2016, Halmashauri imetenga shilingi milioni 114.16 ambazo zitatumika kuweka changarawe katika sehemu itakayobaki katika barabara hiyo ambayo ni kilomita 19.2.

**MHE. SAID M. MTANDA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa fursa ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Swali Namba 118 linauliza je, ni lini barabara ya Nangaru itatengenezwa kwa changarawe na kiasi gani cha fedha kitatumika?

Mheshimiwa Spika, majibu yaliyotolewa hapa yanahusu barabara inayotoka Nangaru kuelekea Milola ambayo muasisi wake ni Mbunge wa Mchinga. Ninakubaliana na haya yaliyoandikwa, lakini msingi wa swali hili ni kuuliza barabara ile inayotoka Matimba kuelelea Nangaru, ambapo kiasi cha shilingi milioni 150 ndicho tunachoitaka Serikali ipeleke kwa sababu Tarafa hii yote ya Nangaru yenye Kata mbili, hivi sasa haipitiki kabisa kwa sababu mvua zimeharibu sana. Halmashauri yangu ilikaa na kuweka kipaumbele kwamba fedha zote za barabara sasa kipaumbele kiwe barabara kutoka Matimba kuelekea Nangaru.

(i) Je, Mheshimiwa Waziri na Wizara hii ipo tayari sasa kutoa shilingi milioni 150; Mfuko wa Mbunge tumeweka pale kidogo milioni tano kuziba mashimo lakini haisaidii; Serikali ipo tayari kutoa shilingi milioni 150 ili kurahisisha mawasiliano kwa wananchi wa Tarafa yote sasa hawana uwezo hata wa kufika Lindi Mjini?

(ii) Naibu Waziri yuko tayari mara baada ya Bunge hili kwenda na mimi eneo la tukio akaone kwa macho yake; na kwa kuwa tayari fedha za Mfuko wa Barabara zipo atakapomaliza ziara hiyo fedha hizo zitapelekwa pale ili kazi ianze mara moja? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, yote anayoyasema Mheshimiwa Mtanda ninayafahamu, hizi barabara alinipeleka yeye mwenyewe akanionyesha na haya matatizo anayoyaeleza ninayafahamu. Anataka twende tena, mimi siwezi kumkatalia Mbunge, kama anataka tufuatane tena mimi nitakwenda naye, tutakwenda mpaka huko kwenye barabara tukaangalie. Kwanza, yeye ni rafiki yangu, kwa hiyo, wala sina tatizo na hilo, tutaondoka tutakwenda naye tukaangalie.

Sasa niweke *records* vizuri, wakati ulipokuwa unataja hii barabara ambayo inazungumzwa hapa, barabara hii sisi tunajua kwamba ipo katika bajeti. *Overall budget* ya Halmashauri ya Wilaya ya Lindi ni bilioni 1.6. Fedha ambazo zimeshapelekwa katika hii Halmashauri mpaka tunapozungumza, *overall,* acha hiyo barabara ambayo anaizungumzia Mheshimiwa Mtanda hapa, tumeshapeleka shilingi milioni 234 zimekwenda kule.

Katika barabara hii ninayoizungumzia, kipengele hiki kinachozungumzwa hapa tulishapeleka milioni 40, ndizo ambazo zimeshapelekwa kule. Sasa anazungumza habari ya shilingi milioni 150 ambazo ziko ndani ya bajeti ambayo inazungumzwa hapa.

Mimi nataka kusema kwa vile hiki kitu kipo kwenye bajeti, mimi ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba hapatakuwa na tatizo lolote kupeleka hizo milioni 150. Nakwenda kuzi-*track*, hivi sasa nimetoka ofisini nimeacha watu wangu wanafuatilia ili kuona fedha hizi zinapatikana kwa ajili ya kwenda kufanya kazi hiyo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, tunaendelea na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma; Mheshimiwa Mariam Kisangi atauliza swali linalofuata, kwa niaba yake Mheshimiwa Ester Bulaya!

Na. 119

**Nafasi za Ajira kwa Vijana**

**MHE. ESTER A. BULAYA (K.n.y. MHE. MARIAM N. KISANGI)** aliuliza:-

Serikali imekuwa ikitangaza nafasi za ajira kwa vijana na wananchi kwa ujumla:-

(a) Je, kwa nini Serikali mpaka sasa haijafuta sharti la uzoefu wa muda mrefu kwa wanaoomba nafasi hizo?

(b) Je, kwa nini watu wanaotoka makazini na kuomba sehemu nyingine wanapata kazi na kuacha nafasi nyingine ikiwa wazi huku wakiacha vijana wasio na ajira wakitembea na vyeti vyao kutafuta ajira bila mafanikio?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma ya mwaka 1999, Toleo la mwaka 2008, uzoefu wa kazi siyo sifa ya kuingilia kazini bali uwezo wa kitaalam kwa kada husika.

(b) Mheshimiwa Spika, endapo mtumishi wa umma ataomba na kupata kazi sehemu nyingine, nafasi yake hujazwa na mtu mwingine, kwa kuwa nafasi za kazi katika utumishi wa umma hupangwa kwa mujibu wa ikama inayotokana na orodha ya kazi *(job list)*. Vijana wasio na kazi wanahimizwa kuomba kazi zinazotangazwa ilimradi wawe na sifa stahiki.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kumuuliza maswali mawili ya nyongeza.

(i) Katika Bunge lako Tukufu, Waziri wa TAMISEMI alisema kuna baadhi ya nafasi ambazo zinafuata vigezo kazini. Leo Waziri mwingine anasema kigezo siyo sifa. Ninataka kujua kwa nafasi zozote za Ukurugenzi na nyingine; vijana watakaoomba watakuwa tayari kupewa nafasi hizo kama uzoefu siyo kigezo?

(ii) Vijana wengi wako mtaani wamemaliza vyuo hawana ajira. Tunajua hakuna Serikali ambayo inaweza ikaajiri vijana wote, lakini mfumo wetu ulivyo, ndivyo ambavyo umewajengea fikra kwamba vijana wanapomaliza vyuo wanaajiriwa Serikalini. Ninataka kujua Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha vijana wanajiajiri kupitia taaluma zao? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, labda tuweke mambo vizuri isije kuonekana Serikali inataka kujikanyaga hapa.

Mimi nilipokuja hapa ninachozungumza kuna mambo mawili yanazungumzwa humu ndani; unazungumza *at entry point*. Unazungumza kwamba mwanafunzi amemaliza *UDOM* au kamaliza Chuo Kikuu cha Dar es Salaam au St. Augustine, kwa mara ya kwanza anaomba kazi, nisome hapa hicho ninachokisema, mimi nimekuja na sera yenyewe ipo hapa, kitabu ninacho hapa, Tamko la Sera;

"Ajira kwa mara ya kwanza, *entry point,* hususan kwa wale wanaoajiriwa kwa cheo cha kuanzia kwenye miundo, itafanyika kwa kuzingatia vigezo vya utaalam bila ya kujali uzoefu, isipokuwa kama kazi husika itahitaji kuwa na uzoefu." Mwisho wa kunukuu. Hii hapa ndiyo ninayoisema. Sasa mtu akiniambia kingine, mimi ninasoma hii ndiyo Sera ya Serikali.

Kuhusu hili la pili analozungumza, kwa hiyo, kwamba imekuwa *quoted* huku na nini, hakuna kitu kipya. Ukizungumza Mkurugenzi Mtendaji, unasema kitu kikubwa zaidi, unazungumza cheo, unazungumza kitu ambacho sasa unataka kuangalia. Unasema hivi; ninataka kumpa Mkurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni, unasema mtu ametoka moja kwa moja unampachika pale, hapana!

Utasema hivi ngoja kidogo, Mkurugenzi hapa nitampa majukumu, kuna mambo ya walimu, kuna wanafunzi, kuna hospitali, kuna barabara, kuna nini. Utahitaji kidogo pale uangalie pia na uzoefu wa huyu mtu ambaye unamzungumzia, hatakuwa ametoka tu Chuo Kikuu cha Dar es Salaam moja kwa moja, lakini Sera ndicho ninachokisema hapa *and I hope* Wabunge watakuwa wameelewa nini kinachozungumzwa hapa.

La pili, hili analolizungumza hapa, nenda Uingereza ile walikuwa Pax Britannica na Marekani wanaitwa Pax Americana, mpaka leo tunavyozungumza, hawajaweza kuwa na ajira kwa ajili ya vijana wao wote. Sera inasema nini? "Endapo Serikali hii itakuwa madarakani, itaweka mazingira ambayo yanawawezesha vijana wao kujiajiri." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, maana yake ni kwamba unawajengea uwezo, huwezi kusema mtu aendeshe gari kama hajui kuendesha gari. Tunachofanya hapa, Sera zetu zinaonyesha, vyuo vya ufundi tunaanzisha kwa ajili ya kujenga mafundi ambao wanaweza kujiajiri wao wenyewe.

Mheshimiwa Spika, nimalizie, kwa sababu Wabunge wanaelewa tunachozungumza hapa, *education system* yetu huko tulikotoka ilikuwa ina-*address the supply side*. Sasa hivi mkimsikiliza Mheshimiwa Kawambwa anapozungumza hapa, *education system* yetu ina-*address the demand side*, nini mahitaji ya soko. Mtoto yeyote anayetoka hapa akienda Chuo Kikuu kama ameomba ualimu, una hakika kuwa huna haja ya kutangaza atatapata hiyo nafasi, kama ni uhandisi atapata hiyo nafasi, kama ni udaktari atapata hiyo nafasi. Ukizungumza habari ya *engineering* na mambo mengine, mambo ya *accounts,* atapata hiyo nafasi. Kwa hiyo, tunapowaambia vijana wetu waombe kulingana na mahitaji ya soko.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Spika, swali nililotaka kuuliza ameuliza Mheshimiwa Ester. Ahsante.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Spika, ajira zimekuwa matatizo, lakini pia nataka kujua ni kwa nini Menejimenti ya Utumishi wa Umma inachelewa kutoa vibali katika Halmashauri zetu ziweze kuajiri? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwanza, bahati nzuri hili ni rahisi zaidi kwa sababu tunashirikiana sisi na wao. Anachokisema hapa ni vile vibali ambavyo vinatoka kwa ajili ya ajira. Kwanza, kuna ile moja ambayo tumekubali sasa tumeziruhusu Halmashauri ziajiri zenyewe huko waliko, kwa maana ya kada ya chini; wahudumu, watendaji wetu wa vijiji na wale wengine wote, hivi imekuwa inaenda vizuri ukiacha wale ambao wanakwenda kujiunga kwa mara ya kwanza sasa kwa mwaka huu wa 2014/2015 ambavyo ni vijiji vipya tulivyovianzisha.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kama anavyosema Mheshimiwa Arfi, wakati upo ucheleweshaji. Ikumbukwe kuwa Waziri huyu tunayemzungumzia hapa, atakwenda kutoa vibali kulingana na fedha iliyopo. Maana yake ni lazima aende akashirikiane na Hazina. Akisema tu nenda kaajiri kule, ndiyo sasa unawakuta watu wamekaa barabarani; tunataka haki zetu, tunaonewa! Ndiyo mambo hayo.

Mheshimiwa Spika, lazima ahakikishe yote hayo yanakwenda sambamba. Nakubaliana na wewe lakini kwa kweli kama mnamsikiliza Mheshimiwa Kombani, sasa hivi wanajitahidi sana katika Wizara ya Utumishi kuhakikisha tunaondokana na hili tatizo ili vibali vitoke katika muda uliopangwa waweze kupata ajira zao na mishahara yao iweze kupatikana wakati huo huo bila kucheleweshwa.

**SPIKA:** Tunaenda Wizara ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, atauliza swali.

Na. 120

**Kuvipatia Umeme Vijiji vya Njombe Kaskazini**

**MHE. DEO K. SANGA** aliuliza:-

Ni muda mrefu sasa tangu itolewe ahadi ya kuvipatia umeme vijiji vya Lyamkena, Kiumba, Ingongolo, Kichiwa, Ibumila, Ikuna, Matingonjola na Wanginyi kutoka umeme wa Makambako kwenda Songea:-

(a) Je, kuna tatizo gani mpaka sasa vijiji hivyo havijapata umeme?

(b) Je, ni lini vijiji hivyo sasa vitapatiwa umeme?

(c) Je, ni lini watu watapatiwa fidia zao?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, Mbunge wa Njombe Kaskazini, lenye sehemu (a), (b), na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli vijiji vya Lyamkena, Kiumba, Ingongolo, Kichiwa, Ibumila, Ikuna, Matingonjola na Wanginyi ni miongoni mwa vijiji vitakavyonufaika na Mradi wa Songea – Makambako unaofadhiliwa na Serikali ya Sweden kwa asilimia 100 kwa upande wa usambazaji. Kwa upande wa usafirishaji umeme, mradi huo unafadhiliwa kwa pamoja na Serikali ya Sweden kwa mkopo kutoka Benki ya Sweden *(AB Svensk Exportkredit Bank)* na Serikali ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, jambo linalokwamisha kuanza ujenzi wa njia ya usafirishaji wa umeme ni kutosainiwa kwa Mkataba wa Mkopo *(Credit Agreement)* kati ya Serikali na *AB Svensk Exportkredit Bank*. Mazungumzo kuhusiana na utiwaji saini wa mkopo wako katika hatua za mwisho.

(b) Mheshimiwa Spika, kazi ya kujenga njia za kusafirisha umeme inatarajiwa kuanza mwezi Julai, 2015 na Mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2016. Hivyo, vijiji vilivyotajwa vinatarajiwa kupata umeme katika kipindi cha mwaka 2016.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia *TANESCO* ilianza kulipa fidia kwa wananchi watakaopitisha Mradi upande wa njia ya kusafirisha umeme *(transmission line)* kuanzia mwezi Aprili, 2014 ambapo Mkoa wa Ruvuma zoezi limekamilika na kwa upande wa Mkoa wa Njombe, mchakato wa ulipaji fidia unaendelea na utakamilika Juni, 2015.

Mheshimiwa Spika, nisisitize kwamba fidia inayozungumzwa ni kwa njia ya umeme ya msongo wa 220 Kv.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza, lakini kabla sijauliza nataka nitoe maelezo mafupi tu ya dakika moja. Kule Njombe na Mkoa wa Iringa sisi katika Mikoa hii miwili katika mashamba yetu wananchi wa Mikoa ya Njombe na Iringa bangi huota bila kulimwa. Hivi sasa sheria iliyopitishwa ombi langu ni kwamba watakapokaa kuchanganua Kanuni na Sheria, waone Mkoa wa Iringa na Njombe bangi inaota bila kulimwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maswali yangu mawili:-

(i) Kama ambavyo nimeuliza kwenye swali langu la msingi la vijiji hivyo vilivyotajwa, wananchi hawa wamekuwa wakipewa matumaini kwa muda mrefu tangu mwaka 2011 kwamba vijiji hivyo vitapata umeme vikiwemo vijiji vya Jimbo la Njombe Kusini ambako Mheshimiwa Spika ni Mbunge. Vikiwepo vijiji vya Wilaya ya Songea Vijiji, Madaba na kadhalika. Ni lini Serikali itawapatia vijiji hivi umeme ili na wao wawe na matumaini kama ambavyo vijiji vingine wanapewa umeme?

(ii) Watu wanaoishi katika vijiji ambavyo nimevitaja ni muda mrefu Serikali haijawapa fidia; umeme wamekosa na fidia wamekosa; ni lini Serikali itawalipa fidia ili nitakaporudi nikawaambie fidia zao Serikali imewaambia itawapa muda fulani? Nakushukuru.

**SPIKA:** Sasa ile bangi tena iliingiaje hapa! Mheshimiwa Waziri, majibu! *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE):** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda nizungumze kwa uelewa wangu kwamba bangi siyo nishati.

Mheshimiwa Spika, katika swali lake la kwanza nimeeleza kwamba wananchi wamekuwa wakipewa matumaini ni kweli na nimeeleza kinachokwamisha ni kutia saini ule mkataba wa makubaliano. Nimeeleza vilevile kwamba ipo kwenye hatua za mwisho na shughuli itaanza Julai, 2015.

Mheshimiwa Sanga, natambua unavyofuatilia suala hili, tuwe na imani, miradi inayohusisha *element* ya pesa za kigeni inakuwa na ucheleweshaji. Nimepitia mradi mzima, pindi wanapotoa ile pesa, mkataba wakishakubaliana, njia nzima itafaidika. Napenda kukiri kwamba nimepitia Njombe Kaskazini na Njombe Kusini, Njombe Kusini *REA I* hamna chochote, *REA II* hamna chochote na kuna vijiji vinane vipo gizani. Tunalifuatilia, mafaili yote yapo mezani kwangu, Njombe Kusini mtafikiriwa na Njombe Kaskazini mtafikiriwa.

Mheshimiwa Spika, kuna vijiji vingine vina utata, kama ambavyo kuna kijiji cha utata Dodoma na Morogoro. Katika eneo lako Mzee Sanga kuna kijiji ambacho kipo kwa Mzee Lwenge na kingine kiko kwako katikati kiko gizani. Hayo ni maeneo ambayo vijana wanafanyia kazi. Mniruhusu wataalam wanishauri kitaalam nisiwajaze maneno. Mambo yote haya yatatekelezwa, waache watendaji wamalizie mikataba yao, pesa zije na pesa hizi hazina matatizo zinatoka Sweden, kazi itatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, fidia kwa wananchi, hili siyo kwa Njombe tu na si kwa Songea tu ni kwa Tanzania nzima. Fidia inayozungumzwa ni kwa msongo mkubwa wa 220 au 400, lakini zile *distribution* za kwenda kwetu, tulikubaliana na

ninaendelea kuwasihi, wanapokuja kuleta umeme kwenye majumba yetu, mkubali tusidai fidia. Tukidai fidia, wigo *(the scope)* wa kusambaza utapungua. Tumekubaliana tunataka Tanzania yote iwashwe umeme.

Mheshimiwa Spika, hayo ndiyo majibu yangu kuhusu Njombe Kusini na Kaskazini. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Tuendelee na swali la Mheshimiwa Suleiman Nchambi Suleiman, kwa niaba yake Mheshimiwa Ndassa.

Na. 121

**Kuongeza *Service Levy* kwenye Mgodi wa Almasi - Mwadui**

**MHE. RICHERD M. NDASSA (K.n.y. MHE. SULEIMAN N. SULEIMAN)** aliuliza:-

(a) Je, ni lini Serikali itaridhia kubakisha asilimia 0.2 (0.2%) ya *royalty* ya Mgodi wa Almasi wa Mwadui kwa Halmashauri ya Kishapu?

(b) Je, ni kwa nini *service levy* isiongezeke kutoka asilimia 0.2 (0.2%) hadi kufikia asilimia 0.5 (0.5%)?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES M. KITWANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Suleiman Nchambi Suleiman, Mbunge wa Kishapu, lenye sehemu (a) na (b), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mrabaha au *royalty* ni tozo ambayo mwekezaji hutozwa na Serikali Kuu kwa kuwekeza katika maliasili ya nchi. Tozo hii hulipwa kama sehemu ya mapato yote yanayotokana na madini yaliyozalishwa. Kwa mujibu wa sheria za nchi, tozo hii hulipwa Serikali Kuu. Aidha, ushuru wa huduma *(service levy),* kwa Halmashauri ya Serikali ya Mtaa hulipwa kwa mujibu wa Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa *(The Local Government Finance Act, 1982*). Kulingana na sheria hiyo, Halmashauri husika hutakiwa kutunga sheria ndogo *(by-laws*) zinazotoa utaratibu wa kutoza ushuru wa huduma kwa kiwango kisichozidi asilimia 0.3 ya mapato yote.

Mheshimiwa Spika, kwa hivi sasa tozo inayostahili kulipwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu ni ya ushuru wa huduma. Kulingana na Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya 1982 kama nilivyoitaja, kiwango cha juu cha tozo ya ushuru wa huduma hakiruhusiwi kuzidi asilimia 0.3 ya mapato halisi ya mlipaji kwa mwaka. Aidha, kwa kuwa sheria huandaliwa kulingana na mahitaji,

ongezeko la tozo hiyo hadi kufikia asilimia 0.5 iliyoombwa na Mheshimiwa inayopendekezwa, linaweza kufanyika iwapo Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa itarekebishwa ili kuruhusu ongezeko hilo.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri, kwa majibu yake mazuri lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Majibu haya yanajitosheleza, sasa naomba kumuuliza Waziri; kwa kuwa mrabaha huu ungeweza pia kuwasaidia wananchi wa Kijiji cha Mabuki ambapo nafikiri unalielewa eneo vizuri, ambapo inasemekana kwamba pana Almasi:-

(i) Nini tamko la Serikali kuhusu mgodi ambao unatarajiwa kuwa mkubwa katika Mji wa Mabuki, Wilaya ya Misungwi kwenye Jimbo la Mheshimiwa Kitwanga?

*(ii)* Kwa kuwa lipo agizo la Serikali la kurudisha vifaa vilivyokamatwa kule Mererani kwa wachimbaji wadogo wadogo na suala hili limekuwa ni la muda mrefu na wenyewe wamekuwa wakilalamika. Nami kama Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini, suala hili limeshafika kwetu. Je, ni lini Serikali itarudisha vifaa hivyo kwa wachimbaji wadogo wadogo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES M. KITWANGA):** Mheshimiwa Spika, natambua kwamba Mabuki ipo katika Jimbo langu na kweli kulikuwa na mwekezaji ambaye anasuasua. Tunaangalia katika utaratibu ambao tumejiwekea, kuhakikisha wawekezaji wote ambao wamehodhi na hawajaweza kuanza kufanya maendeleo katika maeneo yao, wote wananyang'anywa leseni na wananchi wenye uwezo na Wawekezaji wenye uwezo waweze kupewa nafasi hizo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mwekezaji huyo pamoja na yeye, kama atakuwa hajafanya kama ambavyo aliingia mkataba na Serikali, basi leseni yake iko hatarini kufutwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vifaa vya Mererani, ninamwomba Mwenyekiti wangu wa Kamati ya Nishati na Madini, atambue tu kwamba kuna mihimili mitatu na mhimili mwingine ambao ni Mahakama, unalifanyia kazi hili suala, naomba nisilizungumzie hapa Bungeni.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mwanjelwa, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa tuliambiwa *STAMICO* walipewa kuuendesha Mgodi wa Makaa ya Mawe wa Kiwira lakini ni muda mrefu sasa Mgodi huu umesahaulika na mahali pale imekuwa ni tatizo la kupoteza fedha za Serikali na ajira imekuwa ni shida, wananchi wamekaa pale kwa muda mrefu. Ninaomba Mheshimiwa Waziri atueleze ni nini *status* ya Mgodi huu mpaka sasa hivi?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES M. KITWANGA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa Mgodi huu umechukua muda mrefu, lakini kama ambavyo nimejibu katika kipindi hiki cha Bunge kwamba, wawekezaji ambao walikuwepo wameshindwa kuendeleza; na kupitia Serikali sasa hivi tumetangaza tena *tender* ili kuhakikisha kwamba tunapata mwekezaji ambaye ataweza kushirikiana na Serikali kuweza kuuendeleza Mgodi huu. Ninamwomba Mheshimiwa Mbunge aruhusu utaratibu uendelee na mwekezaji atakapopatikana, yeye atafahamishwa na wananchi wote watakuwa wameelekezwa.

**SPIKA:** Tuendelee na Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Said Amour Arfi, atauliza swali linalofuata!

Na. 122

**Ujenzi wa Barabara ya Mpanda - Uvinza**

**MHE. SAID A. ARFI** aliuliza:-

Je, ni lini barabara ya kutoka Mpanda hadi Uvinza itajengwa kwa kiwango cha lami ili kuunganisha Mikoa ya Rukwa, Katavi na Kigoma?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mbunge wa Jimbo la Mpanda Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Mpanda - Uvinza, yenye urefu wa kilomita 194, ni sehemu ya Barabara Kuu ya Tunduma - Sumbawanga - Mpanda - Uvinza - Kigoma - Kidahwe - Kasulu - Kibondo - Nyakanazi.

Mheshimwia Spika, Serikali imeanza maandalizi ya ujenzi wa barabara hii kwa kuigawa katika vipande mbalimbali. Sehemu ya Kidahwe - Uvinza (kilomita 76.5) imekamilika kujengwa kwa kiwango cha lami. Sehemu ya Kidahwe -

Kasulu na Nyakanazi - Kibondo tayari kuna Makandarasi wanajenga kwa kiwango cha lami. Sehemu ya Mpanda - Uvinza (kilomita 194) imekamilika kufanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu ili sehemu hii nayo ijengwe kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, hii ndiyo juhudi ya Serikali katika kuhakikisha Mikoa ya Rukwa, Katavi na Kigoma, inaunganishwa kwa barabara za lami.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Nina maswali mawili ya nyongeza:-

Ninashukuru jitihada zinazofanywa na Serikali lakini pia kwa majibu ya jumla jumla tu ya Mheshimiwa Waziri.

(i) Nataka kufahamu *status* ya barabara hii ya kutoka Mpanda kwenda Uvinza kilomita 194; kama unavyosema katika majibu yako sehemu hii nayo ijengwe kwa kiwango cha lami, yaani umekamilisha upembuzi yakinifu na usanifu. Ninataka kujua ni lini sasa ujenzi wa barabara hii unaanza?

(ii) Umuhimu wa kuunganisha Mkoa wa Katavi na Kigoma ni sawa sawa umuhimu wake na kuunganisha Katavi na Mkoa wa Tabora. Najua jitihada zinazofanywa na Serikali juu ya barabara ya kutoka Mpanda kwenda Tabora kupitia Sikonge. Je, ni lini sasa barabara hii inaanza kujengwa na taratibu zimefikia wapi?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, kuhusu kipande cha kutoka Mpanda mpaka Uvinza kilomita 194, Serikali imefanya usanifu barabara yote na mwaka wa fedha huu ambao tunaongea, tuliweka bajeti ya shilingi bilioni 4.5 kwa ajili ya kuanza kujenga kipande cha kilomita 35 kutoka Mpanda mpaka Vikonge. Taratibu za manunuzi zinaendelea, tupo kwenye hatua za mwisho kuweza kupata mkandarasi aweze kuanza kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili kuhusu mipango iliyopo ya Serikali kati ya Mpanda na Tabora; kwanza, Serikali imeweza kufanya usanifu barabara yote karibu zaidi ya kilomita 350 imekamilika na sasa hivi tupo kwenye hatua za mwisho kukubaliana na Benki ya Afrika, wamekubali kufadhili ujenzi wa barabara hiyo. Kwa hiyo, taratibu hizo zinaendelea za Kiserikali.

Mheshimiwa Spika, nina imani kabisa barabara ya kutoka Mpanda mpaka Tabora itajengwa kwa kiwango cha lami.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kakoso swali la nyongeza.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, ninakushuru kwa kunipa nafasi hii. Wakati tunasubiri kujengwa barabara ya lami kati ya Mpanda kwenda Kigoma, barabara hii imeharibika sana na inahitaji matengenezo ya dharura.

Je, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha matengenezo ya dharura yanafanyika katika kipindi hiki tunachosubiri ujenzi wa lami?

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kama alivyojibu Mheshimiwa Naibu Waziri, kuhusu mipango na mikakati mbalimbali ya kuhakikisha barabara ya kutoka Kigoma - Mpanda hadi Sumbawanga mpaka Tunduma inakamilika kwa kujengwa kwa kiwango cha lami na hasa kwa kuzingatia kwamba barabara hii inaunganisha kutoka Tunduma, Sumbawanga, Mpanda, Kigoma, Nyakanazi kwenda mpaka Mtukula na hadi Ugunda; eneo hilo ambalo amelitaja ambalo lina jumla ya kilomita 194, tutalitengeneza kwa kutumia fedha za *Road Fund* ambazo katika bajeti ya mwaka huu tumezitenga kwa ajili ya kuhakikisha barabara hii inapitika wakati tukisubiri mipango mahususi ya kuijenga sehemu hiyo kwa kiwango cha lami ili ikaunganishwe na sehemu ya Uvinza hadi Kigoma, ambayo tayari imekamilika kwa kujengwa kwa lami kilomita 76.6.

**SPIKA:** Tunaendelea na Wizara ya Fedha; Mheshimiwa Rajab Mbarouk, kwa niaba yake Mheshimiwa Amina Mwidau!

Kwanza, tuchukue nafasi hii kukupongeza kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa kwanza mwanamke wa Kamati ya Hesabu za Serikali. Karibu sana, tunakupongeza sana. *(Makofi)*

**MHE. AMINA M. MWIDAU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa shukrani hizo na ninawashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya *PAC* kwa kunipitisha.

Kwa niaba ya Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohammed, naomba sasa swali lake namba 123 lipatiwe majibu.

Na. 123

**Taasisi ya *Pride Tanzania***

**MHE. AMINA MOHAMED MWIDAU (K.n.y. MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED)** aliuliza:-

Taasisi ya *Pride Tanzania* ni moja ya Taasisi ambazo hutoa mikopo kwa wananchi na wafanyabiashara ndogo ndogo hapa nchini:-

(a) Je, hadi sasa Taasisi hiyo imekopesha kiasi gani cha fedha?

(b) Je, mtaji wa Taasisi hiyo ukoje?

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbarouk anauguliwa na mzazi wake, yuko Hospitali ya Muhimbili.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ADAM K. MALIMA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohammed, Mbunge wa Ole, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya *Pride Tanzania* ni Asasi isiyo ya Kiserikali iliyosajiliwa kama Kampuni tarehe 5 Mei, 1993 chini ya wadhamini wasio na hisa *(Company Limited by Guarantee, Not Having Share Capital),* kulingana na Sheria ya Makampuni *Cap, 212* ya mwaka 2012. Lengo la kuanzishwa kwa Asasi hiyo ni kuwawezesha walengwa wake kiuchumi kwa kutoa mikopo kwa wajasiriamali wadogo na wa kati sehemu za mijini na vijijini. Asasi hii ina mtandao wa jumla ya matawi 71 katika Mikoa yote na baadhi ya Wilaya za Tanzania Bara na Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa Asasi ya *Pride Tanzania* imeweza kukopesha wajasiriamali mbalimbali idadi ya mikopo inayofikia milioni 1,700,000, yenye jumla ya thamani ya shilingi bilioni 805. Idadi hii inajumuisha mikopo 62,350 iliyotolewa kwa wajasiriamali walioko Unguja na Pemba yenye jumla ya thamani ya shilingi bilioni 23.67.

Mheshimiwa Spika, mtaji wa Asasi hii umechangiwa na:-

(i) Misaada kutoka katika Mashirika au Taasisi mbalimbali *(Grant/Aid)* bilioni 3.3, asilimia 4 ...

**SPIKA:** Jamani eeh tuko ndani ya Bunge, mazungumzo yanazidi mno!

Mheshimiwa endelea!

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ADAM K. MALIMA):** Mheshimiwa Spika, naomba nirejee hapo. Mtaji wa Asasi hii umechangiwa na:-

(i) Misaada kutoka katika Mashirika na Taasisi mbalimbali *(Grant/Aid)* bilioni 3.3, asilimia 4;

(ii) Limbikizo la ziada *(Retained Earnings)* bilioni 9, sawa na asilimia 10;

(iii) Hatifungani *(Corporate Bond)* bilioni 4.6, sawa na asilimia 5;

(iv) Mikopo kutoka asasi za kifedha za ndani shilingi bilioni 31, asilimia 35; na

(v) Mikopo kutoka Mifuko ya Kifedha ya Nje *(Microfinance Investiment Funds)* shilingi bilioni 40, sawa na asilimia 45. Kwa hiyo, jumla ya mtaji ni shilingi bilioni 88.5 kwa maana ya asilimia 100 ya mtaji wake.

**MHE. AMINA M. MWIDAU:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali ya nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, Taasisi hii ya *Pride Tanzania* ilipoanzishwa chini ya *guarantee* ya Serikali ilikuwa ina-*appear* kwa *CAG,* ilikuwa inakaguliwa na *CAG,* lakini ghafla ikapotea kwenye uso huo.

(i) Nakuomba Mheshimiwa Waziri utuambie; kwa nini *Pride* imepotea kwenye Mashirika au Taasisi ambazo zinatakiwa zikaguliwe na *CAG;* ni sababu zipi za msingi zilizopelekea ikapotea ghafla?

(ii) Nia na madhumuni ya Taasisi hii ni kuwakopesha Watanzania, lakini wengi wao sasa hivi badala ya kwenda mbele wanarudi nyuma kutokana na mikopo ambayo inasababisha wananyang'anywa vitu kutokana na riba kubwa. Kama kweli nia yake ni kuwasaidia Watanzania; je, wana mkakati gani wa kuweza kupunguza riba ili waweze kuwasaidia Watanzania kama ilivyokuwa nia yao? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ADAM K. MALIMA):** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Amina Mwidau, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, tukubaliane kwamba *Pride* ni *Limited By Guarantees (LBG).* Sasa kwa misingi ya kampuni hiyo, *Pride* inawajibika kwa wale wanachama wanaochangia ili kuwezesha Shirika hili kuendelea. Kwa hiyo, *is not limited by shares but limited by guarantee.* Kuna misingi mbalimbali ya *limited by guarantee,* kuna kampuni ambazo ni *CICs* na kuna kampuni nyingine ambazo *by share capital* zinawajibika kuwa na masuala ya faida na kuwasilisha taarifa zao kama hizo. Sasa swali ni kwamba, kwa nini *CAG* ameacha kuikagua *Pride?*

Mheshimiwa Spika, hata ukiangalia kwa taarifa nilizosema, wale wachangiaji wa *Pride,* hakuna Taasisi ya Umma pale isipokuwa zile Taasisi za Kifedha ambazo nyingine zinawezekana zitakuwa zimechangia mle ndani. Kwa sababu kwa sasa hivi sina *exact* ya wale wa ndani ambao wanachangia mle ndani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, inawezekana kwamba kutokana na wachangiaji wa sasa hivi wanachama, kwa misingi ya *LBG,* kwa maana ya *Limited By Guarantees,* ndiyo inawafanya wasiwajibike tena kuchangia chini ya *CAG*. Utaratibu wa uchangiaji ule wa awali, inawezekana ndiyo ilikuwa sababu kwa nini *CAG* anaingia mle kama sehemu ya uchangiaji ndani ya *Pride* ilikuwa inawajibika kwa Sekta ya Umma.

Mheshimiwa Spika, hili la pili, mikopo ina riba kubwa; ni kweli, watu wengi wanaokopa *Pride* wamelalamikia mikopo mikubwa, lakini ndiyo tatizo la *Micro Finance* kwamba kimsingi *Pride* ni Shirika limeasisi hili suala la *Micro Finance,* kwa hiyo, ilipokuwa inaanza nadhani mwanzoni asilimia ya mikopo yake ilikuwa kama 30, ilikuwa ni mkubwa kweli. Hivi sasa tunakubaliana kwamba, ni kweli *Pride* kwa muda wa miaka 22 inatakiwa tayari iwe imefika sehemu ambayo inaweza kujihami, ina imani na wateja wake, ina imani na watu wanaokopeshwa pale, kwa hiyo, ingeweza kushuka. Ninaamini mkakati wake wa sasa hivi ni kushuka zaidi ili kuweza kuwa na watu wengi zaidi katika mfumo wake wa ukopeshaji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abuu Jumaa!

**MHE. ABUU H. JUMAA:** Mheshimiwa Spika, nimeridhishwa na majibu ya Waziri.

**SPIKA:** Mheshimiwa Msabaha!

**MHE. MARIAM S. MSABAHA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nami naomba kumuuliza Naibu Waziri swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa *Pride* inatoza riba kwa wafanyabiashara wadogo wadogo; je, Serikali inanufaika vipi; yaani ni asilimia ngapi ambayo Serikali inanufaika na hili Shirika la *Pride?*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ADAM K. MALIMA):** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Mariam Msabaha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kulipa riba ni utaratibu kwa mikopo yote, *whether* ukichukua kwa Shirika la *Pride,* ukichukua Benki au ukichukua *Commercial Bank,* wote wanatoa mikopo yao kwa msingi wa riba. Kwa maana hiyo, katika biashara zao zile, baada ya kumaliza biashara zao wakatathmini mahesabu yao, kodi stahili inatakiwa kulipwa Serikalini. Kwa hiyo, kwa maana hiyo, kama utaratibu wa taasisi zote za kifedha zinazofanya kazi zao na kupata faida, wakimaliza kupata faida yao na kutathmini taarifa zao, lazima pawe na *element* ya kodi kulingana na faida wanayopata.

Na. 124

**Vituo vya Mafuta Nchini Kukwepa Kulipa Kodi**

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED** aliuliza:-

Vituo vingi vya mafuta ya petroli na dizeli vimekuwa vikikwepa kulipa kodi kwa kutotoa risiti hata pale mnunuzi anapodai:-

Je, Serikali haioni ni busara kutoza kodi hiyo kwa jumla pale vituo hivyo vinaponunua mafuta ya petroli na dizeli?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L. MCHEMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa sheria zipo kodi kuu nne zinazotozwa kwenye bidhaa hizi, yaani kodi ya mapato, kodi ya ushuru wa bidhaa, ushuru wa mafuta na ushuru wa petroli.

Mheshimiwa Spika, kodi za ushuru wa bidhaa, ushuru wa mafuta na ushuru wa petroli hukusanywa forodhani *(at source)* mara tu bidhaa hizi zinapoingizwa nchini isipokuwa kwa mafuta ya petroli na dizeli yanayokwenda nchi za jirani. Kodi hizi hulipwa forodhani na makampuni yanayoingiza mafuta ya petroli na dizeli kwa kuzingatia kiasi cha ujazo wa lita zinazoingizwa nchini kabla ya kuuzwa kwenye vituo vya mafuta.

Mheshimiwa Spika, ulipaji wa kodi ya mapato hususan kwa makampuni yanayouza mafuta, unafuata mfumo wa wafanyabiashara kujikadiria wenyewe na kulipa kodi kama ilivyoainishwa kwenye Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura Namba 132 na kisha ukaguzi wa hesabu hufuata baadaye. Utaratibu huu wa kukusanya kodi unatumika pia kwa kuwakadiria wafanyabiashara wa shughuli zingine. Hata hivyo, baada ya kubaini kuwa kuna udhaifu katika utoaji risiti ambao husababisha upotevu wa mapato, Serikali imeanza mfumo wa matumizi ya mashine ya kodi za *electronic* kwenye biashara mbalimbali ikiwa ni pamoja na vituo vya kuuzia mafuta.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo ni vyema ikaeleweka kuwa, mfumo wa matumizi ya mashine za *electronic* katika kutoa risiti za mauzo umetekelezwa kwa awamu mbili; awamu ya kwanza ikiwa ni kwa wafanyabiashara waliosajiliwa kwa Kodi ya Ongezeko la Thamani; na awamu ya pili ikawa inawahusu wafanyabiashara wengine waliobaki. Vituo vingi vya mafuta hapa nchini havijasajiliwa na Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT)* kwa kuwa mafuta ya petroli na dizeli hayatozwi Kodi ya *VAT*. Matumizi ya mashine za kodi za

*electronic* kwa wafanyabiashara wa vituo vya mafuta imeanza kutekelezwa katika awamu ya pili ya mashine hizi ambazo zilianza Julai mwaka 2013.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, pamoja na kupokea fikra mbadala ya Mheshimiwa Mbunge na kama ilivyo kwa wadau wengine, naomba nimuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba mawazo yatafanyiwa kazi. Hata hivyo, napenda kusisitiza kwamba kama mwananchi atanunua mafuta kwenye kituo na ataacha kudai risiti, basi muuzaji na mnunuzi mtakuwa mmekiuka sheria na kustahili adhabu kwa mujibu wa sheria.

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini bado nina maswali mawili ya nyongeza:-

(i) Kwa kuwa vituo vingi vya mafuta ya petroli na dizeli hawatumii mashine za kodi za kilektroniki ingawa wanazo. Je, Serikali inatoa Kauli gani juu ya wafanyabiashara hao?

(ii) Je, Serikali ina uhakika gani juu ya vitabu vya risiti vinavyotumiwa na wafanyabiashara hawa wa mafuta ya petroli na dizeli?

Samahani, je, Serikali ina uhakika gani juu ya wafanyabiashara hawa wa vituo vya petroli na dizeli wanaotumia vitabu vya risiti?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L. MCHEMBA):** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Rukia kwa kufuatilia suala la kuihakikishia Serikali haipotezi mapato.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Serikali kutoa tamko juu ya matumizi ya kutoa risiti, niseme kwa sababu hiyo ni sheria, kama kuna mwananchi ataweza kutambua vituo vya mafuta ambavyo havitumii risiti, tunaomba tupate hizo taarifa au afikishe taarifa kwa vyombo vinavyohusika, ili hatua za kisheria ziweze kuchukuliwa. Ni agizo na ni sheria, lazima kila kituo cha mafuta kinapokuwa kimetoa huduma, watoe risiti na ni wajibu kwa wananchi pia wanapokuwa wamepata huduma wadai risiti, ili kuhakikisha kwamba fedha aliyolipa inafika Serikalini.

Mheshimiwa Spika, la pili, kuhusu Serikali ina uhakika gani ama inatumia utaratibu gani wa kuhakikisha vituo vile vinatumia mashine ambazo wanazo lakini hawatumii; nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwa utaratibu huu wa mashine hizo zilizoletwa zina mawasiliano ya moja kwa moja na Makao Makuu ya Mamlaka ya Mapato Tanzania. Kwa hiyo, akiiweka tu asipoitumia maana yake mwisho wa mwezi ama wakati wa kufanya tathmini ya mauzo kwa

Makao Makuu watatambua kwamba, kuna mashine iliyokuwa imewekwa haikutumika.

Mheshimiwa Spika, jambo moja tu ambalo ni la faraja, vituo vingi sana vinavyouza mafuta vinaendeshwa na wanawake na wanawake wana sifa moja kubwa ya kuwa waaminifu. Kwa hiyo, niwaombe tu wale mabosi wao wasije wakawapa maelekezo mengine, tuna uhakika wao watatumia mashine zile kama ziko hapo katika ofisi hizo za kazi. *(Makofi)*

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Mara nyingi wananchi wamekuwa wakijiuliza, katika soko la ndani petroli na dizeli zikiwa zimepanda, bidhaa mbalimbali kama ni sokoni au mahitaji mbalimbali nayo hupanda; lakini ikitokea petroli na mafuta hayo yameshuka bei bidhaa sokoni zinabaki bei ileile, ni kwa nini hali hii inatokea na Serikali inachukua hatua gani? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L. MCHEMBA):** Mheshimiwa Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa Cecilia Paresso, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake la nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika asili ya kupanda na kushuka ama kasi ya kupanda na kushuka kwa bei, kiutaalamu *literature* zinasema kwamba bei zinapopanda huwa zinapanda kwa kasi, lakini zinaposhuka zinashuka kwa taratibu kufuatana na vigezo vinavyotumika; na hata viashiria vile vilivyosababisha bei kupanda vitakapokuwa vimebadilika ni tofauti na pale ambapo vilibadilika kwa ajili ya kupanda.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa swali alilouliza la mafuta *specifically,* utaratibu wa hapa Tanzania sasa hivi kuna mamlaka ambayo inatoa bei elekezi. Kwa hiyo, inategemea kikao kile kilielekeza bei hizo zianze kushuka muda gani na baada ya kujiridhisha kwamba, mwenendo wa bei ya mafuta katika vyanzo vya mafuta itaendelea kuwa ya kushuka ama ya kupanda.

Kwa hiyo, kwa utaratibu ule wa bei elekezi, ile bei elekezi ndiyo inayosema ni lini bei ile ianze kushuka kufuatana na bei ya mafuta kushuka katika chanzo cha mafuta yalikonunuliwa.

Na. 125

**Mkakati wa Kuboresha Ukusanyaji wa Mapato na Matumizi**

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA** aliuliza:-

Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* inakusanya mapato kiasi cha takribani bilioni mia nane kwa mwezi na kuna vyanzo vingine vya mapato; kila mwaka tunapitisha Bajeti ya Serikali, lakini baadaye tunaambiwa Serikali haina fedha hivyo kusababisha Halmashauri zetu kupewa asilimia 30 au asilimia 40 tu ya fedha zilizoombwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo:-

(a) Je, ni lini Serikali itakuwa makini katika kukusanya na kutumia vizuri mapato yake?

(b) Je, Serikali ina mkakati gani wa kupunguza misafara ya viongozi ya ndani na nje ambayo ni mikubwa sana na haina tija?

(c) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha *"Payroll"* ya Serikali haina watumishi hewa?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L. MCHEMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Deogratius Aloyce Ntukamazina, Mbunge wa Ngara, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali muda wote imekuwa katika kukusanya mapato na kudhibiti matumizi. Umakini wa Serikali katika kukusanya mapato yake unajidhihirisha wazi katika mwenendo wa ukuaji wa mapato hayo.

Katika kipindi cha miaka 10, mapato ya Serikali yamekuwa kwa wastani wa asilimia 22 kwa mwaka kutoka shilingi 1,773,709 mwaka wa fedha 2004/2005 na kufikia shilingi 10,252,981 mwaka wa fedha 2013/2014. Ongezeko hilo limetokana na hatua mbalimbali za kisera na kiutawala zilizochukuliwa katika kuimarisha ukusanyaji wa mapato. Ili kuwa na nidhamu na umakini katika matumizi yake, Serikali hufanya matumizi yake kulingana na mapato na kuzingatia vipaumbele vilivyoainishwa katika bajeti ambayo huidhinishwa na Bunge lako Tukufu.

(b) Mheshimiwa Spika, si kweli kwamba misafara ya viongozo ya ndani na nje haina tija. Viongozi wa Serikali na hata Chama Tawala, hufanya ziara ndani ya nchi kukagua, kuhimiza na hata kushiriki katika shughuli za maendeleo, wakati mwingine kushiriki katika kuhamasisha harambee za kuchangia shughuli mbalimbali za maendeleo kama vile zahanati, shule, barabara na hata *VICOBA* na *SACCOS.*

Mheshimiwa Spika, ziara za nje ya nchi pia zina tija kubwa, ziara hizo hufanyika kwa ajili ya kuonana, kujadiliana na kufanya makubaliano na washirika wetu wa maendeleo katika masuala ya misaada, mikopo na

uwekezaji. Ziara hizi hutumika pia kutangaza vivutio na fursa za utalii na kwa hali hiyo, huhamasisha kuvutia watalii. Waheshimiwa Wabunge wanafahamu kuwa Mashirika ya Kimataifa ya Ulaya, Benki ya Dunia, Benki ya Ulaya, Shirika la Fedha la Kimataifa, Benki ya Maendeleo ya Afrika na hata nchi moja moja kama Uingereza, Marekani, Uchina, Japani huutaka ujumbe wa Serikali yetu kufika huko kwenye Mashirika hayo na nchi hizo kwa ajili ya kukamilisha masuala ya misaada, mikopo na hata vitega uchumi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikifanya jitihada za kuhakikisha kuwa watumishi wake wanaolipwa mshahara ni wale tu wanaostahili na siyo wasiostahili kama vile waliofariki, kuacha kazi na utoro ama kufukuzwa kazi.

Mheshimiwa Spika, katika mkakati wa kuhakikisha *Payroll* ya Serikali haina watumishi hewa, hatua kadhaa zimechukuliwa miongoni ikiwa ni pamoja na:-

(a) Tangu Julai, 2014 Serikali imekuwa inalipa mishahara moja kwa moja kwa akaunti za watumishi waliopo kazini kila mwezi. Baada ya Serikali kuweka mfumo wa kielektroniki wa taarifa za watumishi, mfumo huo unampa fursa Afisa Masuuli kila anapofunga ama kurekebisha taarifa za watumishi wake, ikiwemo kuingiza watumishi wapya na kuondoa watumishi ambao hawastahili.

(b) Kufanya uhakiki wa ana kwa ana kwa watumishi wote nchini.

(c) Kufanya tathmini ya mfumo kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, kuboresha ufanisi wa mfumo huo.

**MHE. DEOGRATIUS A. NTUKUMAZINA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu mazuri. Nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa miaka minne mfululuzo Wilaya ya Ngara imekuwa ikipata fedha za maendeleo kidogo sana kati ya asilimia 30 mpaka 40 na bila shaka hii ni sahihi kwa Wilaya nyingi katika nchi yetu. Miradi mingi imekwama kwa mfano miradi mbalimbali ya maji. Ukimuuliza Waziri anakwambia muulize Waziri wa Fedha, huwa najibiwa mimi muulize Waziri wa Fedha. Ninajua kwamba Baraza la Mawaziri au *Cabinet* chini ya Uenyekiti wa Rais lina *collective responsibility* ya kusimamia makusanyo ya mapato na matumizi yake. Sasa hata sisi Wabunge tunapoulizwa na wananchi kwa nini miradi imekwama tunasema Serikali haina fedha.

(i) Je, ni lini tutaondokana na aibu hii ya kusema kila wakati Serikali haina fedha?

(ii) Wakati hatuna fedha za maendeleo na miradi mingi imekwama, Serikali imetumia muujiza gani kufanikisha *BRN;* tunaambiwa kutokana na tathmini iliyofanyika tumefanya vizuri, matokeo mazuri. Sasa katika hali ya Serikali ya kutokuwa na fedha imekuwaje? Tunaambiwa eti Wizara ya Elimu imekuwa ya kwanza, mimi kama mwalimu nimesikitika sana na kushangaa sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L. MCHEMBA):** Mheshimiwa Spika, kwanza, nimpongeze kwa jinsi anavyofuatilia shughuli za Miradi ya Maendeleo jimboni kwake. Nilifika mwenyewe Lulenge na Ngara, nimeona jitihada alizozifanya katika kuyapatia ufumbuzi baadhi ya matatizo yanayoikabili Wilaya yake. Aliuliza tutaondoka vipi na aibu hii ya miradi kutokukamilika kwa Serikali kukosa fedha; jambo moja kubwa ni makusanyo na kwenye hili hii asilimia ambayo ameisemea, Serikali imejipanga kuongeza makusanyo si tu kwa kutumia mamlaka ya mapato, bali hata sehemu zingine ambako yanakusanywa maduhuli na sehemu zingine kama kwenye Halmashauri.

Tumesema Halmashauri nazo waongeze jitihada katika kufanya makusanyo na fedha ambazo wamezitenga ziende kwenye Miradi wahakikishe zinakwenda kwenye miradi hivyo hivyo. Jitihada nyingine ni kama hii tuliyoisema ya kubana matumizi kuhakikisha fedha zinazopatikana zinakwenda kwenye Miradi iliyokuwa imekusudiwa.

Kuhusu mafanikio kwenye *BRN* kwamba yana-*contradict* na sentensi za mara kwa mara kwamba hakuna fedha; niseme tu kwamba Miradi ama Wizara zilizopangiwa kwenye Matokeo Makubwa Sasa zilipewa kipaumbele fedha zinapopatikana, lakini pia katika miradi ile ile mingine ilipata fedha ambazo zilikuwa zimetengwa na mingine ilipata kutoka kwa wahisani wa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, niseme ni kweli kwamba kati ya maeneo ambayo atakuwa amesikia kuwa yamefanya vizuri katika Miradi ya *BRN* ni ukweli yamefanya vizuri. Bahati nzuri Miradi ya *BRN* inaonekana kwa macho siyo Miradi ambayo iko kwenye *records*; ni Miradi ambayo inaonekana kwa wananchi. Kwa hiyo, hiyo ni ya uhakika na ndiyo maana ukipata takwimu zake utaona jinsi ambavyo miradi ile imebadilika kuanzia zoezi la *BRN* lilipoanza na mpaka sasa ambapo inaripotiwa.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Naomba kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa swali la msingi linahusu ukusanyaji wa mapato na mwisho wa watu kusajili pikipiki ambazo nazo zinachangia kwenye mapato ni kesho. Kwa nini Serikali isiongeze muda lakini pia irudishe shughuli hizi Wilayani kwa sababu

wananchi wetu wanakwenda mikoani ambako ni mbali wanashindwa kusajili pikipiki matokeo yake Serikali inakosa mapato; kwa nini isirudishe mambo haya Wilayani na kuongeza muda ambao unaisha kesho? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L. MCHEMBA):** Mheshimiwa Spika, kwanza niwapongeze Wabunge ambao walikuwa wanafuatilia suala la usajili wa pikipiki.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka wiki iliyopita liliombewa Mwongozo na Mheshimiwa…

**SPIKA:** Blandes.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Blandes na Wabunge wamekuwa wakiliulizia. Kwa kifupi tu nijibu kwamba kwa niaba ya Wizara niwatangazie Ofisi za Mamlaka za Mapato kuanzia Makao Makuu na Mikoani kwamba zoezi hilo sasa litaongezewa muda mpaka Desemba ili kuwapa fursa vijana wetu pamoja na wamiliki waweze kukamilisha usajili huo. Nitoe angalizo kwamba wahakikishe katika kipindi hiki kirefu cha kutosha kilichotolewa wakamilishe usajili huo.

Kuhusu kama tunaweza tukapeleka Wilayani, hilo tuwaachie Mamlaka ya Mapato, kwa sababu litahusisha *staffing*, ni suala la kiutawala na Ofisi za Mamlaka ya Mapato ziko katika ngazi za Mikoa. Kwa hiyo, tuziachie katika utaratibu wao wa kufanya kazi. Nisisitize kuwa vijana wetu pamoja na wamiliki wajitahidi kuhakikisha wanatumia muda huo uliotolewa ili utakapofika muda ule wasiwepo tena wengine ambao watakuwa wanahitaji nyongeza. *(Makofi)*

**MHE. SALUM K. BARWANY:** Mheshimiwa Spika, sisi watu wenye ulemavu wa ngozi, familia zetu na wale wachache wanaotutakia mema na kutuhurumia, tunaitaka Serikali ijibu swali letu Namba 126.

Na. 126

**Mauaji ya Watu Wenye Ulemavu wa Ngozi Nchini**

**MHE. SALUM K. BARWANY** aliuliza:-

Mauaji ya watu wenye ulemavu wa ngozi nchini yamekuwa kitendawili kwa sababu yanatulia na baadaye kuibuka tena:-

(a) Je, ni kesi ngapi za mauaji ya walemavu wa ngozi zimeshatolewa hukumu baada ya kufikishwa Mahakamani?
(b) Je, ni kesi ngapi zilizoko Mahakamani zikisubiri hukumu?

(c) Kama zipo, je, kwa nini zinachelewa kutolewa hukumu?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Salum Khalfan Barwany, Mbunge wa Lindi Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kati ya mwaka 2006 na 2015, jumla ya matukio ya uhalifu dhidi ya watu wenye ulemavu ngozi yaliripotiwa nchini. Matukio 41 yaliyohusisha vifo 43, matukio 13 yalihusisha majeruhi 13 na matukio mawili ya kupotea kwa watu wenye ulemavu wa ngozi. Kesi 46 kati ya matukio 56 zilifikishwa Mahakamani ambapo kesi 10 zenye watuhumiwa 12 zilitolewa hukumu ya vifo na nyingine 10 ziko kwenye hatua za upelelezi. Aidha, kesi 26 watuhumiwa wake waliachiwa huru kwa *nolle prosequi* kwa kukosa ushahidi.

(b) Mheshimiwa Spika, kesi 10 zinaendelea kusikilizwa mahakamani katika hatua mbalimbali.

(c) Mheshimiwa Spika, kuchelewa kwa hukumu au upelelezi wa baadhi ya kesi nilizozitaja hapo juu kunachangiwa na sababu nyingi kama vile matokeo ya uchunguzi wa *DNA* kutoka mamlaka ya uchunguzi au na kutokupatikana mashahidi kwa wakati na urahisi.

**MHE. SALUM K. BARWANY:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri.

(i) Katika majibu yako msingi umesema kuanzia mwaka 2006 mpaka mwaka 2015 ni kesi 10 ambazo Mahakama Kuu imeshatoa hukumu ya mauaji ya kesi hizo. Ni nini utekelezaji wa amri hiyo ya Mahakama hadi leo?

(ii) Kuna mtaalam mmoja ametoa maelekezo kwa Serikali na ameshakutana na Waziri Mkuu kwamba kuna chombo *(device)* ambacho mtu mwenye ulemavu wa ngozi akikutwa na athari hiyo hubonyeza hicho kidude na kutoa taarifa yuko wapi na maeneo gani. Je, Serikali ina mpango gani kuwapatia watu wenye ulemavu wa ngozi nchi nzima ili wakae katika tahadhari kupitia chombo hicho?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli Mahakama imetoa hukumu ya kesi 10 zinazowahusisha watu 12 kunyongwa hadi kufa. Taratibu zetu za kisheria zinahitaji *signature* ya Mheshimiwa Rais ili kuidhinisha kifo hiki. Kwa taarifa yangu sijapata taarifa kwamba hukumu hii imeshatekelezwa, lakini tutafuatilia tuone zinachukuliwa hatua kama sheria inavyotaka.

Swali (b) kuhusu *device* ambayo pengine tungewapa watu ambao wana ulemavu wa ngozi kwa ajili ya kuonyesha *distress*, kwa kweli sina taarifa nzuri kuhusu hiki chombo, lakini kwa sababu ya nia nzuri ya Serikali kulinda maisha ya kila raia, basi tutafuatilia na Serikali itajitahidi iwezekanavyo tuweze kuona inapatikana na matumizi yake yanasaidia kuepusha maisha.

**MHE. AL-SHAYMAA J. KWEGYIR:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kama ilivyo kwenye swali la msingi kwamba jamii imekuwa haipati taarifa kwa wakati muafaka kuhusu vita hii muhimu au janga hili lililopo hivi sasa. Mfano, ni tukio lililotokea Kwimba, mtoto Pendo Emmanuel mwenye miaka minne, alitekwa mikononi mwa mama yake. Mtoto huyo ana *albinism*, alitekwa mikononi mama yake wakaondoka naye, mpaka leo hii hatuna taarifa za Pendo Emmanuel.

Wizara inatuambia nini au Serikali inatuambia nini kuhusiana na mtoto huyu Pendo Emmanuel ambaye hatujui yuko wapi mpaka hivi sasa? Tunamwaga machozi kwa ajili ya mtoto huyu yuko wapi? Tunaomba Wizara ituambie. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nimjulishe muuliza swali kwamba machozi nami yananitoka.

Mheshimiwa Spika, ni kwamba ni mambo yanayosikitisha sana na yanatu-*relegate* jamii ya Watanzania kutoka kwenye ubinadamu na tukashuka tukarudi kule ambako historia inasema tumetoka. Hii ni aibu, ni janga na tunatakiwa Watanzania tujiepushe nalo ili tujikoshe dawa tuweze kuonekana binadamu tena.

Kitendo hiki ni kinyume na sheria, lakini pia ni kinyume na ubinadamu. Ninawasihi wote ambao wanashiriki tukiache ili maisha ya wenzetu pamoja na unyanyapaa uliokuwepo basi yatoke na tuweze kuishi nao kama wenzetu wa kawaida.

Mheshimiwa Spika, Pendo alitekewa mikononi kwa mama yake na hapa ndiyo panapoonyesha ugumu kweli wa kuweza kuwalinda wenzetu hawa. Kama mtoto amebebwa halafu bado ananyang'anywa, kwa kweli inaonyesha jamii inahitajika zaidi itoe taarifa na isaidie katika mambo haya. Kutegemea polisi au pengine Serikali, tukishafika kwenye hali ya mtu kalala na mama yake au yuko mikononi, kwa kweli tuko kwenye jambo ambalo ni kubwa kulidhibiti.

Mheshimiwa Spika, Pendo tunamtafuta bado, lakini tuna *clues* na tunao watu 14 ambao tumewakamata kuhusiana na janga hili. Bado hatujafanikiwa

kujua yuko wapi, lakini watu 14 tunaendelea kuwahoji na tunawapeleka mahakamani akiwepo baba mzazi.

**SPIKA:** Haya, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Dkt. Henry Daffa Shekifu, badala yake Mheshimiwa Omari Nundu.

Na. 127

**Ruzuku ya Pembejeo za Kilimo kwa Wakulima wa Mboga na Matunda Wilayani Lushoto**

**MHE. OMARI R. NUNDEU (MHE. DKT. HENRY D. SHEKIFU)** aliuliza:-

Katika mwaka wa fedha 2012/2013 wakati Wizara ya Kilimo ikiwasilisha hotuba yake ya mwaka huo niliiomba Serikali ikaniahidi kushughulikia suala la utoaji ruzuku ya pembejeo za kilimo kwa wakulima wa mboga na matunda Wilayani Lushoto lakini mpaka sasa hakuna kinachoendelea:-

(a) Je, Serikali inasema nini juu ya ahadi hiyo kutekelezwa?

(b) Je, wakulima hao watawezeshwaje hasa ikizingatiwa kuwa kilimo cha mboga na matunda kina gharama kubwa hasa katika kupata mazao yaliyo bora yatakayoingia katika ushindani katika Soko la Kimataifa?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Henry Daffa Shekifu, Mbunge wa Jimbo la Lushoto, lenye sehemu (a) na (b), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikitoa ruzuku ya pembejeo za kilimo kwa wakulima kwa lengo la kuongeza upatikanaji wa pembejeo na kujenga utamaduni wa matumizi endelevu ya pembejeo za kilimo miongoni mwa wakulima nchini na hivyo kuongeza uzalishaji na tija ya mazao nchini.

Hata hivyo, kwa kuzingatia umuhimu wa usalama wa chakula na ufinyu wa bajeti, ruzuku ya pembejeo ya mbolea na mbegu bora imekuwa ikielekezwa kwa mazao makuu ya chakula, mahindi na mpunga pamoja na mbegu za mtama na alizeti.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa mazao ya bustani kwa Uchumi wa Taifa, mwaka 2013/2014 Serikali iliahidi kuangalia uwezekano wa kutoa ruzuku ya pembejeo kwa mazao hayo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kutokana na ufinyu wa bajeti, Serikali haikuweza kupanua wigo wa ruzuku kwa mazao mengine kama mboga mboga na matunda.

Aidha, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Serikali ilitenga jumla ya shilingi 2,412,692,000/= kwa ajili ya ruzuku ya pembejeo kwa mbolea ya kupandia na kukuzia, mbegu za mahindi na mpunga kwa Mkoa wa Tanga, ambapo Wilaya ya Lushoto ilipata jumla ya shilingi 600,852,000/=. Kati ya fedha hizo, ruzuku kwa mbegu bora za mahindi ilikuwa shilingi 81,450,000/=, mbegu bora za mpunga ilikuwa shilingi 20,232,000/= na mbolea ya kupandia na kukuzia zilikuwa shilingi 499,170,000/=.

Mheshimiwa Spika, katika mpango wa kuwawezesha wakulima wa mboga mboga na matunda kupunguza upotevu, kuongeza thamani ya mazao, kupata bei nzuri za mazao na kuongeza uhakika wa chakula, Wizara imejenga jengo la kuhifadhi mbogamboga na matunda *(park house)* na kuweka *container* la baridi *(refrigerated container),* kwa shilingi 400,132,000/= Mjini Lushoto, kwa ajili ya kuhifadhia mboga mboga na matunda kwa vikundi 85 vya wakulima wa Wilaya ya Lushoto na Korogwe, kutoa mafunzo ya hifadhi bora na usindikaji wa mazao kwa wakulima na kuwaunganisha wakulima na masoko ya ndani ya nje ya nchi.

Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau, itaendelea kutafuta masoko ya mazao ya bustani katika nchi mbalimbali zikiwemo za Mashariki ya Kati na Marekani kupitia maonesho mbalimbali ya kilimo na bidhaa pamoja na kutoa mafunzo ya uzalishaji bora wa mazao, hifadhi bora na usindikaji wa mazao kwa wakulima.

**MHE. OMARI R. NUNDU:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake ambayo yanaonyesha kuwa wanatilia maanani ukulima wa Tanga. Kwenye hili la mboga na matunda, mwaka 2012/2013 walishindwa kutoa ruzuku:-

(i) Bado tunataka kujua ni lini ruzuku itapatikana kwa mazao haya ya mboga na matunda?

(ii) Naishukuru Wizara kwa kuweka jitahada za kujua kuwa ruzuku pia inatakiwa kwa mazao makubwa kama mahindi na mpunga na hapa wameweka takribani shilingi 2,412,692,000/= kwa mwaka 2013/2014 kwa mkoa mzima wa Tanga, lakini yamegawanywa alivyotueleza hapa kwa Lushoto.

Nataka kujua mgao huo kwa wilaya nyingine kwa zile pesa ambazo zilibaki takribani shilingi 1,811,840,000/= umekuwaje hasa ukizingatia kwa Wilaya ya Tanga ambayo pia inalima mahindi na mpunga kwa tija ndogo sana? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwenye majibu ya msingi nilisema kwamba tulishindwa kupeleka pesa kwa ajili ya kuhudumia mboga mboga pamoja na matunda kwa sababu ya ufinyu wa bajeti. Sasa anauliza mwaka huu itakuwaje?

Mimi naomba nilieleze Bunge lako na Waheshimiwa Wabunge kwamba bajeti tunapitisha hapa Bungeni, tunapopata bajeti ya kutosha tunaweza tukahakikisha kwamba na wakulima wa mboga mboga wanapata. Wote tumekuwa mashahidi kwamba hata mwaka jana tulipopitisha bajeti hapa kwa ajli ya pembejeo hizi bajeti hiyo haikutoka yote. Tumesema kwamba ni afadhali na ni muhimu zaidi tukatilia maanani kwenye mazao yale makubwa ambayo tunahakika njaa inapotokea tunaweza kuwapa wananchi na wakaweza kupona kuliko kupeleka nguvu zaidi kwenye mbogamboga na matunda.

Mheshimiwa Spika, lakini hata hivyo, tumekuwa na jitahada za kuwaunganisha wakulima hawa pamoja na masoko ya uhakika. Kwa mfano, wakulima hawa wameshaunganishwa na masoko makubwa ya Dar es Salaam pamoja na kule Arusha ambako wanaweza kabisa wakapeleka mazao yao. Pia tunawaunganisha kwa maana ya kutafuta masoko katika nchi nyingine kama nilivyosema nchi za Ulaya huko pamoja na Marekani. Kwa hiyo, jitihada hizi tunazofanya maana yake tunawapatia wakulima hawa soko kubwa zaidi kwa mazao yao na wanapata pesa nyingi kwa ajili ya kuweza kulima mbogamboga pamoja na matunda kwa tija zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mgao wa fedha ambao Mheshimiwa Mbunge anauliza kwa Wilaya nyingine mgawanyo wake ukoje? Nitaonana naye ili niweze kumpa mgao kwa Wilaya nyingine ulikuwa namna gani lakini hapa

kimsingi tulikuwa tumetoa takwimu tu kwa ajili ya swali kama lilivyoulizwa kwa maana ya kule Lushoto. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante. Naomba tuendelee, muda wenyewe umeshakwisha, tuendelee na Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa John Paul Lwanji atauliza swali.

Na. 128

**Kukosekana kwa Mawasiliano ya Simu za Mikononi Tarafa ya Itigi**

**MHE. JOHN P. LWANJI** aliuliza:-

Serikali imeshindwa kuzishawishi kampuni za simu kuweka mawasiliano ya simu za mkononi kwenye Kata za Mwamagembe, Idodyandole na Kitaraka, Tarafa ya Itigi, Wilayani Manyoni:-

Je, Serikali inawaeleza nini wananchi wa maeneo hayo ambao wamesubiri ahadi ya muda mrefu bila mafanikio?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mbunge wa Manyoni Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spkka, ni kweli Serikali imepata changamoto kubwa kuzishawishi kampuni za simu kuweka minara katika Tarafa ya Itigi. Hata hivyo, hatujakata tamaa. Serikali inatambua kilio cha muda mrefu cha wananchi wa Kata ya Mwamagembe wakiongozwa na Mbunge wao Mheshimiwa Lwanji. Kwa hiyo, Kata ya Mwamagembe imejumuishwa katika Mradi wa Mawasiliano ya Mipakani na Maeneo Maalum yaani *Border and Special Zones Pro*ject unaosimamiwa na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote. Mchakato wa zabuni umeshafanyika na taratibu muhimu zinakamilishwa kabla ya ujenzi wa mnara huo kuanza. Aidha, Kata ya Idondyandole imejumuishwa katika mradi wa Mawasiliano Awamu ya IIA unaosimamiwa na Mfuko huo ambapo ujenzi wa mnara katika Kata hiyo unatarajiwa kuanza mwezi Mei mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine, Kata ya Kitaraka inatarajiwa kujumuishwa katika miradi ijayo ya Mfuko kuhakikisha kwamba wananchi wa Kata hiyo wanapata mawasiliano kama ilivyo katika Kata nyingine.

**SPIKA:** Mheshimiwa Lwanji, swali la nyongeza.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, ni takribani miaka mitano sasa majibu ninayopewa kuhusu Kata ya Mwamagembe ni haya haya ya mchakato na leo hii tunaambiwa mchakato umeandaliwa lakini hawawi-*specific* kueleza ni lini hasa mnara utajengwa Mwamagembe. Kwa sababu Idondyandole wamekuwa *specific* wamesema inaanza Mei lakini kwa Mwamagembe, Kata ambayo kwa muda mrefu tumeomba ipate mnara bado tunaambiwa mchakato unaendelea. Ni lini hasa ujenzi utaanza?

Mheshimiwa Spika, la pili, kuna Kampuni inaitwa *Viettel* imepita maeneo hayo, napenda kujua mahusiano yake pamoja na haya makampuni mengine au Mfuko huu wa Mawasiliano?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, utaratibu unaotumika wa sekta binafsi ni kwamba sisi Serikali tunatoa ruzuku na ushawishi kwa makampuni kupeleka mawasiliano. Kwa Kata ya Mwamagembe ahadi tunayompa Mheshimiwa Mbunge ni ahadi ambayo na sisi tunapewa na makampuni ya simu. Katika miezi michache iliyopita kumekuwa na changamoto kubwa sana kwa makampuni yenyewe kupeleka mawasiliano katika maeneo hayo. Ndiyo maana tumeamua kama Serikali sasa kualika kampuni mpya na kuingia nayo mkataba, hiyo kampuni ya *Viettel* na kuielekeza maeneo yote nchini ambayo hayana mawasilino na kuielekeza kwamba ianzie huko kupeleka mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, napenda kumpa taarifa njema Mheshimiwa Lwanji kwamba ujenzi wa minara katika maeneo yafuatayo ya Wilaya ya Manyoni umeanza: Mwamagembe, Mlowa, Kazikazi, Doroto, Mitundu, Mwembeni na Rungwa. Vilevile kampuni hiyo imeanza ujenzi katika maeneo ya Itigi ikiwemo Chikuyu, Mwakasuku, Mwazi, Solya na Sukamahela.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kujibu kwa kifupi tu swali la Mheshimiwa Lwanji ni kwamba ujenzi wa mnara katika Kata ya Mwamagembe umeanza. Nafahamu jambo hili amekuwa analifuatilia, amekuwa anakuja Wizarani kwa muda mrefu na napenda kumpongeza sana kwa mapenzi aliyonayo kwa wananchi wake. Kwa hiyo, ujenzi umeanza Kata ya Mwamagembe.

**SPIKA:** Mheshimiwa Chilolo, swali la nyongeza.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa tatizo la mawasiliano katika Wilaya ya Manyoni ni kubwa pamoja na Tarafa ya Nkonko,

Kata ya Nkonko na Kata ya Sanza ikiwemo Wilaya ya Mkalama Kata ya Mwangeza na Kata ya Nkito. Je, kupitia mtandao huo mpya alioutaja Mheshimiwa Naibu Waziri, atakuwa tayari kuishawishi kampuni hiyo kupeleka pia mawasiliano kwenye Kata hizi nilizozitaja?

**SPIKA:** Kama anazijua aseme, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILINO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, Serikali ilivyoingia katika makubaliano na Kampuni ya *Viettel,* msingi wa kampuni hiyo kupewa leseni na kuanza biashara ilikuwa ni kwamba lazima waanze vijijini na katika maeneo ambayo hayana mawasiliano. Kwa hiyo, tuliwapa orodha ya maeneo yote hapa nchini ambayo hayana mawasiliano na kuwaelekeza kwamba huko ndiko wanakopaswa kuanza.

Kwa hiyo, maeneo ya Kata ya Nkonko, Sanza na Nkito maeneo yaliyojumuishwa na kukabidhiwa kwa kampuni ya *Viettel* ambapo makubaliano yetu ni kwamba wamalize kazi hiyo kabla ya mwezi Julai mwaka huu.

**SPIKA:** Naomba tuendelee na swali linalofuata la Mheshimiwa Jerome Dismas Bwanausi.

Na. 129

**Minara ya Simu kwenye Vijiji vya Kata zilizoko Mpakani mwa Tanzania na Msumbiji**

**MHE. JEROME D. BWANAUSI** aliuliza:-

Serikali ililiambia Bunge kuwa vijiji vya Mkululu, Chiwata, Mpindipindi na Kata zilizopo mpakani mwa Tanzania na Msumbiji vitajenga minara:-

(a) Je, ni lini Kampuni ya *Tigo* iliyopewa kazi hiyo itakamilisha ujenzi wa minara katika maeneo ya Mkululu, Chiwata na Mpindipindi?

(b) Uko umuhimu wa kuwa na mawasiliano kwenye maeneo ya mipakani, je, ni lini ujenzi wa minara katika Kata za Sindano, Mchauru, Mnavira na Chikolopola ambazo zipo mpakani mwa Tanzania na Msumbiji utaanza?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jorome Dismas Bwanausi, Mbunge wa Lulindi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, vijiji vya Mkululu katika Kata ya Mkululu, Chiwata katika Kata ya Chiwata na Mpindipindi katika Kata ya Mpindipindi vilijumuishwa katika zabuni ya Mradi wa Mawasiliano kwa Wote Awamu ya IB unaosimamiwa na *UCAF* uliotangazwa Desemba, 2013 ambapo Kampuni ya Tigo ilishinda zabuni ya kupeleka mawasiliano katika vijiji hivyo. Kwa mujibu wa Kampuni hiyo ya Tigo, vijiji hivyo vinatarajia kufikishiwa huduma ya mawasiliano itakapofika mwezi Juni mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa mawasiliano katika maeneo ya mipakani katika usalama wa nchi. Kwa kutambua umuhimu huo, Serikali ilianzisha mradi wa mawasiliano mipakani na maeneo maalum yaani *Border and Special Zones Project* unaosimamiwa na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote. Katika mradi huo, maeneo ya Kata za Sindano, Mchauru, Mnavira na Chikolopola yamejumuishwa. Katika hatua nyingine, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote kwa kutumia fedha zake umetenga jumla ya shilingi bilioni 3.4 za Kitanzania kwa ajili ya kupeleka mawasiliano katika Kata 12 za mradi huu. Kata 55 zilizobaki zitapelekwa mawasiliano kwa kadri Mfuko utakavyopata fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bwanausi, maswali ya nyongeza.

**MHE. JEROME D. BWANAUSI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunai nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri.

Mheshimiwa Spika, swali langu la kwanza nataka tu Mheshimiwa Naibu Waziri anieleze, tumebaki na miezi miwili tu kufikia mwezi huo wa sita ambao ametoa matumaini kwa wananchi wa Kata ya Mkululu, Kata ya Mpindipindi na Chiwata kwamba watapata mawasiliano. Je, kwa kuwa kule hakuna jambo lolote ambalo limeshafanyika hadi sasa, Mheshimiwa Naibu Waziri anawahakikishia vipi wananchi hao kwamba kweli mwezi Juni mawasiliano yatakuwa yamepatikana?

Swali la pili, kwa kuwa aliahidi kwenye Bunge hili kwamba yeye mwenyewe atatembelea kwenye Kata hizi za Sindano, Mchauru pamoja Mnavira na Chikolopola na naamini atalieleza Bunge hili ahadi yake ataitekeleza lini.

Je, anatekeleza vipi ahadi ya Serikali ambapo alieleza kwamba maeneo yote ya mipakani ndiyo yataanza kupewa umuhimu ikiwa ni pamoja na Kata za

Sindano, Mchauru, Chikolopola na Mnavira ambazo zipo katika mpaka wa Tanzania na Msumbiji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, katika lile eneo ambalo Kampuni ya Tigo ilishinda zabuni ya kupeleka mawasiliano mpaka sasa wameshanunua eneo. Kwa hiyo, kazi iliyobaki ni kazi ya ujenzi na sisi tutawasukuma wafanye kazi hiyo haraka.

Mheshimiwa Spika, vilevile kama nilivyojibu kwenye swali la awali, Kampuni ya *Viettel* inajenga minara katika kijiji cha Nagaga kilichopo katika Kata Lulindi na inaendelea na ujenzi wa minara mingine katika Kata ya Mkululu, eneo la Miba. Vilevile inaendelea na harakati za ujenzi wa mnara mwingine katika eneo la Kata ya Mpindipindi na maeneo ya karibu na Kata hiyo. Vijiji vyote hivi ni katika Jimbo la Mheshimiwa Bwanausi.

Mheshimiwa Spika, lakini nafahamu na kama alivyosema kwenye swali lake kwamba maeneo ya mpakani ni muhimu. Kama nilivyosema awali, Serikali imetenga fedha zake na kuanzisha mradi maalum wa kujenga minara kwa maeneo ya mipakani na tumetoa zabuni na makampuni ambayo yamepata zabuni katika maeneo hayo ni Kampuni ya *Tigo* kama nilivyoelezea.

Mheshimiwa Spika, kwa kufahamu kwamba kuna ucheleweshaji kwa makampuni haya mengine ambayo tumeyazoea, tumeweka msisitizo kwamba Kampuni ya *Viettel* ambayo tumeipa kazi ya kujenga minara katika maeneo ya vijiji ianze katika maeneo ya mipakani. Napenda kumthibitishia Mheshimiwa Bwanausi kwamba kati ya mwezi wa nne au wa tano basi nitaongozana naye kwenda kuzindua ujenzi wa mnara au kuzindua mnara wenyewe katika maeneo ya Mnavira kule mpakani kwa sababu tumeongea na kampuni hii na tuna hakika kwamba wataimaliza kazi hiyo kabla ya kipindi hicho.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha. Naomba niwatambue baadhi ya wageni ambao tunao katika ukumbi huu.

Kwanza kabisa ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge, ninnao wageni wa Mheshimiwa Dkt. Binilith Mahenge, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), yupo Mheshimiwa Erasto Mahenge, Mwenyekiti wa UVCCM - Wilaya ya Makete, yupo Ndugu Micford Michael - msanii wa muziki, Ndugu Saniel Nyambo - Katibu Mwenezi, Kata ya Matamba, Ndugu Peter Tweve - mjasiriamali Makete. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wageni saba wa Mheshimiwa Amos Gabriel Makalla, Naibu Waziri wa Maji ambao ni viongozi wa wafanyakazi wa Kiwanda cha Sukari Mtibwa na

viongozi wa wakulima wa Mtibwa kutoka Mvomero. Hawa nao wasimame walipo, karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wageni kumi na mbili wa Mheshimiwa Herbert James Mntangi ambao ni Kikundi cha Hamasa kutoka Kijiji cha Kibanda, Kata ya Kilulu, Muheza, wasimame walipo. Ahsante sana na karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wageni nane wa Mheshimiwa Abuu Hamoud Jumaa, wakiongozwa na Ndugu Ernest Makungu - Katibu wa CCM, Wilaya ya Kibaha Vijijini. Naomba nao wasimame walipo, ahsanteni sana karibuni. *(Makofi)*

Tuna wageni wa Mheshimiwa Jitu Soni ambao ni wanafunzi 75 na walimu wanne kutoka Shule ya Sekondari ya Dareda ambacho ni Kituo pekee cha Mafunzo cha TEHAMA/*ICT* Mkoani Manyara. Hawa nao wasimame walipo, ahsanteni sana muendelee na hiyo teknolojia. *(Makofi)*

Tuna wageni wawili wa Mheshimiwa Ally Keissy Mohamed ambao Ndugu Costa Ulomi - Mwenyekiti wa CCM, Wilaya ya Igunga na Ndugu Hamadi Hamdani. Naomba wasimame hapo walipo, ahsante sana, karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wageni wa Mheshimiwa Mchungaji Luckson Mwanjale ambao ni Ndugu Samson Bulegi - Mwenyekiti wa Umoja wa Wainjilisti Tanzania, yuko Ndugu Eliuthi Kabelo, yuko Ndugu Shadrack Mwasonya na Ndugu Vera Mushi. Naomba hawa wasimame walipo, ahsante sana, karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wageni waliopo kwa ajili ya mafunzo Bungeni. Hawa ni wanafunzi 30 ambao ni viongozi wa Serikali ya Wanafunzi kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo. Naomba wasimame wote pale walipo kama wapo, nadhani wamekosa nafasi humu ndani.

Tuna wanafunzi 14 na walimu wawili kutoka Shule ya Sekondari ya Azania Dar es Salaam. Hawa nao wasimame pale walipo. Ahsanteni sana, karibuni sana. *(Makofi)*

Kuna Ndugu Giveness Lyaro na Ndugu Thadeo Iramba kutoka Chuo Kikuu cha Makumira Arusha. Hawa wageni wetu wasimame walipo, ahsanteni sana, karibuni sana na wageni wengine wote mnakaribishwa. *(Makofi)*

Matangazo ya shughuli za kazi. Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa Jasson Rweikiza, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa saba watakuwa na kikao, ukumbi namba 231.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo watakuwa na kikao katika Ukumbi wa Msekwa B.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Luhaga Mpina, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa saba watakuwa na mkutano wao katika Ukumbi wa Pius Msekwa.

Baada ya kusema hayo…

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mnyika!

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba Mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 84(1)(2)(3) na (4) na hasa kipengele cha (3), nitasoma vipengele hivyo kama ifuatavyo:-

"*(1) Spika atapeleka Muswada wa Sheria kwenye Kamati inayohusika na Kamati itaanza kuujadili Muswada huo mapema iwezekanavyo.*

*(2) Kamati iliyopelekewa Muswada huo itatoa matangazo au itatoa barua ya mwaliko kumwalika mtu yeyote afike kutoa maoni yake mbele ya Kamati hiyo kwa lengo la kuisaidia katika uchambuzi wa Muswada huo.*

*(3) Bila kuathiri masharti ya Ibara ya 99 ya Katiba, Kamati iliyopelekewa Muswada itakuwa na uwezo wa kufanya marekesho katika Muswada wa Sheria kwa kumshauri Waziri au Mbunge anayehusika na Muswada huo kufanya mabadailiko. Vilevile Serikali itakuwa na uwezo wa kuishauri Kamati ya Kudumu ya Bunge kuhusu kufanya marekebisho au mabadiliko juu ya Muswada Binafsi.*

*(4) Kabla ya Muswada wa Sheria uliofanyiwa mabadiliko haujawasilishwa Bungeni kwa ajili ya Kusomwa ya Mara ya Pili utapelekwa kwenye Kamati inayohusika kwa madhumuni ya kuzingatia mabadiliko hayo.*"

Mheshimiwa Spika, tulipoanza Mkutano huu wa Bunge tulipatiwa ratiba ya Mkutano wa Bunge…

**SPIKA:** Naomba usome na Kanuni ya 85.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 85(1) inasema:-

*"Kamati iliyopelekewa Muswada wa Sheria itakapokamilisha kuujadili Muswada huo, Mwenyekiti wa Kamati atamjulisha Spika kwa maandishi kwamba Kamati imemaliza kuujadili Muswada husika."*

Mheshimiwa Spika, tulipoanza Mkutano wa Bunge, katika ratiba ya Bunge ilionesha kwamba tarehe 27 Machi, 2015, siku ya Ijumaa kungekuwa na Miswada miwili. Muswada wa Sheria ya Baraza la Vijana la Taifa wa mwaka 2015 ambao ni wa Serikali na Muswada Binafsi wa Sheria ya Baraza la Vijana Tanzania wa mwaka 2013 ambao niliwasilisha kwa niaba ya vijana.

Mheshimiwa Spika, natambua kwamba uongozi ulitoa Mwongozo kwamba ni vyema Kamati ikahakikisha Muswada mmoja unaingia Bungeni. Kwa kufuata Mwongozo huo, nilitarajia kwamba masharti haya ya Kikanuni yangefuatwa. Mwaka 2013, Disemba kulisomwa Muswada Binafsi hapa Bungeni kwa Mara ya Kwanza na ukaagiza mwaka huo kwamba Muswada huo uwekwe wazi kwa umma, ukashughulikiwe na Kamati hatimaye Kamati itoe mrejesho.

Mheshimiwa Spika, mwezi Septemba, 2014 Kamati ikakutana na wadau Dar es Salaam ikakusanya maoni juu ya Muswada Binafsi lakini katika Mikutano yote ya Bunge iliyofanyika mwaka huo 2014, Muswada huo haukuletwa Bungeni na Kamati haikukamilisha kazi yake hata Mkutano wa mwanzoni mwa mwaka 2015. Katika hali ya kushangaza kidogo, Januari 2015, Serikali ikaleta Muswada juu ya suala hilo hilo ambao kimsingi haukuwa umezingatia maudhui ya msingi, sitaki kuingia kwenye maudhui, nazungumzia tu kuhusu mchakato.

Mheshimiwa Spika, sasa ni kitu kipi ambacho nakiombea Mwongozo. Kwa sababu kulikuwa na Miswada miwili na kulikuwa na dhamira ya kufikia maridhiano ili hatimaye Muswada mmoja uingie Bungeni. Nilitarajia kwamba masharti ya Kikanuni ya Kanuni ya 84(3) yangefuatwa ili kila Muswada uangaliwe, marekebisho gani yanayohitajika katika Muswada husika, mleta pendekezo awe ni Serikali au Mtoa Hoja Binafsi aambiwe tunahitaji marekebisho X, Y, Z ili Muswada huu ndiyo uingie.

Mheshimiwa Spika, jambo hili halikufanyika kabisa katika Muswada wangu Binafsi. Sijawahi kupata wakati wowote maelezo ya Kamati ni maeneo gani natakiwa kurekebisha ili Muswada huo ukubaliwe kuingia Bungeni wala sijawahi kupata maelezo ambayo Serikali imewasilisha kwa Kamati kueleza Muswada ule uliotangulia una kasoro X, Y, Z ili kuwe na sababu ya kuleta Muswada mwingine tofauti na ule Muswada ulioletwa Mara ya Kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kibaya zaidi katika hatua ya kufanya maamuzi juu ya jambo hili, ukweli ni kwamba uamuzi haukuzingatia hoja, ilipigwa kura tu

ya haraka haraka ya kuamua sasa uende wa Serikali, huu wa Binafsi uwekwe pembeni kabisa.

Mheshimiwa Spika, lakini ambacho nilitaka kukiombea Mwongozo, je, ni halali kwa matakwa haya ya Kikanuni kutokufuatwa na bado uamuzi ukawa kuingiza Muswada mmoja na mwingine kuuacha kabisa?

Pili, je, ni halali kwamba kwa taarifa nilizonazo mimi hata Kamati haijakaa pamoja kuipitia hii taarifa ya Kamati inayotaka kuwasilishwa humu ndani ya ukumbi wa Bunge? Je, ni halali vilevile kwa taarifa ya Kamati ambayo haijaandaliwa kwa pamoja kama Kamati kwa ujumla wao kuja kusomwa na Mwenyekiti wa Kamati bila kukubaliwa na Wajumbe wote? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako juu ya masuala haya ili Bunge lisiendelee kupotoshwa bali lipewe taarifa sasa itakayowezesha Bunge hatimaye kuunda Baraza bora, iwe ni kwa Muswada wa Serikali au ni kwa Muswada Binafsi ili mradi tu liundwe Baraza bora na si uchakachuaji katika hatua mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, katika kipindi hiki tulikuwa na Miswada miwili ya Bajeti; Muswada wa Bajeti ulioletwa na Kamati na Muswada wa Bajeti ulioletwa na Serikali. Vivyo hivyo, tulikuwa na Miswada miwili ya Baraza la Vijana. Mmoja wa Mheshimiwa Mnyika na mwingine wa Serikali. Maagizo ya Spika ilikuwa makundi haya mawili wakae wakubaliane ni namna gani wanaleta hapa Miswada hiyo.

Hata hivyo, kwa mujibu wa Kanuni ya 85, ndiyo maana nikamuomba Mheshimiwa aisome, baada ya hapo Spika anasubiri kuambiwa na Kamati. Mimi nimeandikiwa na Kamati kwamba wamekaa wenyewe wakapiga kura, katika Wabunge kumi na tatu waliokuwa pale, tisa walisema watumie Muswada wa Serikali na wanne walisema watumie Muswada wa Mnyika. Hiyo ndiyo taarifa niliyopewa mimi na kwa mujibu wa Kanuni yangu ndivyo inavyosema. Mimi siendi kwenye Kamati, sileti Muswada wowote hapa mpaka nimeambiwa na Kamati inayohusika kwa mujibu wa Kanuni ya 85(1) kinachosema Kamati iliyohusika ndiyo itamuarifu Spika kwamba wako tayari. Hivyo ndivyo ilivyotokea. *(Makofi)*

Katibu, tunaendelea.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, kuna miongozo mingine, tulikuwa tumesimama.

**SPIKA:** Siwezi kutumia muda mrefu kwa ajili ya miongozo, Mheshimiwa Masoud.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba Mwongozo wako kwa kutumia Kanuni ya 47(1) kuahirisha shughuli za Bunge kujadili jambo la dharura.

Mheshimiwa Spika, suala la amani na utulivu ni suala la watu wote, suala hili halina mjadala na suala hili ni suala kubwa na sote tunalipenda. Kuna viashiria vya uvunjifu wa amani ambavyo sote tunaona kwamba kwa njia moja au njia nyingine kama havikudhibitiwa vinaweza kulipeleka Taifa hili mahala pabaya sana.

Mheshimiwa Spika, jana wakati wa mkutano wa hadhara wa Chama cha Wananchi *(CUF)* uliokuwa ukifanyika Makunduchi, wasamaria wema walitoa taarifa kwamba wakati wa kurejea kwa msururu/msafara huo kutatokea matukio ya uvunjifu wa amani. Chama cha Wananchi *(CUF)* ikatoa taarifa kwa *OCD* Wilaya ya Kusini, *OCD* Wilaya ya Kusini akatoa taarifa Makao Makuu Zanzibar ili kutoa ulinzi na ulinzi ulitolewa kutoka pale Makunduchi hadi kufika Fuoni. Makubaliano yalikuwa kwamba wakifika Fuoni askari wa Wilaya ya Mjini wachukue zamu yao kuusindikiza msururu/msafara wa *CUF* hadi wafike mjini salama wa salimin.

Jambo ambalo halikutokea na linatusikitisha, kufika pale Fuoni, askari wa Wilaya ya Mjini ambao wangesindikiza msafara ule hawakuwepo na hapo ndipo mashaka yalipotokea, watu walipigwa chupa, walilengwa vigae, walichomwa na vitu vya ncha kali na hadi hivi ninavyozungumza Mheshimiwa Spika watu hao hivi sasa wengine wako Mnazi Moja na hospitali ya Al-Rahma. Taarifa zilizopo, gari lililotumika, *plate numbers* zilitolewa lakini pembeni lilikuwa limeandikwa BHAA maana yake ni gari la Mwakilishi wa Bububu.

Mheshimiwa Spika, hili jambo kubwa, halikubaliki, ni jambo ambalo halivumiliki, ni mfululizo wa matukio, ukiachia lile la Lipumba, ukiachia lile la Wilaya ya Dimani kutiwa moto hivi karibuni, lakini sasa inaelekea kuna mbinu za makusudi kukiandama Chama cha Wananchi *(CUF)*. Hatujui kama ni kampeni ama ni jambo gani, ni viashiria vibaya sana vya kuvunja amani.

Mheshimiwa Spika, hili jambo ambalo tunalizungumza linatia uchungu kweli. Ni kwa nini basi hatupati msaada wowote hali hii inapotokea? Naomba nitoe hoja jambo hili lijadiliwe ili tujue ni nini ambacho kinaendelea.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Hoja ya namna hii haiungwi mkono na mtu yeyote. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Masoud naomba utumie Kanuni 50 ulete maelezo yaliyoandikwa vinginevyo hatuwezi sisi kushughulikia suala hilo. Tumia Kanuni 50 leta Maelezo ya Binafsi hapa. Mheshimiwa Gekul!

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) juu ya kauli ambayo Serikali ilitoa katika Mkutano wa 18 wa Bunge kuhusu malipo kwa wakulima wa mahindi.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilisema tarehe 30 Machi, 2015 ambayo ni siku ya leo ingelipa madeni ya wakulima wa mahindi kwa nchi nzima yenye zaidi ya shilingi bilioni 87. Hadi hivi tunavyozungumza kwa Kanda yangu ya Kaskazini ambapo Mkoa wa Manyara ni miongoni mwa Mikoa hiyo, Mkoa wa Manyara mpaka sasa unadai shilingi bilioni nne wakulima hao hawajalipwa.

Mheshimiwa Spika, kinachosikitisha wakulima ambao wanadai ni wale wakulima halisi si wafanyabiashara. Wale wafanyabiashara wengi wao wameshalipwa lakini wale wenye gunia 50 mpaka 100 mpaka sasa wanadai zaidi ya shilingi bilioni nne na kati ya shilingi bilioni saba ambazo Kanda inadai Mkoa tu wa Manyara ni shilingi bilioni nne.

Mheshimiwa Spika, leo ni tarehe 30 Machi, 2015, ni kwa nini Serikali au Waziri wa Kilimo asije hapa akatueleza ni kwa nini haijalipa pesa za wakulima hao wa mahindi au ni lini zitalipwa kwa sababu wakulima hao wamevumilia vya kutosha?

Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako.

**SPIKA:** Ahsante. Tutatoa Mwongozo huu kwa muda muafaka. Katibu!

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako.

**SPIKA:** Mheshimiwa Keissy na wewe ni Mwongozo gani?

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, huku hutuoni tumesimama.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba Mwongozo wako kutokana na mambo yaliyotokea leo asubuhi kuhusu swali la Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohamed, swali namba 123 lililokuwa linahusu Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, tusipoangalia nchi hii itaingia kwenye mambo ya *EPA* au wizi wa Rada. Hii *Pride Tanzania* chanzo chake Mheshimiwa Waziri amekibana, ni pesa kutoka Serikali ya Norway ziliingia nchini kwa ajili ya kusaidia wafanyabiashara wadogo wadogo lakini mpaka sasa kuna baadhi ya watu wamehodhi *Pride Tanzania* kuwa ni mali yao binafsi. Hizi ni pesa zilitoka Norway kuja nchini Tanzania kusaidia wafanyabiashara wadogo wadogo lakini baadhi ya viongozi wamefanya kuwa ni mtaji wao na ni mali yao binafsi na mpaka sasa ni deni la nchi kutoka Serikali ya Norway.

**SPIKA:** Naomba sema Mwongozo wako sasa.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, sasa naomba Mwongozo wako kuhusu jibu alilotoa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha kwamba *Pride Tanzania* ni taasisi ya watu binafsi wakati ni hela za wananchi wote, ni kodi yetu, ni deni letu kutoka Norway?

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Joseph Mbilinyi.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, maana nimesimama sana, nilianzia kwenye maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kuna hali tete inaendelea huko nje ambayo kwa kweli kwa ilipofikia sasa ni hatari kwa usalama wa Taifa. Mbeya maduka yamefungwa kwa siku kadhaa sasa, mpaka leo maduka bado yamefungwa, hali ni mtanziko, wananchi hawaelewi, wako kwenye tahayari, tunajaribu kuomba miongozo lakini hakuna msemaji wa Serikali anayetoa *statement* kuhusu kinachoendelea katika suala hili.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nataka kuuliza, huyu Minja huyu ambaye wafanyabiashara wanam-*support* kwa nini hapewi dhamana, ameua, amebaka au amefanya nini kinachosababisha hapewi dhamana ili atoke nje sasa watu waongee na tuangalie tunakwenda vipi mbele? Wafanyabiashara wa Mbeya wengi walikuja hapa wanakataliwa kuingia humu ndani. Wengine wanakuja wanakwenda kuonana na Waziri Mkuu, unaonana vipi na wafanyabiashara bila kushirikisha wawakilishi wao ambao ni Wabunge katika vikao hivyo ili kufikia muafaka wa hili jambo linaloendelea la maduka kufungwa? Humu ndani tunazungumzia Serikali kukusanya mapato. Mnazungumzia kukusanya mapato wakati mnapoteza mapato kwa maduka kufungwa, wananchi wanateseka kwa kukosa bidhaa, watu hawawezi hata kununua *panadol* kwa sababu maduka yamefungwa…

**SPIKA:** Mwongozo nifanye nini, msinihutubie, Mwongozo nifanye nini?

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Spika, *why everyday* unani-*interfere* wakati naongea? Hapa naongea…

**SPIKA:** Wewe mwenyewe unahutubia nifanye nini sasa?

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** *Everybody is talking* nikiongea mimi lazima u-*interrupt*. *Okay*, kifupi ni kwamba hali ni tete, inahatarisha usalama wa Taifa huko nje. Mbeya itakapolipuka, msiniite mimi tena kama mlivyoniita mwaka 2011, mwende ninyi wenyewe au aende Mheshimiwa Pinda Waziri Mkuu. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Sasa umesema nifanye nini, umehutubia tu.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Spika, ndiyo utoe Mwongozo Serikali inatakiwa itimize wajibu wake ili kutatua mtanziko huu.

**SPIKA:** Haya tumesikia. Mheshimiwa Opulukwa.

**MHE. MESHACK J. OPULUKWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba Mwongozo wako kwa Kanuni ya 68(7), ila kwa faida ya muda ningependa nisiisome.

**SPIKA:** Hiyo Kanuni tunaijua, sasa sema tu unachotaka.

**MHE. MESHACK J. OPULUKWA:** Mheshimiwa Spika, hivi karibuni kulitokea janga la mafuriko makubwa sana kule Wilayani Kahama na Serikali kwa kweli kwa juhudi ilizozifanya ambazo zilikuwa ni za makusudi na za haraka iliweza kuwasaidia watu wale kwa kupeleka vifaa mbalimbali ikiwemo chakula na pia wadau mbalimbali waliweza kuingilia vikiwemo vyama vya siasa, watu binafsi kwa ajili ya kuwasaidia hawa wahanga wa mafuriko ya pale Kahama ambalo lilikuwa ni jambo jema sana.

Mheshimiwa Spika, lakini hivi karibuni tena, wiki iliyopita vyombo mbalimbali vya habari vimeripoti janga lingine ambalo nadhani ni kubwa kuliko hili la Kahama la njaa Mkoa wa Simiyu. Hivi ninavyoongea, Mkoa mzima wa Simiyu na hususan ikiwemo Wilaya ya Meatu, imetokea njaa kubwa sana na mazao yaliyolimwa na wananchi wa Wilaya hiyo yote yamekauka na hakuna matumaini tena ya kuweza kuvuna kwenye kipindi cha mavuno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mwongozo wangu, ni kwa nini sasa usiweze kuishauri Serikali, badala ya kufuata zile taratibu za kirasimu, Kamati ya Maafa ikae, watu waje watathmini, barua iandikwe, irudi, kama unaweza kuagiza Serikali kwenda Meatu mara moja ikiwezekana hata leo, hata kesho wafanye tathmini hiyo na baada ya siku moja au mbili wawe wameshapata ni kiasi gani cha chakula

kinachohitajika ili wananchi hawa waweze kupelekewa chakula kwa sababu hali ni mbaya na wananchi wanakoelekea inawezekana yakatokea hata maafa makubwa zaidi ya hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, huo ndiyo Mwongozo niliokuwa nauomba kutoka kwenye Kiti chako, ahsante.

**SPIKA:** Haya. Waheshimwia Wabunge, tutumie Kanuni zetu tutapata kazi rahisi kidogo. Kanuni ya 68(7) inasema:-

*"Hali kadhalika, Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba "Mwongozo wa Spika" kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema ili Spika atoe ufafanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa Kanuni na taratibu za Bunge na majibu ya Spika yatatolewa papo hapo au baadaye, kadiri atakavyoona inafaa."*

Mheshimiwa Opulukwa suala lako hili inatumika ama Kanuni ya 50 au ya 28, yanaitwa Maelezo Binafsi. Kama nilivyomruhusu Mheshimiwa Masoud na wewe pia. Huo siyo Mwongozo, mimi sijui kama hilo jambo limetokea humu ndani, sijasikia. Kwa hiyo, nakuagiza wewe uende ukaandike ulete hapa tutakupa muda. Hili suala ulilozungumzia Mheshimiwa Keissy limetokea humu humu ndani ya Bunge, Mheshimiwa Naibu Waziri nataka ueleze.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ADAM K. MALIMA):** Mheshimiwa Spika, kwa ufupi tu kwa ridhaa yako naomba niseme kwamba swali lilikuwa linahusu mtaji wa *Pride* kama ulivyo sasa hivi. Nikasema kwa utaratibu wake *Pride* si kampuni *(Limited by share)*.

Mheshimiwa Spika, kwa utaratibu wa Sheria Na. 212, *Pride* ni kampuni *limited by guarantees*, iko *limited* kwa dhamana na dhamana ni ya wale ambao wanajihesabu kisheria kama wanachama kwa sababu ya michango yao wanayochangia pale.

Mheshimiwa Spika, nimesema hivi, pamoja na kwamba inaweza ikawa ilikuwa ina msingi wa michango yake mwaka 1993 ilipoanzishwa, sasa hivi *Pride* ina mtaji ambao umefikia shilingi bilioni themanini na nane ambapo kati ya hizo asilimia arobaini na tano ni wachangiaji wanahisa waliotoka nje. Sasa inawezekana kwamba michango kutoka Norway na taasisi nyingine za kifedha za nje zimeingia kwenye ile asilimia arobaini na tano. Asilimia nyingine ni pamoja na *retained funds*, asilimia nyingine ya mitaji ni pamoja na mikopo kutoka taasisi za fedha za humu ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, swali langu lilikuwa kubaini waliochangia mitaji wote na kwa maana hiyo, kama sasa hivi *Pride* ina matumizi nje ya yaliyokusudiwa inadhibitiwa na sheria mbili. Moja, Sheria ya *Microfinance* ya taasisi ndogo za kifedha ambayo inadhibiti kupitia Benki Kuu na ya pili ni kupitia *Cap.212* kulingana na wanahisa au hao waliochangia katika mtaji huo.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba tu Mheshimiwa Keissy anielewe kwamba jibu lilikuwa ni hilo siyo alivyoliweka yeye.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**SPIKA:** Ahsante. Katibu!

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Baraza la Vijana Tanzania wa mwaka 2015
### *(The Youth Council of Tanzania Bill, 2015)*

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mtoa Hoja.

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Baraza la Vijana Tanzania pamoja na marekebisho yake sasa Usomwe kwa Mara ya Pili.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kushiriki Mkutano wa Kumi na Tisa wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Aidha, kwa masikitiko makubwa, napenda kuungana na wewe Mheshimiwa Spika, Kamati ya Maendeleo ya Jamii pamoja na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pole nyingi kwa familia, ndugu na jamaa wa Mbunge mwenzetu, Marehemu Kapt. John D. Komba, Mbunge wa Mbinga Magharibi, kwa kifo kilichotokea ghafla tarehe 28/2/2015 Jijini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua hafasi hii pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii chini ya Mwenyekiti wake Mheshimwia Said Mohamed Mtanda, Mbunge wa Mchinga kwa ushirikiano wao mkubwa waliouonyesha katika maandalizi ya Muswada huu muhimu kwa vijana na Taifa letu kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwishasema hapo awali, Muswada huu unawasilishwa katika Bunge lako Tukufu kwa mara ya pili. Mapendekezo ya kutungwa kwa sheria hii yanatokana na hali halisi ya mabadiliko yatokanayo na

utandawazi na teknolojia duniani, kukua kwa demokrasia, kupanuka kwa wigo wa ushiriki na ushirikishwaji wa vijana katika shughuli za maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Masuala haya yanapelekea kuwepo haja ya kuwa na chombo cha kitaifa cha kuwaunganisha vijana bila kujali itikadi zao za kisiasa, imani zao za kidini, tofauti zao za rangi na jiografia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Baraza la Vijana Tanzania litakaloundwa litakuwa ni chombo cha kuisaidia Serikali kuwafikia vijana kwa urahisi. Baraza litakuwa jukwaa rasmi la vijana kuweza kuzungumzia masuala muhimu yanayohusu maisha yao ikiwa ni pamoja na kubaini changamoto zinazowakabili, kubuni mikakati ya kuzitatua kwa maana ya kuzitekeleza, kuishauri na kuisaidia Serikali katika utekelezaji wake. Baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na ukosefu wa maadili bora, ukosefu wa ajira, matumizi ya dawa za kulevya, matatizo ya kiafya na usawa wa kijinsia katika shughuli za kujiletea maendeleo. Kwa kuzingatia dhana ya malezi na maongozi, Wizara yangu itaendelea na wajibu wake wa kuwezesha shughuli za Baraza la Vijana ili kufanikisha malengo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, chimbuko la Muswada huu ni kutekeleza Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana ya mwaka 2007, Ibara ya 3(11) inayotamka wazi kuwa Serikali itawezesha kuundwa kwa Baraza la Vijana na kuanzisha mfumo wa kisheria ili kuliwezesha kufanya kazi. Vilevile, uundwaji wa Baraza la Vijana Tanzania ni hatua muhimu ya utekelezaji wa mikataba mbalimbali ya Kikanda na Kimataifa ambayo Tanzania imeridhia. Kwa mfano, Mkataba wa Vijana wa Afrika wa 2006 ulioridhiwa na Bunge lako Tukufu mwaka 2012. Makubaliano ya Kikanda ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Baraza la Sekta ya Maendeleo ya Vijana, Watoto, Watu Wenye Ulemavu na Jinsia. Pia, utakuwa ni utekelezaji wa makubaliano ya Umoja wa Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*) na Nchi za Jumuiya ya Madola kupitia mpango wa Vijana wa Jumuiya ya Madola *(Commonwealth Youth Program)* ambayo Tanzania ni mwanachama.

Mheshimiwa Spika, hali ilivyo sasa. Kwa mujibu wa takwimu za Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012, idadi ya vijana wenye umri kati ya miaka 15 mpaka 35 katika nchi yetu ni takribani milioni 16.2 ambao ni sawa na 35% ya Watanzania wote. Vilevile asilimia 68 ya nguvukazi ya Taifa letu inatokana na vijana wenye umri uliotajwa hapo juu. Kimsingi vijana wetu wengi wameitikia wito wa Serikali wa kuanzisha asasi zao kwa mujibu wa sheria za nchi. Kwa sasa inakadiriwa kuwepo asasi za vijana takribani 6,776 zenye wanachama milioni 6,800,000. Kwa sababu hiyo, kuundwa kwa Baraza la Vijana kisheria kutawezesha kuwaunganisha vijana kupitia kwenye asasi zao na kujadili namna ya kutatua kero za kiuchumi na kijamii zinazowakabili na kupanga namna ya kuzitatua kwa maendeleo yao, jamii zao na Taifa kwa ujumla bila kujali tofauti zao za aina yoyote. Kimsingi Baraza hili litakuwa kiunganishi kizuri kati ya Serikali na vijana.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu pamoja na kuendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ambayo ni kuwawezesha vijana kimakuzi, ushauri nasaha, kiuchumi, mafunzo na uendelezaji wa ujuzi, bado zipo changamoto mbalimbali kama nilivyozitaja hapo awali ikiwa ni pamoja na kutokuwepo kwa sheria rasmi iliyotungwa kwa ajili ya kuunda Baraza la Vijana.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Vijana Tanzania linalotarajiwa kuundwa litakuwa ni chombo kinachojitegemea kisheria na kumilikiwa na vijana wenyewe. Majukumu yake yatawekwa bayana kwa mujibu wa sheria na Serikali itawezesha utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, madhumuni na sababu. Muswada huu unakusudia kutunga Sheria ya Baraza la Vijana Tanzania *(The Youth Council of Tanzania 2015)* ili kuwa na chombo cha Kitaifa cha kuwawezesha vijana kujadili masuala yao, kutambua majukumu yao, kukuza maadili mema, kukuza moyo wa umoja, uzalendo, uwajibikaji na kujitolea kwa malengo chanya miongoni mwao katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, mpangilio wa Muswada. Muswada huu umegawanyika katika sehemu sita kama ifuatavyo:-

Sehemu ya Kwanza, kifungu cha 1 - 3. Sehemu hii inaainisha masharti ya awali kama vile jina la sheria inayopendekezwa, madhumuni na tafsiri ya istilahi zilizotumika ndani ya sheria hii. Sehemu hii pia inaainisha madhumuni ya sheria ambayo ni kuweka Jukwaa la Vijana kwa ajili ya kujadili mambo yao, kuishauri Serikali kuhusu masuala yanayohusiana na maendeleo ya vijana nchini, kuunda chombo cha kuhamasisha vijana kujitolea, kushiriki katika shughuli za maendeleo, kutengeneza mitandao miongoni mwao na wadau wengine pamoja na kujenga maadili miongoni mwa vijana bila kujali tofauti zao.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Pili, kifungu cha 4 - 15. Sehemu hii inaweka masharti mbalimbali juu ya uanzishwaji, uanachama, muundo na kazi za Baraza. Pia sehemu hii inafafanua mamlaka ya Baraza na vyombo vya utendaji katika ngazi ya Taifa, Mkoa na Wilaya.

Mheshimiwa Spika, uanzishwaji na uanachama wa Baraza, kifungu cha 4. Kutaanzishwa Baraza litakalojulikana kama Baraza la Vijana Tanzania lenye mamlaka ya kushtaki na kushtakiwa. Baraza hili litafanya kazi Tanzania Bara ingawa litakuwa na fursa ya kushirikiana na Mabaraza na taasisi nyingine ndani na nje ya nchi ikiwemo Zanzibar. Uanachama wa Baraza utakuwa wa wazi na hiari kwa asasi za vijana zilizosajiliwa kwa mujibu wa sheria husika. Kanuni zitakazotungwa zitaweka utaratibu wa kuhakikisha uwakilishi wa vijana kuanzia

ngazi ya kijiji hadi Taifa umezingatiwa. Aidha, Baraza halitakuwa taasisi ya kisiasa au ya kidini katika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, muundo wa Baraza, kifungu cha 5. Kutakuwa na Baraza ngazi ya Taifa, Mkoa na Wilaya. Katika ngazi ya Taifa, Baraza litaundwa na Mwenyekiti, Katibu na Mwakilishi mmoja kutoka Baraza la Vijana la kila Mkoa. Mojawapo ya sifa muhimu ya viongozi wa Baraza ngazi ya Taifa ni kuwa na elimu ya shahada ya kwanza au zaidi ili kuwawezesha kuwa na uelewa mpana katika masuala mbalimbali ya kitaifa na kimataifa.

Mheshimiwa Spika, kazi za Baraza zitakuwa kama zilivyo katika kifungu cha 6 ikiwa ni pamoja na:-

(i) Kuhamasisha na kuendeleza ari ya kujenga umoja wa Kitaifa, kujitolea, kujitegemea na kujituma miongoni mwa vijana;

(ii) Kuendeleza tafiti mbalimbali zinazohusiana na masuala ya maendeleo ya vjana;

(iii) Kuendeleza na kutangaza Sera ya Maendeleo ya Vijana pamoja na sera nyingine zinazowahusu;

(iv) Kuendeleza na kuhamasisha usawa wa jinsia miongoni mwa vijana; na

(v) Kuendeleza masuala yanayohusiana na vijana wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, mamlaka ya Baraza, kifungu cha 7. Baraza litakuwa na mamlaka ya kuingia kwenye mkataba, kudhibiti na kusimamia mali zake, kupokea zawadi na misaada na kuingia katika mashirikiano na vyombo vingine kama itakavyoonekana inafaa katika kuendeleza malengo yake kwa idhini ya Waziri mwenye dhamana ya maendeleo ya vijana. Itaweza kushirikiana na taasisi nyingine kama *ILO, UNFPA* na *UNICEF*.

Mheshimiwa Spika, muundo na majukumu ya Baraza la Mkoa. Baraza la Mkoa litaundwa na Mwenyekiti, Katibu na Wajumbe thelathini wanaowakilisha Wilaya zinazohusika katika Mkoa huo. Kazi za Baraza la Mkoa zitakuwa ni kuishauri Serikali katika ngazi ya Mkoa kuhusu masuala ya maendeleo ya vijana, kuchagua wawakilishi wa Mkutano Mkuu na kazi nyingine kama itavyoagizwa na Baraza katika ngazi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, muundo na majukumu ya Baraza la Vijana la Wilaya. Baraza la Vijana litaundwa na Mwenyekiti, Katibu na Wajumbe wasiozidi thelathini wanaowakilisha taasisi za vijana zilizosajiliwa kwa mujibu wa sheria ndani ya Wilaya husika. Majukumu yake yatakuwa ni kuishauri Serikali katika

ngazi ya Wilaya kuhusu masuala ya vijana na kuchagua wawakilishi wa Wilaya katika Baraza la Mkoa.

Mheshimiwa Spika, Sekretarieti ya Baraza ngazi ya Taifa. Sekretarieti itakuwa chini ya Katibu Mtendaji wa Baraza na itasaidiwa na watendaji wengine wa Baraza ngazi ya Taifa kama itakavyofafanuliwa kwenye Kanuni za sheria hii.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tatu, kifungu cha 16 - 18. Sehemu hii inaelekeza juu ya mikutano mbalimbali ya Baraza. Kutakuwa na Mkutano Mkuu ambao Wajumbe wake ni Mwenyekiti na Katibu wa ngazi ya Taifa, Mwenyekiti na Katibu wa Baraza wa kila Mkoa na Mwenyekiti wa Baraza wa kila Wilaya.

Pia kutakuwa na Mkutano Mkuu wa Baraza la Vijana la Mkoa ambapo Wajumbe wake ni Wajumbe thelathini wa Baraza la Mkoa na wawakilishi wawili kutoka Wilaya za Mkoa husika. Vilevile kutakuwa na Mkutano Mkuu wa Baraza la Vijana la Wilaya. Wajumbe wa Mkoa huu ni thelathini wa Baraza la Wilaya na wawakilishi thelathini wasiokuwa Wajumbe wa Baraza la Wilaya kutoka katika asasi ndani ya Wilaya zao.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nne, kifungu cha 19 - 21. Sehemu hii inabainisha uanzishwaji wa Bodi ya Ushauri ya Baraza. Kazi za Bodi zitakuwa ni kulishauri Baraza katika utekelezaji wa mamlaka na kazi zake kama ilivyoainishwa na sheria hii. Wajumbe wake ni Mwenyekiti atakayeteuliwa na Rais, Mkurugenzi wa Maendeleo ya Vijana, Wawakilishi wa Ofisi ya Mwanasheria wa Serikali na vijana watano watakaoteuliwa na Baraza la Vijana.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tano kifungu 22 - 24. Sehemu hii inaweka bayana vyanzo vya mapato, makadirio ya mapato na matumizi pamoja na ukaguzi wa hesabu za Baraza.

Mheshimiwa Spika, mapato ya Baraza yatatokana na fedha au mali zitakazoingia kwenye Baraza kutoka kwa wawezeshaji mbalimbali wakati wakitekeleza kazi zao chini ya sheria hii. Mapato mengine yatatokana na michango mbalimbali kutoka mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa utaratibu utakaoridhiwa na pande husika.

Vilevile zawadi yoyote itakayotolewa kwa Baraza pamoja na mikopo bila kuathiri kifungu cha 7(1)(d). Baraza litaandaa makadirio ya matumizi ya kila mwaka pamoja na kuweka utaratibu wa kukagua hesabu zake kwa kila mwaka wa fedha. Pamoja na vyanzo vilivyotajwa sheria imeweka mazingira ya kuliwezesha Baraza kutafuta vyanzo vingine vya mapato kwa utaratibu utakaowekwa.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya sita, kifungu cha 25. Sehemu hii inampa Waziri mamlaka ya kutunga Kanuni zitakazoainisha uundwaji wa Kamati za Baraza, majukumu ya mamlaka za Serikali za Mitaa kuhusiana na shughuli za Baraza la Wilaya na Mkoa, utaratibu wa uchaguzi na uteuzi wa viongozi wa Baraza ngazi zote pamoja na masuala mengineyo yatakayoainishwa katika sheria hii.

Mheshimiwa Spika, hitimisho. Kutungwa na kuanza kutumika kwa Sheria ya Baraza la Vijana Tanzania kutakuwa na matokeo chanya yafuatayo:-

(i) Kuwa na Baraza la Vijana la Tanzania linalowaunganisha na kuwawezesha vijana wote nchini kujadili masuala yanayowahusu bila kujali tofauti zao za aina yoyote;

(ii) Kuwa na chombo kitakachowezesha usimamizi na uratibu endelevu wa asasi mbalimbali za vijana nchini;

(iii) Kuanzisha mamlaka ya Kiserikali itakayoratibu shughuli za vijana kupitia Wizara yenye dhamana ya maendeleo ya vijana; na

(iv) Kuweka utaratibu na mipaka ya namna Baraza la Vijana litakavyosimamia shughuli au kazi za asasi za vijana.

Mheshimwa Spika, endapo Bunge lako Tukufu litapitisha Muswada huu kuwa sheria na Mheshimiwa Rais akaridhia, sheria hii itakuwa mwongozo mzuri katika kuwaunganisha vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Hoja imeungwa mkono.

Waheshimiwa Wabunge wote wanaotaka kuleta *amendments* katika Muswada huu pamoja na Serikali, napenda hayo majedwali yafike kwa Katibu wa Bunge mapema. Majedwali yanayotolewa tukiwa humu ndani ama dakika chache kabla ya Kamati ya Bunge Zima tutakuwa hatujitendei haki wenyewe, kwa sababu sheria hizi tunatunga kwa ajili ya wananchi na siyo kwa ajili yetu sisi wenyewe. Unakuta Mbunge ametoka huko kaleta jedwali lake hapa halafu anang'ang'ania kwa sababu anaungwa mkono tu na rafiki zake lakini wengine hawakupitia majedwali hayo, kwa kweli inaumiza sana.

Sasa wote pamoja na Serikali pelekeni mapema kwa katibu wa Bunge majedwali yenu ili kusudi ayasambaze. Wale wanaotaka kuleta majedwali ya marekebisho kabla ya saa saba yawe yameshapelekwa ili kusudi wote wanaohusika wawe wameyapitia na kujadiliana huko nje ili tulete hapa kitu chenye uhakika. Kama yapo majedwali ya Serikali nayo pia hatujayapata. Kwa hiyo, kabla ya saa saba kama watu hawajapeleka majedwali hayo kwa Katibu hatutayapokea, tutayachukulia kama yamechelewa, basi! *(Makofi)*

Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati iliyoshughulikia Muswada huu.

**MHE. SAIDI M. MTANDA – MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII:** Mheshimiwa Spika, maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, kuhusu Muswada wa Sheria ya Baraza la Vijana Tanzania wa mwaka 2015 *(The Youth Council of Tanzania Act, 2015)*.

Meshimiwa Spika, utangulizi. Kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013, Kanuni ya 86(5), naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii kuhusu Muswada wa Sheria ya Baraza la Vijana Tanzania wa mwaka 2015 *(The Youth Council of Tanzania Act, 2015)*.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea mbele, naomba kutumia fursa hii kuendelea kutoa pole kwako na kwa familia ya Mheshimiwa Kapt. John Damiano Mtokambali Komba, kufuatia kifo chake na kwa kuwa alikuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati hii, Kamati yangu imepata pengo kubwa. Naomba kuliarifu Bunge lako kwamba Makamu Mwenyekiti mpya wa Kamati hii amepatikana kupitia vikao vyake halali vya Kamati ambaye ni Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba, Mbunge wa Manyovu.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ilipokea Miswada miwili inayohusiana na uanzishwaji wa Baraza la Vijana Tanzania. Muswada wa kwanza ni Muswada Binafsi uliowasilishwa na Mheshimiwa John J. Mnyika na Muswada wa pili ni Muswada wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, awali Kamati ilikutana Dar es Salaam tarehe 20 – 31 Oktoba, 2014 kujadili Muswada Binafsi ambapo pamoja na mambo mengine iliwaita wadau na Mtoa Hoja ambao walitoa maoni yao mbele ya Kamati. Maoni ya wadau na mapendekezo ya Kamati ilionesha kuwa Muswada huo haukuwa tayari kwa wakati huo na hivyo ulirejeshwa kwa Mheshimiwa Spika kwa dokezo la tarehe 06 Novemba, 2014.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ilipokea Muswada wa Serikali kuhusu hoja ya uanzishwaji wa Baraza la Vijana Tanzania. Kamati ilipata nafasi ya

kuujadili kwa kina, kupata maoni, ushauri na mapendekezo ya wadau kama inavyoonesha kwenye taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hoja zote mbili zilizofika mbele ya Kamati zilikuwa na dhamira moja na maudhui yake yanafanana, Kamati yangu haikuona busara kuleta hoja zote mbili ndani ya Bunge hili. Hivyo iliwataka Serikali na Mtoa Hoja Binafsi kukutana, kushauriana na kisha kupata muafaka wa Muswada gani utakaoingia ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu pia ilipata nafasi ya kujadili hoja zote mbili na kufanya uamuzi wa kidemokrasia wa mashauriano na maridhiano juu ya Muswada upi uingie ndani ya Bunge.

Aidha, katika kufanya maamuzi kwa mujibu wa Kanuni zetu, Kamati yangu ilitumia Kanuni ya 117(6) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Aprili, 2013 inayosema na nanukuu:-

*"Akidi ya Mkutano wowote wa Kamati ya Kudumu itakuwa theluthi moja ya Wajumbe wote wa Kamati."*

Mheshimiwa Spika, kwenye kikao hicho, Wajumbe wa Kamati walikuwa kumi na tatu (13) kati ya Wajumbe 22 wa Kamati hii. Hivyo theluthi moja ni Wajumbe ni saba (7). Wajumbe tisa (9) walipiga kura ya kutaka Muswada wa Serikali usomwe Bungeni na Wajumbe wanne (4) walitaka Muswada Binafsi usomwe Bungeni. Waliopiga kura ni hawa wafuatao; mimi Mwenyekiti Said Mohamed Mtanda…

**SPIKA:** Inatosha idadi sisi majina yenu hatuna haja nayo.

**MHE. SAIDI M. MTANDA - MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa vitabu mnavyo, orodha ya Wajumbe waliohudhuria na kupiga kura iko pale.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Kanuni ya 117(7) na nanukuu:-

*"Mambo yote yatakayojadiliwa na Kamati yataamuliwa kwa kufuata maoni ya walio wengi kati ya Wajumbe wa Kamati waliohudhuria na kupiga kura."*

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, maoni ya Kamati ya walio wengi kwamba Muswada wa Serikali ndiyo usomwe ndani ya Bunge yalipitishwa kwa mujibu wa Kanuni zetu.

Mheshimiwa Spika, mwisho Kamati ilikubaliana kwa pamoja kwamba mambo yote ya msingi yaliyomo kwenye Muswada Binafsi yatumike kuboresha Muswada wa Serikali utakaowasilishwa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata nafasi ya kupokea na kujadili maoni ya wadau wa Muswada huu katika vikao vilivyofanyika katika Ukumbi wa Pius Msekwa hapa Dodoma kuanzia tarehe 22 - 25 Machi, 2015. Aidha, taasisi mbalimbali zilialikwa kwa ajili ya kutoa maoni yao na taasisi hizo zinaonekana vizuri kwenye vitabu mlivyopewa.

Mheshimiwa Spika, wadau mbalimbali walifika mbele ya Kamati na kutoa maoni yao. Kwa namna ya pekee nitambue Kituo cha Televisheni cha *Clouds* kupitia kipindi cha *Clouds 360* kwa kuendesha vipindi vilivyolenga kuchambua Muswada huu na kutoa fursa kwa vijana kueleza maoni yao kwa uhuru. Napenda kuwahakikishia kuwa maoni yao yalifika mbele ya Kamati. Ahsante sana Kijakazi Yunus na Hudson Kamoga waendeshaji wa kipindi hiki. Endeleeni kulisaidia Taifa letu na Taifa lijue kuwa viongozi tunafuatilia habari mbalimbali wanazozitoa kupitia redio, televisheni na magazeti, hivyo vipindi vyenye kuelimisha kama hivi ni muhimu kwa maendeleo yetu.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu unakusudia kutunga Sheria ya Baraza la Vijana Tanzania ya mwaka 2015 kwa lengo la kuwawezesha vijana kutambua majukumu yao, kukuza na kuhimiza maadili mema, kuweka mazingira mazuri ya ushirikishwaji na ushirikiano katika kutekeleza masuala ya maendeleo ya vijana katika ngazi ya Kitaifa na Kimataifa.

Muswada huu umegawanyika katika sehemu kuu sita ambazo Kamati imezifanyia kazi na kutoa mapendekezo ya kuziboresha na hatimaye kuwa na sheria itakayokuwa na manufaa kwa vijana na nchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kwanza. Sehemu hii inaelezea jina la Muswada, Tafsiri, Madhumuni ya Sheria ya Baraza la Vijana Tanzania na tarehe ya kuanza kutumika ambapo Kamati inaona kuwa jina la Muswada libaki kama lilivyo kwa kuwa sheria hii itatumika Tanzania Bara pekee.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Pili. Sehemu hii ina vifungu kuanzia cha 4 - 15 na inaelezea masuala ya kuanzishwa, mamlaka na kazi za Baraza. Baada ya kupitia sehemu hii kwa makini, Kamati inashauri kufanya marekebisho yafuatayo ili kuleta ufanisi katika utekelezaji wa sheria hii.

(i) Kifungu cha 4(3) kisomeke, "Uanachama utakuwa wa wazi na wa hiari kwa kijana yeyote mwenye umri wa kuanzia miaka 15 - 35." Hii itakwenda sambamba pia na tafsiri ya kijana kama inavyosomeka kwenye sheria hii.

(ii) Kifungu cha 4(4) imeeleza kuwa Baraza halitakuwa la kisiasa, Kamati inashauri liongezwe neno "halitakuwa na itikadi za kisiasa na za kidini."

(iii) Kifungu cha 5(1) kisomeke, "Mwenyekiti atachaguliwa na Mkutano Mkuu wa Baraza."

(iv) Kifungu cha 6(1)(g) kiongezwe na kusomeka, "kuhamasisha, kukuza na kuendeleza utamaduni wa Mtanzania."

(v) Kifungu cha 8 kinahusu vyombo vya Baraza la Vijana ambapo Kamati inapendekeza kisomeke, "Baraza la Vijana la Taifa, Baraza la Vijana la Mkoa, Baraza la Vijana la Wilaya na Sekretarieti."

Mheshimiwa Spika, aidha, Kifungu cha 9 kiwe kifungu cha 10 na kifungu cha 9 kiongezwe maelezo ya Baraza la Vijana la Taifa. Pia kwa kila kifungu kinachozungumzia Baraza la Vijana la Wilaya na Mkoa kiongezwe kifungu chenye maelezo kuhusu Baraza la Vijana ngazi ya Taifa.

Sehemu ya Tatu. Sehemu hii ya Muswada ina jumla ya vifungu kumi kuanzia kifungu cha 16 - 25 na inazungumzia mikutano ya Baraza. Katika kifungu cha 18(1) kinaelezea Mkutano Mkuu wa Vijana wa Wilaya maneno; "zilizosajiliwa ndani ya Wilaya husika" yaondolewe kwa sababu yanaonesha ubaguzi wa vijana ambao hawatakuwa wamejiunga katika taasisi au asasi ya vijana na hivyo kutokuwa na uwakilishi wa vijana ndani ya eneo husika. Uangaliwe utaratibu bora zaidi wa kuwashirikisha vijana.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nne. Sehemu hii inazungumzia uanzishwaji na kazi za Bodi ya Baraza ambapo kuna vifungu vya 19 - 21. Kwa maelezo ya Muswada huu, kazi za Bodi zitakuwa ni kulishauri Baraza katika utekelezaji wa mamlaka na kazi zake kama zilivyoorodheshwa katika Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tano. Sehemu hii ya Muswada ina vifungu kuanzia 22 - 24 ambavyo vinaelezea vyanzo vya mapato ya Baraza ambapo mapato yatatokana na fedha au mali zitakazoingia kwenye Baraza kutoka kwa wahisani mbalimbali wakati wa utekelezaji wa kazi zake chini ya Sheria hii. Kamati inaona kuwa vifungu hivi vimejitosheleza kwa maelezo na vitaleta ufanisi katika kusimamia masuala ya fedha katika Baraza.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Sita. Sehemu hii ya Muswada ni masharti ya jumla yanayohusu kanuni ambapo Waziri mwenye dhamana ya vijana amepewa mamlaka ya kutengeneza Kanuni ili kuainisha uundwaji wa Kamati za Baraza, majukumu ya mamlaka ya Serikali za Mitaa, utaratibu wa uchaguzi na uteuzi pamoja na masuala mengine yanayoweza kuainishwa katika sheria hii. Aidha, kuna majedwali matano yanayoainisha masuala mbalimbali katika kufanikisha utendaji wa Baraza la Vijana la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Jedwali la Kwanza la Muswada linazungumzia ujira wa Wajumbe ambapo Kamati inashauri katika kifungu cha kwanza cha Jedwali kisomeke; "Wajumbe wa Baraza watalipwa posho na matumizi mengine kama yatakavyopendekezwa na Bodi na kuidhinishwa na Waziri mwenye dhamana husika na siyo kupendekezwa na Waziri".

Mheshimiwa Spika, aidha, maneno ya pembeni ya kifungu cha 1 katika Jedwali la Kwanza la Muswada yasomeke, "posho ya Wajumbe wa Baraza" badala ya "Ajira ya Wajumbe wa Baraza" kwa sababu Kamati inaamini hii siyo ajira.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa ujumla. Baada ya Kamati yangu kusoma na kupitia Muswada huu, inapenda kutoa maoni na ushauri wa jumla kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kamati imegundua kwamba ni taasisi na asasi zilizosajiliwa tu ndiyo wenye fursa ya kuwa wanachama katika Baraza la Vijana na hivyo kuyanyima fursa makundi mengine ambayo hayajasajiliwa. Kamati inashauri sehemu hii kufanyiwa maboresho na hivyo kuruhusu hata makundi mengine yenye nia njema yanayotambuliwa yaweze kushirikishwa kikamilifu kwenye Baraza hili.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika utengenezaji wa Kanuni izingatiwe kuwa upatikanaji wa Wajumbe wa Baraza katika ngazi ya Wilaya na Mkoa uanzie katika ngazi ya Kata na siyo ngazi ya Wilaya kama ilivyopendekezwa katika Muswada kwa kuwa kwa kuanzia Wilayani haitatoa fursa pana kwa vijana wa vijijini kushiriki kikamilifu katika Mabaraza hayo.

Mheshimiwa Spika, Kamati imegundua kwamba kuna tofauti ndogo ndogo kati ya Muswada wa Sheria ya Baraza la Vijana la Tanzania kwa lugha ya Kiingereza na Kiswahili na kifungu cha 18(2) kimenukuliwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kwamba Wajumbe wa Baraza watateuliwa kwa nyakati tofauti ili muda wao wa kumaliza kipindi chao uwe tofauti. Ni wazo jema lakini Kamati inashauri kwamba kwa kuwa muda wa uwepo wa Baraza upo kisheria na kupangiwa muda wa ukomo, ni vema Wajumbe wote wakachaguliwa kwa wakati mmoja na kama ipo haja ya kuteuliwa mara nyingine sheria inatoa fursa ya kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Serikali kuweka wazi na kuainisha namna ya uteuzi wa Wajumbe wa Kamati wa Baraza la Vijana kwani katika Jedwali la Pili, kifungu cha 4 haijaelezwa kinagaubaga hao Wajumbe watateuliwa na nani.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua kuwa vijana ndiyo uti wa mgongo wa Taifa letu, Kamati inashauri kwamba ni vema majukumu ya Baraza la Vijana yakapanuliwa wigo wake ili Baraza hilo liweze kutetea haki za makundi mengine na siyo vijana pekee.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kwamba ni vema Waziri mwenye dhamana ya vijana akaondolewa katika baadhi ya maeneo hasa mamlaka ya uteuzi wa viongozi wa Baraza la Vijana kwa ngazi zote ili viongozi hao wachaguliwe na vijana wenyewe na Waziri kuridhia na kuidhinisha na siyo yeye kufanya uteuzi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Waziri apewe muda kwa ajili ya kutangaza katika Gazeti la Serikali au Muswada huu uweke tarehe ya kuanza Baraza hili mara baada ya sheria hii kupitishwa na kusainiwa na Mheshimiwa Rais tofauti na inavyosomeka katika kifungu cha 1 cha Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kwamba kazi za vijana ziongezwe ikiwemo kujiwezesha kiuchumi katika shughuli mbalimbali za maendeleo pamoja na kujadili changamoto zinazowakabili vijana na kutafuta ufumbuzi. Aidha, Baraza la Vijana la Mkoa, Wilaya liwe na Wajumbe wasiozidi hamsini badala ya thelathini kama ambavyo imependekezwa katika kifungu cha 9(2) ili kupanua wigo wa ushirikishwaji wa vijana na narudia hii siyo ajira.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Vijana Taifa lipendekeze majina matano ya Wajumbe wa Bodi watakaothibitishwa na Waziri na siyo Waziri kuteua Wajumbe hao.

Mheshimiwa Spika, Jedwali la Kwanza, kifungu cha 1 linazungumzia malipo ya Wajumbe wa Baraza ambapo inaelezwa kuwa malipo yao yataidhinishwa na Waziri. Ni maoni ya Kamati kuwa malipo hayo yapendekezwe na Bodi ya Baraza na kuthibitishwa na Waziri.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Mjumbe atakayeacha kazi au ujumbe atoe taarifa ya kuacha kazi kwa Bodi ya Ushauri na siyo kwa Waziri kama ilivyo katika kifungu cha 3(1)(a) cha Jedwali la Kwanza na Bodi ndiyo itakayotoa taarifa kwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, mwisho, Kamati inaamini kuwa Muswada huu umebeba maoni mengi ya wadau. Kamati inaamini kuwa imepata muda mwingi wa kupata maoni ya wadau na bila shaka itakapokuwa sheria kamili, itaweza kukidhi matakwa na matarajio kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, naomba kukushukuru wewe, namshukuru Mheshimiwa Naibu Spika,

namshukuru Mtoa Hoja, Mheshimiwa Dkt. Fenella Mukangara, Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo; Naibu Waziri, Mheshimiwa Alhaj Juma Selemani Nkamia na wataalam wakiongozwa na Katibu Mkuu, Ndugu Sihaba Nkinga kwa ushirikiano walioipatia Kamati yangu.

Mheshimiwa Spika, pia nawashukuru wadau wote waliofika mbele ya Kamati na kuweza kutoa maoni yao kwa uhuru kabisa kwa njia za kidemokrasia na ninaamini katika *good governance*.

Namshukuru pia Mheshimiwa John Mnyika, kwa mchango mkubwa katika mchakato wa kuhakikisha kwamba Muswada huu unaboreshwa.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, naomba niwashukuru Wajumbe wa Kamati yangu ambao wameorodheshwa kwenye kitabu ambacho mmekabidhiwa.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Katibu wa Bunge na mwisho kabisa naunga mkono Muswada huu na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Sasa nimuite Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada huu, Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, nataka urudi. *(Kicheko)*

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, lakini kabla sijaendelea kwa utangulizi, naomba nisisitize kwamba ripoti au taarifa iliyosomwa na Kamati, hatukufanikiwa sisi sote kama Kamati kuifunga kwa maana ya kwamba baada ya kuandikwa hatukupata nafasi ya kuijadili. Ni kweli tulipiga kura; tisa za CCM na nne za UKAWA lakini maridhiano *always* huwa hayapigiwi kura. Kama tungepata nafasi ya kujadili wakati wa kufunga basi kama ambavyo yalichukuliwa maoni kutoka *Clouds FM* kama alivyosema Mwenyekiti ambayo hayakuwepo *before* na ambayo ni *pro*-CCM siyo kosa *pro*-CCM lakini tungetumia fursa hii kutumia maoni kutoka kipindi cha Pambanua cha *Channel Ten* ambayo ni *neutral*. Kwa hiyo, tungechukua ya *pro*-CCM na ya *neutral* na kuyaweka katika repoti hii, ahsante sana.

**SPIKA:** *I hope* tunatunga sheria ya nchi na siyo ya chama chochote.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Lakini vyombo vya habari viko hivyo na siyo dhambi.

**SPIKA:** Sisi sasa tutunge sheria.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Haya ahsante. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nisome maoni ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani Bungeni kwa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo.

Mheshimiwa Spika, maoni ya jumla. Napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mungu kwa kunipa nafasi nyingine mimi Joseph Mbilinyi, Mbunge wa Mbeya Mjini katika kupigania haki na maslahi ya Watanzania hasa vijana kwa kuwasilisha maoni ya Muswada wa Baraza la Vijana wa mwaka 2015 kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 86(6), Toleo la mwaka 2013.

Aidha, shukrani za kipekee kwa Kiongozi wa Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Freeman Mbowe na Wenyeviti wenza wa UKAWA, Mheshimiwa Profesa Ibrahim Lipumba, Mheshimiwa James Mbatia na Mheshimiwa Dkt. Emmanuel Makaidi kwa kuendelea kuimarisha ushirikiano wetu na *Aluta Continua. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru wananchi wangu kwa kuendelea kuamsha chachu ya mabadiliko kwa kufanya vyema kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Kwa dhati kabisa, napenda kuishukuru familia yangu, marafiki na jamaa zangu kwa kunipa ushirikiano kila napotekeleza majukumu ya ukombozi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Mwalimu Nyerere wakati anahutubia Mkutano Mkuu wa Vijana wa Dunia uliofanyika Dar es Salaam mwaka 1961 aliwahi kusema kuwa:-

*"...kuna watu walio na mawazo ya Kiviktoria, ambao wamepitwa na teknolojia na wana mawazo potofu yasiyo ya utu. Watu hawa wameshindwa kwenda na wakati na wanaendelea kurudia kauli mbiu zao wakidhani ni za kisasa wakati zimeshapitwa na wakati. Watu hawa wanaongelea kuhusu 'amani' huku wakidhuru, wanaongelea kuhusu 'umoja' huku wakiwagawa watu.*" Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, haya ndiyo mawazo na fikra za viongozi na Serikali inayotuongoza sasa ambayo imeendelea kubadilisha kauli mbiu kila mwaka wa kampeni. Serikali hii ambayo Rais wake anajinasibu kuchoka kuwatumikia wananchi, kama mkirejea kauli yake aliyotoa kule nchini China, imeendelea kutugawa Watanzania kwa walio nacho na wasio nacho.

Aidha, Serikali hii imeendelea kuwagawa vijana wa Kitanzania kwa kuwajengea matabaka katika upatikanaji wa elimu ambapo mfumo wa elimu

uliopo umewafanya vijana wa Kitanzania kukosa fursa za kujiendeleza na kuwa watumwa.

Mheshimiwa Spika, takwimu za Serikali za mwaka 2010 *(Tanzania Demographic and Health Survey)* imebainisha kuwa asilimia 28 ya vijana wasichana na asilimia 37 ya vijana wa kiume wenye umri kati ya 15 na 24 ndiyo pekee walipata elimu ya sekondari. Huu ni moja kati ya mfano wa namna ambavyo Serikali haipo makini na masuala ya vijana ikiwemo elimu.

Aidha, changamoto za vijana wa Kitanzania katika kupata mikopo ya elimu ya juu nchini zimeendelea kukua siku hadi siku huku tukishuhudia migomo katika taasisi za elimu ya juu nchini zinazosababisha baadhi yao kufukuzwa vyuo ama kusimamishwa masomo.

Mheshimiwa Spika, leo tukiwa katika harakati za ukombozi, vijana wamekosa mwelekeo kwa kuwa Serikali na viongozi ambao wanaweka mikakati mibovu, sera na sheria mbovu ambazo hazitekelezeki na hazilengi katika kuwakwamua kiuchumi. Haya yote yamesababisha ongezeko kubwa la ukosefu wa ajira, waathirika wa madawa za kulevya, vijana wanaofanya biashara za kuuza miili, vibaka, *panya road*, wauaji, vita baina ya wafanyabiashara ndogo ndogo na mgambo na hata kusababisha baadhi yao kujiua kutokana na ugumu wa maisha.

Aidha, ni Serikali hii ndiyo iliyowataka vijana kujiunga kwa wingi na Kambi za Jeshi na ingewapatia ajira, lakini ikawaacha vijana hao wakiwa hawana mwelekeo mpaka kufikia hatua ya kuandamana.

Mheshimiwa Spika, haya yote hayawezi kutatuliwa kwa kulihadaa kundi kubwa la vijana ambao ndiyo asilimia kubwa ya wapiga kura kila inapofika wakati wa uchaguzi. Makadirio ya wapiga kura mwaka 2015 kwa mujibu wa Taarifa za Ofisi ya Taifa ya Takwimu watakuwa milioni 24, ukizingatia kuwa vijana nchini chini ya umri wa miaka 24 ni asilimia 60, wakati vijana kati ya umri wa miaka 15 na 35 ni karibuni asilimia 31 ya watu wote nchini. Kwa takwimu hizi, bila shaka, wapiga kura wa mwaka huu wengi wao ni vijana.

Mheshimiwa Spika, katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005 na 2010, Serikali ya CCM kwa kugundua kuwa kundi kubwa la wapiga kura ni wazee, iliwahadaa kwa kuwadanganya kuwa wanawaandalia pensheni ya wazee lakini Uchaguzi Mkuu ulipoisha na mara kwa mara Serikali kwa kupitia Waziri Mkuu imekiri kuwa jambo hilo haliwezekani. Kwa kifupi, Serikali ya CCM imetumia mtindo huo wa kutoa matumaini hewa na *fake* kwa kuleta Muswada wa Baraza la Vijana la Tanzania wa mwaka 2015 kwa dharura kwa kuwa wamegundua kuwa kwenye zoezi la uandikishaji kura linaloendelea Njombe

asilimia kubwa ya waliojiandikisha ni vijana na Serikali hii imesoma alama za nyakati kupitia sensa kuwa vijana ni wengi hivyo Muswada huu unaletwa kwa makusudi ili kuwahadaa vijana wa Kitanzania kuelekea uchaguzi mkuu wa 2015.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni baada ya kufanya uchambuzi wa kina wa Muswada huu, tumegundua kuwa umelenga kuunda Shirika la Umma badala ya kuunda chombo huru cha kuwaunganisha vijana nchi nzima bila ubaguzi wa kiitikadi, rangi, kabila na tamaduni zao.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umempa Waziri na Rais madaraka ya uteuzi wa viongozi na bodi ya usimamizi wa Baraza hili. Huu ndiyo mtindo unatoumika katika uteuzi wa Wakurungenzi Wakuu na Wenyeviti wa baadhi ya mashirika ya umma. Vijana wa Tanzania hawataki kuwa na shirika la umma wanataka kuwa na Baraza huru litakalojiendesha kwa mujibu wa sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuelezea masikitiko yangu kwa Bunge lako kuwa Muswada huu wa Serikali umeletwa haraka haraka Bungeni bila kufanyiwa kazi na utafiti na Serikali. Hii inaonesha ni jinsi gani Serikali ya CCM imepatwa na *pressure* kuelekea Uchaguzi Mkuu kwa kushindwa kutatua kero na matatizo ya vijana, ambao kwa muda mrefu wamekuwa wakihadaiwa na kutumiwa kama chambo na CCM ili kupata kura za vijana.

Mheshimiwa Spika, mwaka huu vijana wa Kitanzania wameshtuka, wameelewa, hawadanganyiki, hawanunuliki na wala hawahadaiki tena. UKAWA kupitia Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaendelea kuwa mtetezi nambari moja wa maslahi ya vijana wote Tanzania bila kujali tofauti za kiitikadi ili kukuza ustawi nchini.

Mheshimiwa Spika, ukisoma Muswada huu wa Serikali ulioletwa Bungeni kuanzia ukurasa wa kwanza mpaka wa mwisho, Serikali kupitia Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo bila aibu wala soni, wamedurufu Sheria ya Baraza la Vijana ya Kenya ya mwaka 2009.

Mheshimiwa Spika, kwa lugha nyepesi, Wizara ime-*copy* na ku-*paste* Muswada wa Baraza la Vijana la Kenya na kubadilisha vitu vichache. Hii ni aibu kwa Serikali inayojinasibu kuwa makini na sikivu.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaposhindwa kusimamia vyema maslahi ya watu wa Taifa lake basi ujue kila jambo litafanywa kiujanjaujanja au kwa utapeli kwa nia ya kuwahadaa watu wake wenyewe ambao inawatumikia.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umekosa uhalali kwa vijana kwa kuwa umeandaliwa katika mazingira ya kupoka mamlaka ya vijana, kujisimamia, kujiendesha na kufanya shughuli zao za maendeleo kwa uhuru bila kuingiliwa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kifupi Serikali imefanya makosa mengi kwenye Muswada huu na Kambi ya Upinzani inaupinga kwa kuwa hauna maslahi kwa vijana nchini kubwa zaidi mchakato wa kuandaliwa kwa Muswada huu ulijaa usiri mkubwa na maoni ya wadau yalikusanywa kwa usiri mkubwa juzi tarehe 24 Machi, 2015 hapa Dodoma na Kamati husika ilipata taabu kuratibu uchambuzi wa wadau kwa kuwa wadau wengi hawakualikwa na wala kupata taarifa ya Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, Wabunge wengi wapo humu kwa kura za vijana na wengine wanawakilisha vijana na nitawashangaa Wabunge Vijana ambao wataunga mkono upitishwaji wa Muswada huu ambao ni wazi una upungufu wa kisheria na umeharakishwa kwani maoni ya wadau yamepatikana ndani ya siku tatu ambapo kuna idadi kubwa ya wawakilishi wa vijana toka vijijini ambao hawajapata nafasi ya kuleta maoni yao na leo tunataka kuwaamulia juu ya Baraza na muundo wake ambao haujazingatia mazingira ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, leo hii ukiangalia, kusoma na kuuchambua Muswada wa Vijana wa Zanzibar, una afadhali kuliko hata Muswada huu unaoletwa kwetu.

Mheshimiwa Spika, ajenda ya Baraza la Vijana haijaanza leo Tanzania. Vuguvugu la madai ya vijana kuwa na Baraza lao Kitaifa linatokana na mahitaji ya ushirikishwaji na ushiriki mpana na wenye maana wa vijana kama nguvu kazi ya Taifa katika kuimarisha uchumi wa nchi na kusimamia maslahi ya vikundi mbalimbali vya vijana kabla na baada ya uhuru wa Tanganyika.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kuwa *TANU Youth League* ilifanya harakati za ukombozi na kupelekea Uhuru kamili mwezi Disemba 1961. Muungano wa *TANU* na *ASP* mwaka 1977, ulipelekea kuibuliwa kwa Umoja wa Vijana CCM mara baada ya kuundwa kwa chama kimoja cha siasa CCM, umoja ambao ulipoteza dira na uhalali wa kuwaunganisha vijana wote nchini ikiwa ni pamoja na kuwatetea vijana wote bila kujali tofauti zao kiitikadi, kidini na kikabila wakati wa mfumo wa chama kimoja na hata baada ya Mfumo wa Vyama Vingi mwaka 1992.

Mheshimiwa Spika, historia ya harakati za madai ya vijana kuwa na Baraza Huru la Taifa la Vijana ni ndefu mno. Labda tu nikumbushe kwa ufupi kuwa tangu mwaka 1992, baada ya mageuzi ya mfumo wa vyama vingi hapa nchini, vuguvugu la madai ya Baraza hili yalianza kushika kasi na kupelekea

Serikali kuunda Sera ya Taifa ya Vijana ya mwaka 1996, ambayo pamoja na masuala mengine Serikali iliahidi kupitia Sera hiyo kuunda Baraza hilo, jambo ambalo halikuwahi kufanywa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, baada ya mapitio ya Sera ya Taifa ya Vijana ya mwaka 1996, mwaka 2007 Serikali iliunda Sera mpya ya Maendeleo ya Vijana ya Taifa *(National Youth Development Policy)* iliyozinduliwa mwaka 2008 ambayo pia ilitamka wazi kuwa Serikali itaunda Baraza la Taifa la Vijana. Kwa zaidi ya miaka 20, Serikali ilishindwa kutekeleza Sera zote mbili za Vijana ile ya mwaka 1996 na ile ya mwaka 2008 juu ya uundwaji wa Baraza la Vijana la Taifa. Ndani ya miaka miwili Serikali ilifanya hatua mbalimbali za kufanikisha uundwaji wa Baraza hili bila mafanikio na kuishia kuwahadaa vijana.

Mheshimiwa Spika, vijana wenyewe waliamua kusukuma ajenda ya Baraza la Vijana, mwezi Disemba mwaka 2013, wote ni mashahidi kwamba Bunge hili lilipokea Muswada Binafsi wa Mbunge John Mnyika wa Sheria ya Baraza la Vijana wa mwaka 2013, Muswada ambao ulipitia hatua zote za kupata maoni ya wadau, Muswada ambao Serikali imeamua kuteka wazo na kutupilia mbali maoni ya vijana na wadau wengine ambao walipewa fursa ya kuuchambua na kuwasilisha maoni yao mbele ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii. Maoni hayo yamewekwa kapuni na Serikali imeibuka na Muswada wenye upungufu mwingi mwezi Januari mwaka huu 2015.

Mheshimiwa Spika, nchi za Afrika Mashariki wakiwemo majirani zetu, tunawaiga Kenya zimeweza kuanzisha Mabaraza yake mapema, Uganda mwaka 1993, Kenya mwaka 2009 na Serikali ya Tanzania kwa sababu inazozijua yenyewe imeamua kuuleta Muswada huu mwaka 2015 (mwaka wa *pressure* za uchaguzi).

Mheshimiwa Spika, maoni yanayohusiana na Muswada wa Baraza la Vijana. Muswada huu wa Serikali una upungufu mwingi ambao unalenga kukwamisha juhudi za kuhakikisha kuwa vijana wanapata uhuru wa kuamua mambo yao. Yafuatayo ni marekebisho ya msingi ambayo yanahitaji kuzingatiwa:-

Kwanza, katika taarifa ya Muswada huu yaani '*Notice*'; neno '*objects*' liondolewe kwa kuwa linamaanisha 'vitu' na kuwekwa neno '*objectives*' likiwa na maana ya madhumuni. Aidha, neno hilo '*objects*' limetumika tena kwenye ukurasa wa mwisho unaoelezea madhumuni na sababu za Muswada mara baada ya majedwali ya Muswada.

Mheshimiwa Spika, Uanachama. Kifungu cha 4(3) kinaeleza kuwa uanachama wa Baraza utakuwa wazi na wa hiari kwa Asasi na Taasisi za Vijana zilizosajiliwa kwa mujibu wa sheria husika. Kambi ya Upinzani, inapinga kwa

nguvu zote kipengele hiki kwa kuwa si vijana wote nchini ambao wamejiunga na asasi au taasisi za vijana na hii inatokana na kuwa taasisi na asasi nyingi za vijana zinasajiliwa huku zikiwa na malengo tofauti na kusaidia na kuwafikia vijana wote.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inapendekeza kuwa, vijana wote wapate hiari ya kujiunga na Baraza kwa kupitia kadi za uanachama ambazo watazilipia ada za uanachama toka siku wanayoomba kuwa wanachama hadi pale wanapopoteza sifa ya unachama kutokana na kigezo cha umri.

Vilevile kuwepo wa mfumo wa wanachama wa Baraza kwa kila kijana Tanzania kutasaidia Baraza kuweza kukusanya mapato yake yenyewe na kusaidia katika miradi mbalimbali ya vijana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa kipengele hiki kimewekwa ili kuwadhibiti vijana watakaotaka kuomba mikopo, lakini bado kuna njia mbadala ya kuwapa hiyari vijana kujiunga na Baraza hili, lakini kuwawekea utaratibu wa kujiunga na mashina ya Baraza kwa ngazi za chini ikiwemo mitaa ili kuweza kudhibiti vijana wanaoshindwa kulipa mikopo ama kukimbia dhamana.

Mheshimiwa Spika, Mwenyekiti wa Baraza. Muswada huu unaweka pendekezo la kuwa na Baraza la Vijana ambalo litakuwa na Mwenyekiti, lakini Mwenyekiti huyu atateuliwa na Waziri husika. Mpaka hapa inaonesha nia ya wazi ya Serikali kuendelea kuwatumia vijana kama chambo bila kuzingatia maslahi yao.

Mheshimiwa Spika, mfano mfupi wa kumpa Waziri mamlaka ya kuteua Mwenyekiti wa Baraza la Vijana la Taifa, ni kufanya usanii na viini macho kama ambavyo ilitokea kwenye uteuzi wa Wajumbe wa Bunge Maalum la Katiba ambapo Wajumbe walioteuliwa na Rais kwa tiketi ya vijana walionesha moja kwa moja upendeleo wa Chama Tawala na ndiyo maana baadhi ya Wajumbe wa Bunge Maalum kama Paul Makonda wanajinasibu kuwa wawakilishi wa vijana nchini, leo wanaendelea kuwa Wakuu wa Ulinzi na Usalama kwa kuwa Wakuu wa Wilaya, nafasi ambayo moja kwa moja inahusiana na chama cha kisiasa.

Mheshimiwa Spika, pengine lawama za kupoka uhuru wa vijana na kumpa Waziri rungu la kuwachagulia vijana Mwenyekiti wao wenyewe badala ya vijana kumchagua kupitia Mkutano Mkuu wa Vijana unatokana na ukweli kuwa Serikali imenakili Muswada wa Kenya kila kitu, ambapo ukisoma Sheria hiyo ya mwaka 2009, kifungu cha 5(1) kinampa mamlaka Waziri ya kuteua Mwenyekiti. Hapa ndipo tunaposema kuwa Serikali hii ni dhaifu na ndiyo maana

hata Watendaji wake wanashindwa kuishauri mawazo mapya na yenye tija kwa kuwa kila kitu ni '*business as usual*'.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuweka kifungu cha 4(4) kinachozuia Baraza kujihusisha na masuala ya siasa ama kutumika kama jukwaa la kisiasa, lakini Waziri anayetokana na chama cha kisiasa anapewa mamlaka ya kuteua Mwenyekiti wa Baraza la Vijana kwa mujibu wa kifungu cha 5(1) cha Muswada huu. Kambi Rasmi ya Upinzani inapinga kwa nguvu zote mamlaka haya ya Waziri husika kuteua Mwenyekiti wa Baraza la Vijana ili kuepuka mashinikizo ya kisiasa ambayo yataingilia utendaji na ufanisi wa Baraza na masuala ya vijana wenyewe.

Mheshimiwa Spika, vilevile Muswada huu wa Baraza la Vijana una upungufu kwa kuwa umeshindwa kuweka vifungu vya kisheria vya nafasi ya Makamu Mwenyekiti kuwa sehemu rasmi ya Baraza kwenye kifungu hiki bali umeweka uwepo wa Makamu Mwenyekiti katika Jedwali la Kwanza Kifungu cha 4(3) kinacholiwezesha Baraza kuchagua Makamu Mwenyekiti wake pamoja na kifungu cha 4(6) cha jedwali kinachompa mamlaka Makamu Mwenyekiti wa Baraza kuongoza kikao ikiwa Mwenyekiti hayupo.

Hivyo kwa misingi hiyo Kambi ya Upinzani inapendekeza kuandikwa kwa kifungu kipya kwenye Kifungu cha (5), kitakachoelezea nafasi ya Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Baraza pamoja na sifa za kuteuliwa kwa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Baraza.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha (5) kinachoelezea muundo wa Baraza kifanyiwe mabadiliko kwa kukifuta kifungu cha 5(1) (a) na kukiandika upya kama ilivyo kwenye hotuba kwa kuokoa muda.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inapendekeza kuwepo kifungu kipya kitakachoelezea sifa za Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Vijana. Hii ni kuhakikisha kuwa mambo ya vijana yanasimamiwa na vijana wenye uelewa, weledi, sifa na ujuzi wa masuala yao bila kuathiri ustawi na utashi wao. Hivyo, Kifungu hiki kitasomeka kama ifuatavyo na tutarejea kwenye hotuba yangu kwenye kitabu.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inasisitiza kuwa Serikali haijafanya kazi yake ipasavyo na Bunge hili, iwapo litaruhusu Muswada huu upite ukiwa na upungufu mwingi, sisi Wabunge tutakuwa hatujawatendea haki vijana wa Kitanzania ambao wengi wameweka matumaini yao makubwa kwetu kama wakombozi na watetezi wao. Kwa kifupi, Muswada huu wa ku-*copy and paste* unaonesha udhaifu wa Serikali ya Awamu ya Nne.

Mheshimiwa Spika, uwazi wa Ofisi. Kwa mujibu wa Muswada huu umempa mamlaka Waziri kuwaondoa katika ofisi, Wajumbe wa Baraza la Vijana ambao wameorodheshwa chini ya Kifungu cha (5) isipokuwa Katibu Mtendaji wa Baraza ambaye ni *ex-officio* kupitia Kifungu cha 3(1)(b) cha Jedwali la Kwanza linalotengenezwa kwa mujibu wa Kifungu cha 4(5). Haiwezekani Waziri awavue Ujumbe ama kuwaondosha Wajumbe wakati Baraza ndilo lina mamlaka ya uendeshaji wa shughuli zake.

Mheshimiwa Spika, ikiwa Wajumbe wa Baraza la Vijana wanachaguliwa na vijana wenyewe basi mamlaka ya nidhamu na uwajibishaji iwe kwa vijana kupitia Mkutano Mkuu ili kuweza kufuata taratibu mbalimbali ikiwemo nafasi za kujitetea iwapo Mjumbe wa Baraza atashindwa kutimiza majukumu yake, amepatikana na hatia ama ameshindwa kufuata masharti ya Sheria.

Mheshimiwa Spika, kazi za Baraza. Ukiangalia vifungu vinavyoelezea kazi za Baraza vingi vimewekwa katika minajili ya kuhamasisha na kuipa umaarufu Sera ya Taifa ya Vijana. Kazi hizi zimelengwa kwa shughuli ambazo ni za kusaidia ajenda mbalimbali za vijana, lakini si katika kuwajengea vijana kujikwamua ama kukabiliana na changamoto mbalimbali ikiwemo ukosefu wa ajira, elimu duni, uhaba wa fursa za ujasiriamali na masoko, kukosekana kwa fursa za mikopo na mitaji na kukwama kwa kujitegemea miongoni mwao.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Muswada huu unaletwa si kwa nia njema na kwa kuwa ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali umekopa Kifungu chote cha (6) toka kwa Sheria ya Baraza la Taifa la Vijana ya Kenya, ni dhahiri kuwa Baraza hili litashindwa kufanya kazi Tanzania kwa kuwa kazi hizi za Baraza hazijabeba uhalisia wa kutatua changamoto za Vijana wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inapendekeza kifungu cha (6) cha Muswada huu chenye kuelezea kazi za Baraza *'functions of the Council'* kifutwe na kuandikwa upya ili kukidhi na kuzingatia mahitaji ya vijana wa Kitanzania na ikiwa itashindikana kufutwa kwa kifungu hiki basi Muswada huu uondolewe Bungeni na uletwe upya ukiwa umefanyiwa utafiti zaidi.

Mheshimiwa Spika, samahani! Mheshimiwa anayeongea na Waziri Mkuu pale kidogo sauti iko juu anani-*destruct.*

Mheshimiwa Spika, naendelea sasa na hotuba. Haya ni mapendekezo ya Kambi ya Upinzani Bungeni yanayofanya mabadiliko kwenye kifungu cha (6) cha Muswada wa Baraza la Vijana ambayo yamezingatia mazingira halisi, changamoto, kero na mazingira wezeshi yatakayosaidia kutetea maslahi ya vijana nchini.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo haya yamefanyiwa utafiti wa kina kwa kuhusisha makundi yote ya vijana nchini pamoja na maoni ya vijana yaliyopokelewa kwa njia za barua, ujumbe wa simu, simu, barua pepe na mitandao ya kijamii pamoja na mikutano ambayo Kambi ya Upinzani imefanya na wawakilishi wa vijana kwa nyakati mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, maoni haya ya kazi za Baraza yanahusisha kuwapa mamlaka Baraza ya kufanya kazi zote zinazohusiana na maslahi ya vijana na yenye manufaa kwa Taifa, kuhamasisha ari, uzalendo, uadilifu, umoja, mshikamano, uwajibikaji, heshima, kujitegemea katika masuala ya kilimo, ujasiriamali, shughuli mbalimbali za kiuchumi, kijamii, kitamaduni, kimataifa, kitaifa na pia mapendekezo haya yanalenga kulinda kundi muhimu la watu wenye ulemavu pamoja na kuzingatia usawa wa kijinsia katika ngazi mbalimbali za maamuzi.

Mheshimiwa Spika, aidha, mapendekezo haya mapya yanawapa vijana uwezo wa kuandaa, kupendekeza na kutekeleza programu mbalimbali pamoja na kuusanya fedha kwa ajili ya shughuli na miradi ya maendeleo itakayowanufaisha wao moja kwa moja pamoja na kulipa Baraza uwezo wa kushiriki katika uaandaji na utekelezaji wa Sera na Sheria zinazolenga ama kuhusisha masuala ya vijana moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, kifungu hiki sasa kiandikwe upya na kusomeka pamoja na marekebisho mengine kama ilivyoandikwa kwenye hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Baraza. Kambi ya Upinzani inapendekeza kifungu cha 7 cha Muswada kinachotoa Mamlaka kwa Baraza '*Powers of the Council*' kifutwe na kuandikwa upya kwa kuwa kilichofanyika hapa ni kuonesha kuwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ina umahiri wa kutumia maneno ya Kiingereza kwa mbwembwe ili hali uhitaji wa kisheria ni kuwa na vifungu vinavyoweza kutafsiriwa kwa ufanisi na urahisi na watumiaji ambao walengwa wake wakubwa ni vijana wakulima, wajasiriamali na wafanyabiashara wenye chachu ya kukuza uchumi .

Mheshimiwa Spika, Vyombo vya Baraza, kwa mujibu wa kifungu cha 8 cha Muswada huu, Baraza la Vijana litakuwa na vyombo vitatu ambavyo ni Baraza la Vijana la Mkoa, Baraza la Vijana la Wilaya na Sektretarieti. Hii ina maana kuwa shughuli za kiutawala za Baraza zitaishia katika ngazi ya Wilaya jambo ambalo Vijana wamepinga.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kuwa kila Halmashauri nchini ziliagizwa kutenga asilimia 10 ya mapato yake kwa ajili ya shughuli za Miradi ya Maendeleo ya Wanawake na Vijana, lakini ni Halmashauri ngapi na Wilaya ambazo zimefanikiwa kutenga fedha hizo? Ni vijana wangapi wamenufaika na

fedha hizo? Ni hatua gani kwa Halmashauri ambazo hazikutenga fedha hizo zimechukuliwa na je Halmashauri za Wilaya ziliweza kuwafikia kwa kiwango gani vijana katika ngazi za Kata, Tarafa na Mitaa?

Mheshimiwa Spika, kosa ambalo Bunge lako litafanya na litaingia katika dhambi kubwa vizazi hata vizazi, ni kuwaundia Vijana Baraza ambalo ngazi yake ya mwisho kwa mujibu wa Muswada huu ni Wilaya. Wote tunaelewa jiografia ya nchi yetu na jinsi ambavyo Kata nyingi zina Mitaa au Vitongoji ama Vijiji ambavyo vimeachana kwa umbali mkubwa; kwa misingi hiyo, kuweka uwakilishi wa vijana mpaka ngazi ya Wilaya ni kuwanyima haki vijana ambao wanatoka katika ngazi za Kata, Tarafa, Mitaa, Vitongoji na Vijiji.

Mheshimiwa Spika, pengine woga wa Serikali ni gharama za uendeshaji wa Baraza kuanzia ngazi ya Mkoa mpaka Mitaa, lakini ikiwa Baraza hili limepewa uwezo wa kutafuta, kukusanya ama kuomba misaada, michango na fedha kwa ajili ya uendeshaji, kiko wapi kigugumizi cha Serikali kuweka Baraza hili mpaka ngazi ya mitaa ili kuwawezesha kufanya maamuzi na kushiriki kwa ukamilifu kwa manufaa yao wenyewe?

Mheshimiwa Spika, kwa kauli moja, Kambi ya Upinzani inaliomba Bunge hili lisifanye makosa hayo na kuitaka Serikali iuondoe Muswada huu kwa manufaa ya vijana na maslahi ya Taifa zima, kuliko kuweka mfumo ambao utaminya na kupoka haki za vijana nchini, hasa wenye kutoka sehemu za vijijini. Ikiwa Serikali ambayo chama chake kina Umoja wa Vijana unaoanza kuanzia kwenye Matawi mpaka ngazi ya Taifa, basi hivyo hivyo isipate hofu kuliwezesha Baraza la Vijana kufika mpaka ngazi za Tawi.

Mheshimiwa Spika, tuwaondoe uoga CCM kuwa Baraza la Vijana limewekewa sharti la kutoshiriki katika shughuli za kisiasa ama kufanya maamuzi yanayohusiana na siasa, hivyo hofu yao kuwa Baraza ili likisambaa mpaka ngazi za chini hata matawi linaweza kuwa na nguvu na kufuta mianya ya UVCCM na chipukizi, basi watoe wasiwasi katika kuhakikisha Baraza hili linaanzia ngazi ya Mkoa mpaka Matawi.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Vijana la Mkoa: Kifungu cha (9) cha Muswada huu kinatoa tafsiri ya Baraza la Vijana la Mkoa, muundo wake na kazi zake. Aidha, kifungu hiki kinatoa mamlaka na uhuru kwa Baraza la Mkoa kuwachagua Vijana wawakilishi kuwa Wajumbe wa Mkoa katika Mkutano Mkuu na pia kuwachagua viongozi wake ambao ni Mwenyekiti na Katibu wa Baraza la Mkoa.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani haioni mantiki ya vijana hawa ambao wana uwezo na uhuru wa kuchagua Wenyeviti na Makatibu wa Mkoa

wapokonywe haki ya kumchagua Mwenyekiti wa Taifa wa Baraza. Hivyo mamlaka yanayotolewa na kifungu hiki katika kuchagua Mwenyekiti na Katibu wa Baraza la Mkoa hayana budi pia kufanywa hivyo katika ngazi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu masuala ya haki za vijana yamekuwa yakipigiwa kelele sambamba na utoaji wa fursa na nafasi za uwakilishi unaozingatia masuala ya kijinsia na watu wenye ulemavu. Hivyo Kambi ya Upinzani inapendekeza uwakilishi utakaotoa uwakilishi unaozingatia jinsia na watu wenye ulemavu katika Baraza. Hivyo kifungu cha 9(b) kifutwe na kuandikwa upya ili kuzingatia masuala ya jinsia na watu wenye ulemavu kwa kuwa Mkutano Mkuu wa Baraza la Vijana kwa mujibu wa Jedwali la Nne, Kifungu cha (4) utafanyika mara moja kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Vijana la Wilaya: Kwa mujibu wa Kifungu cha 10, kutaanzishwa Baraza la Vijana katika kila Wilaya. Pia idadi ya Wajumbe wa Baraza la Vijana katika Wilaya isiwe zaidi ya 30 katika Baraza. Aidha, utaratibu wa uendeshaji wa Baraza na upatikanaji wa Wajumbe wa Baraza la Vijana la Wilaya umewekwa katika jedwali la tatu la Muswada huu.

Vilevile muda wa Ujumbe wa Baraza umewekwa usizidi miaka mitatu na Mjumbe anaruhusiwa kuchaguliwa tena kwa kipindi kingine. Kambi ya Upinzani Bungeni, inaendelea kutoa maoni yake kuwa Ujumbe wa Baraza la Vijana usizidi miaka miwili kwa kila kipindi ili kutoa fursa kwa vijana kushiriki katika Baraza hili kwa kupeana nafasi kwa kipindi cha miaka miwili miwili na iwapo mjumbe atachaguliwa tena kwa mara ya pili iwe vipindi viwili vyenye jumla ya miaka minne.

Mheshimiwa Spika, Muundo wa Kamati ya Baraza la Vijana la Mkoa na Kamati ya Baraza la Vijana la Wilaya. Kambi ya Upinzani inapenda kutoa maoni kuwa Muundo wa Kamati ya Baraza la Vijana la Mkoa kama ulivyopendekezwa katika Jedwali la Pili la Muswada Kifungu cha Nne ubadilishwe.

Muundo unaopendekezwa na Kifungu cha 4(a) na (b) unataka Mwenyekiti wa Kamati ya Vijana ya Mkoa na Wajumbe sita watokane miongoni mwa taasisi za vijana zilizosajiliwa ndani ya Mkoa. Aidha, Kifungu cha 4(a) na (b) chini ya Jedwali la Tatu linalotengenezwa kwa mujibu wa Kifungu cha 10(5) cha Muswada, kinatoa elekezo kuwa Mwenyekiti na Wajumbe wa Wilaya watatokana na taasisi zilizopo ndani ya Wilaya na watapokezana, lakini taasisi nyingi hufa baada ya kuanzishwa na kusajiliwa ama kushindwa kufanya kazi zenye maslahi ya Vijana.

Mheshimiwa Spika, hivyo Kambi ya Upinzani inapendekeza kuwa Mwenyekiti na Wajumbe hao wapatikane ndani ya vijana wa Mkoa na Wilaya

ambao ni wanachama wa Baraza la Vijana kama ambavyo tulipendekeza awali kuwa Baraza liwe na Vijana wenye kujiunga kwa hiyari.

Mheshimiwa Spika, Baraza Kugatua Madaraka. Muswada huu umeweka kifungu cha 11 kwa ajili ya ugatuaji wa Madaraka wa Baraza kwa Katibu Mtendaji ama kwa Afisa wa Baraza. Hivyo basi, kifungu hiki kinawapa waliotajwa mamlaka ya kutekeleza kupitia maazimio kazi au majukumu ya Baraza chini ya Sheria hii bila kutoa mwongozo wa ni hatua gani zitachukuliwa iwapo walioidhinishwa kufanya majukumu au kazi maalum watafanya kinyume cha maazimio. Kifungu hiki kifutwe na kuandikwa upya ili kutoa mwongozo. Aidha, kifungu hiki kina upungufu kwa kuwa Wajumbe wa Baraza hawajajumuishwa kuwemo kati ya watu ambao wanaweza kupewa jukumu la kutekeleza maazio ya jumla au kazi maalum kwa niaba ya Baraza.

Mheshimiwa Spika, utangazaji wa maslahi. Pamoja na Muswada huu kuweka utaratibu wa kutangaza maslahi kwa Wajumbe wa Baraza la Vijana chini ya Kifungu cha 12, ni dhahiri kuwa utaratibu uliowekwa haupo wazi na ni dhahiri unaweza kutengeneza mazingira ya Wajumbe wa Baraza kufanya kazi wakiwa na maslahi kwenye mambo yanayohusiana na vijana. Hivyo, kifungu hiki kifutwe na kuandikwa upya kukiwa na mwongozo wa hatua ambazo mjumbe atachukuliwa iwapo atashindwa kutangaza maslahi katika jambo ambalo lipo mbele ya Baraza kuanzia kwenye mikataba, maamuzi au suala lolote linalohusiana na vijana.

Mheshimiwa Spika, Wajumbe wa Bodi. Katika mapendekezo yetu ya awali ya uwepo wa nafasi ya Makamu Mwenyekiti katika kifungu cha 5(1) ambaye pia ametamkwa katika Jedwali la Kwanza Kifungu cha 4(3) cha Muswada huu, bado ipo haja ya Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Vijana aliyechaguliwa na Mkutano Mkuu kuwa mjumbe wa Bodi. Hivyo, kifungu hiki kifanyiwe mabadiliko na kumwongeza Makamu Mwenyekiti kama mjumbe wa Bodi.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 19(2)(e) bado kinaendelea kumpa mamlaka Waziri kwa kuwachagulia Bodi ya Baraza, Wajumbe watano (5) watakaokua Wajumbe wa Bodi baada ya kupendekezwa na Mkutano Mkuu. Tunapendekeza kuwa Mkutano Mkuu wa Baraza la Vijana ufanye uteuzi wa Wajumbe wa Bodi kwa utaratibu utakaokuwa wazi na huru ili watu wenye sifa na wawakilishi watano vijana wapate fursa ya kuwepo katika Bodi hiyo na si kuingiliwa na Waziri.

Mheshimiwa Spika, Majukumu ya Bodi. Kifungu cha 20(1) kinaeleza kuwa kazi ya Bodi itakuwa ni ushauri tu. Vile vile, Kifungu cha 21(2) kinaeleza kuwa Bodi itakuwa na kazi nyingine kama ambavyo itaelezwa na chini ya Muswada huu wa Sheria, lakini, jedwali la tano ambalo ndilo lenye taratibu za uendeshaji

wa masuala ya Bodi hii, haijaweka kazi ama jukumu lolote la Bodi. Hivyo, kwa kifupi Bodi hii inakuwa na kazi moja ya ushauri kwa Baraza, hivyo kuondoa uhalali wake wa kuweza kusimamia ama kufanya maamuzi ambayo yatatekelezwa na Baraza.

Mheshimiwa Spika, moja ya mambo ambayo yamekuwa yakileta ukakasi katika utekelezaji wa shughuli za miradi ya maendeleo ya vijana ni pamoja na kutopatikana ama kutotengwa kwa asilimia tano za fedha za vijana zinazotokana na mapato ya Halmashauri katika Wilaya mbalimbali nchini.

Hivyo, kuna umuhimu wa kuhakikisha Bodi inapewa jukumu la kufuatilia utekelezaji wa agizo hilo unafanyika katika Halmashauri zote nchini pamoja na kupendekeza hatua za kinidhamu dhidi ya Halmashauri ambazo hazitengi fedha hizo ama zinatenga fedha za vijana na kuzitumia kwa matumizi mengineyo. Kambi ya Upinzani inapendekeza Muswada huu uondolewe ili kuweza kupitia upya kazi za Bodi na kuipa majukumu mengine yatakayosimamia na kuwezesha ufanisi wa utendaji wa Baraza la Vijana.

Mheshimiwa Spika, Fedha za Baraza. Kifungu cha 22 (a) Kinasomeka kuwa *"The funds and assets of the Council shall comprise of-(a) such moneys "as may be" appropriated by Parliament for the purposes of the Council;*

Tafsiri ya lugha ya Kiingereza kwenye maneno *"as may be"* yanamaanisha kuwa Baraza linaweza kutengewa fedha na Bunge ama lisitengewe fedha na Bunge. Kama Waziri ndiye anawasilisha makisio ya bajeti ya Baraza la Vijana Bungeni kupitia bajeti ya Wizara ya Vijana, anaweza akaamua kutowasilisha makisio hayo na kuyaombea fedha kwa kigezo kuwa shughuli za Baraza sio kipaumbele cha Wizara kwa mwaka huo wa fedha huku Waziri akisukumwa kufanya hivyo kutokana na tafsiri hiyo ya maneno ya *"as may be"* kisheria. Jambo hili litaweza kulifanya Baraza liwe maskini kwa kushindwa kabisa kutengewa fedha za bajeti zitakazoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaliomba Bunge kufuta maneno *"as may be"* lifutwe na liandikwe neno *"shall"* ili kulazimisha Baraza lipate mgao wa bajeti ya Serikali ili kuwezesha uendeshaji wa shughuli zake.

Mheshimiwa Spika, upungufu ambao upo katika Muswada huu wa kisarufi na majedwali ya Muswada huu yatafanyiwia marekebisho kwa Muswada Rasmi, marekebisho kama yatakavyowasilishwa na Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. Yale ambayo sijayasoma kwenye *podium* yako naomba yaingie kwenye *Hansard* na Wajumbe watafuatilia kwenye hotuba yangu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante.

**MAONI YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI WA WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO MHESHIMIWA JOSEPH O. MBILINYI (MB) KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA BARAZA LA VIJANA TANZANIA YA MWAKA, 2015 *'TheYouth Council of Tanzania Act, 2015'* KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

**MAONI YA JUMLA**

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mungu kwa kunipa nafasi nyingine mimi Joseph Mbilinyi, mbunge wa Mbeya Mjini katika kupigania haki na maslahi ya watanzania hasa vijana kwa kuwasilisha maoni ya Muswada wa Baraza la Vijana wa mwaka 2015 kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 86 (6), Toleo la mwaka 2013. Aidha, shukrani za kipekee kwa Kiongozi wa Upinzani Bungeni Mhe. Freeman Mbowe na wenyeviti wenza wa UKAWA, Mhe. Prof. Ibrahim Lipumba, Mhe. James Mbatia na Mhe. Emmanuel Makaidi kwa kuendelea kuimarisha ushirikiano wetu 'Aluta Continua'. Nawashukuru wananchi wangu kwa kuendelea kuamsha chachu ya mabadiliko kwa kufanya vyema kwenye uchaguzi wa Serikali za mitaa. Na kwa dhati kabisa, napenda kuishukuru familia yangu , marafiki na jamaa zangu kwa kunipa ushirikiano kila ninapotekeleza majukumu ya ukombozi wa Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,** Mwalimu Nyerere wakati anahutubia mkutano mkuu wa vijana wa Dunia uliofanyika Dar Es Salaam mwaka 1961 aliwahi kusema kuwa;

> *'...kuna watu walio na mawazo ya Kiviktoria, ambao wamepitwa na teknolojia na wana mawazo potofu yasiyo ya utu. Watu hawa wameshindwa kwenda na wakati na wanaendelea kurudia kauli mbiu zao wakidhani ni za kisasa wakati zimeshapitwa na wakati. Watu hawa wanaongelea kuhusu 'amani' huku wakidhuru, wanaongelea kuhusu 'umoja' huku wakiwagawa'......*

.

**Mheshimiwa Spika,** haya ndiyo mawazo na fikra za viongozi na Serikali inayotuongoza sasa ambayo imeendelea kubadilisha kauli mbiu kila mwaka wa kampeni, Serikali hii ambayo Rais wake anajinasibu kuchoka kuwatumikia wananchi, kama mkirejea kauli yake aliyotoa kule nchini China, imeendelea kutugawa watanzania kwa walio nacho na wasio nacho. Aidha, Serikali hii imeendelea kuwagawa vijana wa Kitanzania kwa kuwajengea matabaka katika upatikanaji wa elimu ambapo mfumo wa elimu uliopo umewafanya vijana wa kitanzania kukosa fursa za kujiendeleza na kuwa watumwa. Takwimu za Serikali za mwaka 2010 (Tanzania Demographic and Health Survey) imebainisha kuwa asilimia 28 ya vijana wasichana na asilimia 37 ya vijana wa kiume wenye umri kati ya 15 na 24 ndio pekee walipata elimu ya sekondari, huu

ni moja kati ya mfano wa namna ambavyo Serikali haipo makini na masuala ya vijana ikiwemo elimu. Aidha, changamoto za vijana wa kitanzania katika kupata mikopo ya elimu ya juu nchini zimeendelea kukua siku hadi siku huku tukishuhudia migomo katika taasisi za elimu ya juu nchini zinazosababisha baadhi kufukuzwa vyuo ama kusimamishwa masomo.

Leo tukiwa katika harakati za ukombozi, vijana wamekosa mwelekeo kwa kuwa Serikali na viongozi ambao wanaweka mikakati mibovu, sera na sheria mbovu ambazo hazitekelezeki na hazilengi katika kuwakwamua kiuchumi. Haya yote yamesababisha ongezeko kubwa la ukosefu wa ajira, waathirika wa madawa za kulevya, vijana wanaofanya biashara za kuuza miili, vibaka, panya road, wauaji, vita baina ya wafanyabiashara ndogondogo na mgambo na hata kusababisha baadhi yao kujiua kutokana na ugumu wa maisha. Aidha, ni Serikali hii iliyowataka vijana kujiunga kwa wingi na kambi za jeshi na ingewapatia ajira, lakini ikawaacha vijana hao wakiwa hawana mwelekeo mpaka kufikia hatua ya kuandamana.

**Mheshimiwa Spika,** haya yote hayawezi kutatuliwa kwa kulihadaa kundi kubwa la vijana ambao ndio asilimia kubwa ya wapiga kura kila inapofika wakati wa uchaguzi. Makadirio ya wapiga kura mwaka 2015 kwa mujibu wa Taarifa za Ofisi ya Taifa ya Takwimu watakuwa milioni 24, ukizingatia kuwa vijana nchini chini ya umri wa miaka 24 ni asilimia 60, wakati vijana kati ya umri wa miaka 15 na 35 ni karibuni asilimia 31 ya watu wote nchini. Kwa takwimu hizi bila shaka, wapiga kura wa mwaka huu wengi wao ni vijana.

Katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2005 na 2010 , Serikali ya CCM kwa kugundua kuwa kundi kubwa la wapiga kura ni wazee, iliwahadaa kwa kuwadanganya kuwa wanawaandalia pensheni ya wazee lakini uchaguzi mkuu ulipoisha na mara kwa mara Serikali kwa kupitia Waziri Mkuu imekiri kuwa jambo hilo haliwezekani. Kwa kifupi, Serikali ya CCM imetumia mtindo huo wa kutoa matumaini hewa na feki kwa kuleta muswada wa Baraza la vijana la Tanzania wa mwaka 2015 kwa dharura kwa kuwa wamegundua kuwa kwenye zoezi la uandikishaji kura linaloendelea Njombe asilimia kubwa ya waliojiandikisha ni vijana na Serikali hii imesoma alama za nyakati kupitia sensa kuwa vijana ni wengi hivyo Muswada huu unaletwa kwa makusudi ili kuwahadaa vijana wa kitanzania kuelekea uchaguzi Mkuu wa 2015.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani bungeni baada ya kufanya uchambuzi wa kina wa muswada huu tumegundua kuwa umelenga kuunda shirika la umma badala ya kuunda chombo huru cha kuwaunganisha vijana nchi nzima bila ubaguzi wa kiitikadi, rangi, kabila na tamaduni zao. Muswada huu umempa Waziri na Rais madaraka ya uteuzi wa viongozi na bodi ya usimamizi wa Baraza hili. Huu ndio mtindo unatoumika katika uteuzi wa

wakurungenzi wakuu na wenyeviti wa baadhi ya mashirika ya umma. Vijana wa Tanzania hawataki kuwa na shirika la umma wanataka kuwa na baraza huru litakalojiendesha kwa mujibu wa sheria.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuelezea masikitiko yangu kwa Bunge lako kuwa muswada huu wa Serikali umeletwa haraka haraka bungeni bila kufanyiwa kazi na utafiti na Serikali. Hii inaonesha ni jinsi gani Serikali ya CCM imepatwa na presha kuelekea uchaguzi mkuu kwa kushindwa kutatua kero na matatizo ya vijana, ambao kwa muda mrefu wamekuwa wakihadaiwa na kutumiwa kama chambo na CCM ili kupata kura za vijana. Mwaka huu vijana wa kitanzania wameshtuka, wameelewa, hawadanganyiki, hawanunuliki na wala hawahadaiki tena. UKAWA kupitia Kambi rasmi ya upinzani Bungeni inaendelea kuwa mtetezi nambari moja wa maslahi ya vijana wote Tanzania bila kujali tofauti za kitikadi ili kukuza ustawi nchini.

**Mheshimiwa Spika,** ukisoma muswada huu wa Serikali ulioletwa Bungeni kuanzia ukurasa wa kwanza mpaka wa mwisho, Serikali kupitia Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo bila aibu wala soni, wamedurufu Sheria ya Baraza la Vijana ya Kenya ya mwaka 2009 kwa lugha nyepesi , Wizara 'imekopi na kupesti' muswada wa Baraza la vijana la Kenya na kubadilisha vitu vichache. Hii ni aibu kwa Serikali inayojinasibu kuwa makini na sikivu.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali inaposhindwa kusimamia vyema maslahi ya watu wa taifa lake basi ujue kila jambo litafanywa kijanjajanja au kwa utapeli kwa nia ya kuwahadaa watu wake wenyewe ambao inawatumikia. Muswada huu umekosa uhalali kwa vijana kwa kuwa umeandaliwa katika mazingira ya kupoka mamlaka ya vijana, kujisimamia, kujiendesha na kufanya shughuli zao za maendeleo kwa uhuru bila kuingiliwa na Serikali. Kwa kifupi Serikali imefanya makosa mengi kwenye muswada huu na Kambi ya Upinzani inaupinga kwa kuwa hauna maslahi kwa vijana nchini. Kubwa zaidi mchakato wa kuandaliwa kwa muswada huu ulijaa usiri mkubwa, na maoni ya wadau yalikusanywa kwa usiri mkubwa juzi tarehe 24.03.2015 hapa Dodoma, na kamati husika ilipata taabu kuratibu uchambuzi wa wadau kwa kuwa wadau wengi hawakualikwa na wala kupata taarifa ya muswada huu.

**Mheshimiwa Spika,** wabunge wengi wapo humu kwa kura za vijana na wengine wanawakilisha vijana na nitawashangaa wabunge vijana ambao wataunga mkono upitishwaji wa muswada huu ambao ni wazi una mapungufu ya kisheria na umeharakishwa kwani maoni ya wadau yamepatikana ndani ya siku tatu ambapo kuna idadi kubwa ya wawakilishi wa vijana toka vijijini ambao hawajapata nafasi ya kuleta maoni yao na leo tunataka kuwaamulia juu ya Baraza na muundo wake ambao haujazingatia mazingira ya Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,** leo hii ukiangalia, kusoma na kuuchambua muswada wa Vijana wa Zanzibar, una afadhali kuliko hata muswada huu unaoletwa kwetu.

**Mheshimiwa Spika,** ajenda ya Baraza la vijana, haijaanza leo Tanzania. Vuguvugu la madai ya vijana kuwa na baraza lao kitaifa linatokana na mahitaji ya ushirikishwaji na ushiriki mpana na wenye maana wa vijana kama nguvu kazi ya taifa katika kuimarisha uchumi wa nchi na kusimamia maslahi ya vikundi mbalimbali vya vijana kabla na baada ya uhuru wa Tanganyika.

Ikumbukwe kuwa **TANU Youth League,** ilifanya harakati za ukombozi na kupelelekea Uhuru kamili mwezi Disemba 1961. Muungano wa TANU na ASP mwaka 1977, ulipelekea kuibuliwa kwa **Umoja wa Vijana CCM** mara baada ya kuundwa kwa chama kimoja cha siasa CCM, umoja ambao ulipoteza dira na uhalali wa kuwaunganisha vijana wote nchini ikiwa ni pamoja na kuwatetea vijana wote bila kujali tofauti zao kiitikadi, kidini na kikabila wakati wa mfumo wa chama kimoja na hata baada ya mfumo wa vyama vingi mwaka 1992.

Historia ya harakati za madai ya vijana kuwa na baraza huru la Taifa la Vijana ni ndefu mno. Labda tu nikumbushe kwa ufupi, kuwa tangu mwaka 1992, baada ya mageuzi ya mfumo wa vyama vingi hapa nchini, vuguvugu la madai ya Baraza hili yalianza kushika kasi na kupelekea Serikali kuunda sera ya Taifa ya Vijana ya mwaka 1996, ambayo pamoja na masuala mengine Serikali ili-ahidi kupitia sera hiyo kuunda Baraza hilo, jambo ambalo halikuwahi kufanywa na Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya mapitio ya sera ya Taifa ya Vijana ya mwaka 1996, mwaka 2007 Serikali iliunda sera mpya ya Maendeleo ya Vijana ya Taifa (National Youth Development Policy) iliyozinduliwa mwaka 2008 ambayo pia ilitamka wazi kuwa serikali itaunda baraza la Taifa la Vijana.

Kwa zaidi ya miaka 20, serikali ilishindwa kutekeleza sera zote mbili za vijana ile ya mwaka 1996 na ile ya mwaka 2008 juu ya uundwaji wa Baraza la Vijana la Taifa. Ndani ya miaka miwili serikali ilifanya hatua mbalimbali za kufanikisha uundwaji wa baraza hili bila mafanikio na kuishia kuwahadaa vijana.

**Mheshimiwa Spika,** Vijana wenyewe waliamua kusukuma ajenda ya baraza la vijana, mwezi Disemba mwaka 2013, wote ni Mashahidi kwamba Bunge hili lilipokea Muswada Binafsi wa Mbunge John Mnyika wa Sheria ya Baraza la Vijana wa mwaka 2013, muswada ambao ulipitia hatua zote za kupata maoni ya wadau, muswada ambao serikali imeamua kuteka wazo na kutupilia mbali maoni ya vijana na wadau wengine ambao walipewa fursa ya kuuchambua na kuwasilisha maoni yao mbele ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii, maoni hayo yamewekwa kapuni, na serikali imeibuka na muswada wenye mapungufu mengi mwezi Januari mwaka huu 2015.

Nchini za Afrika Mashariki wakiwemo majirani zetu tunawaiga 'Kenya' zimeweza kuanzisha mabaraza yake mapema, Uganda mwaka 1993, Kenya mwaka 2009 na Serikali ya Tanzania kwa sababu inazozijua yenyewe imeamua kuuleta muswada huu mwaka 2015 (mwaka wa presha za uchaguzi).

**MAONI YANAYOHUSIANA NA MUSWADA WA BARAZA LA VIJANA**

**Mheshimiwa Spika,** muswada huu wa serikali una mapungufu mengi ambayo yanalenga kukwamisha juhudi za kuhakikisha kuwa vijana wanapata uhuru wa kuamua mambo yao.

Yafuatayo ni marekebisho ya msingi ambayo yanahitaji kuzingatiwa;

Kwanza katika taarifa ya muswada huu yaani 'NOTICE'; neno 'objects' liondolewe kwa kuwa linamaanisha 'vitu' na kuwekwa neno 'objectives' likiwa na maana ya madhumuni. Aidha , neno hilo 'objects' limetumika tena kwenye ukurasa wa mwisho unaoelezea madhumuni na sababu za Muswada mara baada ya majedwali ya muswada.

**Uanachama**

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 4 (3) kinaeleza kuwa uanachama wa Baraza utakua wazi na wa hiari kwa asasi na taasisi za vijana zilizosajiliwa kwa mujibu wa sheria husika.

Kambi ya Upinzani, inapinga kwa nguvu zote kipengele hichi kwa kuwa si vijana wote nchini ambao wamejiunga na asasi au taasisi za vijana nah ii inatokana na kuwa taasisi na asasi nyingi za vijana zinasajiliwa huku zikiwa na malengo tofauti na kusaidia na kuwafikia vijana wote.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi ya Upinzani inapendekeza kuwa vijana wote wapate hiari ya kujiunga na Baraza kwa kupitia kadi za uanachama ambazo watazilipia ada za uanachama toka siku wanayoomba kuwa wanachama hadi pale wanapopoteza k sifa ya unachama kutokana na kigezo cha umri. Vilevile, kuwepo wa mfumo wa wanachama wa Baraza kwa kila kijana Tanzania kutasaidia Baraza kuweza kukusanya mapato yake yenyewe na kusaidia katika miradi mbalimbali ya vijana.

Pamoja na kuwa kipengele hiki kimewekwa ili kuwadhibiti vijana watakaotaka kuomba mikopo, lakini bado kuna njia mbadala ya kuwapa hiyari vijana kujiunga na Baraza lakini kuwawekea utaratibu wa kujiunga na mashina ya Baraza kwa ngazi za chini ikiwemo mitaa ili kuweza kudhibiti vijana wanaoshindwa kulipa mikopo ama kukimbia dhamana.

**Mwenyekiti wa Baraza**

**Mheshimiwa Spika,** muswada huu unaweka pendekezo la kuwa na baraza la vijana ambalo litakuwa na Mwenyekiti lakini mwenyekiti huyu atateuliwa na waziri husika. Mpaka hapa, inaonesha nia ya wazi ya Serikali kuendelea kuwatumia vijana kama chambo bila kuzingatia maslahi yao. Mfano mfupi wa kumpa waziri mamlaka ya kuteua Mwenyekiti wa Baraza la Vijana la taifa ni kufanya usanii na viini macho kama ambavyo ilitokea kwenye uteuzi wa wajumbe wa Bunge maalumu la katiba ambapo wajumbe walioteuliwa na raisi kwa tiketi ya vijana walionesha moja kwa moja upendeleo wa chama tawala na ndio maana baadhi ya wajumbe wa bunge maalumu kama Paul Makonda wanajinasibu kuwa wawakilishi wa vijana nchini, leo wanaendelea kuwa wakuu wa ulinzi na usalama wa wilaya (mkuu wa wilaya), nafasi ambayo moja kwa moja inahusiana na chama cha kisiasa.

**Mheshimiwa Spika,** pengine lawama za kupoka uhuru wa vijana na kumpa Waziri rungu la kuwachagulia vijana Mwenyekiti wao wenyewe badala ya vijana kumchagua kupitia mkutano mkuu wa vijana unatokana na ukweli kuwa Serikali imenakili muswada wa Kenya kila kitu ambapo ukisoma Sheria hiyo ya mwaa 2009 kifungu cha 5 (1) kinampa mamlaka waziri ya kuteua mwenyekiti. Na hapa ndipo tunaposema kuwa Serikali hii ni dhaifu na ndiyo maana hata watendaji wake wanashindwa kuishauri mawazo mapya na yenye tija kwa kuwa kila kitu ni 'business as usual'.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kuweka kifungu cha 4 (4) kinachozuia Baraza kujihusisha na masuala ya siasa ama kutumika kama jukwaa la kisiasa , lakini waziri anayetokana na chama cha kisiasa anapewa mamlaka ya kuteua mwenyekiti wa Baraza la vijana kwa mujibu wa kifungu cha 5 (1) cha Muswada huu; Kambi rasmi ya upinzani inapinga wa nguvu zote mamlaka haya ya waziri husika kuteua Mwenyekiti wa Baraza la Vijana ili kuepuka mashinikizo ya kisiasa ambayo yataingilia utendaji na ufanisi wa Baraza na masuala ya vijana wenyewe.

Vile vile, muswada huu wa Baraza la vijana una mapungufu kwa kuwa umeshindwa kuweka vifungu vya kisheria vya nafasi ya makamu mwenyekiti kuwa sehemu rasmi ya Baraza wenye kifungu hiki bali umeweka uwepo wa makamu mwenyekiti katika jedwali la kwanza Kifungu cha 4 (3) kinacholiwezesha Baraza kuchagua makamu mwenyekiti wake pamoja na kifungu cha 4 (6) cha jedwali kinachompa mamlaka makamu mwenyekiti wa Baraza kuongoza kikao ikiwa Mwenyekiti hayupo. Hivyo, kwa misingi hiyo Kambi ya Upinzani inapendekeza kuandikwa kwa kifungu kipya kwenye Kifungu cha 5, kitakachoelezea nafasi ya mwenyekiti na makamu mwenyekiti wa Baraza pamoja na sifa za kuteuliwa kwa mwenyekiti na makamu mwenyekiti wa Baraza.

Kifungu cha 5 kinachoelezea muundo wa Baraza kifanyiwe mabadiliko kwa kukifuta kifungu cha 5(1) (a) na kukiandika upya kama ifuatavyo;

*'5 (1) a chairman and vice chairman elected by the General Assembly;*

Aidha, Kifungu cha 5 (1) (b)) kinachotoa nafasi moja ya uwakilishi kwa kila mkoa, kiboreshwe kwa kuongeza nafasi tatu ambazo zitazingatia uwiano wa kijinsia , watu wenye ulemavu na lakini pia ikumbukwe kutokana na jiografia ya nchi yetu, baadhi ya mikoa ina idadi kubwa ya watu hasa vijana na hivyo kutoa nafasi moja ni kunyima fursa uwakilishi bora katika baraza. Kambi ya Upinzani inapendekeza maboresho yafuatayo;

*'5 (1)(b) three representatives, of which, one shall be a male and another female representative for gender representation purposes.'*

Aidha, Kifungu cha 5 (3) kinachoelezea sifa za Mwenyikiti wa Baraza kifutwe na kuandikwa upya chini ya kifungu kipya kinachopendekezwa kitakachosomeka kwa maneno ya pembeni kama *'Mwenyekiti na makamu mwenyekiti wa Baraza'* yaani *'Chairman and vice chairman of the Council'*.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi ya Upinzani inapendekeza kuwepo kifungu kipya kitakachoelezea sifa za Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Vijana. Hii ni kuhakikisha kuwa mambo ya vijana yanasimamiwa na vijana wenye uelewa, weledi, sifa na ujuzi wa masuala yao bila kuathiri ustawi na utashi wao.

Hivyo Kifungu hiki kitasomeka kama ifuatavyo;

*5 (3) a person shall not be elected a Chairman or vice chairman unless such person-*

*(a) is a Tanzanian;*
*(b) possesses at least undergraduate degree from a recognised higher learning institution;*
*(c) has demonstrated abilities to lead, mobilize and unite youth regardless of their social, political, racial, ethnical and religious preferences;*
*(d) possesses high integrity, ethical and moral values to the aspirations of youth for both national and international communities.*
*(e) not exceed 31 years at the time of election of a Chairmanor vice chairman of the Council;*
*(f) has resided in Tanzania for five years;*
*(g)is a youth as defined under this Act.*

**Mheshimiwa Spika,** Kambi ya Upinzani inasisitiza kuwa Serikali haijafanya kazi yake ipasavyo na bunge hili, iwapo litaruhusu muswada huu upite ukiwa na mapungufu mengi, sisi wabunge tutakua hatujawatendea haki vijana wa kitanzania ambao wengi wameweka matumaini yao makubwa kwetu kama wakombozi na watetezi wao. Kwa kifupi, muswada huu wa 'kopi and pesti' unaonesha udhaifu wa Serikali ya awamu ya nne.

**Uwazi wa Ofisi**

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa muswada huu, umempa mamlaka waziri kuwaondoa katika ofisi, wajumbe wa Baraza la vijana ambao wameorodheshwa chini ya Kifungu cha 5 isipokua Katibu Mtendaji wa Baraza ambaye ni *ex officio* kupitia Kifungu cha 3 (1) (b) cha Jedwali la wanza linalotengenezwa kwa mujibu wa Kifungu cha 4 (5). Haiwezekani waziri awavue ujumbe ama kuwaondosha wajumbe wakati Baraza ndilo lina mamlaka ya uendeshaji wa shughuli zake.

**Mheshimiwa Spika,** ikiwa wajumbe wa Baraza la Vijana wanachaguliwa na vijana wenyewe basi mamlaka ya nidhamu na uwajibishaji iwe kwa vijana kupitia Mkutano Mkuu ili kuweza kufuata taratibu mbalimbali ikiwemo nafasi za kujitetea iwapo mjumbe wa Baraza atashindwa kutimiza majukumu yake, amepatikana na hatia ama ameshindwa kufuata masharti ya Sheria.

**Kazi za Baraza**

**Mheshimiwa Spika,** ukiangalia vifungu vinavyoelezea kazi za baraza vingi vimewekwa katika minajili ya kuhamasisha na kuipa umaarufu Sera ya Taifa ya vijana. Na kazi hizi zimelengwa kwa shughuli ambazo ni za kusaidia ajenda mbalimbali za vijana lakini si katika kuwajengea vijana kujikwamua ama kukabiliana na changamoto mbalimbali ikiwemo ukosefu wa ajira, elimu duni, uhaba wa fursa za ujasiriamali na masoko, kukosekana kwa fursa za mikopo na mitaji na kukwama kwa kujitegemea miongoni mwao. Na kwa kuwa muswada huu unaletwa si kwa nia njema na kwa kuwa ofisi ya mwanasheria mkuu wa Serikali umekopa Kifungu chote cha 6 toka kwa Sheria ya Baraza la Taifa la vijana ya Kenya ni dhahiri kuwa, baraza hili litashindwa kufanya kazi Tanzania kwa kuwa kazi hizi za Baraza hazijabeba uhalisia wa kutatua changamoto za vijana Tanzania.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi ya Upinzani inapendekeza kifungu cha 6 cha muswada huu chenye kuelezea kazi za *baraza 'functions of the council'* kifutwe na kuandikwa upya ili kukidhi na kuzingatia mahitaji ya vijana wa kitanzania na ikiwa itashindikana kufutwa kwa kifungu hiki basi muswada huu uondolewe bungeni na uletwe upya ukiwa umefanyiwa utafiti zaidi.

**Mheshimiwa Spika,** haya ni mapendekezo ya Kambi ya upinzani bungeni yanayofanya mabadiliko kwenye kifungu cha 6 cha muswada wa Baraza la vijana ambayo yamezingatia mazingira halisi, changamoto, kero na mazingira wezeshi yatakayosaidia kutetea maslahi ya vijana nchini. Mapendekezo haya yamefanyiwa utafiti wa kina kwa kuhusisha makundi yote ya vijana nchini pamoja na maoni ya vijana yaliyopokelewa kwa njia za barua, ujumbe wa simu, simu, barua pepe na mitandao ya kijamii pamoja na mikutano ambayo Kambi ya Upinzani imefanya na wawakilishi wa vijana kwa nyakati mbalimbali.

Maoni haya ya kazi za baraza yanahusisha kuwapa mamlaka Baraza ya kufanya kazi zote zinazohusiana na maslahi ya vijana na yenye manufaa kwa taifa; kuhamasisha ari, uzalendo, uadilifu, umoja, mshikamano, uwajibikaji, heshima, kujitegemea katika masuala ya kilimo, ujasiriamali, shughuli mbalimbali za kiuchumi, kijamii, kitamaduni, kimataifa , kitaifa na pia mapendekezo haya yanalenga kulinda kundi muhimu la watu wenye ulemavu pamoja na kuzingatia usawa wa kijinsia katika ngazi mbalimbali za maamuzi.

Aidha, mapendekezo haya mapya yanawapa vijana uwezo wa kuandaa, kupendekeza na kutekeleza programu mbalimbali pamoja na kuusanya fedha kwa ajili ya shughuli na miradi ya maendeleo itakayowanufaisha wao moja kwa moja pamoja na kulipa Baraza uwezo wa kushiriki katika uaandaji na utekelezaji wa sera na Sheria zinazolenga ama kuhusisha masuala ya vijana moja kwa moja.

**Mheshimiwa Spika,** kifungu hiki sasa kiandikwe upya na kusomeka pamoja na marekebisho mengineyo kama ifuatavyo tofauti na yale yaliyomo kwenye Muswada huu yaliyokopwa na Serikali toka Sheria ya Baraza la Vijana la Kenya;

*The functions of the Council shall be to;*

*(a) to engage in all youth related matters that benefit both youth and the nation;*
*(b) sensitize self reliance, patriotism, national identity, accountability, participation, respect, integrity, corporation, responsibility and morale in matters impacting youth in social, economic, political and cultural perspectives;*
*(c) advocate on matters concerning youth with disabilities in both national and international levels;*
*(d) advocate on matters that promote gender mainstreaming and equality in policy formulation and implementation on both local and international levels;*
*(e) establish and develop national dialogues and forums that will promote youth engagement in development;*
*(f) promote the implementation of National Youth Policy*

*(g) establish, develop, maintain and strengthen relations between international youth councils and systems;*
*(h) To fundraise, in accordance of laws of the country for youth development programmes;*
*(i) initiate and launch youth related programs that promote agricultural, educational, financial, technological, social and cultural aspects;*
*(j) recognise and award potential players in advocacy for youth' agendas and issues;*
*(k) promote adaption of regional and international conventions in regards to youth matters;*
*(l) advocate on establishment and control of national youth bank;*
*(m) promote enactment and amendment of policies and laws impacting youth;*
*(n) participate and engage the government in youth related matters;*
*(o) engage in any activity that promotes and safeguards the welfare of youth in all levels;*
*(p) advocate the involvement of youth in all decision making processes at both local and international levels.*

***Mamlaka ya Baraza***

**Mheshimiwa Spika,** Kambi ya upinzani inapendekeza kifungu cha 7 cha muswada kinachotoa mamlaka kwa Baraza 'Powers of the Council' kifutwe na kuandikwa upya kwa kuwa kilichofanyika hapa ni kuonesha kuwa ofisi ya mwanasheria mkuu ina umahiri wa kutumia maneno ya kiingereza kwa mbwembwe ilhali uhitaji wa kisheria ni kuwa na vifungu vinavyoweza kutafsiriwa kwa ufanisi na urahisi na watumiaji ambao walengwa wake wakubwa ni vijana wakulima, wajasiriamali na wafanyabiashara wenye chachu ya kukuza uchumi .

**Mheshimiwa Spika,** kifungu hiki sasa kisomeke ifuatavyo;

7.(1) The Council shall, for effective discharge of its functions under this Act, have powers to;
(a) enter into contracts after the approval by General Assembly;
(b) administer, manage and control its assets in such manner and purposes for which the Council is established;
(c) receive and keep any grants, aids, donations and endowments made to the Council or any other monies in respect of the Council and make disbursements thereafter in accordance with the Provisions of this act and any other law;
(d) with the approval of General Assembly , enter into associations with such bodies and or organisations within and outside Tanzania as it may consider appropriate in furtherance of the purposes for which the Council is established.

(e) open and manage a banking account or accounts for which the funds and monies received by the Council shall be kept and out of which transactions for payments by the Council shall be made.
(g) form a committee or task group to assist the discharge of functions of the Council;

(2) where the Council or one of its members receives any gift , grants or donations, shall declare the same to the Minister and respective bodies or organs.

(3) The Council may, in writing, authorize a member or its staff to exercise on its behalf, any of its powers as it may specify, but the exercise of such powers shall, to the extent required by the Council, be reported within the specified time to a meeting of the Council.

**Vyombo vya baraza**

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa kifungu cha 8 cha muswada huu , Baraza la vijana litakua na vyombo vitatu ambavyo ni baraza la vijana la mkoa, baraza la vijana la wilaya na sektretariati. Hii ina maana kuwa , shughuli za kitawala za baraza zitaishia katika ngazi ya wilaya jambo ambalo vijana wamepinga. Ikumbukwe kuwa kila halmashauri nchini ziliagizwa kutenga asilimia 10 ya mapato yake kwa ajili ya shughuli za miradi ya maendeleo ya wanawake na vijana lakini ni halmashauri ngapi na wilaya ambazo zimefanikiwa kutenga fedha hizo? Ni vijana wangapi wamenufaika na fedha hizo? Ni hatua gani ambazo halmashauri ambazo hazikutenga fedha hizo zimechukuliwa? Na je halmashauri za wilaya ziliweza kuwafikia kwa kiwango gani vijana katika ngazi za kata, tarafa na mitaa?

**Mheshimiwa Spika,** kosa ambalo bunge lako litafanya na litaingia katika dhambi kubwa vizazi hata vizazi ni kuwaundia vijana baraza ambalo ngazi yake ya mwisho kwa mujibu wa muswada huu ni wilaya. Wote tunaelewa jiografia ya nchi yetu na jinsi ambavyo kata nyingi zina mitaa au vitongoji ama vijiji ambavyo vimeachana kwa umbali mkubwa; kwa misingi hiyo, kuweka uwakilishi wa vijana mpaka ngazi ya wilaya ni kuwanyima haki vijana ambao wanatoka katika ngazi za kata, tarafa, mitaa, vitongoji na vijiji.

**Mheshimiwa Spika,** pengine woga wa Serikali ni gharama za uendeshaji wa baraza kuanzia ngazi ya mkoa mpaka mitaa. Lakini ikiwa baraza hili limepewa uwezo wa kutafuta, kukusanya ama kuomba misaada, michango na fedha kwa ajili ya uendeshaji, kiko wapi kigugumizi cha Serikali kuweka baraza hili mpaka ngazi ya mitaa ili kuwawezesha kufanya maamuzi na kushiriki kwa ukamilifu kwa manufaa yao wenyewe?

**Mheshimiwa Spika,** kwa kauli moja, kambi ya upinzani inaliomba bunge hili lisifanye makosa hayo na kuitaka Serikali iuondoe muswada huu kwa manufaa ya vijana na maslahi ya taifa zima, kuliko kuweka mfumo ambao utaminya na kupoka haki za vijana nchini hasa wenye kutoka sehemu za vijijini. Ikiwa Serikali ambayo chama chake kina umoja wa vijana unaonza kuanzia kwenye matawi mpaka ngazi ya taifa, basi hivyo hivyo isipate hofu kuliwezesha baraza la vijana kufika mpaka ngazi za tawi.

Na tuwaondoe uoga CCM kuwa baraza la vijana limewekewa sharti la kutoshiriki katika shughuli za kisiasa ama kufanya maamuzi yanayohusiana na siasa, hivyo hofu yao kuwa baraza ili likisambaa mpaka ngazi za chini hata matawi linaweza kuwa na nguvu na kufuta mianya ya UVCCM na Chipukizi basi watoe wasiwasi katika kuhakikisha baraza hili linaanzia ngazi ya mkoa mpaka matawi.

**Baraza la Vijana la Mkoa**

**Mheshimiwa Spika,** kifungu cha 9 cha muswada huu kinatoa tafsiri ya baraza la vijana la mkoa, muundo wake na kazi zake. Aidha, kifungu hiki kinatoa mamlaka na uhuru kwa baraza la mkoa kuwachagua vijana wawakilishi kuwa wajumbe wa mkoa katika mkutano mkuu na pia kuwachagua viongozi wake ambao ni mwenyekiti na katibu wa Baraza la mkoa.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi ya upinzani haioni mantiki ya vijana hawa ambao wana uwezo na uhuru wa kuchagua wenyeviti na makatibu wa mkoa wapokonywe haki ya kumchagua mwenyekiti wa taifa wa Baraza. Hivyo, mamlaka yanayotolewa na kifungu hichi katika kuchagua mwenyekiti na katibu wa Baraza la mkoa hayana budi pia kufanywa hivyo katika ngazi ya taifa.

**Mheshimiwa Spika,** kwa muda mrefu masuala ya haki za vijana yamekua yakipigiwa kelele sambamba na utoaji wa fursa na nafasi za uwakilishi unaozingatia masuala ya kijinsia na watu wenye ulemavu. Hivyo Kambi ya Upinzani inapendekeza uwakilishi utakaotoa uwakilishi unaozingatia jinsia na watu wenye ulemavu katika Baraza.

Hivyo kifungu cha 9 (b) kifutwe na kuandikwa upya ili kuzingatia masuala ya jinsia na watu wenye ulemavu kwa kuwa Mkutano Mkuu wa Baraza la vijana kwa mujibu wa Jedwali la nne , Kifungu cha 4, utafanyika mara moja kwa mwaka.

Sasa kifungu cha 9 (b) kisomeke kama ifuatavyo;

*'9 (b) nominate and approve three youth representatives for the General Assembly , of which such persons shall consist of a male, female and from a disabled community for representation purposes respectively.'*

**Mheshimiwa Spika,** mapendekezo hayo mapya yana lengo la kuwapa vijana uwakilishi unaozingatia usawa wa kijinsia na makundi ya watu wenye ulemavu.

Vilevile, kifungu cha 9 (4) kifanyiwe marekebisho kwa kuondoa maneno ya 'of the Regional Youth Council' baada ya neno 'members' kwa kuwa neno hili limetumika mara mbili kwenye sentensi moja. Kuondoka kwa neno hilo hakutoathiri tafsiri ya sheria bali utaleta matumizi bora ya maneno na sarufi.

Kifungu hii sasa kisomeke kama ifuatavyo;

*'9 (4) Matters relating to mode of appointment of members, meetings, quorum and other procedural matters of the Regional Youth Council shall be as set out in the Second Schedule to this Act.'*

Aidha, kwa ufafanuzi bora wa kisheria ni vyema kwa neno 'katibu mtendaji' yaani 'Executive Secretary' kama linavyotumika katika kifungu cha 9 (5) , likapewa tafsiri ya kisheria kwenye kifungu cha pili cha muswada huu(tafsiri) ili kuondoa utata wa kisheria.

**Baraza la Vijana la Wilaya**

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kifungu cha 10 , kutaanzishwa baraza la vijana katika kila wilaya. Na pia idadi ya wajumbe wa baraza la vijana katika wilaya isiwe zaidi ya 30 katika baraza. Aidha, utaratibu wa uendeshaji wa baraza na upatikanaji wa wajumbe wa baraza la vijana la wilaya umewekwa katika jedwali la tatu la muswada huu.

Vilevile, muda wa ujumbe wa baraza umewekwa usizidi miaka mitatu na mjumbe anaruhusiwa kuchaguliwa tena kwa kipindi kingine.Kambi ya Upinzani Bungeni, inaendelea kutoa maoni yake kuwa ujumbe wa baraza la vijana usizidi miaka miwili kwa kila kipindi ili kutoa fursa kwa vijana kushiriki katika baraza hili kwa kupeana nafasi kwa kipindi cha miaka miwili miwili na iwapo mjumbe atachaguliwa tena kwa mara ya pili iwe vipindi viwili vyenye jumla ya miaka minne.

**Muundo wa Kamati ya Baraza la Vijana la Mkoa na Kamati ya Baraza la Vijana la Wilaya**

**Mheshimiwa Spika,** Kambi ya Upinzani inapenda kutoa maoni kuwa Muundo wa Kamati ya Baraza la vijana la mkoa kama ulivyopendekezwa katika Jedwali la Pili la Muswada Kifungu cha nne ubadilishwe. Muundo unaopendekezwa na Kifungu cha 4 (a) na (b) unataka Mwenyekiti wa Kamati ya Vijana ya Mkoa na wajumbe 6 watokane miongoni mwa taasisi za vijana zilizosajiliwa ndani ya mkoa.

Aidha, Kifungu cha 4 (a) na (b) chini ya Jedwali la Tatu linalotengenezwa kwa mujibu wa Kifungu cha 10 (5) cha Muswada, kinatoa elekezo kuwa Mwenyekiti na wajumbe wa wilaya watatokana na taasisi zilizopo ndani ya wilaya na watapokezana lakini taasisi nyingi hufa baada ya kuanzishwa na kusajiliwa ama kushindwa kufanya kazi zenye maslahi ya vijana. Hivyo, Kambi ya Upinzani inapendekeza kuwa Mwenyekiti na wajumbe hao wapatikane ndani ya vijana wa mkoa na wilaya ambao ni wanachama wa Baraza la Vijana kama ambavyo tulipendekeza awali kuwa Baraza liwe na vijana wenye kujiunga kwa hiyari.

**Baraza Kugatua Madaraka**

**Mheshimiwa Spika,** muswada huu umeweka kifungu cha 11 kwa ajili ya ugatuaji wa madaraka wa Baraza kwa Katibu mtendaji ama kwa afisa wa baraza. Hivyo basi, kifungu hiki kinawapa waliotajwa mamlaka ya kutekeleza kupitia maazimio kazi au majukumu ya baraza chini ya Sheria hii bila kutoa mwongozo wa ni hatua gani zitachukuliwa iwapo walioidhinishwa kufanya majukumu au kazi maalumu watafanya kinyume cha maazimio. Kifungu hiki kifutwe na kuandikwa upya ili kutoa mwongozo.

Aidha, kifungu hiki kina mapungufu kwa kuwa wajumbe wa baraza hawajajumuishwa kuwemo kati ya watu ambao wanaweza kupewa jukumu la kutekeleza maazio ya jumla au kazi maalum kwa niaba ya Baraza.

**Utangazaji wa maslahi**

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na muswada huu kuweka utaratibu wa kutangaza maslahi kwa wajumbe wa Baraza la Vijana chini ya Kifungu cha 12, ni dhahiri kuwa utaratibu uliowekwa haupo wazi na ni dhahiri unaweza kutengeneza mazingira ya wajumbe wa baraza kufanya kazi wakiwa na maslahi kwenye mambo yanayohusiana na vijana. Hivyo, kifungu hiki kifutwe na kuandikwa upya kukiwa na mwongozo wa hatua ambazo mjumbe atachukuliwa iwapo atashindwa kutangaza maslahi katika jambo ambalo lipo mbele ya baraza kuanzia kwenye mikataba, maamuzi au suala lolote linalohusiana na vijana.

**Uteuzi wa Katibu Mtendaji**

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kifungu cha 14 (1) kinampa mamlaka waziri ya kuchagua katibu mtendaji wa baraza la vijana kutoka majina matatu ambayo yamependekezwa na vijana. Ni dhahiri kuwa, mfumo mzima wa upatikanaji wa viongozi wa baraza umewekwa ili udhibitiwe na Serikali na hivyo kuweka mianya ya viongozi wa baraza kushinikizwa na Serikali katika kutekeleza majukumu yake na kusimamia masuala ya vijana.

**Mheshimiwa Spika,** ni katika mifumo ya nchi hii ambayo tunaona jinsi wateule mbalimbali wabavyokuwa watumwa wa watawala ama wale waliochagua na kwa mazingira hayo, haiwezekani na hatutokubali waziri apewe mamlaka ya kuchagua Katibu wa Baraza la vijana.
Katika uteuzi wa wajumbe wa bunge maalumu la katiba, asasi na makundi mbalimbali ya vijana yalipeleka majina ya watu wanaotaka wawawakilishe na mamlaka ya uteuzi ilikua ni kwa Raisi, lakini wote hapa ni mashahidi kuwa wawakilishi wa vijana wengi waliteuliwa na kuonyesha kuwa walikua ni wa chama tawala na misimamo yao katika kusimamia haki za vijana kwenye mchakato wa katiba ililalamikiwa na vijana wa kila kona za nchi hii.

Kambi ya upinzani, inaitaka Serikali ifute kipengele hichi na kulipa Baraza mamlaka ya kufanya uchaguzi wa katibu mtendaji kwa taratibu zao na akishapatikana, jina lake litapelekwa kwa waziri kwa ajili ya kuidhinishwa.

**Kamati za Baraza**

**Mheshimiwa Spika,** katika muswada huu kumewekwa vifungu ikiwemo kifungu cha 7(1) (f) na chini ya kifungu cha 15 (4) vinazungumzia kuhusu uwepo wa kamati ambazo zinaweza kuundwa na baraza, ingawa katika majedwali ya muswada huu kuna utaratibu na mwongozo wa kamati za mikoa na wilaya bado kuna uhitaji wa muswada hii kuhakikisha unaweka kamati za kudumu za Baraza ambazo zitakua na kanuni za kuziendesha na kupatikana kwa wajumbe wake na utaratatibu wa kuziendesha.

Kwa mapungufu haya na umuhimu wa muswada kuwa na vifungu vitakavyotoa mwongozo wa kisheria wa kamati zinazoweza kuundwa na baraza, Kambi ya upinzani inaitaka Serikali kwa mara nyingine kuondoa muswada huu na kufanya utafiti upya na sio ‘business as usual’

**Mkutano Mkuu**

**Mheshimiwa Spika,** sehemu ya tatu ya muswada ina vifungu mbalimbali vinavyoelezea kuhusu mikutano ya Baraza. Moja ya vifungu vyenye mapungufu ni kifungu cha 16 (2) (a) ambacho kinaelekeza mkutano mkuu kupendekeza mwenyekiti wa baraza. Kambi ya upinzani inaendelea kusisitiza

kuwa, mwenyekiti wa baraza la vijana atachaguliwa na vijana wenyewe kupitia mkutano mkuu na jina lake litaidhinishwa na waziri husika wa masuala ya vijana. Vilevile, kifungu hiki kinaweka mgogoro baina ya Baraza na waziri husika kwa kuwa Kifungu cha 16 (1) kinaeleza kuwa Mkutano Mkuu ndio chombo cha juu cha kutoa maamuzi hivyo endapo Waziri atateua Mwenyekiti wa Baraza basi Mutano Mkuu hauwezi kuwa chombo cha juu cha Maamuzi cha Baraza la Vijana.

Kifungu cha 16 (2) (a) sasa kitasomeka kama ifuatavyo;
'*16 (2) (a) elect the Chairman of the Council;*'

Aidha, Kifungu cha 16 (2) (b) kiandikwe upya na kusomea ifuatavyo;
*'16 (2) (b) elect the members of the Board'*... ili bodi hii ipewe mamlaka ya kufanya kazi si kama chombo cha ushauri bali Bodi kamili. Hivyo maneno 'Advisory Board' yani 'Bodi ya ushauri' yafutwe kila yalipoandikwa na kusomeka kama 'Bodi' na ifafanuliwe upya atika Kifungu cha 2 cha Tafsiri.

**Mheshimiwa Spika,** aidha Kambi ya upinzani inapendekeza vifungu vifuatavyo viongezwe ili kuwezesha mkutano mkuu kufanya kazi;

*16(1) (e) to improve and adopt operational guidelines of the Council;*
*(f) to consider and, if necessary, implement, proposals and or resolutions made by other governing structures in relation to urgent matters.*

**Uanzishwaji wa Bodi**

**Mheshimiwa Spika,** kifungu cha 19 kinatoa mwongozo wa kisheria wa uanzishwaji wa bodi ambayo itakua na Mwenyekiti ambaye atachaguliwa na Raisi chini ya Kifungu cha 19 (a). Kifungu hiki moja kwa moja kimeiga mfumo wa bodi za usimamizi wa mashirika ya umma hivyo kulifanya Baraza lionekane kuwa ni ama ni shirika la umma au ni shirika la kiserikali badala ya kuwa chombo huru cha vijana; na kifungu hiki kimempa Rais madaraka makuu ya uteuzi wa mwenyekiti wa bodi ya usimamizi wa shughuli za Baraza la Vijana.

Aidha, ikumbukwe kuwa Rais bado ana madaraka ya kufanya uteuzi wa wenyeviti wa bodi katika mashirika ya umma na hivyo kujihusisha na bodi ni kuongeza urasimu wa upatikanaji wa Mwenyekiti na pia kuna uwezekano wa kuwa na upendeleo katika uteuzi kwa kuwa Rais tayari anakuwa kiongozi wa chama fulani cha siasa. Baraza la vijana sio na halipaswi kuwa shirika la umma badala yake liwe ni chombo huru cha vijana.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi rasmi ya Upinzani inapendekeza kuwa kazi ya Uteuzi wa Mwenyekiti wa Bodi ya Baraza la Vijana usifanywe na Rais na badala yake ufanywe na Mkutano Mkuu wa Baraza la Vijana kwa nafasi hii kutangazwa na

apatikane mtu kufuatana na sifa na weledi ambaye ana ujuzi na uzoefu katika masuala ya usimamizi wa shughuli za bodi na masuala ya vijana.

**Wajumbe wa Bodi**

**Mheshimiwa Spika,** katika mapendekezo yetu ya awali ya uwepo wa nafasi ya Makamu mwenyekiti katika kifungu cha 5 (1) ambaye pia ametamkwa katika Jedwali la Kwanza Kifungu cha 4 (3) cha Muswada huu, bado ipo haja ya Makamu Mwenyekiti wa Baraza la vijana aliyechaguliwa na Mkutano Mkuu kuwa mjumbe wa Bodi. Hivyo, kifungu hiki kifanyiwe mabadiliko na kumuongeza Makamu Mwenyekiti kama mjumbe wa Bodi.

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 19 (2) (e) bado kinaendelea kumpa mamlaka Waziri kwa kuwachagulia Bodi ya Baraza, wajumbe watano (5) watakaokua wajumbe wa Bodi baada ya kupendekezwa na Mkutano Mkuu. Tunapendekeza kuwa Mkutano Mkuu wa Baraza la Vijana ufanye uteuzi wa wajumbe wa Bodi kwa utaratibu utakaokuwa wazi na huru ili watu wenye sifa na wawakilishi watano vijana wapate fursa ya kuwepo katika bodi.

**Majukumu ya Bodi**

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 20 (1) kinaeleza kuwa kazi ya Bodi itakua ni ushauri tu. Vilevile, Kifungu cha 21 (2) kinaeleza kuwa Bodi itakua na kazi nyengine kama ambavyo itaelezwa na chini ya Muswada huu wa Sheria. Lakini, jedwali la tano ambalo ndilo lenye taratibu za uendeshaji wa masuala ya Bodi hii, haijaweka kazi ama jukumu lolote la bodi. Hivyo, kwa kifupi Bodi hii inakua na kazi moja ya ushauri kwa Baraza hivyo kuondoa uhalali wake wa kuweza kusimamia ama kufanya maamuzi ambayo yatatekelezwa na Baraza.

**Mheshimiwa Spika,** moja ya mambo ambayo yamekua yakileta ukakasi katika utekelezaji wa shughuli za miradi ya maendeleo ya vijana ni pamoja na kutopatikana ama kutotengwa kwa asilimia 5 za fedha za vijana zinazotokana na mapato ya halmashauri katika wilaya mbalimbali nchini hivyo, kuna umuhimu wa kuhakikisha Bodi inapewa jukumu la kufuatilia utekelezaji wa agizo hilo unafanyika katika halmashauri zote nchini pamoja na kupendekeza hatua za kinidhamu dhidi ya halmashauri ambazo hazitengi fedha hizo ama zinatenga fedha za vijana na kuzitumia kwa matumizi mengineyo.

Kambi ya Upinzani inapendekeza muswada huu uondolewe ili kuweza kupitia upya kazi za Bodi na kuipa majukumu mengine yatakayosimamia na kuwezesha ufanisi wa utendaji wa Baraza la Vijana.

**Fedha za Baraza**

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 22 (a) Kinasomeka kuwa "The funds and assets of the Council shall comprise of-(a) such moneys "as may be" appropriated by Parliament for the purposes of the Council; Tafsiri ya lugha ya kiingereza kwenye maneno "as may be" yanamaanisha kuwa Baraza linaweza kutengewa fedha na bunge ama lisitengewe fedha na bunge. Kama Waziri ndio anawasilisha makisio ya bajeti ya Baraza la Vijana bungeni kupitia bajeti ya Wizara ya Vijana, anaweza akaamua kutowasilisha makisio hayo na kuyaombea fedha kwa kigezo kuwa shughuli za Baraza sio kipaumbele cha Wizara kwa mwaka huo wa fedha huku waziri akisukumwa kufanya hivyo kutokana na tafsiri hiyo ya maneno "as may be" kisheria. Jambo hili litaweza kulifany Baraza liwe masikini kwa kushindwa kabisa kutengewa fedha za bajeti zitakazoidhinishwa na Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi ya Upinzani inaliomba Bunge kufuta maneno *"as may be"* lifutwe na liandikwe neno *"shall"* ili kulazimisha baraza lipate mgao wa bajeti ya Serikali ili kuwezesha uendeshaji wa shughuli zake.

**Mheshimiwa Spika,** mapungufu ambayo yapo katika muswada huu ya kisarufi na majedwali ya Muswada huu yatafanyiwia marekebisho kwa majedwali rasmi ya marekebisho kama yatakavyowasiilishwa na wabunge wa Kambi ya Upinzani Bungeni.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha.

.....................................................
Joseph O. Mbilinyi (MB),
Waziri Kivuli wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo
30.03.2015

**SPIKA:** Sasa nitamwita Mheshimiwa John Mnyika, atafuatiwa na Mheshimiwa Ester Bulaya, atafuatiwa na Mheshimiwa Mgimwa.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nizungumze maneno machache katika muda huu na masuala mengine naamini katika hatua ya Bunge kukaa kama Kamati yatawasilishwa wakati tutakapokuwa tunapitia Majedwali mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, la kwanza, ni muhimu tukapewa nakala kabla ya kusitishwa kwa shughuli za Bunge saa saba mchana ya Jedwali ambalo Serikali inapaswa kuwa imekwishaliandaa la ni namna gani na ni katika maeneo yapi Serikali imekubaliana na maoni na mapendekezo ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu, yapo baadhi ya mambo ambayo yametokana na maoni ya wadau, ambayo baadhi machache yako kwenye taarifa ya Kamati, lakini kama Serikali hatutaona kwa vitendo kwamba, kuna jedwali la Serikali kwa vyovyote vile tutakuwa sawasawa tumeuziwa mbuzi kwenye gunia na tutawauzia vijana mbuzi kwenye gunia. Kwa hiyo, hilo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, niungane na Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwamba Serikali Muswada iliouleta haukuzingatia kwa ukamilifu maudhui na mapendekezo yaliyotokana na maoni ya wadau. Nieleze vilevile kwamba, pamoja na kauli ambayo ilitolewa katika mazingira yasiyo rasmi tarehe 20 Septemba, 2014 tukiwa Dar es Salaam kwamba Serikali inakwenda kuandaa Muswada wake kwa kuzingatia maudhui vilevile kwa ukamilifu ya Muswada Binafsi, ili kusiwe na sababu ya Muswada binafsi uliotokana na maoni ya vijana bali kuwe na Muswada mmoja wa Serikali; nieleze vilevile kama muwasilishaji wa Muswada Binafsi kwamba Serikali haikuzingatia kikamilifu maudhui ya Muswada Binafsi ambao haukutokana na maoni binafsi, bali maoni na mapendekezo ya vijana tuliokutana nao.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa maneno mengine nieleze tu ujumbe niliopewa na Taasisi mbalimbali za vijana baada ya kuupitia Muswada wa Serikali. Vijana wanasema hivi; kama Serikali haitaleta Jedwali la Marekebisho yenye kuzingatia maoni yao hakuna sababu yoyote ya kupitisha Sheria ya kutengeneza Baraza bovu, kukawa na Baraza bovu, ni afadhali kusiwe na Baraza badala ya kuwa na Baraza bovu kwa sababu ni hatari zaidi kwa mustakabali wa vijana nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hili, natarajia Wabunge wenzangu wa vyama mbalimbali ambao wanaguswa na masuala ya vijana, harakati hizi za vijana zilianza muda mrefu na miaka mingi sana. Waziri Kivuli ameiweka historia kwenye kumbukumbu, sina sababu ya kurudia kwa sababu ya muda huu mdogo wa uchangiaji.

Mheshimiwa Spika, lakini niseme tu mwaka 1998 kwenye Kongamano la Iringa ambao wakati huo baadhi ya Wabunge kwa sasa siyo vijana tena, walikuwepo kwenye harakati hizo za vijana, wengine sasa ni Mawaziri, akina Mheshimiwa Lukuvi, Waziri wa Ardhi na viongozi wengine.

Mheshimiwa Spika, miaka ya baadaye miaka ya 1999 Kongamano la *VETA*, miaka ya 2000 miaka yote hiyo, akina Mheshimiwa Lusinde sasa ni Mbunge wakati huo alikuwepo upande wa pili, alikuwepo kwenye hizo harakati, Walikuwepo wengi kweli! Walikuwepo wengi kweli kweli akina Mheshimiwa Nchimbi walikuwepo wakati huo!

Mheshimiwa Spika, sasa umefika wakati, yale maneno ambayo wengi wenu mlipokuwa vijana mlikuwa mnayasema kwamba itatungwa, itatengenezwa Sheria ya Baraza bora, sasa Muswada uko mbele yenu, uamuzi ni wenu, ama kutekeleza matakwa ya vijana na msimamo mliousimamia mlipokuwa vijana kwa manufaa ya vijana na watoto na watoto wa watoto wenu au kuyasaliti matumaini ya vijana na kuingia kwenye historia ya usaliti wa matumaini ya vijana.

Mheshimiwa Spika, tunao kwenye Bunge hili vilevile Wabunge vijana kwa umri na Wabunge vijana walioteuliwa na vyama vyao kwa tiketi za vijana. Itakuwa ni ajabu kama vijana wamesema Muswada huu ni bomu utaleta Baraza bovu na vijana wamependekeza nini kifanyike kupatikana Baraza bora, tutawashangaa hapa kama kuna Mbunge kijana atakayesimama kusaliti maoni na matumaini ya vijana wa Tanzania.

**SPIKA:** Waache watu waseme wanavyoona!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, nami niache niendelee kusema maoni yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema nitawashangaa vilevile wazee wetu humu ndani ambao hamna Baraza la Wazee, akinamama hamna Baraza la Wanawake, lakini sasa kuna ajenda ya Baraza la Vijana kwa maslahi ya watoto wenu, ya vijana wenu na ya watoto wa watoto wenu, kama na ninyi mtashiriki kuendelea kuchakachua maoni ya vijana likatengenezwa Baraza bovu badala ya Baraza bora kwa maslahi ya vijana.

Mheshimiwa Spika, kengele ya kwanza imegongwa; niseme tu nitashangaa kama matumaini haya yakisalitiwa. Nitambue sana mchango wa Taasisi za Vijana; Mheshimiwa hakutaja Taasisi za Vijana kwa majina! Taasisi hizi ambazo zimetoa maoni kwa Serikali vilevile kwa nyakati mbalimbali kabla ya kuandikwa kwa Muswada Binafsi zilitoa maoni vile vile.

Nitambue pia mchango wa Mawakili vijana wakiongozwa na John Malya na Mawakili wengine wa ndani ya Serikali na Mawakili wa nje ya Serikali, Mawakili vijana na wanasheria wa ndani ya Bunge ambao walishiriki katika kutoa maoni katika kuboresha Muswada binafsi.

Mheshimiwa Spika, nilitarajia kwamba Muswada ule binafsi kwa sababu uliandaliwa kwa maoni ya watu na Taasisi mbalimbali wa mwaka 2013, ungepewa nafasi ya kwanza ya kuingia Bungeni na safari hii Serikali ndiyo ambayo ingetakiwa ilete mapendekezo ya marekebisho ya namna gani ya kuboresha Muswada katika Vifungu ambavyo Serikali haikubaliani navyo, lakini

gurudumu limegeuzwa tumeletewa mambo yale yale ya Serikali kuleta Miswada mibovu itetewe ipite iwe Sheria!

Mheshimiwa Spika, pamoja na gurudumu hili kugeuzwa natarajia kwa uongozi wako, tutapewa wakati wa kutosha wa Wabunge mbalimbali wa vyama mbalimbali kuleta Majedwali ya Marekebisho, tufanye kazi ya Kibunge ya kutunga Sheria iliyo bora. Tukiikubalia Serikali kutengeneza *precedence* kwamba, kila unapoletwa Muswada wa Kamati, unapoletwa Muswada Binafsi wa Mbunge, Serikali inachakachua na kutengeneza Muswada wake! Bunge hili litaingia kwenye historia ya kutotumia vizuri Kanuni zake kutoa fursa kwa Kamati zake za Bunge na kutoa fursa kwa Wabunge wake kutunga Sheria bora kwa maslahi ya nchi yetu ambayo ndio kazi kuu zaidi ya Bunge, badala yake wakati wote tutaiacha Serikali ilete Miswada ambayo imekwishachakachuliwa na tupate muda kidogo sana wa marekebisho na hatimaye tutunge Sheria mbovu.

Mheshimiwa Spika, nayasema mambo haya si tu kwa Waziri wa Maendeleo ya Vijana! Nayasema vilevile kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kama Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni. Naamini Mheshimiwa Waziri Mkuu atatoa uongozi ili Sheria hii ya Baraza la Vijana, Sheria hii ya Vijana isiwe kaburi kwako la kisiasa kwa vijana kujua wewe umeiongoza Serikali humu Bungeni kutunga Sheria mbovu ya kuchakachua mawazo na mapendekezo ya vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa yeyote yule mwenye ndoto za kujaribu kutaka kuomba kura za vijana, vijana wa Tanzania wanasikiliza leo…

*(Hapa kengele ya pili ililia kuashiria kumalizika muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Haya, ahsante. Naomba *amendments* zote mradi zifike ile saa yangu niliyosema, sina tatizo, hata zikiwa mia moja na zitakazoibiuka hapa sitapokea, maana mtakuwa mmetuchanganya. Kwa hiyo, zote saa saba ziwe zimepelekwa kwa Katibu wa Bunge kwa mujibu wa utaratibu na zimefikiriwa kwa makini.

Nilisema atakayefuatia Mheshimiwa Esther Bulaya, halafu Mheshimiwa Mgimwa, halafu Mheshimiwa…

Kwanza, Mheshimiwa Ester Bulaya!

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Nianze kwa kuipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu Bungeni kwa sababu, kimekuwa kilio cha vijana siku nyingi na walioanza harakati za kupigania Baraza la Vijana akina Dkt. Balozi Kamala, akina Mheshimiwa Emmanuel Nchimbi, kaka

yangu Lusinde, wapo wengi, lakini tumeona kwenye Bunge lililopita, pamoja na wewe Mnyika, ulikuwa mdogo.

Mheshimiwa Spika, tumeona katika Bunge lililopita Wabunge vijana walivyoanza kupigania Baraza hili liwepo! Sisi pia tumeendeleza jitihada za wenzetu bila kujali itikadi zao za vyama! Sasa leo tunabishana nini? Suala ni Muswada kuja au Muswada wa nani kuja?

Mheshimiwa Spika, nimepitia Miswada yote miwili lengo lao ni moja na nasema kwa sababu leo nimefunga. Tumekuwa Wabunge vijana bila kujali itikadi zetu tukikutana, kuonana na baadhi ya vijana wadau iwe ofisi ya Kambi, iwe nyumbani kwangu na jana Mheshimiwa Mnyika ulikuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya yote ni kwa sababu tunajua vijana wa Tanzania wanataka chombo chao, kama Bunge lazima tuboreshe huu Muswada! Ni kweli, kuna mambo siridhiki nayo na ninazo hapa orodha za vijana wadau wamenipa akina Upendo Peneza, vijana wa UVCCM, mengi yanalingana. Sasa kama vijana hatuna haja ya kuanza kutupiana mipira lawama za kisiasa! Tuje tuboreshe huu Muswada, tumwambie Waziri kwenye mamlaka haya hatukutaki, nami nasema hatukuhitaji uwepo kushiriki kuchagua Viongozi wa vijana! Ndiyo! Tunataka tuwepo hapa tutunge Sheria siyo lazima kitu unachokiona wewe mimi nikione sawa, hapana! Ndio maana tuko tofauti! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huwezi leo hii ukasema kuna mambo mawili yameachwa, basi maoni yote ya wadau hayakuzingatiwa! Siyo sawa! Nimeshiriki kwenye Kamati ya Mheshimiwa Mtanda na nimesoma hapa Taarifa yao, wanasema Viongozi hawa wa Baraza wachaguliwe na Baraza lenyewe na mimi na-*support* hivyo. Haiwezekani Waziri ukajiingiza katika kumchagua Mwenyekiti wa Baraza, Baraza litakuwa lako siyo la vijana! Hayo ndiyo tunayotakiwa tuyaseme hapa! Haiwezekani Katibu ukamchagua wewe! Haiwezekani Wajumbe wa Bodi nao uwachague wewe, hili litakuwa Baraza la Serikali siyo Baraza la vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana tunasema Wabunge bila kujali itikadi zetu kuacha blabla za kisiasa tushiriki wote, tutunge huu Muswada. Hatuhitaji kuendelea kuwagawa vijana kiitikadi kupitia Muswada huu kwa sababu tu kuna oni moja au maoni mawili hayakuwepo, sio dhamira yetu! Wala sio dhamira ya waasisi wetu ambao wameanza harakati hizi kupigania Baraza la Vijana tangu tukiwa shuleni na mpaka leo; tunashukuru tunaingia katika historia ya kuhakikisha chombo hiki kinaletwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nami naunga mkono huu Muswada na niseme kabisa nitaleta *amendment*. Mheshimiwa Waziri naomba ujiondoe kabisa kwenye suala la kung'ang'ania kumpata Mwenyekiti, Wenyeviti wa

Baraza wachaguliwe na Wajumbe wenyewe wa Baraza wa Mkutano Mkuu. Nimeona hapa maoni ya Kamati ikiongozwa na kijana mwenzangu, tulichaguliwa wote Baraza la Vijana UVCCM, Said Mtanda na wote tulikuwa kwenye harakati ya kupigania hili Baraza, ameyaweka humu.

Mheshimiwa Spika, tunataka vijana wenyewe wamchague Mwenyekiti wao, tunataka Wajumbe wa Bodi wachaguliwe na vijana wenyewe, lakini nimeona kuna kipengele pia, Mheshimiwa Waziri na wewe umejiweka kwamba, wewe ndiyo uidhinishe mashirika gani wajiunge, haiwezekani! Vijana wawe huru kujiunga na Mashirika ya Kimataifa, wewe wakupe taarifa. Tukifanya hivyo tutatoa uhuru mkubwa wa vijana kujiamulia mambo yao wenyewe.

Mheshimiwa Spika, lakini kingine ukienda kwenye Kifungu cha 7 haiwezekani leo hii eti vijana watakaoingia kwenye Baraza waishie kwenye *NGO!* Vijana wengi ambao wanapata tabu na maisha magumu, wanaokosa mikopo wako vijijini na wengi hawako kwenye hizi *NGO, unless otherwise* tuwalenge vijana *graduates* ambao wao ukizungumzia tatizo lao kubwa ni ajira, hawa hapa ambao wana-*suffer* kwenye Kata, ambao wanapata tabu kwenye Vijiji, ndiyo tunaowazungumzia na tukiweka utaratibu huu wa kuwa wao pia wawe *member* bila kujiunga kwenye Asasi na vijana hawa wakawa wanashiriki na kujadili matatizo yao hata ongezeko la vijana kuja mijini litapungua. Kwa hiyo na hicho nacho kipengele tukinanii...

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri alifikiri nini vijana, Baraza hili li-*hang* kwenye *level* ya Wilaya na haya mapendekezo ya wadau pia yapo na nimeona hata Kamati wamegusia, haiwezi Baraza likaishia level ya Wilaya *at least* lingefika hata kwenye *level* ya Kata kule ndiko kwenye vijana maskini na moja ya sababu ya kuundwa hili Baraza wa-*discuss* mambo ya maendeleo yao yanayowahusu. Kwa hiyo, haya maendeleo ya vijana yawe *discussed* kwa kuishia kwenye *level* ya Wilaya haiwezekani! Kuna vijana wengi kwenye kata wana matatizo yao lukuki, lakini pia ikifika huko usimamizi wake utakuwa mzuri kutokana na mfumo wetu wa utawala, watashirikiana na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, sasa hili la kusema Baraza hili liishie kwenye ngazi ya Wilaya kwa kweli tutaleta marekebisho na nimeshapeleka tangu saa nne, yapo Ofisini kwako na ni mapendekezo lukuki, kuanzia mstari wa kwanza mpaka jedwali la mwisho. Hii yote tunafanya kazi tuhakikishe vijana wetu wanapata Baraza bora.

Mheshimiwa Spika, inawezekana kuna mambo yameachwa, lakini tukija hapa tukajenga hoja kwa uzito wake, hawa Wabunge wote wanapenda vijana bila kujali itikadi zetu, yakawekwa kwa sababu na wanaoandika hii Miswada ni binadamu, haijawahi kutokea kuna Muswada wa Serikali umekuja hapa umekamilika, ndiyo maana lipo Bunge, wote kwa ajili ya kuiboresha na

kuhakikisha tunaunda Baraza la Vijana lililo imara lenye maslahi ya vijana wote bila kujadili itikadi ya vyama vyetu na ndiyo waasisi wetu walianza bila kujali itikadi zao, walikutana na leo hii tuko hapa sisi tuliopata fursa ya kuhakikisha tunatunga hii sheria, tutunge sheria bora. Wabunge vijana waliokuwepo waliendelea nao na sisi tupo. Kwa hiyo, sioni ni *issue* kubwa kwamba Muswada wa nani umekuja, umekuja huu na ukiangalia nimesoma yote miwili tofauti yake ni kama asilimia kumi au ishirini ambayo Bunge linaweza likayafanya hayo yote.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimeongea kwa ufupi, nitaleta marekebisho yangu na nimeshayafikisha ofisi kwako tuhakikishe tunapata chombo imara. Ni kweli kuna upungufu katika Muswada wa Serikali ulioletwa, lakini ni kazi yetu Bunge kuhakikisha tunafanya marekebisho na tunaleta chombo imara.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ahsante.

**SPIKA:** Ahsante, nilisema nitamwita Mheshimiwa Godfrey Mgimwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla halafu atafuatiwa na Mheshimiwa Mchuchuli!

**MHE. GODFREY W. MGIMWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, ningependa pia kuipongeza Serikali kwa kuhakikisha kwamba Muswada huu unafika Bungeni na tunaujadili na hatimaye kupata sheria.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa ningependa kueleza mambo machache sana. Mambo hayo ni kwamba Muswada huu kwanza utakuwa Muswada bora sana. Nasema hivi kwa sababu gani? Baraza hili ambalo linakwenda kuundwa ni Baraza bora ambalo ukiangalia kwa namna kubwa sana utaona kwamba ni vijana ambao wamekuwa wakifanya utaratibu wa kupata Baraza hili kwa muda mrefu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu mchakato wa kupata Baraza hili haujaanza jana wala haujaanza juzi, mchakato umeanza muda mrefu sana. Ukitaka kuangalia kwa hali ya kawaida utaona kwamba wenzetu walioongea wametamka kwamba kupata majadiliano na maamuzi imechukua siku tatu jambo ambalo siyo la kweli. Tumepata utaratibu huu kwa muda mrefu, tumeweka majadiliano kwa muda mrefu, kama alivyoeleza Mheshimiwa Ester ni kwamba utaratibu huu umeanza tokea enzi za miaka ya 1990. Sasa mtu atakapokuja kusema tumefanya utaratibu wa siku tatu kupata maamuzi siyo sahihi.

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa kuwa naamini kabisa yaliyoelezwa au yaliyotungwa na wenzetu waliopita ni ya muhimu na tutakwenda kuyafanyia kazi na mimi kama kijana nina kila sababu ya kuishukuru Serikali kwa kuhakikisha kwamba Baraza hili linakwenda kuundwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, waongeaji waliopita wameongea na wamesema kwamba kuna upungufu mwingi, lakini hawatamki huo upungufu ni upi na unaelezwa tu kwamba kuna upungufu, tumeiga Kenya, Uganda, tumeiga wapi? Kwani kuna tatizo gani kuiga, kuna tatizo gani kama mtu utakuwa umekopi kitu ambacho kinaweza kukuletea tija? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile sisi kama Watanzania tuna utaratibu wetu wa maisha, sisi hatukurupuki, hatuamki asubuhi na kusema tutakwenda kuandaa Muswada wetu, lazima tuchukue muda kuupima, kuchukua maoni na kuhakikisha kwamba tunafanikiwa kwa ajili ya Muswada huu ambao utakwenda kuwa wa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, tatizo ninalolipata ni katika uteuzi wa hawa viongozi wetu. Ningependa kusema kwamba Mheshimiwa Waziri lazima awepo kuhakikisha kwamba yale majina matatu yaliyoidhinishwa ili kuhakikisha kwamba anaya-*pick*, maana yake analiangalia jina moja kwenda la pili, kwenda jina la tatu, lakini watakaochagua wawe wahusika, sisi wenyewe vijana, Mheshimiwa Waziri aweze kuwapale kuidhinisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matatizo yatakayokuja kutokea hapo baadaye ikiwa kama utaratibu huu hautafuatwa ni kwamba tutaingiza tena masuala ya itikadi, jambo ambalo tumelikataa.

Mheshimiwa Spika, mambo mengine ya msingi ambayo ningependa kuyagusia, utaratibu huu lazima uende kwenye roots kule kwa vijana wenyewe chini, tuweze kuangalia kwamba vijana wetu au sisi kama vijana hatupo mjini tu, tunafika mpaka Vijijini, tunafika kwenye ngazi za Kata.

Sasa utaratibu wa kufika kwenye ngazi ya Wilaya siyo utaratibu mzuri, nafikiri ingekuwa vyema tuangalie vijana, tukawagusa kule walipo, kwenye maeneo husika, vijana ambao ndiyo wanaotuletea maoni, watuambie matatizo yao ni yapi tuweze kuyapeleka kwenye utaratibu wa Wilaya, Mkoa na hatimaye Taifa.

Mheshimiwa Spika, ninavyotazama hali halisi ya Muswada ni kwamba mambo ya muhimu tukiangalia hasa kwenye masuala ya Mfuko wa Vijana, pesa ambayo itatengwa kwa ajili ya vijana. Idadi tuliyoelezwa mpaka sasa hivi ni kwamba kuna idadi ya vijana milioni 16 au zaidi kidogo. Sasa pesa ambazo tutakuwa tunazitenga kwa ajili ya vijana, kwa idadi hii ambayo tunayo, ni muhimu sana pesa hizi ziweze kuwagusa na zikawafikie vijana kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, vilevile ikiwa kama tutasema kuna Mfuko huu na tuna Baraza la vijana halafu pesa hizi au hizi *funds* haziwafiki vijana ambao ndiyo

nguvu kazi ya Taifa, tutakuwa tunalipeleka Taifa letu mahali pabaya. Kwa hiyo, ningependa tuhakikishe kwamba pesa ambazo zinakwenda kutengwa kwa ajili ya vijana, lakini vilevile kwa ajili ya masuala mazima yote ya Baraza lazima yaweze kuwafikia walengwa kwa muda unaotakiwa ili kuhakikisha kwamba Baraza hili linafanya kazi, kuhakikisha kwamba Baraza hili linadumishwa lisiwe tu Baraza la muda mfupi liweze kuwa Baraza la muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, lakini pia mambo mengine ambayo ningependa kugusia ni kwamba nimefurahishwa kwamba halitagusa itikadi. Mapendekezo ya Kamati ni kwamba lisiweze pia kuingia kwenye masuala ya dini, ni vizuri sana tukaangalia mapendekezo ya Kamati kama yalivyoelezwa tukaona umuhimu wa kujitenga au kuhakikisha kwamba itikadi zetu za vyama, itikadi zetu za kidini na mambo mengine ambayo yanaweza yakaleta mgawanyiko katika Taifa letu tunayapuuzia na tusiweze kuyaleta kabisa.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo nimeliona ni katika uteuzi wa viongozi wetu. Inaonesha kwamba kwa wale ambao wako kwenye ngazi ya Taifa, lazima wawe na angalau shahada ya kwanza wale viongozi. Sasa ili tuweze kupata Baraza bora elimu ni kitu cha msingi sana, isiwe tu kwa ajili ya wale wa ngazi ya Taifa, lakini ngazi ya mikoa pia tuweze kuwaangalia, tuangalie wanaweza kukaa na elimu kiasi gani. Je, tuwaweke kwamba wawe kidato cha nne, wawe kidato cha sita au tuwaangalie vipi hao.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa wale ambao wako kwenye ngazi za chini ambazo ndiyo ngazi ya Wilaya pia lazima ielezwe dhahiri kwamba je, mtu akiwa na elimu kiasi hiki tunawezaje tukamkubali huyu mtu, tunaweza tukamtenga mtu aliye na elimu na asiye na elimu. Kwa maana hiyo ikiwa kama mtu yuko kwenye Wilaya lakini ana uwezo mkubwa wa utendaji kazi, lakini hana hiyo shahada moja na anataka agombee nafasi ya Taifa, tunawezaje kumnyima. Kwa hiyo, ni vyema sana tuangalie pia na uwezo isiwe tu elimu peke yake ingawa elimu ni muhimu, lakini pia uwezo wa utendaji kazi wa mtu mmoja mmoja ni lazima tuuzingatie.

Mheshimiwa Spika, tunaelezwa kabisa kwamba utaratibu wa upatikanaji wa viongozi ni kwa kuteuliwa na Baraza lenyewe kwenye Mkutano Mkuu. Ikiwa katika mkutano ule kuna viongozi ambao siyo waadilifu, lakini wana elimu je tuwakubali, tuwapitishe? Kwa hiyo, ndiyo hapo ambapo tunakwenda kuona umuhimu wa Waziri husika kuhakikisha kwamba haya yote ambayo tumeweza kuyaona kwenye wagombea hawa wanaotaka uongozi Waziri aweze kuwa na mkono wake kuhakikisha kwamba hawa watu au hawa wagombea wanapita katika namna inayotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, napenda kukushukuru. Naipongeza tena Serikali, lakini vile vile naipongeza sana Kamati kwa kazi nzuri

waliyoifanya, mimi kama kijana nina kila sababu ya kuendelea kuishukuru Serikali na kuhakikisha kwamba tunapata Baraza bora la vijana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, atafuatiwa na Mheshimiwa Kuruthum na Mheshimiwa Mama Sitta ataingia, haa! Kwendeni huko, kutunga sheria huko. Sheria inatungwa na wote. *(Kicheko)*

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuchangia kwenye Muswada huu adhimu asubuhi hii ya leo. Awali ya yote niutambulishe umma, mimi si kijana tena kama ilivyokuwa mwaka 2010 nilipokuwa naingia kwenye Bunge hili, nimetoka rasmi kwenye ujana takriban miaka minne iliyopita na ndiyo maana sasa nimefikia umri wa kugombea Urais, namshukuru Mungu. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hii tu kwamba kuna watu kama mimi leo hii katika umri huu tunaweza kufikiria kugombea nafasi kubwa kama ya Urais achilia mbali kuamua kugombea kama nilivyofanya mimi na ma-*comrade* wengine humu ndani akina Mwigulu Mchemba, akina Lazaro Nyalandu, akina January Makamba, ni ishara tosha kwamba Taifa letu siku zote limekuwa likithamini nafasi ya vijana kwenye kujenga Taifa hili na historia inatufundisha kwamba harakati za ukombozi kutoka kwenye mikono ya wakoloni miaka ile ya hamsini pamoja na kwamba wazee waliongoza harakati hizi, lakini vijana walikuwa chachu kubwa ya kutaka mabadiliko kutoka kwenye utawala wa kikoloni na vijana wa enzi hizo akina Mwalimu Julius Nyerere wali-*champion* jitihada za mapambano na baada ya uhuru jitihada za mapinduzi kuelekea Tanzania mpya ambayo tunayo leo hii.

*(Hapa kengele ililia kabla ya muda wake)*

**SPIKA:** Mmekosea naomba hiyo mrekebishe.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Hata kuchangia sijaanza.

Hivyo harakati za vijana katika nchi yetu zimekuwa zikipewa kipaumbele siku zote na mimi kwa muktadha huo niipongeze Serikali kwa dhati ya moyo wangu kwa kuamua sasa kuleta Muswada wa Sheria ya Vijana kwenye Bunge lako Tukufu ili tuweze kuufanyia kazi. Niipongeze zaidi Serikali kwa kutunga Sera ya Vijana miaka ile ya 2008/2009 na ambayo ilipelekea kutoa tamko la kuundwa kwa Baraza hili kwa mujibu wa sheria na sasa leo tuna Muswada kwenye meza tukiujadili.

Mheshimiwa Spika, harakati za vijana zimechangiwa na watu wengi na hivyo hata Mheshimiwa Mnyika alipoamua na yeye kuleta Muswada wake binafsi kwenye Bunge lako ili tuweze kuunda Baraza hili amechangia katika

haraka hizo kama ambavyo wengine tumechangia haraka za vijana katika nafasi mbalimbali. Hivyo naye nichukue fursa hii kumpongeza kwa kutia chachu na kuikimbiza Serikali, ndiyo kazi ya Kibunge wakati Serikali mara nyingine inaweza ikachelewa chelewa, ama akilala ama ikaona si kipaumbele, sisi Wabunge kazi yetu ni kupiga kelele ili kuiamsha Serikali ifanye kazi yake ipasavyo.

Mheshimiwa Mnyika usijisikie umeporwa hoja yako lakini naomba utambue tu kwamba hoja ya kuunda Baraza la Vijana katika nchi yetu, *to start with* haikuwa ya kwako kwa sababu ilikuwepo toka siku nyingi. Hivyo wewe ulifanya kazi yako ya Kibunge ya kutia chachu kwa Serikali kuleta sheria hii Bungeni, kwa sababu kuundwa kwa Baraza la Vijana, ni jambo ambalo limepiganiwa na watu wengi kama ulivyosema wewe mwenyewe, lilianza toka enzi za *TANU Youth League* miaka ya 60 mpaka kuja Umoja wa Vijana wa CCM miaka ile ya 70.

Pia harakati hizo zimeanza na wengine ni wazee wetu akina Mheshimiwa Lukuvi, hata mama yangu alikuwa kwenye harakati hizo akiwa Mwenyekiti wa Vijana Mkoa wa Tabora, miaka hiyo, mpaka na mimi mtoto nikaja nikarithi miaka ile ya 90. Tunaona kaka zetu akina Nchimbi, akina Dkt. Kamala, akina Mheshimiwa Lusinde wote nao katika nyakati tofauti tofauti wamekuwa *champion* harakati za kuundwa kwa Baraza la Vijana na hata kupelekea Sera ya Vijana ya mwaka 2008/2009 kuandikwa na kutamka wazi kwamba Serikali itaunda Baraza la Vijana. Hivyo kwa kuanzia tu hoja hii huwezi kudai asilimia mia kwamba ilikuwa ni ya kwako na kwamba umeporwa na kwamba sheria inayoundwa haina maana yoyote, haijazingatia maoni ya wadau, si kweli. *(Makofi)*

Tufanye kazi ya Kibunge turekebishe tunapoona kuna upungufu ili sheria iwe nzuri zaidi, lakini tusianze kulaumiana, tusianze kugombea fito, tunajenga nyumba moja na wewe nafahamu umepita *TYVA* Taasisi ambazo zilianzishwa hata wewe hukuwepo wakati zinaanzishwa, sisi tulikuwepo, sisi wengine tumeshashiriki harakati za vijana Kimataifa, kupitia *Global Youth Coalition on AIDS* kupitia *International Students Conference on Aids*, kupitia *IFMSA*, zote taasisi hizi mimi nimeshiriki nikiwa kama Mwenyekiti wake na ni za Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, hivyo haraka za vijana huwezi hata siku moja ku-*claim* kudai kwamba ni za kwako, umezianza wewe, hapana, mimi siwezi kudai hivyo, naamini hata kaka zetu akina Nchimbi hawawezi kudai hivyo. Akina Nyalandu tumewakuta wakiendesha harakati za vijana ndani ya Bunge, nao hawawezi kudai kwamba harakati hizo zilikuwa ni za kwao. Hivyo sasa tumefika wakati muafaka wa sisi kuangalia sheria hii ina upungufu gani, turekebishe tuweze kusonga mbele na siyo kusema kwamba sheria yote ni ya hovyo, ina mambo mazuri.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, wengine wana mtazamo kwamba kwenye kipengele cha saba, kwa mfano Kambi ya Upinzani, kaka yangu Mheshimiwa Mbilinyi anasema kifutwe ama kiandikwe upya, ni mapendekezo ya kuangalia, siyo kifutwe chote, tunaweza tukarekebisha hapa na pale na ndiyo kazi tunayopaswa kufanya hapa tutakapokaa kama Kamati, kwamba turekebishe hapa, tubadilishe hiki, lakini siyo kwamba Ofisi ya Mwanasheria Mkuu haiku-*draft* kipengele hicho *properly*.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na pendekezo la Mheshimiwa Ester Bulaya kwamba pengine tumpunguzie Waziri mwenye dhamana na mambo ya vijana mamlaka ya kuteua Wajumbe ama kuliweka Baraza chini yake kama taasisi iliyo chini yake hapana, lakini pia nakubaliana na maoni ya Kamati, lakini pia maoni ya Mheshimiwa Mgimwa kwamba tujitahidi kuhakikisha Baraza hili linabaki mikononi mwa vijana wenyewe, lakini Serikali iwe inatupia jicho. Kwa hiyo, Serikali iwe ina *eyes on*, *hands off approach* isiingie ndani sana, lakini ichungulie.

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu kwa sisi ambao tumewahi kushiriki harakati mbalimbali za vijana, tunafahamu vijana wanaweza wakaingia kwenye mihemko ya hatari na vijana tayari tumeshafahamu kwamba sasa hivi wanakaribia milioni 20 katika nchi yetu. Ni watu wengi sana, kama ukiwajengea taasisi ambayo ni imara sana na wakaji-*organize* na siku moja wakaamua kupinga kitu inaweza ikawa *threat* kwenye amani yetu. Wengine sisi tumeshiriki harakati hizo kwa vitendo na tunafahamu ushawishi wanaoweza kuwa nao vijana. Hivyo, lazima Serikali yetu iwe na jicho, iwe inaangalia, lakini isiangalie isiweke mikono yake ndani, hilo hatuwezi kulikwepa tuseme ukweli tu, hatuwezi kulikwepa.

Mheshimiwa Spika, sisi tumewahi kuwa viongozi wa vijana katika nafasi mbalimbali na tumeona saa nyingine wewe kiongozi unashindwa ku-*control* mihemuko ya wenzako wanakushinda, wanakuwa na ushawishi hata wewe wanakuondoa. Tunafahamu harakati za pale Chuo Kikuu miaka ya 90 zilipotufikisha na wale walikuwa ni vijana. Akina Dkt. Kitilya Mkumbo miaka ya mwanzoni ya 2000, akina Mheshimiwa Zitto Kabwe, akina Marehemu Mukiri Gervas, akina Dkt. Deogratius Michael, akina Dkt. Ulimboka, tunafahamu walipofika, lakini saa nyingine kiongozi unataka ku-*control* mihemuko ya wenzako unashindwa, ukiwa kama kiongozi wa vijana.

Mheshimiwa Mnyika hujawahi kuwa Rais wa Serikali ya Wanafunzi mimi nimewahi. Nitakupa taarifa tu kwamba kuna wakati umekaa kwenye Kikao unaendesha Kikao cha Mkutano Mkuu wa wenzako wanakushinda kwa hoja, wanakushinda kwa ushabiki na unashindwa ku-*control* unalazimika kufuata wanachokitaka.

Sasa katika mazingira ya namna hiyo, lazima tukubaliane kwamba vijana tuwape uhuru, tuwape fursa ya kujadili mambo yao, kupanga mambo yao, kuendesha mambo yao na kuwa na mfumo wa kuwasiliana nchi nzima, lakini ni lazima tukubaliane kwamba Serikali iwe na jicho lake ili tuweze ku-*control* kinachotoka kwenye vichwa *vibrate* na *dynamic* vya vijana wetu. Hilo ni jambo la msingi.

Mheshimiwa Spika, wengine tumeendesha harakati hapa Bungeni za kusaidia vijana waweze kuanzishiwa Mfuko wao, waweze kuanzishiwa benki yao, waweze kupata mitaji, japokuwa Serikali imekuwa na ahadi nyingi kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana kwenye Wilaya kule, tunaona pia hakuna utekelezaji na hili ni kwa Serikali sasa. Kuanzisha Baraza ni jambo moja, kuhakikisha Baraza linaleta faida chanya kwa vijana ni jambo lingine kabisa. Ushauri wangu, Serikali itekeleze ahadi zake kutenga asilimia kumi ya *collections* za Halmashauri kwenye miradi ya vijana ni jambo la lazima.

*(Hapa kengele ya pili ililia kuashiria kumalizika muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa *time*.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mchuchuli, atafuatiwa na Mheshimiwa Margret Sitta!

**MHE. KURUTHUM J. MCHUCHULI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami nipate kuchangia katika Muswada huu muhimu sana unaotuhusu sisi vijana.

Mheshimiwa Spika, kwanza nachukua nafasi hii pia kuwapa pole wanachama wa Chama cha Wananchi *(CUF)* ambao jana wamepata maumivu kwa kupigwa. Nawapa pole sana, lakini nawaambia tukaze buti mapambano lazima yawe na changamoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kipekee pia napenda kumpongeza Mheshimiwa John Mnyika kwa sababu ametusaidia leo kusukuma Serikali kuleta huu Muswada, bila Mnyika kusukuma tungeona bado ni hadithi zile zile ambazo zimechukua takribani miaka mingi tu zaidi ya kumi, harakati zimeanza siku nyingi, lakini Muswada ukawa haujaja, lakini baada ya Mheshimiwa Mnyika kuongeza nguvu kidogo, Serikali imeleta Muswada, kwa hiyo tunashukuru sana na tunampongeza kwa juhudi zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuchangia Muswada, nitaanza na hicho kifungu cha 4(3) ambacho kinaongelea kwamba uanachama uwe wa wazi na wa hiari, naona maoni ya Upinzani yamezungumzia lakini nitajazia hapo. Kwamba tunaendelea kuiomba Serikali iache fursa kwa vijana wawe huru kujiunga, kijana ambaye anataka kujiunga na hili Baraza la Vijana awe huru kujiunga na asiwekewe vikwazo, kama ambavyo wamesema kwamba watatumia taasisi zilizosajiliwa, mimi napinga hii kwa sababu tuna uzoefu.

Mheshimiwa Spika, katika Bunge la Katiba tulisema tutapata wadau wa 201 kutumia taasisi mbalimbali, lakini uliona watu walitumia nafasi za taasisi mbalimbali kuwaleta watu wa kada na itikadi moja badala ya kuzingatia umuhimu au nafasi za watu husika. Wote tumeona hilo, mvuvi anakuja Katibu wa CCM wa Wilaya, sijui Mganga wa Kienyeji anakuja nani. Kwa hiyo, tunaomba wasiseme hizo taasisi kwa sababu vijana wana uhuru wa kujiunga na wasitumie tena nafasi hiyo kufanya Baraza hili litekwe na Chama cha Mapinduzi badala ya kuwa Baraza huru la Vijana kama ambavyo vijana tunatarajia.

Mheshimiwa Spika, lakini nataka kuchangia Muswada katika kipengele kinachozungumzia Mkutano Mkuu. Mkutano Mkuu wa Taifa ule, nilikuwa najaribu kuangalia *composition* pale, wanazungumzia kwamba Mkutano Mkuu ule utaundwa na Mwenyekiti wa Mkoa na Katibu wake, Mjumbe kutoka kwenye Wilaya, lakini pia wanasema Mjumbe mwingine mmoja yeyote kutoka kwenye Wilaya.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia hotuba ya Mheshimiwa Waziri katika ukurasa wa 12, yeye mwenyewe anatuambia kwa sasa hali halisi tuna vijana takribani milioni 16, lakini ukiangalia Baraza kuu lile ambalo linaundwa kwa kutumia mfumo huu wa Serikali litakuwa linachukua takribani mia tatu na kidogo.

Mheshimiwa Spika, sasa ninavyoona ule uwakilishi tusiubane. Tunazungumzia vijana milioni 16, kwa hiyo, tunahitaji tuwe na Mkutano Mkuu ambao kidogo utajaribu kuchukua vijana wengi. Kwa mfano, ukichukua mfano Chama cha Wananchi *(CUF)*, Mkutano Mkuu takribani 800 lakini wanachama wako wangapi mnaona hilo. CCM Mkutano Mkuu mko watu wangapi, kwa hiyo tujaribu kuchukua idadi ambayo kidogo italingana na idadi ya vijana kwa sasa ambao Tanzania wapo ambao ni takribani milioni 16.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, napendekeza na nitaleta *amendment* pia, napendekeza idadi iongezwe. Kwa mfano, tunaweza tukasema badala ya kusema kwenye Wilaya mtu mmoja sasa tuseme Wilaya ilete watu watatu.

Kwa hiyo, italeta labda Baraza kuwa na watu 600 tu ambao pia itakuwa bado ni *affordable* wataweza kulimudu na kuweza kuliendesha. Najua Serikali

wanaweza kusema kwamba kigezo kitakuwa ni gharama, lakini uwakilishi wa watu milioni 16 lazima tuangalie kwa mapana yake kupata watu wanaotosha kwa nchi nzima ili Baraza liweze kutoa maoni ambayo yata-*cover* vijana wote.

Mheshimiwa Spika, lakini pia najaribu kuangalia Muswada wenyewe kwenye mpangilio. Kama ambavyo kasema Mheshimiwa Mnyika kwa sababu aliuleta kwa haraka, kwa hiyo kuna baadhi ya makosa, kwa mfano, wanazungumzia Mkutano Mkuu, wanasema Mkutano Mkuu utaukuta umezungumzia kwenye ibara 12, lakini ukienda 12 utakuta wamezungumzia kitu kingine tofauti, unakuta 16 ndiyo wanazungumzia *General Assembly*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa ile haraka haraka ya kuleta huu Muswada, kuna baadhi ya mambo katika mpangilio hayajakaa sawa. Kwa hiyo, naiomba Serikali iangalie vizuri na kupanga vizuri kwa kila ibara au kipengele kiendane, ukisema kwamba 16 unakuta kitu hiki, basi ukikute kilekile na badala yake usikute kitu kingine. Kwa hiyo, nategemea wa mwisho ambao tutapitisha hapa Bungeni, Mheshimiwa Waziri atayachukua hayo mambo na ataweka vizuri zaidi ukilinganisha na huu ambao umeletwa kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, lakini bado ukiangalia katika Ibara hiyo ya nne (4), bado nasisitiza kwamba ule uhiari katika uanachama wetu. Mheshimiwa Said Mtanda, Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii pia amezungumzia hiyo, kwa hiyo, naendelea kusisitiza kwamba ifanyiwe kazi. Pia uwakilishi katika Wilaya, wanasema tunaunda Baraza la Wilaya kwa mfano, ambalo litachukua watu 30.

Mheshimiwa Spika, naomba uwakilishi wa Wajumbe katika Wilaya uendane moja kwa moja na uwakilishi wa watu kutoka kila Kata. Kama hivyo, tunavyosema Baraza lianzie kwenye ngazi ya Kata, kwa sababu tunaamini kwenye Kata kule ndiyo kuna vijana wale ambao hasa ndiyo tunawapata wale vijana halisi na siyo kuelea elea tu kuanzia kwenye ngazi ya Wilaya ambayo inazungumziwa ambayo haina ufafanuzi.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu wanasema Wajumbe 30, lakini Wajumbe 30 hawajazungumziwa popote, wanapatikana kwa mtindo gani? Kwa hiyo, tunataka Serikali, tunamtaka Waziri aje kutuambia, wale wajumbe wanapatikana kwa utaratibu gani kwa sababu vinginevyo tutawapata watu ambao siyo halali. Kwa hiyo, naomba tena kwamba, tunaposema tusiweke kima, kusema kwamba lazima wawe 30, kwa sababu kuna tofauti katika Wilaya zetu. Kuna Wilaya nyingine utakuta ina Kata 30, Wilaya nyingine ina Kata 14, Wilaya nyingine ina Kata 19, Wilaya nyingine ina Kata 20, kwa hiyo kuna utofauti wa ukubwa wa maeneo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunavyoona kuna tofauti katika ukubwa maeneo, kwa mfano, Wilaya ya Pangani ni ndogo huwezi ukafafanisha na Wilaya ya Rufiji. Wilaya ya Rufiji ni kubwa ina Kata karibu 29, Pangani ina Kata 13 kwa maana kwamba *population* ya eneo pia izingatiwe katika uwakilishi. Kwa hiyo, ninachoomba kusema tuzingatie idadi ya wawakilishi kwenye Wilaya kutokana na ukubwa pia wa Wilaya. Kwa hiyo, tusiseme 30 tu, tuseme kuundwa kutokana na Kata, kama Kata zipo 30 mfano, watoke wawakilishi vizuri na siyo tu Baraza liwe lina-*hang* kwenye Wilaya.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba hilo lizingatiwe kwamba idadi ya wanachama wa Baraza uzingatie eneo na watu katika sehemu ambayo Baraza linaundwa. Kwa hiyo, pia itakwenda kwenye ngazi ya Mkoa na pia inaweza ikapelekea kubadilisha utaratibu wote na muundo wote kulingana na mahitaji na eneo husika.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, tunapitisha hapa Sheria, lakini tunasema tunaomba kanuni zitungwe haraka, kwa sababu hakuna faida kama tutapitisha hapa, halafu bado ikaendelea kusuasua mpaka Waziri atakavyotaka aipitishe. Itakuwa haina maana kwamba tunapitisha Sheria kutunga Baraza halafu Baraza lenyewe mpaka Waziri atakapopitisha badala kwenda haraka.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii adimu ya kuchangia kuhusu hoja iliyoko mezani kuhusu uanzishaji wa Baraza la Vijana Tanzania. Pia nichukue nafasi hii kuwashukuru wanawake wa Mkoa wa Tabora ambao wameendelea kunipa ushirikiano wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana Wizara ya Vijana, Utamaduni na Michezo, kwa kazi nzuri waliyoifanya hadi tukafikia siku ya leo kujadili Muswada uliowekwa mezani. Hongera sana Mheshimiwa Waziri na Wizara yote kwa ujumla, lakini pia niwashukuru Kamati inayohusika ya Maendeleo ya Jamii kwa kazi nzuri waliyoifanya kutokana na taarifa waliyoitoa, hongereni Kamati inayohusika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimefurahi, siku ya leo ni siku ya muhimu sana kwa sababu Muswada huu ni muhimu sana. Vijana wanapokumbukwa ni jambo la msingi na tunaipongeza Serikali inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi kwa kuleta Muswada huu. Hongera sana Chama cha Mapinduzi, hongera Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niliangalia sana ukurasa wa 44 nikafurahishwa sana na kazi za Baraza na kilichonifurahisha zaidi ni suala la kuendeleza umoja wa

vijana, vijana Watanzania ambao tunawategemea sana ni muhimu wakawa na umoja. Kwa hiyo, napongeza sana kazi ya Baraza la kuendeleza umoja wa vijana. Pia kuendeleza utaifa, kuendeleza moyo wa kujitolea na wakati huo huo kuendeleza moyo wa kujituma. Kwa kweli Baraza likifanya kazi vizuri, tunaamini vijana wetu waliopo sasa watanufaika sana na nchi yetu itaendelea.

Mheshimiwa Spika, pia nimefurahi kwa sababu katika kazi nyingine ambayo walipewa ni kuhamasisha usawa wa kijinsia. Kwa hiyo, ni vizuri kama Baraza tangu mwanzo likaanza kujenga hoja au suala la umuhimu wa kuwa na usawa wa kijinsia kwa kweli nchi yetu itapiga hatua katika suala la kuendeleza maendeleo kwa pamoja kwa wote akina baba na akina mama. Si hivyo tu pia Baraza limepewa jukumu la kuangalia masuala yanayohusiana na wenzetu wanaoishi na ulemavu. Suala hili limenifurahisha sana kwa sababu mambo yatakayoshughulikiwa yatakuwa hata na hii vita dhidi ya *albino* na wale wote ambao hawanufaiki vizuri na maendeleo ya nchi yetu, hilo jambo limenifurahisha sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa muda siyo mwingi sana ningepeleka sasa hoja zangu katika masuala ya maombi. Nafikiri kitu cha kwanza, niiombe Serikali mara baada ya sheria hii kuwekwa sahihi na Mheshimiwa Rais, basi kazi ya kwanza iwe elimu, vijana wapewe elimu ya kutosha ili waweze kujua Baraza hili litaendeshwaje. Wakianza bila kupewa elimu inayohusika, wanaweza wasiwe na mwanzo mzuri, kwa hiyo elimu ni muhimu sana ili kusaidia Baraza lianze kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tutaiomba Serikali na hasa Wizara inayohusika iandae ziara wakaone kule ambako Mabaraza ya namna hii yamefanya kazi vizuri. Wakiangalia kule ambako wenzao wanafanya vizuri, naamini Mheshimiwa Waziri atakuwa na taarifa wapi Mabaraza yanafanya kazi vizuri. Waende wakajifunze, kuangalia kwa wenzenu ni njia mojawapo pia ya kujifunza ili na ninyi muanze vizuri.

Mheshimiwa Spika, pia naunga mkono wenzangu wote Waheshimiwa Wabunge waliosema kwamba uongozi uanzie ngazi ya Kata usianzie ngazi ya Wilaya tu. Tunaomba Serikali ishushe uongozi hata kwenye ngazi ya Kata kwa sababu nchi yetu ilivyo tunapozungumzia Wilaya, Wilaya ni kubwa sana na tukitaka tupate maoni ya watu wengi au vijana wengi zaidi, basi tufikishe uongozi katika ngazi ya Kata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuchukua nafasi hii kuiomba Serikali, kwa mfano, Serikali sasa hivi imekuja na Sera mpya ya Elimu ya mwaka 2014. Ningeomba jambo ambalo vijana wetu wanahitaji kwa sasa hivi ni masuala ya ufundi wa aina mbalimbali. Kwa hiyo, ningechukua nafasi hii kuiomba Serikali hasa kwa kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kuhakikisha kwamba

vijana wetu wanapata mafunzo mengi ambayo yatawawezesha kujiajiri wao wenyewe lakini pia kuajiriwa. Vilevile kuwe na utaratibu ambao vijana wanaopata mafunzo pia wasaidiwe jinsi ya kupata vifaa vitakavyowawezesha kuanzisha shughuli zao wenyewe ili waweze kumudu maisha yalivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningechukua nafasi hii pia kuikumbusha Serikali, ilikuwa imeanzisha utaratibu, sijui uliishia wapi wa kuoanisha kwa karibu mafunzo yanayotolewa *VETA* na mafunzo yanayotolewa kwenye *FDCs* kwa sababu naamini kabisa kwamba *VETA* peke yake haiwezi kuwafikia vijana wengi, lakini wakiunganisha nguvu ya *VETA* na Vyuo vya Wananchi yaani *FDCs* mafunzo yanaweza kuwafikia vijana wengi zaidi kuliko kutegemea *VETA* tu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naamini kabisa Serikali ilikuwa na mkakati, basi iendeleze mkatati ambao utawawezesha vijana wengi zaidi kupata mafunzo ya ufundi ili waweze kumudu maisha yao. Kwa sababu tunajua sasa hivi ajira ni haba, lakini wakiwezeshwa kupata ufundi wa aina mbalimbali basi inaweza kusaidia kujiajiri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia nichukue nafasi hii kuomba Halmashauri na kumwomba Mheshimiwa Kigwangalla ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya TAMISEMI kuwabana TAMISEMI ili fedha zinazotengwa asilimia tano(5%) ya vijana iende iwafikie kama ilivyokusudiwa na wakati huo huo nichukue pia kuwaomba asilimia tano (5%) zilizotengwa kwa ajili ya kuendeleza akinamama pia iwafikie.

Mheshimiwa Spika, naamini kabisa kama TAMISEMI, Halmashauri zote, zikitenga fedha asilimia tano ya bajeti nzima ikawaendea vijana inaweza kuwasaidia. Kwa sababu nimeshafika Wizara ya Vijana na kuulizia kiasi kinachotengwa kwa ajili ya kukopesha vijana katika sehemu mbalimbali ikiwemo Urambo, utaona kwa mwaka mzima kwa mfano, sasa hivi ni vikundi vitatu tu ambavyo vimepata, ambavyo ukiangalia ni vichache sana ukilinganisha na mahitaji ya vijana wengi walioko kwenye Wilaya.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niiombe Serikali kama nilivyosema hasa TAMISEMI, fedha zinazotengwa kwa ajili ya vijana zipelekwe na fedha zinazotengwa kwa ajili ya akina mama zipelekwe, kwa sababu bila kuwasaidia vijana kuwa na miradi ambayo itawawezesha kumudu maisha, vijana wetu watakaa vijiweni, bila kufanya kazi yoyote ambayo siyo vizuri, lakini kukiwa na utaratibu wa kuwakopesha vijana, tena ikiwezekana hata hii asilimia iangaliwe iongezwe zaidi kwa sababu vijana ni wengi zaidi kwa sasa hivi. Hii asilimia tano inaweza pia kuwa imepitwa na wakati, kwa hiyo tuwaongezee fedha wapate mikopo ya aina mbalimbali ili waweze kunufaika kwa kujitegemea, kwa sababu si jambo zuri vijana wakaa bila kazi yoyote.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi nzuri wanayofanya Wizara kwa kuja na Muswada huu, napendekeza pia kuna vikosa vidogo vidogo kwa upande wa Muswada ulioandikwa kwa Kiingereza na pia kuna vikosa vidogo vidogo vilivyoandikwa kwenye upande wa Muswada wa Kiswahili. Naamini kwamba mtaangalia ili mrekebishe na maeneo mengine ambayo hayaeleweki vizuri kwa mfano kama ukurasa wa 44, pia ukiangalia kifungu cha 5(1)(b) mimi naamini lililokusudiwa siyo hilo, linaweza likawekwa vizuri ili lijulikane kabisa mnalomaanisha nini, idadi ya vijana wanaokwenda kwenye Baraza la Taifa.

Mheshimiwa Spika, basi baada ya kusema hayo, sina mengi, naunga mkono hoja na nawaomba Wabunge wenzangu, hakuna Sheria iliyokamilika, sisi tupitishe hii kama kutakuwa na upungufu baadaye utafanyiwa marekebisho, lakini kwa leo tuungane mkono wote, tuipitishe hii, vijana wapate Baraza lao, tunaamini kabisa watafanya kazi kwa kushirikiana, bila kujali wanatoka chama gani kwa sababu kusudio la Muswada huu ni kujenga umoja wa vijana, umoja wao wa kulipenda Taifa lao, moyo wa kujituma. Tuunge mkono hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na hongereni Wizara inayohusika. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MHE. SAID M. MTANDA:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mwongozo wa Spika, kufanyaje? Saa imefika.

Waheshimiwa Wabunge, kama mnavyoona saa imefika. Sasa natoa maelekezo kwamba nimeshaelezwa *amendments* ziko nyingi sana. Sasa kuliko sisi tuvurugane hapa, wote wenye *amendments* wanabidi waende kule Ukumbi wa Pius Msekwa, wawasilishe *amemndments* zao, zijadiliwe kwa urefu kule, halafu mchana tukirudi wafuatao wajiandae; Mheshimiwa Moses Machali, Mheshimiwa Luhaga Mpina, Mheshimiwa Sara Msafiri, Mheshimiwa Wenje, Mheshimiwa Betty Machangu, Mheshimiwa Esther Matiko, Mheshimiwa Nasibu Omar na Mheshimiwa Hokororo na wengine watatajwa wakati huo.

Kwa hiyo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wakati tunasitisha shughuli za Bunge niliwataja wafuatao kwamba watachangia; Mheshimiwa Moses Machali atafuatiwa na Mheshimiwa Luhaga Mpina, baadaye Mheshimiwa Sara Msafiri. Mheshimiwa Moses!

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa nami nichangie Muswada ulioko mbele yetu, Muswada wa Sheria ya Baraza la Vijana la Taifa.

Mheshimiwa Spika, kimsingi nimepitia Muswada huu kwa kina na kuona pengine yako mambo ambayo yanahitaji kuweza kufanyiwa marekebisho ili kuhakikisha kwamba tunakuwa na Baraza bora ambalo linaweza likawa ni huru katika kuzungumza mambo mbalimbali ambayo yanawahusu vijana na changamoto mbalimbali ambazo zinawakabili.

Mheshimiwa Spika, changamoto ya kwanza ambayo inajitokeza katika Muswada huu; na nilikuwa kwenye Kamati ambapo Waheshimiwa Wabunge ambao walikuwa wana majedwali ya marekebisho, kuna mambo kadha wa kadha ambayo yamejitokeza mojawapo ikiwa ni namna ya kuwapata Wajumbe wa Baraza, kwa maana ya hasa kwenye ngazi ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, pia imejitokeza *concept* ya kwamba wengine wana mitazamo kwamba kuwepo na Mabaraza mpaka kwenye vijiji lakini pia kuwepo na mpaka kwenye Kata. Sasa swali linakuja, ni namna gani ambavyo tunaweza tukawapata vijana ambao watakuwa ni Wajumbe wa Mabaraza ya Vijana, lakini pia ni Wajumbe wa Mabaraza ya Wilaya? Bado kuna *contradiction*. Ukisoma Muswada huu, hautoi jibu kamili.

Mheshimiwa Spika, sasa ushauri wangu ni nini? Nilikuwa nashauri, ni vyema tukawa na Mabaraza ya Wilaya kama Muswada ambavyo unapendekeza, lakini pia tukawa na Mabaraza ya Mikoa lakini pia Baraza la Taifa. Hawa Wajumbe wa Baraza la Wilaya wasiwe 30 kama ambavyo Muswada unajaribu kutueleza Waheshimiwa Wabunge leo hii, badala yake ni vyema tukawa na *representation.*

Sheria itamke kwamba tuwe na Wawakilishi kutoka katika kila Kata kama katika kila Kijiji itashindikana. Tuwe na wawakilishi kutoka katika kila Kata ambao wataingia kwenye Baraza la Wilaya, ambalo litakuja kuwachagua Wawakilishi wa Wilaya kwenye Baraza la Mkoa na Baraza la Mkoa litatupatia Wajumbe wa kwa ajili ya Baraza la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama tutakwenda na mtazamo wa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge ambao wanasema tuwe na Baraza mpaka kwenye Kata, swali linabaki pale pale, tunawapataje hawa? Je, labda tuwapeleke kwenye Mkutano Mkuu wa Vijiji na Mitaa kwenye Serikali za Mitaa watu wafanye *application* kule kisha wapigiwe kura? Inawezekana pia usiwe ni utaratibu ambao ni mzuri.

Mheshimiwa Spika, nafikiri siyo jambo baya tukipanua kwamba Mabaraza haya yakaweza kufika mpaka kwenye Kata au yakaenda mpaka kwenye vijiji, sina tatizo na suala hilo. Lakini lazima tuangalie pia suala la gharama, je, tuko kwenye *position* ya kusema kwamba kama Taifa pengine tuwe na Mabaraza haya mpaka kwenye Vijiji, au mpaka kwenye Kata haraka haraka, au inabidi twende hatua kwa hatua?

Mheshimiwa Spika, leo tukomee kwenye Wilaya na pengine tunaweza tukajitathmini kadiri ambavyo tunaenda halafu baadaye tunaweza tukaona kwamba labda ipo haja sasa pengine twende kwenye Kata halafu twende vijiji.

Mheshimiwa Spika, nikubaliane na Muswada kwamba tukomee kwenye Wilaya, lakini utaratibu wa kuwapata Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Wilaya watoke katika kila Kata kama siyo katika kila Kijiji. Tukifanya hivyo, inawezekana. Lakini sasa je, hata hivyo hawa Wawakilishi ambao watakuja kuwa ni Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Wilaya tutawapataje?

Mheshimiwa Spika, nimejaribu kuangalia kama ambavyo nisema mwanzoni, Muswada haujaweza kutoa majibu tutawapataje. Vinginevyo twende kwenye Mikutano Mikuu ya Vijiji pamoja na Mitaa, kwa maana ya Halmashauri za Miji, Manispaa na Majiji.

Nadhani ipo haja tuongeze kwenye Muswada wetu kifungu katika Muswada huu ambacho kitatoa fursa Serikali ianzishe asasi moja ya kiraia, iwe asasi moja. Huu utaratibu wa kuwa na asasi sijui unasikia labda Mheshimiwa Juma Nkamia ana *NGO* yake huko, unasikia Mheshimiwa Machali, nami nina *NGO* yangu, yupo sijui Mheshimiwa Said Mtanda ana *NGO* yake; kwanza *NGOs* hizi hazipo katika vijiji vyote. Viko vijiji unaweza ukaenda usizikute hizi asasi za kiraia.

Mheshimiwa Spika, ikiundwa asasi moja ya kiraia kwa ajili ya vijana, iwe *dedicated* kwa ajili ya vijana, vijana wapewe fursa ya kuweza kujiunga, iwe ni kama chama chao, lakini ni *NGO,* kule kupitia asasi ile, ndipo vijana hao wanaweza wakawa wanachaguana kwenye *level* kama ni za vijiji au ni kwenye *level* ya Kata, wakikusanyika wale wanachama katika Mkutano Mkuu wao wa Kata au wa Kijiji watachaguana ili kuweza kupata *representatives* ambao watakwenda kwenye Baraza la Wilaya. Tukifanya hivi kama tutakuwa na asasi moja ya kiraia kuliko kuwa na utitiri wa asasi mbalimbali za vijana, najua inawezekana zikaja zikafunguliwa nyingine, *briefcase NGOs* kwa sababu ya maslahi yao binafsi.

Sasa bahati mbaya hata hili wazo nimekuja kulipata wakati tukiwa kwenye Kamati, hata kwenye Jedwali la Marekebisho sikuweza kufikiri kitu cha namna hii. Wanasema unapokusanyika na watu wakati mwingine unajifunza

mambo mengine. Lakini naona kwamba ni wazo la msingi ambalo linaweza likatusaidia kuweza kutatua kitendawili ambacho kimeshindwa kujibiwa na Muswada ambao uko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, pengine kiti chako kinaweza kikafikiria kuona kwamba tunafanyaje kuweza kutoka hapa ambapo tumenasa kuliko kuwa na utitiri wa asasi mbalimbali za kiraia.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia Muswada huu, unajaribu kulifanya Baraza la Vijana kuwa kama ni *unit* ya Serikali au Idara ya Serikali ndani ya Wizara ambayo inashughulika na masuala ya vijana, jambo ambalo kwa mtazamo wangu naliona siyo sahihi sana. Tunahitaji kama Taifa kuwa na Baraza la Vijana ambalo ni huru, Baraza ambalo litakuwa huru katika kuhakikisha kwamba linapokuwa linatekeleza majukumu yake, litajadili mambo mbalimbali, changamoto mbalimbali ambazo zinawakabili vijana, changamoto za ajira na kadha wa kadha.

Mheshimiwa Spika, sasa leo nimesoma kwenye Muswada inaonesha kwamba Mkutano Mkuu wa Taifa utakapokusanyika, utalazimika kupendekeza majina matatu ili kusudi katika yale matatu Waziri mwenye dhamana na masuala ya vijana ndiye amteue Mwenyekiti wa Taifa. Hili jambo halijakaa vizuri.

Mheshimiwa Spika, athari ambazo zitatokana na mfumo huu wa kumpata Mwenyekiti wa Baraza hilo, hali kadhalika na kumpata Katibu Mtendaji, au Katibu wa Baraza la Vijana ni kwamba huyu Mwenyekiti hatakuwa na sauti kwa Waziri wakati mwingine kuweze ku-*critic* kwenye *issues* ambazo wanaona hawakubaliani na mtazamo au na mlengo wa Waziri na baadhi ya Watendaji wa Wizara.

Kwa hiyo, tunashauri, wengine tumependekeza kwenye Jedwali la Marekebisho, tunataka kuona Mwenyekiti anachaguliwa na Baraza la Vijana kupitia Mkutano Mkuu moja kwa moja. Haya masuala kwamba wao wanamwona mtu fulani anafaa, halafu watoke ndipo aende akateuliwe na Waziri, hili jambo siyo sahihi sana. Ni sawa sawa leo hii sisi Waheshimiwa Wabunge hapa tumekusanyika, wakati tunamchagua Spika, labda tupendekeze majina matatu ya kumpaka Spika, kisha labda tumpelekee Rais ndipo aseme sasa mimi ninamtaka huyu. Hii *philosophy* inakuwa bado haijatulia.

Hali kadhalika kwenye nafasi ya Katibu, inapendekezwa pia hivyo hivyo kama ambavyo imependekezwa kwa Mwenyekiti. Naomba kwa nafasi ya Katibu kwa sababu huyu ni Mtendaji, Baraza baada ya kuwa limempata Mwenyekiti, litangaze nafasi ya Katibu Mtendaji. Watu mbalimbali kutokana na *qualifications* ambazo zimeainishwa na Baraza waombe. Watakapoomba,

watachujwa kwanza huko chini na kutokana na utaratibu ambao wamejiwekea, halafu labda kama ni majina matatu yataingizwa kule, waende wakajieleze kwenye Baraza, Baraza limchague mtu mmoja.

Mheshimiwa Spika, huu utamaduni wa kusema kwamba Baraza lipendekeze majina matatu kupeleka kwa Waziri, bado tunamnyima nguvu huyu Katibu Mtendaji, na hiki chombo tunazidi kukifanya kwamba ni sehemu ya Serikali, wakati tulikuwa tunahitaji tuwe na Baraza la Vijana ambalo litakuwa *independent*. Tuhakikishe tu kwamba kuna *linkage* baina ya Baraza hilo pamoja na Serikali ili kuhakikisha Serikali ita-*facilitate* na ku-*coordinate* mambo yote ambayo yanahusiana na masuala ya *finance*. Utaratibu huu utalikosema Baraza kutokuwa huru. Haya yamekwenda tukiangalia baadhi ya vifungu, hata hivyo hivyo kule Mikoani, kuna kama *element* ya Waziri atafanya, sijui nani atafanya.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Mengine nitazungumza wakati Bunge limekaa kama Kamati. Ahsante.

**SPIKA:** Leo umejadili Muswada, tunashukuru sana. Leo umejadili Muswada! Mheshimiwa Luhaga Mpina, atafuata Mheshimiwa Sara Msafiri. *(Makofi)*

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Nami nianze kwa kuchangia moja kwa moja. Nilikuwa naangalia hapa kwenye *funds of the council.* Chanzo cha mapato cha hili Baraza la Umoja wa Vijana, nimeona chanzo kikubwa inategemea hasa bajeti ya Serikali pamoja na *Local Government*, kwa maana ya michango inayotokana na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, lakini maeneo haya ndiyo maeneo ambayo mara nyingi yamekuwa hayatoi fedha kwenye taasisi zake na kwenye Wizara zake, ni kama maeneo ambayo yalishazidiwa.

Kwa hiyo, hofu yangu kubwa, nimevipitia pia vipengele vingine ambavyo vitaliwezesha Baraza hili kupata fedha. Sioni kipengele ambacho kitakuwa cha uhakika zaidi wa upatikanaji wa fedha wa Baraza hili. Kwa hiyo, itakuwa sawa na taasisi nyingine ambazo tumeziunda kwa mategemeo makubwa na nguvu kubwa lakini zimeshindwa kufanya kazi kwa sababu ya ukosefu wa fedha. Kwa hiyo, hiyo ni changamoto kubwa.

Mheshimiwa Spika, mfano, sasa hivi mapato ya Halmashauri sasa hivi yamekuwa yakiingiliwa na Serikali kila wakati. Serikali imekuwa ikitoa maelekezo kila wakati hata bila kuzingatia msimu wa bajeti, kama msimu wa bajeti umefikiwa. Naweza kutolea mfano, Serikali kwa mfano sasa hivi sisi tunaokusanya ushuru wa pamba, fedha zote za ushuru wa pamba tumelipwa

mpaka sasa hivi asilimia 16 tu kutokana na maelekezo ya Serikali ya kukataa kwamba fedha hizo Halmashauri zisikusanye, na badala yake itakusanya Wizara au Bodi ya Pamba, matokeo yake fedha hizo mpaka leo hatujalipwa na hatujafanya chochote.

Mheshimiwa Spika, tulipendekeza mambo mengi sana kutekeleza kupitia bajeti yetu, kwa maana ya Halmashauri, lakini mpaka sasa hivi hiyo bajeti mpaka inakutwa na bajeti nyingine na fedha hizo Serikali haijatupatia, mwaka wa fedha unafika mwisho, hatujapata fedha. Sasa hata kama ungekuwa na *commitment* ya kuchangia kwenye Baraza kama hili, na kama wabunge wengine ambavyo wamelalamika juu ya kuchangiwa kwa asilimia tano, huwezi kuchangia kwa sababu Serikali mara nyingi sana imekuwa ikiingilia mapato yanayotokana na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, natumia nafasi hii kwamba Serikali iache kabisa kuingilia mapato ya Serikali za Mitaa. Serikali za Mitaa ziachwe zifanye kazi zake kama zinavyotakiwa kufanya, lakini vilevile fedha yetu ya ushuru wa pamba Serikali itulipe haraka sana ili tuweze kuendelea na shughuli nyingine za maendeleo pamoja na kuhakikisha kwamba vijana wetu wanapata fedha katika maeneo ya shughuli ambazo wanajiendesha.

Kwa hiyo, tahadhari yangu katika kifungu cha 22 ni kwamba lazima tutafute uhakika zaidi wa fedha ili kuliwezesha hili baraza liweze kufanya kazi sawa sawa.

Mheshimiwa Spika, nimeangalia pia kwenye kifungu cha 6; zile *functions of the council*, nilivyozipitia nikaona kwamba bado kuna *function* moja ambayo ni muhimu sana ambayo ilitakiwa kuwekwa, kwamba shughuli za vijana hizi zimetawanyika kwenye sekta mbalimbali. Ziko elimu, afya, ujenzi, miundombinu, mawasiliano, zimetawanyika kwa ujumla wake. Kwa hiyo, ni lazima tuwe na kifungu ambacho hii *council* sasa itahusika kuziangalia sheria zetu, itahusika kuziangalia sera zetu tulizonazo ambazo zinawasaidia vijana kwa maana ya kupata ajira, zinawasaidia vijana kwa maana ya kupata kazi.

Mheshimiwa Spika, nitatolea mfano. Sasa hivi tatizo kubwa hata tungeanzisha *council*, Baraza hili lote, shughuli za vijana na shughuli za ajira kwa ujumla katika Taifa hili zimekaa vibaya, kwa maana ya sheria zetu. Mfano naweza kutolea tu Sheria ya Manunuzi. Sheria ya Manunuzi sasa hivi inatoa ukomo wa Shilingi bilioni kumi kuruhusu kutangaza *tender* ya Kimataifa, hilingi bilioni kumi, nilisema hata huko nyuma.

Mheshimiwa Spika, kikomo hiki ni kidogo sana. Ilitakiwa kiongezwe kikomo cha kuajiri *tender* ya Kimataifa, *at least* kuanzia hata kwenye shilingi bilioni 50, ndiyo sasa unaweza ukasema kwamba tutangaze tenda ya Kimataifa ili

kuwezesha vijana wengi kupata ajira, kwa maana ya tenda nyingi sana za ujenzi wa barabara, ujenzi wa majengo na ujenzi wa miradi ya maji wangepata vijana wetu wakandarasi walioko hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, lakini sasa unakuta kazi zote hizi tunaziuza kwa watu, bajeti yetu inachukuliwa yote kwenda nje, vijana wetu wanabaki hawana ajira. Taifa kwa sasa lina tatizo kubwa sana la ajira, ni lazima sheria zetu tuzirekebishe.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, nchi haina haina *local content* (uzingatiaji wa wazawa), haina! Sasa mambo haya lazima Baraza kama hili liwe ndiyo jicho la kuionesha Serikali kwamba hapa kuna tatizo. Je, vijana wa Tanzania wamezingatiwa vipi kwenye madini? Inatosha tu kwamba mkigundua leo madini hapa, anakuja mwekezaji anachukua ardhi, anachukua madini, anawekeza na vijana wengine wote wanaozunguka eneo hili na Watanzania wanakosa ajira kwenye maeneo hayo. Inatosha hiyo? Lazima liwepo jicho ambalo litakuwa linaonesha kwamba hapa maslahi ya vijana lazima yazingatiwe; na maslahi hayo yazingatiwe basi na Muswada wetu huu.

Mheshimiwa Spika, tuna ugunduzi wa gesi, kubwa kabisa, gesi, mafuta yanagunduliwa, je, uzingatiwaji wa wazawa ambao ndio vijana wetu wanaotakiwa kushiriki kwenye uchumi, wamezingatiwa vipi katika ugunduzi huo? Au ndiyo hivyo hivyo, tunaita *Statoil,* tunamkabidhi mgodi mzima wa gesi halafu Watanzania wanahangaika, wanatembea nchi nzima mpaka viatu vinakwisha, hakuna ajira wakati nchi yao ni tajiri, ina gesi lakini inavunwa na kufaidika na Watanzania wanaotoka nje.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni lazima kifungu hiki kiwekwe ili kuhakikisha kwamba sasa hili Baraza la Vijana, kazi yao kubwa isiwe ku-*promote* tu, lazima wa-*review laws* na *policies* ambazo zina-*affect* maendeleo ya vijana. Kwa hiyo, naona kifungu hicho ni muhimu sana kiweze kuwekwa.

Nimeona kwenye kifungu cha sheria hiki kwamba kuna tafiti mbalimbali ambazo zitakuwa zinafanywa, nami nakubaliana hizi tafiti zifanywe. Kwa mfano, mpaka sasa hivi hakuna jicho lolote lile la nchi ambalo linaionesha; na kutoka Wizara ya Ajira na kwenye Tume ya Mipango sijawahi kuona. Wametuonesha, kwa mfano sasa hivi vijana wetu wanapokwenda kusoma Chuo Kikuu, nani anayewaonesha kwamba *labour market demand* sasa hivi inasema nini? Ma-*engineer* wangapi wanaohitajika katika Taifa? Wanasayansi wangapi wanaohitajika katika elimu ya madini? Hakuna mahali popote.

Mheshimiwa Spika, vijana wanakwenda kusoma tu, hakuna mtu anayewapa dira kwamba lazima sasa waende wakasome hiki, kwa maana ya kwamba soko la ajira lina nafasi. Matokeo yake, wanasoma kozi ambazo mwisho wa siku wanatembea kutafuta ajira, hakuna mahala pa kuipata ajira

kwa sababu hakuna mahala popote palipoandikwa panapoonyesha kwamba sisi kama Taifa tuna nafasi za ajira hizi; mtu akisoma ukisomea udaktari kuna uhakika wa kuajiriwa siku hiyo hiyo umemaliza. Matokeo yake vijana wetu wanasomea *Business Administration, Political Science,* mwisho wa siku *degree* zile wanatembea nazo hakuna ajira.

Mheshimiwa Spika, mbaya zaidi, taasisi na mashirika yetu pamoja na Makampuni ya nje wanaajiri watu kutoka nje kwa sababu ndio walio na hizo *professions*. Sisi hapa tunabaki, vijana wetu wanakosa ajira na tumewasomesha kwa gharama kubwa na mikopo juu, lakini hatujaweza kuwaelekeza wasome kitu gani. Kwa hiyo, hilo ni jambo la msingi sana kuona kwamba *labor market demand* na vijana kwa sababu sasa wanapata Baraza lao, lazima litunze hizi takwimu za kuonyesha kwamba wasome wapi na wafanye nini kulingana na mahitaji ya soko la ajira linavyowaeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa limezungumzwa suala lingine zuri la kuunganisha, kwamba hili Baraza litakuwa kiungo kikubwa sana na Mabaraza mengine duniani na Afrika. Ukienda kwenye Bunge la Afrika utaikuta *caucus* ya vijana ambapo tupo mle vijana, nami kijana wenu mliyenituma kwenda kule nipo kwenye lile Baraza la Vijana tunapanga mambo ya vijana wa Afrika na changamoto zao. Sasa Baraza letu litakuwa kiungo kikubwa sana na *caucus* kama hizo za Mabunge ya Africa, *SADC* pamoja na duniani kwingine kote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vijana walio wengi wametawanyika kwenye *diaspora*…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Sara Msafiri, atafuatiwa na Mheshimiwa Wenje.

**MHE. SARA M. ALLY:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii nami niweze kujadili Muswada uliokuwa mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kutoa pongezi kwa Serikali kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kuleta Muswada huu mbele yetu leo.

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu tangu kuundwa kwa Sera ya Vijana ya Taifa mwaka 2006 sasa hivi ni miaka nane ambapo sera ilitamka kwamba kutakuwa na Baraza la Vijana litakaloshughulikia masuala ya vijana na hili Baraza litakuwa Kitaifa. Kwa hiyo, miaka nane imeshapita, leo ndiyo tunaletewa huu Muswada.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali pamoja na kuchelewa, lakini nawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba Muswada huu kwa njia yoyote ile lazima upite tu.

Mheshimiwa Spika, muda mrefu sana vijana walikuwa kwenye makundi mbalimbali ili waweze kupata jukwaa la kuongelea masuala yao. Kwa mfano, utawakuta vijana kwenye vyama vya siasa au kwenye madhehebu ya dini, wana umoja wao na kwenye klabu za michezo. Wanakwenda kule, pamoja na kushiriki katika shughuli kama za kisiasa, lakini kupata fursa ya kupata jukwaa la kusema mambo yao. Kwa hiyo, nasema kwamba kupitia Baraza la Vijana ndiyo litakuwa ni jukwaa ambalo tukiwa na *structure* au muundo mzuri, litatusaidia kutatua matatizo ya ajira kwa vijana, litatusaidia kutafuta mikopo kwa vijana, tutapata ufumbuzi wa jinsi vijana watakavyopata taarifa mbalimbali za kisiasa, kiuchumi na Kimataifa kupitia jukwaa hili. Kwa hiyo, nasema hili Baraza ni la muhimu na ni lazima Muswada huu upite.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo, ukiangalia kwenye Kifungu cha 18 kuhusu Mkutano wa Vijana wa Wilaya, utaona kwamba kuna vijana watano ambao wanachaguliwa na ni Wawakilishi na sifa zake zimetajwa kwamba ni lazima wawe wanatokana na taasisi zilizokuwa kwenye Wilaya na vilevile ziwe ndani ya Wilaya ile ile.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono Muswada kwa sababu moja tu, lazima hiki chombo kiwe na sura ya Kitaifa ili isije ikatokea kwamba wanatokea vijana labda wanatoka mjini wanaunda taasisi kwenye maeneo ya pembezoni wanakwenda huko wanajisajili kama wametoka Ulanga au Kilombero kumbe ni vijana wametoka tuseme ni Dar es Salaam au maeneo mengine kutokana na jinsi watakavyochangamkia fursa hiz,i wakawanyima fursa vijana waliokuwa pale.

Mheshimiwa Spika, kwa vile hizi nafasi ni za uwakilishi kwenye Mkutano, nashauri hiki kifungu cha tatu kibaki hivi hivi kwamba ni lazima wawe Wawakilishi kutoka taasisi za vijana. Kwa sababu wao tayari wana mwamko, wanashughulikia masuala yanayohusu vijana. Kwa hiyo, unawakuta kabisa wanajenga picha ya kuwawakilisha vijana kwa sababu tayari wanashiriki kwenye hizo shughuli, kuliko kutafuta kijana yeyote tu kwa vile anatoka kwenye ile Wilaya.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa sababu hiki ni chombo na wanaingia kwenye vikao hivi ambavyo vinafanya maazimio na kusimamia utekelezaji, lazima wawe na *address,* tujue tunawapataje hawa vijana. Kwa mfano, tuseme unatoka Mvomero, wewe kwa vile ni kijana wa Mvomero, unataka kuwa mwakilishi. Tutakupataje tukitaka kuitisha Mkutano? Unafanya shughuli gani za

vijana ambazo zitatufanya tujue wewe ni *competent* kwenye *area* hii tuombe ushauri kwako? Kwa hiyo, wale ambao moja kwa moja wanashiriki kwenye masuala ya vijana na wana taasisi zimesajiliwa, zipo rasmi, ni rahisi kuwawakilisha vijana kutoka kwenye ile Wilaya. Kwa hiyo, naunga mkono.

Mheshimiwa Spika, jambo ambalo nashauri, ni lazima sasa utengenishwe uwakilishi wa vijana kwenye mikutano iwe kwenye ngazi za Wilaya, Mkoa au Taifa na uanachama wa kijana kujiunga na Baraza. Kwa sababu kila kijana ana sifa ya kuwa mwanachama, lakini kila kijana anaweza kukosa sifa za mwakilishi kwenye mkutano.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sasa chombo kinapoundwa, ni lazima kuwe na uhuru, kijana ajiunge na awe mwanachama kwenye Baraza. Hata yale masuala ya kusimamia sera na utekelezaji na taarifa zake, hawa vijana waliokuwa nje ambao hawana taasisi, bado wanataka hiyo fursa ya kujua kinachoendelea kuhusu maslahi yao na maisha yao na hatma ya vijana.

Kwa hiyo, bado hivi vyombo vinavyoundwa, kama ni mikutano ya Wilaya au Mikoa, viongozi ni lazima wawajibike kushuka kwenye Vijiji na Kata kwa sababu wawakilishi ni wachache, wakaelimishe wenzao, wakatoe taarifa, hatma ya mikutano waliyoifanya na maazimio waliyofikia kuhusu vijana. Kwa hiyo, lazima kuwe na uanachama na uwakilishi kwenye mikutano, kuwe na sifa zijitenganishe. Nimesoma Muswada nimeona hakuna kutenganishwa kati ya uwakilishi kwenye mkutano na sifa za kuwa mwakilishi na sifa za kijana kuwa mwanachama. Hii itanyima fursa ya kutafuta vyanzo vya fedha.

Mheshimiwa Spika, tukiwa na wanachama watalipa *fees* ya uanachama. Hata *clubs* za michezo, tunalipa *fees* ya uanachama, hata kwenye vyama vya siasa tuna uanachama; kila taasisi ikiundwa kuna uanachama na unalipia ada. Sasa tunajinyima wenyewe vyanzo vingine vya mapato kwa kung'ang'ania tu kwamba ni lazima utokane na taasisi.

Mheshimiwa Spika, vijana tupo milioni 16, hatuwezi wote tukianzisha *NGO* leo kuwa na sifa ya kuchaguliwa kuwa kwenye uwakilishi wa kwenye mikutano. Kwa hiyo, lazima uanachama na uwakilishi utenganishwe.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 19 kinasema kwamba Mwenyekiti wa Bodi atateuliwa na Mheshimiwa Rais. Hiyo sina tatizo, lakini naomba Mwenyekiti wa Baraza la Vijana la Taifa ateuliwe na Wajumbe. Kwa sababu yeye kazi yake, anatokana na Wajumbe.

Kwa hiyo, Katibu Mtendaji ndiyo atokane na Serikali. Katibu ndiyo anakuwa *link* kati ya Serikali na vijana, lakini Mwenyekiti yeye ndiye anabeba bendera au sura ya lile Baraza. Haiwezekani ateuliwe tena na Serikali. Katibu

ateuliwe na Serikali, Mwenyekiti ateuliwe na Serikali, ile Bodi ukiiangalia yote ina sura za Serikali. Kwa hiyo, haiwezekani, ni lazima kuwe na *checks and balance*. Lazima kuwe na uhusiano kati ya vijana waliokuwa nje ambao hawapo kwenye Serikali na wale watakaopata fursa.

Mheshimiwa Spika, nashauri kwamba hawa watendaji, nafasi zitangazwe vijana wenye sifa waombe, nami naona wapo. Kwa mfano, sasa hivi tuna Maafisa vijana kwenye Wilaya na Mikoa. Wale wanaweza, kwa sababu hiki chombo kikianzishwa nina hakika ule mfumo wa kwanza utakufa tu. Sasa hawa ndiyo wawe *accommodated* kwenye huo mfumo mpya, ambao wanajua masuala ya vijana na kule ambapo hakuna *human resources,* nafasi zitangazwe ili vijana waombe. Lakini naomba Mwenyekiti nafasi yake lazima agombee na achaguliwe.

Mheshimiwa Spika, kitu kingine nilichotaka kuongelea ni masuala ya ajira. Hiki chombo kama tunakiunda, ni lazima kitegue kitendawili cha ajira kwa vijana. Hatuwezi tukasimama hapa kila siku tunalinda ajira za ndani tu kwamba wageni wasiingie, tujiajiri sisi wenyewe Watanzania. Soko la Ajira la Dunia halisemi hivyo. Anayeajiriwa ni yule mwenye sifa. Kwa hiyo, tukiwa na chombo kama hiki sasa kitatusaidia, kama je, wanahitajika vijana wenye *skills* zipi? Je, huko kwenye nchi za wenzetu tunataka tupeleke ajira kwa vijana wenye utaalamu upi? Je, wanahitaji madaktari huko Zimbabwe, wanahitaji madaktari *South Africa,* wanahitaji wataalamu wa *counseling*? Hiki chombo ndiyo kazi yake.

Kwa hiyo, nasema kwamba hiki chombo kisiwe cha kutoa maelekezo tu, kwa sababu ukisoma *structure* nzima iliyokuwa pale, unaona Baraza la Vijana la Taifa ndiyo linafanya kazi, lakini ukipita kwenye Mikoa na Wilaya, wanapewa maelekezo kutekeleza yale waliyoazimia kwenye Taifa tu. Lazima kuwe na utaratibu, huyu Mwenyekiti au Katibu kama ni wa Wilaya, Baraza la Wilaya, kuwe na utaratibu nao waingie kwenye vikao vya Serikali kwenye uwakilishi. Kwa mfano, kwenye *RCC,* kule ndiyo tunakotengeneza picha ya bajeti ya Mkoa mzima. Hawa vijana wana mambo yao kwenye Mkoa! Sasa lazima kama ni Mwenyekiti au Katibu awe na yeye ni mwakilishi aingie kwenye vikao ili aweze kutetea maslahi ya vijana na aangalie, je, yale yaliyoelezwa na vijana yametekelezwa na yapo kwenye mpango? Kwa sababu ni lazima masuala ya vijana yaingie nayo kwenye mipango ya Taifa, yasiwe tu yanakaa yanakuwa kama chombo cha kisiasa. Lazima kiangalie maeneo mengine na fursa nyingine.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba sana suala la Mwenyekiti iwe ngazi ya Wilaya, Mkoa au Taifa lazima achaguliwe, lakini Katibu atokane na utendaji kwa sababu yeye ndiye anasimamia na kuratibu masuala yote, lakini Mwenyekiti yeye ni lazima achaguliwe.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Sasa nitamwita Mheshimiwa Wenje atafuatiwa na Mheshimiwa Betty Machangu, atafuatiwa na Mheshimiwa Esther Matiko, lakini simuoni.

**MHE. EZEKIEL D. WENJE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa fursa hii nami niweze kuchangia katika huu Muswada unaounda Baraza la vijana katika Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, naomba kusema kwamba jana nilikuwa namwangalia mtumishi wa Mungu Dkt. Mazman Row ambaye ni Marehemu hivi sasa, katika hotuba yake moja alisema maneno yafuatayo; "*great leaders invest in people, not in buildings.*" Kwamba viongozi mahiri wanawekeza katika watu, siyo kwenye majengo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nini nimesema hili? Utanielewa kadri ninavyozidi kuchangia kwa nini nimeanza na neno hili.

Mheshimiwa Spika, kazi ya Bunge hili tulilonalo ni kutunga sheria na siyo kupitisha sheria. Hili Bunge kazi yake ni kutunga sheria na hizi sheria siyo lazima ziletwe kutoka Serikalini kila siku. Hili Bunge *is just a rubber stamp Parliament*. Tunapitisha sheria zinazoletwa na Serikali kila siku.

Mheshimiwa Spika, unapoongoza taasisi kubwa kama hii ya Bunge, wewe kama kiongozi nategemea kwamba uta-*encourage,* yaani utachochea Wabunge wako wawe na ubunifu na fikra yakinifu, wawe *innovative, innovative*, uchochee *their thinking,* namna pekee ya kufanya hivyo ni ku-*encourage* walete *private Bills*, wa-*sponsor private Bills* ndani ya Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, ni aibu sana kwamba Mbunge wako John Mnyika amekaa chini akajifungia, akasoma kwa bidii, akatumia muda wake mwingi kusoma, akatengeneza Muswada wenye kurasa kadhaa, tena akatafsiri kwa Kiingereza na Kiswahili akaleta ndani ya Bunge, ikasomwa kwa mara ya kwanza, *only to be thrown out of the Parliament,* ikatupwa tu!

Mheshimiwa Spika, *what your chair have done, you killed;* umeua *innovative* ya Mheshimiwa John Mnyika. *You have killed his creativity!*

**SPIKA:** Soma Kanuni!

**MHE. EZEKIEL D. WENJE:** *You have killed his energy!*

**SPIKA:** Naomba ukae chini! Kufuatana na Kanuni *you can not attack the chair of the chair.* Kuna utaratibu wa kufuata. Kwa hiyo, naomba u-*withdraw* maneno yako yote! Siyo sahihi!

**MHE. EZEKIEL D. WENJE:** Mheshimiwa Spika, waliosoma wanasema,…

**SPIKA:** Naomba ujadili Muswada!

**MHE. EZEKIEL D. WENJE:** *"Telling the King that he has a bad breath, is not a sin, you are only trying to spare the King embarrassment in the public." That is what I am trying to do here.*

**SPIKA:** Kanuni hazikuruhusu!

**MHE. EZEKIEL D. WENJE:** Mheshimiwa Spika, na-*withdraw*!

**SPIKA:** *Thank you very much!*

**MHE. EZEKIEL D. WENJE:** Mheshimiwa Spika, naomba niweke msingi kwamba sishutumu kiti, lakini ninachosema ni kwamba ndani ya Bunge hili Waheshimiwa Wabunge wanapoleta *private members Bill,* hii ni sehemu ya kazi yao. Tunatakiwa tu-*encourage critical thinking* na ubunifu wa Wabunge wetu.

Mheshimiwa Spika, kwa kitendo hiki, nilikuwa naongea na Mheshimiwa John Mnyika ametoka ndani ya Bunge yuko *very down.* Nami naamini kwamba hatathubutu tena kutengeneza Muswada Binafsi. Hatathubutu tena! Kwa sababu amejitahidi, ametumia nguvu nyingi na maarifa na akili sana, akaleta ikasomwa mara ya kwanza, halafu ikapelekwa ikatupwa huko, *through back door in the name of* Kamati imekaa na wakakubaliana uletwe Muswada wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, ninachohoji ni kwamba hivi Serikali ilikuwa wapi mpaka wasubiri Mheshimiwa John Mnyika alete *Bill* ndiyo na wao walete ya kwao? *Where was the Government?* Tukisema Serikali inalala, mnasema eti tunatumia maneno makali dhidi ya Serikali!

Mheshimiwa Spika, kuna watu wengi wamesema humu ndani kwamba kuna watu wengi wameendesha harakati za kusaidia vijana. Nampongeza sana Mheshimiwa John Mnyika kwa sababu *he has worked the talk.* Watu wengi, yaani *they talk to the talk. They talk, talk and talk,* lakini Mheshimiwa John Mnyika *has worked the talk.* Kwa hiyo, hii ndiyo ina-*distinguish between* Mheshimiwa John Mnyika na hao watu wengine ambao walianzisha harakati miaka hiyo yote lakini hawakuwahi kuleta hata *Bill*.

Mheshimiwa Spika, kama hii ya Mheshimiwa John Mnyika haitoshi, Kamati ya Bajeti ilileta Muswada, akina Oscar, wale wanasheria, watumishi wa Bunge, wamefanya kazi kubwa ya kuandika Muswada; wameshatengeneza Muswada, ndiyo Serikali nao wanakuja, *through back door* na Muswada mwingine, ule Muswada ukatupwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nini unaruhusu haya? Kwa nini unaruhusu haya ku-*discourage energy* na *efforts* ambazo Waheshimiwa Wabunge wanaleta? *Their creativity, you are killing them! This is what I am saying. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika historia nimekaa hapa kwa miaka mitano ambayo Mungu ameniwezesha kukaa hapa. Miaka mitano hii nimegundua kwamba Bunge ambalo ni gumu mno ku-*sponsor private members Bill* ni Bunge la Tanzania. *Is quite frustrating!* Sasa sijui kwa nini tulikuja hapa! Hivi sisi tumekuja kupitisha sheria? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna hoja binafsi za Wabunge zililetwa humu, nakumbuka January Makamba alileta hoja kuhusu pango, ku-*regulate* masuala ya pango, hiyo hoja ilikwenda kwenye *dustbin* baada ya kuwa *tabled* hapo*, it went to the dustbin* na Bunge linakwisha. Mheshimiwa Zitto Kabwe alikuja na hoja hapa, *it went to the dustbin;* Mheshimiwa Nassari alikuja na hoja zote ziliwekwa kwenye orodha lakini *they went to the dustbin.*

Mheshimiwa Spika, hii *trend is killing us,* yaani hii ni kwamba hakuna Mbunge mwingine anayeweza kuthubutu kutengeneza *private members Bill.* Unaleta ya nini? Kwa hiyo, *I am very confident* ninaposema kwamba hili Bunge ndiyo moja ya Mabunge ya Afrika inayopitisha sheria, halitungi sheria. *You have turned us to be rubber stamps, which is not fair.*

Mheshimiwa Spika, *this Parliament, I must say is very incompetent under your watch. Very incompetent under your watch! And that is why* tunaleta *private members Bills* zinatupwa tu na unaona ni kawaida tu. *You have killed Honorable John Mnyika, I am telling you!* Ameondoka hapa *he is very down*! Labda umtafute leo um-*counsel what you have done to him*.

Mheshimiwa Mnyika anatengeneza *Bill* ya *45 pages,* mpaka anatafsiri kwa Kiswahili halafu mnarusha tu, mnaona ni kama karatasi ya kwenda kufungia vitumbua na mnaona ni kawaida tu, *this is unfair! You are discouraging our energy!* Hii siyo kwenye Bunge lako tu, hata kwenye Bunge la Tisa, Mheshimiwa Zitto Kabwe alileta Muswada wa Maadili, ilifia kwenye Ofisi ya Spika Mheshimiwa Sitta, anayejiita Spika wa Viwango…

**SPIKA:** Mheshimiwa Wenje, kwa nini unapenda kujadili watu?

**WABUNGE FULANI:** Ajadili hoja!

**MHE. EZEKIEL D. WENJE:** Mheshimiwa Spika, naomba nimwambie dada yangu Mheshimiwa Ghasia kwamba *sometimes is better to be quite to be thought a full than to speak and clear the doubt*.

Mheshimiwa Spika, naomba niendelee!

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa John Mnyika ametengeneza *Bill*, Serikali imekuja na *Bill* kwa *certificate of urgency,* yaani hati ya dharura. Hotuba ya Kambi ya Upinzani inasema kwamba kilichofanywa na Serikali ni *copy and paste* kwenye *Youth Bill* ya Kenya ambayo ni aibu nyingine. *What was the need of the rush?* Mlikuwa mnakimbilia wapi? Mimi nilitegemea kama mlikuwa na mawazo mbadala, mngechukua *Bill* ya Mheshimiwa John Mnyika, na hayo mawazo yenu, halafu mkafikia *consensus* ikaletwa *Bill* ambayo ina *consensus.* Mnakwenda mnachukua *Bill* ya watu, mna-*copy* na ku-*paste* halafu mnakuja hapa mnapiga kifua kwamba eti Serikali ina ubunifu. *What is this?* Huwezi *creativity! (Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Nilifikiri nimekupa nafasi unachangia, kumbe unasema sema tu.

Waheshimiwa Wabunge, haya aliyoyasema Mheshimiwa Wenje, yote hayana msingi na wala hakuwa na hoja kwa sababu kufatana na kifungu 21 cha Kanuni zetu, kinasema hivi:-

*"Kutakuwa na Mshauri Mkuu wa Bunge wa Mambo ya Sheria ambaye atakuwa ni Msaidizi Mkuu wa Katibu Mkuu kwa maswali yote yanayohusu Sheria. Pamoja na kazi nyingine Mshauri wa Bunge wa Mambo ya Sheria atashughulikia mambo yafuatayo: moja, ni kutoa ushauri wa kisheria kuhusu Miswada yoyote ya Sheria inayowasilishwa Bungeni; kuchambua Miswada ya Sheria inayowasilishwa Bungeni; na kuwasaidia Wabunge kupata uelewa sahihi wa Miswada hiyo; kutoa ushauri kwa Mbunge kupitia Kamati ya Kanuni za Bunge kuhusu marekebisho yoyote yanayohitajika kufanyika katika Kanuni za Kudumu za Bunge; kutoa huduma za ushauri wa kisheria kwa Kamati za Bunge na Wabunge kila inapohitajika kufanya hivyo; kuandaa Miswada ya Sheria ya Kamati, Miswada binafsi ya Sheria na hoja binafsi za Wabunge."*

Kwa hiyo, nimeunda kitengo hicho na siyo kuleta hoja Mbunge Binafsi au Kamati au nini ili mradi kuleta. Kuna taratibu zake na taratibu zote ni lazima zifuatwe. Hatuwezi kuwa kwa sababu tunataka kuonekana tunagonga nini, basi tunaleta tu utaratibu. Sisi tuna kitengo na ni lengo letu kuimarisha kitengo hiki kusudi haya anayoyasema Mheshimiwa Wenje yafanyike. Sasa lawama zitatoka wapi?

Tunaendelea na Mbunge anayefuata. Kengele iligonga. Mheshimiwa Betty Machangu, atafuatiwa na Mheshimiwa Esther Matiko, halafu atafuata Mheshimiwa Nassib Omar.

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Muswada huu wa kuweka mamlaka na kazi ya Baraza la Vijana. Naomba niwaambie Wajumbe wenzangu kwamba Mabaraza ya Vijana hayakuanza leo, yalianza miaka ya zamani, kwa mfano Afrika ya Magharibi, zilizokuwa Jumuiya za Koloni la Wafaransa nchi za Afrika ya Magharibi mwaka 1950. Mabaraza haya yalikuwa yanasimamia maendeleio ya kilimo katika hizo nchi, maendeleo ya afya na maendeleo ya mambo yote ambayo yaliyoonekana ni ya kusaidia wananchi kijamii na kiuchumi.

Kwa hiyo, siyo kwamba leo Tanzania tunaanza Baraza, basi inakuwa kwamba ni sisi tumeanza. Lakini pia mwaka 1997 aliyekuwa mwasisi wa nchi ya *South Africa* Mheshimiwa Nelson Mandela, Baraza la Vijana pia lilianza na lilikuwa pia lina sababu hizo za kusimamia, asasi zote za vijana kwa ajili ya kuangalia kwamba wanatekeleza Sera ya Maendeleo ya Vijana katika ile nchi.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwamba ni wakati muafaka wameleta hii, ni kweli kwamba itasimamia Sera ya Maendeleo ya Vijana na tuna uhakika kwamba kama itatekelezwa vizuri kutakuwa na maendeleo, kutakuwa na tofauti katika hali ilivyo sasa hivi. Idadi ya vijana duniani ni kubwa. Sasa hivi ukiangalia asilimia 60 mpaka 70 ni vijana na kuna matatizo makubwa sasa hivi ya ajira duniani kote. Kwa mfano, *South Africa* kuna ukosefu wa ajira kwa asilimia 25.6, Spain 26.9, Kenya kwa mwaka 2013 ilikuwa mpaka asilimia 40 ya ukosefu wa ajira na Tanzania tuko asilimia 12.9.

Kwa hiyo, naamini kabisa uanzishwaji wa hili Baraza utasaidia sana kwenye nyanja kama ukosefu wa ajira, namna ya kupata ajira, kitu gani kifanyike ili kijana ajiinue kiuchumi. Siyo lazima ajira ya ofisini, lakini zinaweza kuwa pia ni ajira nyingine za kiuchumi kama Kilimo Bora.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwa Serikali ni katika kifungu kile cha 10(2). Ukiangalia kifungu hiki, kwanza nikianza na kile kifungu cha 4(3) kinasema, "*membership of the Council shall be open and voluntary to youth organisation registered in accordance with the relevant laws.*" Lakini sasa unajiuliza, hii ni *cut across* kwa Wilaya na kwa Mkoa au ni kwa Taifa tu?

Mheshimiwa Spika, ukija kwenye kifungu cha 10(2) wanasema, "*the District Youth Council shall be composed of such number of members not exceeding thirty members.*"

Mheshimiwa Spika, naungana na wenzangu ambao wamewahi kusema, kwamba nia yetu tunataka kuondoa vijana wanaokuja mjini wabaki kule vijijini wafanye kazi, wapate ajira kule waliko waweze kutengeneza ajira.

Kwa hiyo, maendeleo yatakuwa ni kule vijijini. Lakini hawa vijana wako kwenye Kata zetu na vijiji vyetu. Kwa hiyo, ningeshauri hii idadi tunayosema 30, badala ya vijana 30 iwe kwamba Baraza hili litakuwa na kila kijana mwakilishi kwenye kila Kata.

Mheshimiwa Spika, kwenye Wilaya kuna Kata tofauti, kuna Wilaya moja unaweza kukuta ina Kata 12 na kuna Wilaya nyingine ina Kata 33, kuna nyingine ina Kata 36.

Kwa hiyo, ningeshauri hawa wawakilishi wa hili Baraza watokane na Kata kwa sababu nia yetu tunataka kupeleka maendeleo kule angalau awakilishe vijana walioko kule vijijini na yumkini akija kwenye Baraza la Mkoa au la Taifa, kuna mambo ambayo wataelekezwa ili waweze kwenda kuunda vikundi huko katika maeneo.

Mheshimiwa Spika, tunasema ni *registerd* au asasi ambazo zimesajiliwa, lakini kule kwenye Kata kuna Maafisa Maendeleo ya Jamii ambao wanaweza kusaidia yule mwakilishi anayechaguliwa akasiadia vijana kule wakaunda asasi za kiraia zisizo za Serikali ambazo zinaweza kusaidia kupata maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kuna wakati mwingine unakuta Mkurugenzi ana fedha ile 5% anataka kuwapa makundi ya vijana, lakini hana vijana, hana vikundi vya vijana vilivyosajiliwa. Kwa hiyo, kwa namna hii inamaanisha kwamba kama huyu mwakilishi anayetoka kwenye Kata, huku ngazi za juu watakuwa wameshawaelekeza la kufanya na yumkini vikundi vitakuwa vingi kule kwenye Kata.

Kwa hiyo, hata Mkurugenzi wa Halmashauri atakapokuwa na pesa za Serikali anataka kutoa mikopo, nina uhakika kabisa kwamba atapata vijana wengi ambao watakuwa wamejiunga kwenye vikundi kwa ajili ya kupata mikopo. Namna hiyo pia itasaidia kwamba kule kwenye Kata sasa vijana wetu kama ana mradi mzuri, hana haja ya kuhangaika kuja mjini na tujue kwamba asasi iliyosajiliwa kwenye Mji mmoja wa Wilaya, haimaanishi ni ya wale vijana wanaotoka vijijini, inawezekana kabisa ni vijana waliotoka miji mikubwa kama Dar es Salaam, inawezekana ni vijana wako maofisini wana kazi nzuri, lakini wana ka *NGO*. Nilikuwa naomba uwakilishi wa hawa Wajumbe wa Baraza hao 30 usiwe ni 30, badala yake iwe ni mwakilishi kutoka kwenye kila Kata.

Mheshimiwa Spika, nikienda kwenye kifungu cha 18, kinasema, "Mkutano Mkuu wa Wilaya utakuwa ni chombo cha juu katika masuala yote yanayohusu vijana katika ngazi ya Wilaya." Lakini huu Mkutano utakuwa na watu saba,

labda kama sijaelewa. Kwa sababu utakuwa na Mwenyekiti, Katibu na wawakilishi watano kutoka taasisi za vijana zilizosajiliwa ndani ya Wilaya husika. Kama anamaanisha basi taasisi za vijana, kama anaaminisha wawakilishi watano kutoka kwenye taasisi tano, maana yake ni kwamba kuwe na watu saba. Sasa najiuliza, kama ni Mkutano Mkuu wa Wilaya, kwa nini wale Wajumbe wa Baraza wasiwekwe kwenye huu Mkutano? Wale Wawakilishi waliotoka kwenye Kata, kwa nini wasiwekwe kwenye huu mkutano?

Mheshimiwa Spika, maana yake ni kwamba hizo taasisi za vijana tunazosema zimesajiliwa, sina uhakika kama kweli hizo taasisi huko vijijini zipo, sina hakika sana. Kwa hiyo, naomba Serikali iangalie hilo kwamba kweli kuna hizo taasisi ambazo zimesajiliwa? Zimesajiliwa nia yake ni nini? Yaani lengo lao ni nini, wanafanya nini?

Mheshimiwa Spika, kuna jambo lingine ambalo nilikuwa ninaomba kuiomba Serikali, kwamba sasa tunaanza hili Baraza la Vijana, lakini naomba Serikali ifanye utafiti kama alivyosema Mjumbe mmoja kuhusu pesa, kwamba Serikali ifanye utafiti wa kina kuhakikisha kwamba wanajua kweli vyanzo vya mapato vitapatikana vipi. Kama ni bajeti, basi ni kweli kila mwaka watapata bajeti kama zinavyopata Halmashauri za Wilaya lakini ikiwa tofauti na hiyo maana yake ni kwamba haya Mabaraza yatakuwa ni chanzo cha kuanza kugombana watakapokuwa wanakutana hawa vijana.

Mheshimiwa Spika, nashauri kwamba Serikali isiwape tu muda wote wapewe pesa, nilikuwa nafikiri kwamba vile ambavyo wanataka kuwa huru, *let them be free*! Kwa hiyo, nao wawe *innovative* wabuni vyanzo vya mapato ilimradi Serikali ijue ni vyanzo gani, isije ikawa ni hela inapokelewa kutoka *Boko Haram*.

Jambo lingine nilikuwa naomba pia kuwe na usiammizi madhubuti, kwamba Mabaraza haya yanaweza kuanza kwa nia njema kabisa, lakini baadaye yakatekwa na Wanasiasa ikawa ni nyumba ya wanasiasa kwenda kuleta fujo na kuwafundisha vijana mambo ambayo hayana faida kwao.

Naomba Serikali iangalie ni namna gani itaweka udhibiti mkubwa kabisa kwamba haya Mabaraza yawe kweli ni kwa ajili ya kuwakilisha vijana kwenye mambo ya maendeleo na siyo kujiingiza kwenye itikadi za siasa.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Nilimwita Mheshimiwa Esther Matiko, atafuatiwa na Mheshimiwa Nassib Omar, halafu atafuatiwa na Mheshimiwa David Silinde.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuweza kunipatia fursa nami kuweza kuchangia kwenye Muswada wa Sheria ya Baraza la Vijana Tanzania mwaka 2015.

Kwanza kabisa napenda kutoa pole kwa vijiji vya Kibaso, Ketawasi, Kigongo na vingine vyote ambavyo vimekumbwa na baa la njaa zaidi ya wananchi 40,000 kwenye Wilaya ya Tarime wamepata matatizo ya chakula kwa sababu ya ukame na uharibifu wa tembo.

Kwa hiyo, naomba sana Waziri Mkuu na Waziri wa Nchi kwa maana ya Sera, Uratibu na Bunge, kupitia Kitengo cha Maafa mhakikishe wananchi hawa 40,000 wanapatiwa chakula *as soon as possible*. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nichangie sasa kuhusu Muswada wa Sheria wa Baraza la Vijana. Ni dhahiri kabisa na Mheshimiwa Waziri ametamka kwamba hili Baraza linakwenda kupewa mamlaka kamili ya kuweza kujiendesha. Kulingana na kauli ya Waziri na walichokiandika, nashauri kwamba na wenzangu wamesema kwamba mamlaka makubwa aliyopewa Mheshimiwa Waziri, kwanza ukiangalia huu Muswada umeletwa kwa hati ya dharura, lakini kifungu namba moja kinasema...

**SPIKA:** Haujaletwa kwa hati ya dharura. Wa hati ya dharura siyo huu.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Pamoja na hayo, utaona kwamba kifungu namba moja kimempa Waziri mamlaka ya kuweza kuamua ni lini sheria ianze kutumika. Tunatambua uhitaji mkubwa wa Baraza hili la Vijana katika nchi yetu na tunatambua urasimu mkubwa ambao unakuta tukishatunga sheria zikaenda, zinachukua muda mrefu sana kwa Mawaziri kutunga Kanuni au kuweza kutoa kwenye gazeti ili iweze kutumika.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nashauri Bunge kwa umoja wetu tuweke *time frame*, tuamue ni baada ya muda gani Mheshimiwa Waziri awe tayari ameshasema sheria ianze kutumika. Pili, mamlaka aliyopewa Waziri kwamba Baraza linapendekeza majina matatu, halafu yanakwenda kwa Mheshimiwa Waziri kuweza kuamua ni yupi awe Mwenyekiti, kwa kweli tunakuwa tunabaka mamlaka ya Baraza zima. Hii imeelezwa kwenye kifungu 5(1).

Mheshimiwa Spika, naomba kabisa Mheshimiwa Waziri kwa hili aachie Baraza ili wao wenyewe waweze kuchagua Mwenyekiti wao na Katibu Mtendaji, nayo pia ilikuwa imewekwa kwamba Mheshimiwa Waziri ndiyo ashughulikie iweze kuondoka.

Mheshimiwa Spika, lingine, huwezi ukasema Baraza, Waziri ndiyo ataamua washirika wake wawe ni akina nani, yaani leo Waziri akae na aamue Baraza la

Vijana tunataka lishirikiane na shirika fulani aidha la ndani ya nchi au nje ya nchi. Tuache hiki chombo kiwe na mamlaka kamili.

Mheshimiwa Spika, lingine nitaenda kuzungumzia muundo wa Baraza. Kwanza kabisa, ni Baraza katika ngazi ya Taifa, utaona kabisa Watanzania kwa ujumla wake wametengwa. Vijana, kwanza muundo wote kwa ujumla, umewatenga vijana. Huwezi kusema kwamba Wanachama wa Baraza la Vijana wa Taifa watakuwa ni wale waliaojiandikisha kwenye asasi na taasisi.

Mheshimiwa Spika, tutambue wazi kabisa kuwa asilimia kubwa ya Watanzania kwa ujumla wanaishi vijijini. Katika hawa milioni 16 walioainisha, zaidi ya asilimia 70 wanapatikana na vijijini na katika wale wanaopatikana vijijini ni zaidi ya asilimia 95 hawana asasi wala taasisi zilizosajiliwa kisheria. Sasa kama lengo kubwa ni kuhakikisha kwamba vijana wote wanaweza kuchukuliwa kwa ujumla wao, huwezi kuweka hiki kipengele, kinakinzana.

Mheshimiwa Spika, nashauri turuhusu vijana wote wanaokidhi mahitaji ya kuitwa kijana waweze kuwa wanachama hai wa Baraza la Vijana wa Taifa bila ya kuweka vigezo ambavyo vinaenda kuwatoa wengi wao kwa asilimia zaidi ya asilimia 90. Labda mtuambie hili Baraza limeundwa kwa madhumuni ambayo ni *hidden.* Lakini kama mmeunda kwa madhumuni ya dhati ya kuwasaidia vijana wa Kitanzania, naomba sana tuondoe hii dhana ya kusema kwamba ni taasisi ama asasi ambazo zimesajiliwa. Tutambue kwamba kuna makundi mbalimbali kwenye jamii yetu ambayo hayajasajiliwa lakini yanatambulika kwenye jamii husika.

Kuna waendesha bodaboda, wapiga debe, madereva, wakulima, mamalishe; vikundi vingi ambavyo havijasajiliwa kwa mujibu wa sheria hii. Sasa mkisema kwamba lazima wakidhi hitaji la kuwa taasisi au asasi, haikubaliki. Inakuwa lengo halijatimia, kama wenzangu walivyosema hapa, tunakuja kutumika kama *rubber stamp* tu ili mwisho wa siku muutangazie Umma kuwa mmeunda Baraza, lakini Baraza ambalo linakwenda kuwaneemesha watu wachache na siyo vijana wa Kitanzania ambao kwa wingi wao ni maskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nije kwenye muundo sasa wa Baraza ngazi ya Taifa, mmesema hapa kwamba watakuwa ni wale wenye *degree* au zaidi ndiyo watakuwa wamechaguliwa kuingia kwenye Baraza la Taifa. Mimi nikajiuliza sana, kama wanaoingia ni wenye *degree* au zaidi, Bunge hili wakati mnatengeneza Katiba, Rasimu ya Warioba ilisema *form four* watu wawe Wabunge; na mnajua majukumu ya Bunge, hata Miswada ikija imeandikwa Kiingereza na Kiswahili, mkaondoa mkasema ajue kuandika na kuhesabu sijui na kufanya vitu gani. *(Makofi)*

Leo mnaweka *discrection* ya vijana kwamba ni lazima wawe na *level* ya juu kabisa ya elimu. Mnasahau kwamba vijana wa Kitanzania kwa asilimia isiyopungua 60 hawajafika hata *form four*. Ndiyo najiuliza, huu Muswada unamaanisha kweli kumkomboa kijana wa Kitanzania masikini ambaye ameshindwa kufika *form four, form six* mwenye *certificate* na mwenye *Diploma?*

Mheshimiwa Spika, naomba hili pia kama mlivyojipendelea Wabunge, mkaamua kuondoa kipengele cha *form four* mkaweka kwamba ni lazima ajue kusoma na kuandika, najua mkiweka hii, ni lazima watakuja wenye *degree*, wenye *Ph.D* kama tulivyo humu. Kuna watu wana *Ph.D,* wana *degree*, wana *masters*, kuna *form four,* kuna darasa la saba. Hakuna haja ya kuweka ubaguzi. Kama mlivyoamua kujipendelea na hapa muache muweke. Kuna watu huku mpaka wengine hawajamaliza Darasa la Saba lakini wapo Bungeni.

**MBUNGE FULANI:** Darasa la pili wapo!

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Kwa hiyo, msiwanyanyase Watanzania vijana ambao ni masikini, ambao walishindwa kupata hiyo elimu ambayo mmeiweka kwasababu ya uzembe wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kingine kwenye muundo wa Wilaya, kwanza mnaji-*contradict*. Mmesema kwamba Wajumbe watano kutoka katika asasi au taasisi zilizosajiliwa kwenye Wilaya. Kuna Wilaya nyingine utakuta kuna hizi *groups* za vijana ambazo mnazisema, hakuna hata vikundi vitano vilivyosajiliwa. Kwa hiyo, mwone kwamba mwisho wa siku sijui hata mmefanya tafiti zipi. Mtakuta mnaacha *group* kubwa sana la vijana ambao hawajasajiliwa kwenye hizo asasi au taasisi.

Mheshimiwa Spika, hili naweza kuongea *with refference* hata na Wilaya ya Tarime au Wilaya nyingi ambazo ziko Mkoa wa Mara. Hatuna asasi za vijana au taasisi ambazo zimesajiliwa kwa mujibu wa sheria. Wengi wao ni vikundi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naomba kama wenzangu wengine wengi walivyopendekeza, tushushe mpaka kwenye ngazi ya Kata, lakini pia kwenye ngazi ya Kata tusi-*limit*. Tusiseme kwamba ni asasi au taasisi zilizosajiliwa, tuache iwe kwamba au asasi na taasisi nao waje na wawakilishi wao, tena izingatie *gender,* awepo mwanamke na mwanaume na ikiwezekana mzingatie na wenzetu wenye ulemavu kwa maana Wajumbe angalau watatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini asasi kujumlisha na Kata, kila Kata itoe hao Wajumbe kwenda kwenye Baraza la Wilaya na kwenye Kata pia wawe wanajiendesha. Kama kweli tunadhamira ya dhati ya kuwakomboa vijana wetu wa Kitanzania kama ilivyoelezwa madhumuni ya Muswada huu…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa David Silinde, atafuatiwa na Mheshimiwa Eugine Mwaiposa.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia fursa hii ili nami angalau nichangie Muswada wa kuanzisha Baraza la Vijana la Tanzania wa mwaka 2015.

Mheshimiwa Spika, kuna uhitaji wa Baraza la Vijana ambao hakuna kijana yeyote anaweza akapinga. Lakini unapokuwa unahitaji Baraza la Vijana ni lazima tuwe na *purpose,* yaani *purpose* ya Baraza la Vijana ni nini? Lengo hasa ni nini? Yaani ni nini ambacho kinakwenda kufanyika?

Mheshimiwa Spika, Baraza la Vijana la CHADEMA (BAVICHA) *purpose* yake ni kuwaunganisha vijana wa CHADEMA wawe wamoja, kuwaunganisha vijana wajiunge na CHADEMA. *That is the main purpose*. UVCCM (Umoja wa Vijana wa CCM) *purpose* yao kubwa ni kuunganisha vijana wa CCM nchi nzima na mambo mengineyo.

Mheshimiwa Spika, sasa nilikuwa napitia hapa huu Muswada wa Serikali, nilikuwa natafuta *purpose* kuu ni ipi? Siioni mantiki, sijaiona! Ni bora ukawa na Baraza la Wakulima ukajua linaunganisha wakulima ambao mwisho wa siku *outcome* tutaiona. Ni nini *outcome* ya hiki kitu?

Mheshimiwa Spika, unajua ukiangalia kimantiki, hakuna mantiki, *it is just an illusion*. *That is what I can see*! Nazungumza *with logic,* tujadili kitu ambacho kinakwenda kuonekana. Hamna *purpose*, hamna lengo kuu kwenye Muswada mzima wa sheria hii. Kikubwa tu humu ni Mikutano ya Baraza, tena ngazi ya Wilaya na ngazi ya Mkoa, mwisho. Kazi kubwa sana ambayo mmeitaja kwenye Mkutano Mkuu wa Wilaya, ni kuishauri Sekretarieti ya Tawala ya Wilaya. Kuishauri! Hao Wilaya mkishawashauri wakikataa?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mwisho wa siku ni kama vile tunataka kufanya *politics* tu, *I can see it is politics.* Labda inawezekana kukawa na shida vilevile hata huku Serikalini kwa Mawaziri wenyewe. Unajua nilikuwa napitia hapa mtu akiwa Waziri wa Vijana, Mchezo, ni lazima aendane na huo ujana na michezo yenyewe, kuanzia umri na namna yenyewe. Sasa Kenya mwaka uliopita kulikuwa na Waziri wa Vijana, Ababu Namwamba amepewa Uwaziri akiwana miaka 30. Uganda kulikuwa na Waziri wa Vijana na Michezo, Ronald Kabuhule amepewa Uwaziri ana miaka 26, leo ana miaka 30. Sisi hapa Waziri wetu wa Vijana, Mheshimiwa Mama Fenella Mkangala ana miaka 60, yaani *it doesn't make a sense*! Ndiyo inaleta shida. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, leo Muswada, kidogo kuna mambo mengi ya msingi ambayo yameondolewa. Sitaki kumjadili Mheshimiwa Nkamia. Kuna mambo mengi sana ambayo yameondolewa. Kwa mfano, kwenye Muswada wa Mheshimiwa Mnyika alikuwa anataka pawepo na Mfuko wa Maendeleo ya Vijana. Wizara imeliondoa hili jambo kwa sababu moja kubwa tu. Kule karibu kila mwaka huwa tunawatengea zaidi ya shilingi bilioni sita ambazo zinatakiwa ziende katika ngazi zetu za Halmashauri. Zile fedha kule hazifiki na ndiyo sehemu ya ulaji.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeona utakapoanzisha Baraza ukawapa uwezo wa huu mfuko, maana yake unatoa zile fedha Wizara ya Utamaduni, Michezo na Vijana inakwenda kwenye Baraza. Hawawezi wakakubali hawa kwa sababu *they are not concerned* na Vijana. Hili ndiyo tunashindwa kuliona *sense* yake. Kenya na Uganda wameliona, yaani Wizara zinaendana, sisi tumeshindwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna wiki za vijana ambazo zimekuwa zikifanyika kila mwaka mwezi Oktoba, kunakuwa na fedha na ulaji mkubwa. Wizara wamezuia, hivi vyote wameondoa kwa sababu haya yote tulitaka yasimamiwe na Baraza la Vijana wenyewe Taifa.

Mheshimiwa Spika, kinachoonekana hapa ndiyo tunaita kukosa ubunifu. Sheria yetu yote hii; someni Sheria ya Baraza la Vijana ya Kenya, yote hii ni *copy and paste,* hakuna utakachokosa, mpaka nukta. Tunasema kwa sababu tunasoma na tunajua. Sasa tunapowaeleza haya Serikali mnaona kama vile tunazungumza vitu visivyokuwa na hoja, tunawaambia vitu ambavyo mmechemka. Sasa tunapokuwa tunawaeleza vitu kama hivi, mnashindwa kuelewa nini tunachokihitaji.

Mheshimiwa Spika, napenda Serikali inapokuja itueleze *purpose* ni nini? Maana yake usije ukatengeneza sheria ambayo baadaye itakuja kukuangamiza wewe mwenyewe. Wazee wetu, waasisi wa Mataifa yote, walipokuwa wanapigania uhuru, walitengeneza sheria wakidhani watakaa madarakani maisha yao yote, matokeo yake sheria zile zile ndiyo zilikuja zikawaumiza wengi. Mataifa yote ambayo yalifanya mabadiliko, ninyi nyote ni mashuhuda. Sheria walizitunga wenyewe, walijitengenezea makaburi wenyewe, mwisho wa siku ndiyo yakaja kuwaua hao hao. Sasa na hizi sheria ni lazima tuje tuziangalie lengo kuu la Muswada huu ni nini?

Mheshimiwa Spika, sheria hii inaleta ajira! Hakuna ajira kwenye sheria hii, sheria hii inaenda kuleta fedha, hakuna! Yaani hakuna kitu, hakuna lengo kuu la Muswada. Inasikitisha kuwa na Taifa la namna hii. Sasa sijui ni wapi ambako tunaelekea, lakini ni lazima tuangalie mara mbili mbili.

Mheshimiwa Spika, kimezungumzwa hapa kigezo cha watu kujiunga na Mabaraza, kushika nafasi za uongozi kwenye Baraza hili. Tunazungumza *degree*, tunaweka *level* kubwa sana ya *degree*. Ni kubwa mno, tukiulizana humu Wabunge wangapi wana *degree,* ni tatizo. Tukisema ni wangapi wana *Diploma,* ni tatizo! Hii ndiyo tunaita ubinafsi. Yale masuala yanayotuhusu sisi Wabunge tunajiwekea vitu vya chini kabisa. Kama ilivyokuwa kwenye Katiba, Mheshimiwa Warioba alisema angalau kidato cha nne tu mtu awe Mbunge, nini kilichotokea hapa? *Ndombolo ya Solo* ndani ya Bunge! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni lazima ishushwe mpaka darasa la saba, ama kushuka zaidi hata ya hapo, anayejua kusoma na kuandika hata kama hajafika darasa la saba. Kwa sababu linatugusa sisi, haliwagusi watu wa mbali. Wale wa mbali tukiona tu hii kitu, tunawawekea *barrier*, *degree* moja, haiwezekani! Ni lazima tuliangalie hili mara mbili mbili.

Mheshimiwa Spika, Baraza hili litengenezwe na vijana wote wa rika zote, vijana wote wawe wana ruhusa ya kuenda kujisajili. Ni wangapi wana *NGO*? Momba kuna *NGO's* hazizidi hata tatu. Utakuta inayohusika na *HIV*, sasa hivi angalau kuna watu wa kilimo na mifugo. Hazipo hizi taasisi mnazotaka zisizo za Kiserikali, watazitoa wapi? Ni Wilaya ngapi? Kwa hiyo, mwisho wa siku ni kwamba watakaokuwa viongozi wa hizi ni watu wa maeneo ya Mijini. Watu wa vijijini hazitawagusa. Vijana wapo maeneo yote mpaka katika ngazi za vijiji. Haya ndiyo ambayo tumekuwa tunawaambia. Tunataka haya ndiyo yaingie, lakini hatuwezi kuingiza huu Muswada; ingekuwa ni *my own opinion,* ningeshauri hili jambo ni bora tukalisitisha, likaenda tukalipangia muda…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante. Nilisema nitamwita Mheshimiwa Eugine Mwaiposa atafuatiwa na Mheshimiwa Felix Mkosamali, atafuatiwa na Mheshimiwa Lema.

**MHE. EUGINE E. MWAIPOSA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ili nami niweze kuchangia hii hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, naungana na wenzangu, lakini pia niwapongeze sana Mawaziri wanaohusika na Serikali kwa kuleta Muswada huu ambao ulikuwa unasubiriwa kwa kipindi kirefu sana.

Mheshimiwa Spika, napenda kujielekeza kwenye muda wa kukaa madarakani viongozi watakaochaguliwa. Katika Muswada tumeona wale Wajumbe wanaochaguliwa wanatakiwa wakae miaka mitatu. Nilikuwa nataka

nishauri tu Serikali kwamba ingependezwa sana kama muda huu ungeongezwa kidogo ukawa miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, kwa jinsi vijana walivyo *active,* miaka mitatu itakuwa ni miaka michache sana ya vijana kuweza kuonesha ufanisi wao katika nafasi ambazo watakuwa wamepewa. Kwa hiyo, nilikuwa nashauri na kuiomba Serikali iangalie ni namna gani inaweza kufanya ifike miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nilikuwa nataka nichangie ni kuhusu kazi za Baraza. Pamoja na kazi ambazo zimeainishwa, tatizo kubwa sana la Vijana nchini ni ajira. Napenda sana kama sera hii au kazi mojawapo ya Baraza hili la Vijana lingekwenda ku-*address* tatizo kubwa la ajira walilonalo Vijana.

Kwa hiyo, napenda sana kuishauri Serikali iangalie ni namna gani inaweza ikaongeza kipengele kingine ambacho kitalifanya Baraza hili liweze kutafuta fursa mbalimbali za kiuchumi, za kibiashara, za kijamii nje na ndani ya nchi ili vijana waweze kuajiriwa. Kwa mfano, kushughulika na kilimo, waweze kuwashauri vijana wenzao, waweze kutafuta wafadhili kwa ajili ya kusaidia kilimo cha umwagiliaji, kufanya biashara nje ya nchi na ndani ya nchi na vitu vinavyofanana na hivyo.

Kwa hiyo, wakipata fursa hiyo ya kuweza kushughulikia matatizo ya ajira nadhani tatizo la ajira pia hapa nchini linaweza likapungua kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Spika, nataka nioneshe *concern* yangu pia kwenye suala la uanachama. Kama ambavyo wengine wamezungumza, kwenye sheria hii kunaonesha kwamba asasi na taasisi ndizo ambazo zinaruhusiwa kuwa na uanachama katika Baraza.

Mheshimiwa Spika, lakini ikumbukwe kabisa kwamba vijana walio wengi hawana asasi wala hawako kwenye taasisi. Wale ambao wana asasi na taasisi, tayari ni wajanja, wao hawana shida ya ajira wengi wao, lakini hawana shida ya mambo mengine mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli wapo vijana ambao wana shida, hawajaweza hata kuunda hizi asasi wala taasisi ambao wapo chini kwenye Kata na kwenye Vijiji.

Mheshimiwa Spika, nilifikiri kwamba Serikali ingeangalia namna ya kupanua wigo zaidi ili na vijana ambao wapo kwenye Kata waweze kutengenezewa utaratibu wa kuwa na Uanachama katika Baraza hili.

Mheshimiwa Spika, muundo wenyewe wa Baraza unaeleza kwamba vijana waanze kujiunga kutoka kwenye Wilaya, lakini vijana wengi wako kwenye Kata, Vijiji na kwenye Mitaa. Hawatapata uwezo wa kuchangamkia fursa hii ya kuundwa kwa Baraza hili.

Naiomba sana Serikali iangalie ni namna gani inaweza kuwafikia vijana hawa waliopo huko chini ambao wengi wao kama ambavyo wenzetu wamesema hapa, ndiyo wanaotoka vijijini kuja kutafuta fursa za ajira na mambo mengine na maisha mazuri mjini. Wakiruhusiwa tu au wakitengenezewa utaratibu wa kujiunga vizuri kwenye Baraza hili, basi uwezekano wa kubakia huko walipo unaweza ukawa mzuri zaidi na tukaweza kuwanufaisha hasa katika eneo la kilimo huko vijijini.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya hapo, nilikuwa nataka tu nimsaidie aliyemaliza kuongea kabla yangu, aliuliza madhumuni ya sheria hii.

Mheshimiwa Spika, wakati nilipokuwa nasoma, nilikumbuka kwamba nimekuta madhumuni ya sheria yameorodheshwa, tena yapo mengi kwenye ukurasa wa 42. Yapo mengi, yameorodheshwa pale, kwa hiyo, ni kiasi cha kusoma na kujiridhisha.

Mheshimiwa Spika, naona kuwa hatakuwa analitendea Bunge hili haki kwa kuwahadaa wananchi kwamba Muswada mzima huu hauna madhumuni. Una madhumuni yake na yameorodheshwa pale, lakini zaidi pia kuna kazi ya hili Baraza, nazo zimeorodheshwa pale.

Kwa hiyo, Watanzania wajue kabisa kwamba Muswada huu ni mzuri, umetengenezwa vizuri. Hizi propaganda za kwamba ni ku-*copy* na ku-*paste* hiyo haiwezi ku-*hold water*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kwamba Muswada huu ulikuwa umesubiriwa kwa kipindi kirefu na nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge tuupitishe bila kujali *propaganda* ambazo zinaelezwa na wenzetu ili vijana wetu waweze kuwa na chombo hiki ambacho kitawasaidia sana.

Mheshimiwa Spika, ni hayo ambayo ningependa nishauri. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Kwanza niwatambue wageni wangu.

Kuna wageni Wanachuo 41 kutoka Chuo cha *Edger Maranatha School of Nursing.* Sijui kipo wapi hiki? Karibuni sana waganga wetu, naomba tu msimame msalimie Waheshimwa Wabunge. Ahsanteni sana, karibu sana. Hiyo kazi ni wito

wa Mwenyezi Mungu, kwa hiyo, tuaamini kabisa mtafanya hivyo, kwa sababu uhai wa binadamu mnashirikiana na Mungu. Karibuni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Felix Mkosamali, atafuatiwa na Mheshimiwa Nassib Omar!

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa nami nichangie huu Muswada ambao unatuhusu sisi vijana.

Mheshimiwa Spika, ukitaka ku-*copy* sheria ya Kenya ya Vijana ni lazima ukumbuke kwamba Kenya wameshafanya mabadiliko ya Katiba yao ambayo hiyo Katiba yao imezungumza mambo ya vijana, ambapo hiyo Katiba ya Kenya katika utekelezaji wake wamejiwekea muda na watapitia sheria zote ambazo walizitunga kabla ya Katiba hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ukichukua ule Muswada ambao unazungumza mambo ya zamani ya Kenya utegemee kwamba hivi karibuni wanaweza kufanya mabadiliko kwa sababu bado wanapitia sheria zao zote ili ziendane na dunia ya kidemokrasia.

Sasa tunachosema, wamezungumza Waheshimiwa Wabunge wengi wa vyama vyote, vijana na wengine, dunia tuliopo sisi vijana wa sasa hivi ni dunia ya kidemokrasia.

Kwa hiyo, kitu tulichokitegemea kwanza kwenye Muswada huu siyo kuteua watu, wala siyo kuweka urasimu. Uundwaji wa Mabaraza haya kuanzia huko chini, miaka yenu ninyi wakati mnaanza akina Mzee Mwandosya na wengine ndiyo mlianza watu wanaendesha nchi kibabe, kidikteta wamekuja mpaka miaka hii wengine wamechukua nchi kwa kupindua.

Mheshimiwa Spika, dunia tunavyozungumza sasa hivi, ni haki za binadamu na demokrasia. Haya mambo ya nchi zetu hizi za Kiafrika zilikotoka, siyo hapa! Hatuwezi kuendelea huko!

Mheshimiwa Spika, hata kama mtalazimisha mkifikiri kwamba mnaweza kuwa na mfumo wa kuteua watu, mtahama tu! Dunia itawalazimisha kuhama kwa sababu haya mambo ya uteuzi, nchi zote ukienda Kenya, Malawi, wapi na nchi zote ambazo ndiyo dunia ya sasa hivi, hatuko kwenye siasa za u-*communism* ambapo Rais anafanya kila kitu. Tumeshahama huko! Hatuko kwenye siasa ambazo Waziri anaonekana ndio mtu wa kufanya kila kitu. Tupo kwenye dunia nyingine.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mnapotunga hizi sheria zinazotuhusu sisi vijana ni lazima mjiulize, tunatunga sheria za vijana wa miaka ipi?

Kwa mfano, hii dunia tuliyopo sisi, akina Obama wanachaguliwa kuwa Marais miaka 44. Hata sisi wakati mnatutungia sisi vijana kwamba miaka 35 tusigombee Urais mpaka tuwe na miaka 40, nasi tunatakiwa tuwaambie kwamba nanyi mkifikisha miaka kadhaa, tunaona hamfai kugombea nafasi hizi. Ndiyo maana tunaanzisha haya Mabaraza na sisi tujitetee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haiwezekani nchi za Kiafrika jitu lina miaka 90, mtu anadondoka anaendelea kuongoza vijana wa miaka hii tunataka haya Mabaraza yawe yanazungumza mambo ya namna hii. Ndiyo sababu ya kuanzisha!

Mheshimiwa Spika, kama mlivyoandika kwenye madhumuni kwamba ni kuangalia tu mambo ya vijana, hapana! Kazi ya Baraza hili ni kuangalia pia mambo kwamba ni sahihi wazee kufanya jambo hili? Hili jambo linaendana na wakati huu au ni jambo ambalo limepitwa?

Mheshimiwa Spika, na sisi tutakapofikia umri wenu, watakuja vijana watatuambia, ninyi kina Mkosamali mlikuwa mnatumia *smart phone* kipindi hicho, sasa hivi hizo ni za kishamba, ziko hivi! Kwa hiyo, Muswada mmeunyima demokrasia! Muswada bado unapendekeza kuteua mambo ambayo dunia haiko huko! Dunia inataka uhuru, watu wachaguane na nini, ndiyo tunakokwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Baraza hili kazi yake ni kama kioo, tunapotunga sheria maana yake liwe linaalikwa, linaangalia, kila sheria inayopitishwa na Bunge, Sera za Serikali zimeangalia vipi masuala ya vijana. Kwa hiyo, litakuwa lina-*foresee* kuanzia utungaji wa sera kama ambavyo hata nchi nyingine Mabaraza ya Wanawake yapo. Kwa sababu litakuwa ni *neutral,* maana yake litakuwa lina-*fair comment* kwa Serikali na sekta binafsi kuhusu mambo ambayo yanawahusu vijana. Kwa hiyo, lazima uliache hili Baraza liwe huru kuliko kuliweka hivi jinsi lilivyo.

Mheshimiwa Spika, ukijaribu kuangalia hata wakati huu Muswada unajadiliwa, baadhi ya mambo vijana tunakubaliana. Sasa utashangaa kwa nini tunafika Bungeni kwa yale ambayo tulikuwa tunakubaliana sisi wa Upinzani na Chama Tawala, tulipaswa kuwa tumeshayamaliza kabla ya Muswada huu kuja huku! Lakini kwa sababu kuna urasimu katika utungaji wa sheria unakuta tunakuja hapa tunabishana hata kwa mambo ambayo hayana sababu.

Mheshimiwa Spika, lakini pia Muswada huu licha ya kuangalia ku-*foresee* utungaji wa sera na sheria, lazima Baraza hili lifanye kazi ya kuangalia utekelezaji wa sera na sheria hizo. Liangalie je, Sekretarieti ya Ajira inafanya kazi, inaajiri kwa upendeleo au haifanyi hivyo? Baraza hili liangalie mifumo kwa mfano, ya haya mambo ya juzi Uhamiaji wanateuana ndugu na nini, liangalie

je, vijana ni sawa sawa? Baraza hili lazima lifikirie fursa za vijana wa Kitanzania na vijana wa nchi zingine!

Mheshimiwa Spika, sasa ukiangalia Muswada huu, ni kwamba wengi wamezungumza ukianzia kwenye Mabaraza ya Wilaya yana changamoto kubwa, namna yanavyopatikana, namna yanavyoondolewa, uwajibikaji wake ukoje; wanaondolewaje hawa viongozi! Yote hii haipo, kuanzia Wilaya, Mkoa mpaka Taifa.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana sisi kama alivyosema Mheshimiwa Silinde, sio sawa sawa Waziri mwenye miaka 60 kuongoza Wizara ya Vijana. Wewe una miaka 60! Wewe maana yake ni mzee, hauko kwenye umri wa kati, utakuwaje *flexible* kujadili mambo haya ya vijana? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wazo hili ni zuri, lakini ukilitazama bado limeminywa. Sio wazo la kisasa, haliendani na vijana wa sasa hivi. Ni wazo lile unakuwa na Waziri Mzee anatafuta vijana dhaifu dhaifu, kwa sababu mfumo wenu wakati mnaanza ulikuwa ni vijana mnafikiria kwamba watakuja kuwa sijui, mlikuwa mnaita Taifa la kesho, sisi tumeshashituka, hatuko huko, tunataka tushiriki kwenye shughuli za Serikali sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii hatutengenezi kama Umoja wa Vijana wa CCM, *no!* Ndiyo maana ule Umoja wa Vijana wa CCM mlivyokuwa mmeuweka, mlijikuta mmewabana, vijana wengi wakawa wanashindwa kupumua, wanashindwa kugombea nafasi mbalimbali! Halafu Makamanda wa Vijana mnachukua wazee ndiyo mnawavisha mnasema ni Makamanda wa Vijana, wazee! Mtu ana miaka 80 mnasema ndiyo Kamanda wa Vijana. Sasa sijui anakimbizaje hawa vijana na anawafundishaje huyu mzee? Na Waziri wa Vijana tena mnaweka mtu mzee ambaye haendani na vijana hawa! Kwa hiyo, ni wazi kwamba mambo haya yaliyoko kwenye huu Muswada bado hayaendani na hali ya sasa, hayako huko! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Tutaachaje kuwa *rubber stamp* wakati hamjadili Muswada? Hamjadili Muswada!

Mheshimiwa Nassib Omar! Halafu atafuatia Mheshimiwa Lema, Mheshimiwa Gekul, kisha atafuatia Mheshimiwa Mangungu!

**MHE. NASSIB SULEIMAN OMAR:** Mheshimiwa Spika, kwanza tumshukuru Mungu sana mwingi wa rehema kwa neema zake nyingi juu yetu. Pili, nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii. Lakini vilevile tumuombee sana

Makamu Mwenyekiti wa Kamati hii, Marehemu John Komba, ili Mungu amuweke mahali pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii na naunga mkono mia kwa mia hoja hii. Lakini mimi nitajikita zaidi katika kujibu hoja za waliozungumza dhidi ya Kamati yetu ya Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, Miswada yote miwili ilikuja katika Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Muswada Binafsi ulikuja tarehe 20 hadi tarehe 31 Oktoba, 2014; ulijadiliwa kwa kina na baada ya kujadiliwa kwa kina ulionekana una upungufu, haukukidhi vigezo na viwango na kwa hiyo, Muswada huu ukarejeshwa.

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa la Muswada ni kwamba ulikuwa kama unataka kujenga jukwaa au chombo ambacho kitashinikiza Serikali, chombo ambacho kitaleta ugomvi baina ya vijana na Serikali! Na hili tuliliona na sisi hatukulikubali, kwa sababu hatima yake ingeleta sintofahamu baina ya vijana na Serikali.

Mheshimiwa Spika, tarehe 23 hadi 25 Machi mwaka huu, tulikutana Msekwa na ukaja Muswada wa Serikali. Muswada huu tuliupitia sote barabara na kwa kina na baadaye tukafanya maamuzi, baada ya kutokupata muafaka tukaja na maamuzi ya kupiga kura; kura tisa zilipatikana kwa Muswada wa Serikali na kura nne kwa Muswada Binafsi.

Mheshimiwa Spika, tofauti kubwa baina ya Muswada wa Serikali na Muswada Binafsi ni zifuatazo:-

Muswada wa Serikali una nia ya kujenga umoja, kuleta ushirikiano wa vijana katika ujenzi wa Taifa. Hili ni suala muhimu sana kwa sababu Baba wa Taifa alijikita zaidi katika ujenzi, umoja wa Taifa letu na huu Muswada ambao leo unasomwa hapa umejikita zaidi katika umoja wa kujenga Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Muswada huu unatokana na Sera ya Taifa ya Vijana ya mwaka 2007. Kwa hiyo, una msingi, umewekwa juu ya msingi maalum mzito, lakini Muswada Binafsi unaning'inia, hauna pahala pa kuanzia ulipoanza, umeletwa tu! Na hapa tunaambiwa kwamba Muswada wa Serikali ni *copy and paste,* lakini kama utausoma kwa kina utaona Muswada Binafsi ndiyo kwa kweli ni *copy* na *paste* na someni mtaona! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali kuanzia mwaka 2007 hadi leo ilipata nafasi ya kuwaendea watu mbalimbali kupata ushauri, kupata maelekezo, ndiyo baadaye ikaja na Muswada huu, lakini Muswada ambao ulikuja Binafsi

haukuangalia hayo, umeletwa kiharaka haraka na kwa kweli haukidhi haja ya kuja hapa na kupitishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa tuangalie labda faida nyingi ambazo Muswada huu unazo. Muswada huu utakuwa ni jukwaa la vijana katika kukabili changamoto mbalimbali. Vijana wana changamoto mbalimbali, wana tatizo la ajira, tunajua kwamba sasa hivi wanafunzi tele tu wanamaliza kila mwaka wanatafuta ajira na wengi wapo vilevile hawana ajira. Kwa hiyo, hili litakuwa ndilo jukwaa maalum la kuweza kutatua matatizo yao. Lakini vilevile kuna elimu ya juu sasa hivi, mikopo haitoshi, wengi wanakuwa wanabakia nyumbani hawana mikopo; hili vilevile litakuwa ni jukwaa kwa ajili ya vijana.

Mheshimiwa Spika, vilevile Muswada huu ukipita, utaweza kusaidia kutoa ushauri kwa Serikali ili Serikali iweze kusaidia katika mambo mbalimbali. Mfano, katika mambo ya dawa za kulevya, mambo ya maadili na mengineyo. Kwa hiyo, Bodi hii itakuwa na ushauri wa kuishauri Serikali katika mambo haya.

Mheshimiwa Spika, labda kwa kumalizia niseme tu kwamba, *point* ya Waziri kuwa ana umri mkubwa naona sio kitu ambacho kina mantiki kuzungumzwa hapa, kwa sababu umri wa Waziri hauhusiani kabisa na kuleta hii Bodi hapa. Kwa hiyo, nafikiri msijikite zaidi katika masuala ya umri, bora mngeleta *points* ambazo zingeweza kusaidia katika… *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuchangia.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwanza kabisa niwape pole sana Wabunge wenzangu waliomaliza hivi karibuni hasa wa upande wa Upinzani kwa sababu wanavyotegemea kitu kizuri kitoke upande huo wa kwenu, wanakuwa wanategemea kitu ambacho hakiwezekani kabisa, hawajui kama mmechoka.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka niwape pole akina Mheshimiwa Mkosamali na Mheshimiwa Silinde, kwa sababu matarajio yao kwamba kitu kizuri kinaweza kutoka upande huo wa pili, ni kosa kubwa kabisa! Ni sawa sawa na kufikiri mapambio yanaweza yakaimbwa kuzimu.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia hii sheria ama huu Muswada unaopendekezwa, tatizo kubwa ni Serikali kukosa fikra chanya ni namna gani inaweza ikatatua tatizo la ajira la vijana. Na sasa mnakuja na Miswada mbalimbali ukiwemo huu mkifikiri kuwepo na Baraza la Vijana kunaweza kukasababisha ama kukaleta tija katika maisha ya vijana.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Vijana la Tanzania lisingekuwa la msingi sana leo kama Serikali ingekuwa imeimarisha viwanda, Serikali ingekuwa ina

mashamba, Serikali ingekuwa imeboresha reli yaani ni rahisi kusafirisha mizigo, inge-*cut inflation,* Serikali ingekuwa na miradi mbalimbali ambayo vijana wengi wangeweza kuajiriwa.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia madhumuni au makusudi ya Baraza la Vijana, huoni ni wapi Baraza limeelekezwa litakuwa na mkakati wa kutafuta fedha kwa ajili ya vijana. Kama Serikali yenye *TRA,* yaani inayokusanya kodi imeshindwa kuwasaidia vijana, imeshindwa kutengeneza nchi, leo Taifa hili halina kazi, asilimia kubwa ya vijana wako mitaani, hakuna ajira, mkafikiria kuwa na Baraza la Vijana linaweza likatatua shida za vijana, huko ni kufilisika akili.

Mheshimiwa Spika, vijana hawataki Mabaraza! Kila Chama kina Baraza lake, CCM wana UVCCM, CHADEMA wana BAVICHA na vyama vingine. Vijana kwa wakati huu wanataka kuona Serikali inajenga barabara vijijini, kuona Serikali inajenga vituo vya afya vijijini.

Mheshimiwa Spika, ili kupunguza ongezeko la watu mijini ni lazima uimarishe maisha ya vijiji ambako watu wanatoka. Ukifanya hivyo, maana yake ni kwamba kule vijijini, mashamba yangelimwa, bidhaa zingepatikana na barabara kama zingekuwa ni nzuri kungekuwa na *supply* ya kutosha ya vyakula ambayo ingeweza kupunguza hata *inflation* na maisha kuwa mepesi kwa sababu, kuna *connection* kati ya vijijini na mjini na kuishi vijijini isingekuwa ni jambo gumu.

Mheshimiwa Spika, lakini inaonekana sasa kama Baraza hili litakuwa ni *solution* ya maisha ya vijana. *Solution* ya maisha ya vijana ni Serikali kujua wajibu wake kwa wananchi wote, ni Serikali kuwa na msingi na fikra chanya kuhusu ukombozi wa uchumi wa Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, leo vijana walioko mitaani ambao hawana kazi, hata ukiwatengenezea Baraza kwenye Taifa ambalo kiwango tu cha riba cha ukopaji wa fedha, kama unataka kufanya biashara leo katika Tanzania, ukikopa fedha katika *commercial bank,* benki za ndani, riba ni kati ya 18% na 22%, yaani maana yake ni kwamba, mtu anayechukua mkopo wa milioni 100 benki, kwa mwaka anatakiwa kulipa milioni 22 kama riba!

Mheshimiwa Spika, hata mkitengeneza Baraza la Vijana la aina gani wakati riba zenyewe za kwenye *commercial bank* ambako watu wanatakiwa wakakope fedha kwa ajili ya biashara, kiwango chake ni kama hicho, huwezi kabisa kuleta ukombozi katika Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, kama leo mabenki yetu yangekuwa na riba chache na riba ndogo katika utoaji mikopo ya kibiashara, leo nchi hii ingeweza kuwa na viwanda vingi, watu wangeweza kukopa fedha nyingi wakafanya *long term*

*investiment* ambayo ni pamoja na viwanda. Lakini inashindikana kuwa na *long term investiment* kwa sababu riba ni kubwa, kwa hiyo, viwanda vya watu binafsi vinakosekana, viwanda vya Serikali vinakosekana, na ndiyo sababu kwenye Bunge hili hili, Wizara ya Viwanda na Biashara ilishawahi kutamka kwa kinywa kwamba wamekosa bilioni 20 na wanatafuta dola milioni moja kumlipa mtu wa *Continental* ili aweze kuachia hisa zake *General Tyre.*

Mheshimiwa Spika, sasa kama Serikali inaweza ikakosa bilioni 20 ili kufufua kiwanda cha matairi, ikakosa dola milioni moja kumlipa mbia wa *Continental* ili ile hisa yote iwe ni ya Serikali, hata ukiwa na Baraza la aina gani huwezi kusaidia nchi.

Mheshimiwa Spika, ili vijana wa Kitanzania waondokane na ukosefu wa ajira na maisha magumu ni lazima kabisa muelewe mfumo wa uchumi unavyo-*operate,* muelewe mabenki yetu na riba zake, lakini ni lazima viongozi wawe na *attitude.*

Mheshimiwa Spika, wenzangu wamemlalamikia Mheshimiwa Waziri, pamoja na *style* yake nzuri ya nywele na umri wake, lakini umri unaweza ukawa sio kigezo sana. Lakini mimi niseme kabisa Baraza hili la Vijana halitakuwa na tija kama mambo ya msingi katika Taifa hili hamtayaangalia ikiwa ni pamoja na kujenga viwanda.

Mheshimiwa Spika, leo Dar es Salaam kuna kitu kinaitwa Kurasini sijui nini, maana yake ni kwamba bidhaa zote zinazotengenezwa China sasa zitakuwa zinaletwa Tanzania na kutakuwa na *major wholesale* ya Wachina; maana yake ni kwamba unaenda kuua *exposure* ya Watanzania waliokuwa wanasafiri kwenda kutafuta vitu ambao walikuwa wanapata pamoja na *exposure,* safari yao itaishia Dar es Salaam. Ukisikiliza lengo kipindi kile wanajadili humu Bungeni, ilikuwa ni kwamba Wazambia watakuja, Wazimbabwe watakuja kununua vitu na kitakachopatikana ni hela ya *guest* na hela ya chakula na hela ya chips.

Mheshimiwa Spika, huwezi kuwasaidia vijana kwa kuongeza Mabaraza. Huwezi kuwasaidia vijana kwa kuongeza Mabaraza, utawasaidia vijana kwa kujua mfumo wa uchumi unavyo-*operate* sasa, utawasaidia vijana kwa kufufua viwanda vilivyokufa, utawasaidia vijana, leo hata bodaboda iliyokuwa inaonekana ina madhara makubwa, Serikali imeifanya ni sehemu ya mapato muhimu na mnawasumbua vijana wa bodaboda mitaani!

Mheshimiwa Spika, Serikali hii imeishiwa fedha mpaka *traffic...,* na Mheshimiwa Chikawe anisikie, *traffic* barabarani wamepewa *target* ya kukusanya mapato. Yaani makosa ya barabarani ni chanzo cha mapato ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kulipa watu mishahara. Leo barabarani kila gari limepewa *target.*

Mheshimiwa Spika, Arusha gari moja ya *traffic* wanatakiwa wakusanye shilingi 1,500,000/= kwa siku! Wamepewa *target* ya karibu bilioni tatu kwa siku! Kwa hiyo, sasa hivi hata ukikutwa hujafunga mkanda ama unacheka, lazima ulipe *fine* kwa sababu hizo ndiyo posho zinaletwa Bungeni ili Mheshimiwa Spika uwalipe Wabunge wako waweze kukaa hapa.

Mheshimiwa Spika, sasa kama Serikali imekosa fikra ya ku-*create mechanism* ya kutafuta fedha kwenye nchi yenye rasilimali kama hii, inaanza kutumia *traffic* barabarani kukusanya mapato na posho za Wabunge na mishahara ya walimu, Serikali hii inakopa fedha kwenye mabenki ya biashara yenye riba 22% …
*(Hapa sauti ilikatika ghafla)*

**SPIKA:** Angalau umejadili. Mheshimiwa Gekul, Mheshimiwa Mangungu, halafu Mheshimiwa Msigwa.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana umenipa nafasi na mimi nitoe maoni yangu machache katika Muswada wa Baraza la Vijana ambao uko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, kuna usemi wa Kiingereza unasema; *whenever purpose is not known, the abuse is inevitable* (panapokuwa na sababu ambazo hazijulikani, basi usitegemee kwamba yale mambo uliyoyataka yatatekelezwa).

Mheshimiwa Spika, Muswada huu wachangiaji wengine wamezungumza vizuri sana, wameeleza ni kwa jinsi gani Muswada umeletwa baada ya kuona kwamba Mbunge mwenzetu amefanya *initiatives* za kuleta Muswada, lakini Serikali ikaona ije mbio mbio sasa waweze kum-*pre-empt* Mheshimiwa Mnyika, ndiyo maana Muswada umejaa upungufu mwingi sana.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia Muswada huu ulipaswa tu utendewe haki, kwa sababu ni kilio cha vijana cha muda mrefu, kwa sababu ni mahitaji ya vijana kwa muda mrefu. Lakini kwa sababu Serikali yetu lazima ishituliwe kidogo ndiyo ifanye kazi, Mheshimiwa Mnyika alivyoishitua, ndiyo maana unaona Serikali ilikuja mbio ku-*copy* na ku-*paste* Muswada ambao wengine wanasema umetoka Kenya na maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, *purpose* ya Muswada huu, sababu hasa ya Muswada huu ni nini? Ukiangalia kwenye sehemu ya *objectives* na *functions* za Baraza zimefinywa sana na mambo mengi ambayo vijana wanahitaji katika Taifa la Tanzania kwa sasa hayajaelezwa kwenye maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana huwezi kuepuka marekebisho mengi katika Muswada huu kwa sababu Serikali haikuwa na maandalizi ya kutosha katika maandalizi ya Muswada huu, na hili limeanza kujionesha na wewe ni shahidi kwamba hata sasa marekebisho bado yanajadiliwa na Kamati kwa sababu yeyote aliyeko humu hakuridhika na Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, nchi za Maziwa Makuu katika vikao vyao ambavyo vinafanyika mara kwa mara, wameanza kulibaini hili kwamba vijana wasipodhibitiwa mapema wakapatiwa wanayoyataka wao, ni bomu kwa mataifa yetu.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba vijana hawa wanapokosa masuala ya msingi katika nchi zao, masuala ya ajira, mikopo kwa ajili ya elimu zao katika vyuo vikuu na maeneo mengine, vijana hao wanajiunga kwenye vikundi ambavyo unasikia vya magaidi na vitu kama hivyo. Kwa hiyo, Serikali ijitafakari ni kwa nini huu upungufu wote umeonekana katika Muswada huu wa vijana. Je, nia yenu ni ya dhati kuwasaidia vijana wa Kitanzania?

Mheshimiwa Spika, leo kama tutakuwa wakweli na wazalendo katika nchi yetu ya Tanzania, tatizo kubwa la vijana ni ajira na hili ni bomu la muda mrefu sana na ni kwa sababu pia nchi yetu tumeua viwanda, nchi yetu hatusikilizi chochote, Watanzania tumekuwa wamachinga, hakuna chochote tunachozalisha, vijana hawa wanaotoka kwenye vyuo vikuu hawajui pa kukimbilia hata wapate mitaji.

Mheshimiwa Spika, asubuhi tulikuwa tunahoji masuala ya *Pride Tanzania* hapa asilimia 30 ya riba katika mikopo. Hata taasisi za benki, vijana hao hawana *access* na hizo taasisi za Benki.

Mheshimiwa Spika, lakini angalia sasa tuna mifuko mingi sana ya vijana, mingine iko Wizara ya Kazi, Wizara ya Maendeleo na Vijana, pesa zingine ziko Halmashauri, pesa zingine ziko wapi…, lakini Muswada huu hausemi na haujaeleza kabisa kama vijana hao wanaweza wakawa na benki yao, vijana hawa wanaweza wakawa na mfuko wao.

Mheshimiwa Spika, Wabunge wengine wamesema kwamba Wizara mnakuwa na wasiwasi, mnashituka shituka, mnakuwa hamjielewi elewi katika suala la pesa. Ndiyo maana hata kwenye Muswada huu ukisoma, wanazungumza masuala ya yule *Secretary General* anateuliwa na Waziri, lakini pia Mwenyekiti anateuliwa na Waziri na wengineo wengi wengi.

Mheshimiwa Spika, Muswada umekuwa wa kibaguzi sana ndiyo maana nasema hamjaufanyia maandalizi. Muswada umekuwa wa kibaguzi katika suala la uanachama, mmesema kwamba wanachama hawa lazima watokane

na *NGO* mbalimbali na taasisi ambazo zimesajiliwa, lakini sisi Wabunge au mimi pia nashauri kwamba suala la watu kujiunga kwenye Baraza lao la Vijana liachiwe huru kila mmoja awe huru aingie kwenye Baraza anavyotaka tangu hapo umri unaruhusu.

Mheshimiwa Spika, lakini pia Muswada huu umekuwa wa kibaguzi katika suala zima la *structure*, naangalia hata kwenye Muswada wenu mlioleta hata *national level* ilikuwa haipo, sasa ndiyo mnaleta kwenye *amendment* ya Serikali. Muswada huu unatakiwa uoneshe *structure* yote kama ni *national level, regional level, district level,* kama ni kwenye Kata, kama kwenye Mitaa, kwa sababu lengo ni nzuri ni kupata hawa vijana watoe maoni yao katika Baraza lao.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, *structure* nzima tu ya Baraza la Vijana ambalo limeletwa na Muswada huu pia ni ya kulipua tu, imeeleza kwa Mkoa na kwenye Wilaya. Kwa hiyo, Waziri hataepuka *amendments* za kutosha katika Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umekuwa na ubaguzi katika uteuzi, kuna Wajumbe wanateuliwa na Waziri katika ngazi hizo za Mikoa na Wilaya. Kwa nini Wajumbe hao wasiingie tu kwenye Baraza, kwa nini wateuliwe mpaka na Waziri, mna wasiwasi gani? Hata kama ni kuwabana kiasi hicho, mnafikiri mtawazuia vijana wasitoe maoni yao mkiwateua? Kwa sababu unaweza ukawateua lakini mwisho wa siku wasiongee lugha yako unayotaka. Na huu Muswada sasa ni baguzi katika eneo pia la uteuzi, una Wajumbe wa kuteuliwa, kuna Wajumbe wanatoka *NGO* mbalimbali na vitu vingine ambavyo havieleweki kabisa na vijana wala hawawezi kuwaelewa.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umekuwa baguzi pia katika suala zima la kulipa posho za vikao. Kuna posho mnalipa ninyi Wizara, kuna posho zinalipwan a Serikali za Mitaa huko, kwa hiyo, Muswada ambao Serikali haielewi *purpose* ya Muswada huu ni nini.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana ni vizuri tu tukawatendea haki Watanzania vijana ambao ni asilimia kubwa kwa sasa, tuwajengee mazingira katika sheria hii, kila kijana katika suala la *membership* aingie anavyotaka yeye tangu hapa anajisikia kujiunga na Baraza hili ili atoe maoni yake katika kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, katika Muswada imeelezwa kwamba vijana hawa watakuwa wanatoa ushauri katika ngazi za Serikali, ngazi za Mikoa, ngazi za Wilaya, lakini pia mwanzoni sijui kwenye marekebisho sasa, ambapo hamjaweka hata *national level* na hizi ngazi za chini, maana yake hawa vijana mlikuwa hamtaki hata ushauri kwenye ngazi zingine.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Wabunge wakiongea, tukizungumza suala la Serikali kukimbilia Miswada pale inapoona Wabunge wanafanya *initiatives* za kuleta Miswada, ndiyo mambo haya mnaleta chakula hakijaiva, ndiyo maana mnaleta *contradiction* nyingi sana. Haiwezekani, hayaingii kwenye akili ya yeyote, Mwenyekiti wa Baraza la Vijana eti ateuliwe na Waziri. Hiki kitu hakipo, wala msikizungumze, hata vijana wa Kitanzania hawatakiwi kujua mambo hayo ambayo mpaka sasa mnayaendeleza.

Mheshimiwa Spika, hivi unasema kijana kwenye ngazi ya Baraza la Taifa awe na elimu ya *degree,* kwenye ngazi ya Mkoa mbona hamsemi, kwenye ngazi ya Wilaya mbona hamsemi elimu ya huyo kijana? Lakini mbona kwenye ngazi za Kata na huku chini hamsemi kwamba awe na elimu gani huyo Mwenyekiti au mnataka wote wawe na *degree*; na wakati wa Bunge la Katiba tulisema tuanze na sisi, mbona hamkutaka Wabunge tuwe na *degree,* mlitaka tuwe na darasa la saba? Hili la elimu pia lijadiliwe kwenye ngazi, kama ngazi ya Taifa ni elimu fulani, basi na ngazi zingine waangalie.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, Muswada pia umetaja Kamati mbalimbali ambazo zitaundwa. Ukitafuta hizo Kamati *composition* yake ikoje, hiyo Kamati inafananaje, ni Kamati ya masuala ya *agriculture* au masuala ya ajira, au masuala ya UKIMWI? Hizo Kamati hazisemwi kabisa kwenye Muswada, zimetajwa tu kuna Kamati zitaundwa, hazieleweki.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana tangu asubuhi leo nimeanza kujadili huu Muswada, nimesema ni Muswada ambao Serikali imekurupuka, wakauleta mbiombio kuzima hoja ya Mheshimiwa Mnyika, hilo mtake msitake ndiyo ukweli, inabidi tu mkubali! Haiwezekani hata hizo kamati tu hazipo kwenye maana huku, unapoangalia ni kamati za namna gani na *composition* zikoje, hamtaki kuzisema, hamjaeleza kwenye Muswada. Halafu sasa kweli Waziri anakuja ana-*present* Muswada haueleweki mbele wala nyuma, unaishia tu ngazi ya Mkoa na Wilaya! Hivi ni *structure* ya wapi katika nchi hii, mfumo upi huo? Hivi hata *Decentralization by Devolution* ndiyo iko hivyo kweli?

Mheshimiwa Spika, ni vizuri tuwape vijana kile wanachokitaka. Muswada huu basi katika *functions* zake uzungumzie masuala ya ajira, vijana wa Kitanzania wanapata wapi *networks* za ajira, vijana wa Tanzania wanaokwama hawapati mikopo katika elimu ya juu, Baraza hili linawasaidiaje?

Mheshimiwa Spika, halafu lingine, suala la pesa, Wizara kukaa na fedha za vijana, hapana! Hili Baraza lihakikishiwe lina *funds* za kutosha, lina pesa za kutosha, halafu waweze kuendesha Baraza vizuri. Lakini cha kusikitisha hata kwenye Muswada mme-*stipulate,* mmeeleza kwamba hata marafiki wa Baraza hili Mheshimiwa Waziri mpaka uwajue.

Mheshimiwa Spika, hivi hata kama mnasema ni *pressure group,* hivi *pressure group* inaanzia wapi? Kama vijana wana kazi, wako *busy* kazini, viwanda vipo, nchi hii inaeleweka, unafikiri hao vijana hizo *pressure group* watafanyia wapi?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, haiwezekani Serikali iliyopo madarakani ikawa inazima yaani masuala ya vijana kwa kuwabana uteuzi mara mpaka sijui mpaka tuone na marafiki zenu, kana kwamba mtawasaidia au mtawazuia hao vijana kudai haki zao. Ni vizuri Serikali ikawa na upole katika haya, iyarekebishe.

**SPIKA:** Ahsante. Sasa nitamwita Mheshimiwa Mangungu, atafuatiwa na Mheshimiwa Msigwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Paresso, halafu atafuatiwa na Mheshimiwa Lusinde.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Nakushukuru kunipa nafasi na mimi niweze kuzungumza kuchangia Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, inaweza ikafika wakati ambapo Bunge lako…

**SPIKA:** Mheshimiwa Lema, inakuwaje unamkata Spika! Haya tunaendelea. Mheshimiwa Mangungu. *(Kicheko)*

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Naomba dakika zangu zihifadhiwe.

**SPIKA:** Unaanza upya, haya!

**MHE. MURATAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru.

Mheshimiwa Spika, Bunge hili linaweza likafikia wakati likawapotosha sana wananchi. Tumemaliza Muswada wa Sheria ya Bajeti wiki iliyopita, siku ya Ijumaa. Kwenye Muswada ule maelezo ya awali yaliyotolewa na Waziri, maelezo ya awali yaliyotolewa na Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti na maelezo ya awali yaliyotolewa hata na Msemaji wa Kambi ya Upinzani, walisema kwamba tulikuwa na Miswada miwili, kulikuwa na Muswada uliotungwa na Kamati na kulikuwa na Muswada wa Serikali, tulikaa pamoja, tukashirikiana, tukaunda Muswada mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa leo hii umekuja Muswada mwingine, imegongana, kuna Miswada miwili, baada ya kuunganishwa, huo Muswada mwingine inaelekea ulitungwa na malaika ukaletwa humu Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi Wabunge ambao ndiyo tunajifunza kutoka kwenu, ni kweli itafika wakati tutatoa mfano mbaya sana, haiwezekani tukawa na

Bunge la watu kuja kushutumiana, kulaumiana, kutukanana, kusemana na kutoa mifano ya vitu ambavyo hata havipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utungaji wa Miswada, ukiletwa Muswada hapa zipo Kanuni zinazoelekeza mtu yeyote ambaye anaona kwamba kuna kipengele kinatakiwa kifanyiwe marekebisho, unaleta *amendment*, kinakubalika, unashawishi Wabunge, tunapiga kura, mambo yanakwenda na sheria inatungwa. Sasa iwe wewe lazima ufanya na lisipokubalika lako, unauumwa. Mimi nakuambia kama utalitamani kila jambo liwe, siyo kuumwa tu, hata kufa utakufa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, wengi hapa wanachangia wanasema Muswada huu umekuja hauna malengo, hauelezi. Hata hawasikilizi, wanaenda kufuata mambo ya mbali, Kenya, Marekani, sijui wapi.

Mheshimiwa Spika, ukisoma aya ya tano ya hotuba ya Waziri, naanzia na katikati, imesema Baraza litakuwa jukwaa rasmi la vijana kuweza kuzungumzia masuala muhimu yanayohusu maisha yao ikiwa ni pamoja na kubaini changamoto zinazowakabili, kubuni mikakati ya kuzitatua kwa maana ya kuzitekeleza, kuishauri na kuisaidia Serikali katika utekelezaji wake. Unataka malengo gani uelezwe wewe zaidi ya haya? Unaenda kuhangaika na mambo mengi ya kuvuka mipaka, unakwenda wapi na kusema ooh, mara Waziri sijui… mbona wengine hapa ni vijana na wana mambo ya kizee na tunawajua. *(Makofi/Kicheko)*

Sasa niwape habari, huu Muswada mnaoung'ang'ania ninyi kusema kwamba huu ni wetu ulikuwa wa fulani, siyo wake na kama anapinga hili, alioshirikiana nao wapo.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2001 wazo la uanzishwaji wa *East African Youth Coalition* iliundwa na Mheshimiwa Amos Makalla, Mheshimiwa Emmanuel Nchima, Dkt. Deodaraus Kamala, Mheshimiwa Livingstone Lusinde akiwa Chama cha *CUF* na yeye Mheshimiwa John Mnyika akiwa mwanafunzi wa shule ya sekondari ya Tambaza. Sasa wewe ukienda kuzihifadhi *documents* ukakaa nazo, halafu kesho ukaja hapa ukasema hizi zangu, wewe unaweza ukaumba lipi jipya dunia hii? Haya yote tunayosema yalishasemwa, yalishafanywa, yalishatekelezwa, sisi tunayofuata ni vile yalivyofanyika na sisi tunaishi tu na dunia hii tutaiacha tutaenda huko, usijione ni Nabii mpya katika dunia hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati huo *document* hiyo ambayo inazungumziwa, muasisi, Waziri alikuwa ni Ndugu Sebastian Kinyondo na Naibu Waziri wake alikuwa ni Mheshimiwa Lukuvi. Sasa hawa nao walikuwa vijana au walikuwa

wazee? Maana yake tunataka kuhamasishana vitu ambavyo havipo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, lakini ni jambo la kujiuliza pia, hivi sisi wazazi wetu ni vijana au wazee, tunawatoa maana huko nyumbani? Maana yake ni mambo ambayo ya kuuliza? Spika huyu kwa kuwa ni Mbunge mwenzetu, pamoja na utu uzima wake, tumekuwa tukimsema tu kama mtoto mdogo, haiwezekani, lazima mheshimu watu! Ninyi mnaamini mmejizaa? Haiwezekani mambo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yapo mambo mengi sana ambayo yamesemwa; changamoto za vijana tunazozizungumzia hapa, maana nayo vilevile ufundi mwingi unaweza ukajigonga nyundo kwenye vidole. Mheshimiwa Lema hapa anasema kwamba matatizo ya vijana siyo Baraza, lakini wenzie waliotangulia kusema wanasema matatizo ya vijana ni hili Baraza, lakini lilitakiwa liletwe na Mbunge fulani, aah, tuamini lipi sasa kati ya haya? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nataka niseme ipo changamoto kubwa sana kuweza kuwakwamua vijana katika matatizo yanayowakabili, na changamoto hii haiwezi kuwa ya Mbunge, haiwezi kuwa ya Serikali, haiwezi kuwa ya mtu mmoja, hii ni changamoto ya Taifa kwa vijana wenyewe kupata mbinu za kujikwamua.

Mheshimiwa Spika, na sisi kama watunga sheria na watunga sera tuwasaidie kuwawekea mipango itakayoweza kuwasaidia, siyo tunakuja hapa kucheza mchezo tu wa siasa kuwaeleza kwamba sisi ndiyo tunaweza tukawa wema zaidi kulikoni hao wengine. Umefanya lipi hata moja ambalo unaweza ukatuambia kwamba katika kusaidia vijana mimi nimefanya hili moja, zaidi ya kuwashiwishi kwamba waende kupita barabarani wanapoteza jasho na nini bila kuwa na kazi maalum ambayo inatakiwa ifanywe? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, changamoto zilizopo kwenye Muswada huu, pamoja na mambo mengine, wamezungumzia wengine kwamba kwa nini huyu mtendaji awe anateuliwa, mtendaji anateuliwa kwa sababu moja kati ya vyanzo vya mapato vitatokana na fedha za umma na CAG atakuwa anakagua huu mfuko!

Mheshimiwa Spika, sasa lazima kuwe na mtu ambaye anawajibika, hatuwezi tukabuni tu tukawa na watu tu ambao hatujui wanatokea wapi. Tumeona changamoto kubwa sana kwenye vyama vya siasa, hela za ruzuku zinakwenda lakini tunaona vioja tu, tunaona vioja vikubwa na hatujawahi kusikia kama hivyo vyama hata vimewahi kusaidia hata siku moja kujenga hata choo, lakini fedha zinakwenda na watu wanaendelea na maisha yanakwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hili la Mtendaji Mkuu kuteuliwa na Waziri ni lazima liwepo kwa sababu zitakuwa zinaenda fedha za umma na ni jambo la msingi linalotakikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na mengine, najua wachangiaji wengine wameyasema vizuri, naomba niunge mkono hoja na tusiwe na mawazo ya kuwa tunapinga kila jambo, matokeo yake tunaweza tukaamini kwa kupinga hata Mungu kama yupo.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kidogo.

Mheshimiwa Spika, tumekusanyika hapa kwa pamoja kama Wabunge kwa mustakabali wa Taifa letu, tuchangie mawazo ya pamoja kwa ajili ya kuuboresha Muswada huu. Lakini naomba niseme kidogo kwamba sisi ni matokeo ya kizazi kilichopita, niliwahi kusema siku moja, *we are the product of previous generation but not prisoners of the previous generation* (sisi ni matokeo ya kizazi kilichopita lakini sisi sio wafungwa wa fikra na mawazo yaliyopita). Na sisi kama kizazi cha leo tunawajibika kwa *generation* ya kwetu na kuiandaa *generation* inyaokuja.

Mheshimiwa Spika, nasikitika ndugu yangu Mheshimiwa Mangungu amegeuka, amekuwa yeye ndiyo Serikali, anajaribu kutoa majibu ya Serikali wakati Waziri mwenye hoja atakuwepo hapa na atatoa majibu. Hatuna haja ya kutupiana madongo hapa, tunahitaji tuangalie tatizo la vijana wetu na namna gani tuweze kulitatua.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walipiga kelele)*

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Tukitaka kupiga kelele hata mimi naweza nika-*shout* na madebe matupu ndiyo yanapiga kelele. Mimi ni zamu yangu nimepewa, mnipe nafasi. *Why are you shouting? Listen!* Sikiliza vizuri.

Mheshimiwa Spika, tuko hapa kwa ajili ya kujenga Taifa letu kama Wabunge, tatizo ni fikra ambazo ziko kwenye vichwa vya watu, tunataka tutunge sheria ambazo zinalinda ukomo wa uongozi wetu, hatujui hata *lifespan* ya kwetu.

Mheshimiwa Spika, tunalalamikia madaraka makubwa anayopata Waziri, tulishuhudia juzi hapa wakati wa Bunge la Katiba, tena Waziri huyu huyu, Mheshimiwa Tundu Lissu anaongea hapa, aliamrisha *TBC* wazime, ndiyo maana

tunapinga Miswada kama hii ambayo madaraka makubwa anayo… ndiyo ni kweli! Ndiyo maana tunasema madaraka mna…

**SPIKA:** Waheshimiwa, naomba tutulie tujadili tu, ila sasa kila mtu atoe *facts* za kutunga sheria, *rubber stamps* zinatokana na hivyo, watu hawajadili halafu wana *rubber stamp*. Haya tuendelee.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, tatizo wengine wanajibu hoja wakati wao sio watoa hoja, inatulazimu na sisi tujibu sasa, kwa sababu wanajibu hoja wao hawajatoa hoja hapa.

Mheshimiwa Spika, tunapinga mamlaka ya Waziri kwa sababu tumeona madaraka yanatumiwa vibaya watu wanapokuwa kwenye nafasi hizi. Vyombo kama hivi, Baraza kama hili na maeneo mengine yanatumika kisiasa, watu wanaona kama hii ni *platform* ya kisiasa na ndiyo maana tunataka Baraza hili kiwe chombo huru.

Mheshimiwa Spika, leo ukisema Waziri ahakikishe anaweza kuwachagulia marafiki vijana, unawanyima fursa, kwa sababu vijana hawa atalazimisha achague wale wenye mrengo wa chama chake, tutageuza hiki chombo kianze kutumika kisiasa. Tunataka vijana wote ambao bila kujali itikadi zao za kisiasa wakiingia kwenye chombo hiki wawe huru kutoa mawazo yao.

Mheshimiwa Spika, vijana wa leo wako *responsible* kwa *generation* yao, wazee walikuwa na muda wao walifanya mambo mazuri na vijana wa leo wana kila sababu ya kujifunza mambo mazuri kutoka kwa wazee. Yapo mambo mazuri ambayo wazee walitufundisha, lakini kuna mambo ambayo wazee waliyafanya hayatufai katika *generation* ya leo, wana haki ya kuyakataa. Bado sasa hivi tuna wajibu wa kuandaa *generation* inayokuja tuwawekee mazingira mazuri ambayo hawa watu watakuwa *innovative*, *creative* wanawaza mapana kwa ajili ya *generation* inayokuja.

Mheshimiwa Spika, leo Muswada huu unasema kwamba kanuni azitunge tena Waziri, yeye aanze ku-*control* tena kanuni katika chombo ambacho watakuwa vijana wenyewe wanataka kufanya mambo yao! Na ndiyo maana tumesema sisi siyo wafungwa wa kizazi kilichopita. Kizazi kilichopita kilikuwa na mambo mazuri na mabaya, lakini yale yaliyofaa kwa wakati wake.

Mheshimiwa Spika, hili Bunge lazima liwe Bunge la kimapunduzi, hatuwezi kuendelea kuwa na Bunge ambalo lina mawazo ya mwaka 1965. *Challenges* za sasa hivi sio za miaka ya 1965, siyo za miaka 1975, sio za miaka ya 1980. *We have got our own challenges*, vijana wana *challenges* zao, lazima tuwape *freedom*, vijana wa sasa hivi hawataki kufungwa fungwa, *they want to think on their own.*

Mheshimiwa Spika, mtoto ukimfunga funga hawezi kufikiri, tuwaache vijana wafikiri, tutafute chombo kingine ambacho sio cha kisiasa ambacho kita-*regulate* kama wanakosea, na bado tuna wazee ambao tutawapa ushauri. Ndiyo maana tunasema mamlaka hizi ambazo tunataka tu-*invest* tena kwa Waziri ni mamlaka ambazo zinaturudisha kwenye mfumo wa kisiasa siasa.

Mheshimiwa Spika, *life span* yetu tukiwa tunatunga sheria hapa ambazo zinaangalia miaka mitano ya kuwa kiongozi, hatulitendei haki Taifa. Miaka mitano unaweza kuwa kiongozi, baada ya miaka mitano unaweza usiwe kiongozi. Lakini tuwe na fikra ambazo zinaenda *beyond our generation* kwamba tunachokitunga hiki kinasaidia kizazi kinachokuja, kwa sababu hatimaye *as christians we believe* tunaishi miaka 70/80. Sasa tukianza kugombana hapa kwa *lifespan* ambayo ni ndogo, badala ya kuangalia mambo yenye tija na faida kwa Taifa letu, tutakuwa hatutendi haki. Na ndiyo maana mwenzangu Mheshimiwa Silinde amezungumza hapa kwamba lazima tujue lengo kuu la Baraza hili ni nini.

Mheshimiwa Spika, *Mazman Law* anasema *until purpose is known, existence has got no meaning* (ni mpaka makusudi yajulikane, kuwepo kwa hicho kitu hakuna maana). Lazima kama Taifa, kama Wabunge tukae, huu Muswada tunautunga wa nini, hatima yake ni ustawi wa Taifa letu, hatimaye tunataka tuwe na vijana wazuri, tuwe na vijana ambao wanaweza kujitegemea.

Mheshimiwa Spika, lazima tujue malengo makuu ya Muswada huu ni nini, ni *political platform* kwamba watu watumie hili jukwaa kwa ajili ya kujinufaisha kisiasa au tunataka tuwakwamue vijana wetu wahame katika hali ya uduni waende mbele? Haya ndiyo masuala ambayo kwa pamoja tunatakiwa tujadiliane badala ya kutupiana lawama ambazo hazina maana.

Mheshimiwa Spika, hoja ya Mheshimiwa Mnyika ilikuwa siyo mbaya, ni ya kujenga. Lakini vilevile kama Wabunge sio jambo jema kwamba tunamaliza miaka mitano hakuna Mbunge hata mmoja anaingiza Muswada Binafsi unapita, Bunge la Tisa hivyo hivyo. Hayo ni masuala ya kujiuliza, tunakuja hapa kufanya nini? *This is a chamber of dialogue*, watu lazima wa-*dialogue*, watu wa-*reason* watu wa *question*, watu wa-*argue*. Tu-*reason* kwa pamoja, lakini wengine ni mafundi wa kuzomea tu, unazomea, toa hoja yako basi, hakuna!

Mheshimiwa Spika, mimi ningeshauri tushirikiane wote kwa pamoja, lengo ni ustawi wa Taifa letu, lengo sio kuzomeana, lengo sio nani bingwa wa kupiga makofi hapa, lengo ni kujenga hoja ambazo zitaleta ustawi wa Taifa letu, hatimaye tuache kizazi kinachokuja kiwe katika mazingira bora zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi niseme, ningeomba hizi *posts* za kisiasa na ninavyozungumza kwamba Waziri asiwe na mamlaka makubwa siku-*target* wewe, mimi nazungumza Uwaziri. Maana kesho sio lazima uwe Waziri wewe na bahati nzuri Serikali ijayo hamtakuwa Mawaziri ninyi.

Mheshimiwa Spika, sasa lengo ni kuangalia hii nafasi ya Uwaziri na usiangalie kwamba nchi hii itakuwa inatawaliwa na ninyi tu, tunaangalia zisiwepo nafasi za kisiasa ambazo zinawabana hawa vijana, hawawezi kufikiri kwa upana, hawawezi kudadisi, hawawezi kuhoji, lazima tuwape *freedom,* waogolee, wahoji, wadadisi, ndiyo uvumbuzi umetokea duniani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ombi langu, hatuna sababu ya kutupiana vijembe. Sisi wote tunajenga nyumba moja, nyumba njema na nzuri kwa ajili ya kizazi kinachokuja.

Mheshimiwa Spika, Profesa wangu aliwahi kuniambia, ukifika mahali kama huwezi kupafanya pawe bora, acha kama palivyo, wajibu wetu ni kuiacha Tanzania iwe bora kuliko tulivyoikuta badala ya kutupiana vijembe.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mangungu, amenishangaza leo, haoni kama hata maandamano ni haki ya msingi, Mbunge mzima huoni kama maandamano ni haki ya msingi, *we are not even begging, that is our right, one of our rights we need to exercise*. Sasa watu wanashangaa hata maandamano yako Kikatiba, Mbunge unashangaa maandamano! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Paresso, atafuatiwa na Mheshimiwa Lusinde na Mheshimiwa Mtanda.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia. Nitakuwa na mchango mchache tu kwa sababu ukiwa mchangiaji wa mwisho mambo mengi yanakuwa yameshasemwa.

Mheshimiwa Spika, pia nimpongeze Mheshimiwa Mnyika, pamoja na kwamba Muswada wake haukufika hatua ya mwisho kujadiliwa, lakini angalau amejitahidi na nafikiri apongezwe sana kwa sababu hakuna Mbunge yeyote ambaye ameweza kuandika Muswada Binafsi na angalau hata kufikia hatua ya Kamati, hakuna hata mmoja.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni Mheshimiwa Mnyika amejaribu, anapaswa kupongezwa sana, lakini pia baada ya Mheshimiwa Mnyika kuwasilisha na ndiyo Serikali ikakumbuka na yenyewe ikaanza kuandika. Maana

yake bila Mheshimiwa Mnyika kuandika hata Serikali isingeleta, tungemaliza Bunge hili, Muswada huu usingeletwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo kama utangulizi, nina maoni machache ya jumla kuhusiana na Muswada huu. Kwanza kuhusu uanachama, Muswada umeeleza kwamba uanachama wa Baraza hili utakuwa wazi, lakini watakaokuwa wanachama ni vijana walioko katika asasi na taasisi; na kwa mujibu wa takwimu alizotoa Waziri wakati anasoma hotuba yake hapa, anaonesha vijana 6,800,000 tu ndiyo walioko katika taasisi na asasi, lakini jumla ya vijana wote nchi hii ni 16,200,000. Maana yake ukiwachukua vijana 6,800,000 waingie kwenye Baraza, bado umeacha kundi kubwa la vijana ambao kwa jumla yake wako takribani milioni 16 wanaachwa bila kuingia kwenye Baraza hili.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, suala la uanachama wa vijana kuingia kwenye Baraza hili, wawe ni vijana wote wa umri wa miaka 15 mpaka 35 na sio tu walioko katika hizi asasi ambazo Muswada unapendekeza.

Mheshimiwa Spika, lakini suala lingine ni muundo wa Baraza hili. Muundo wa Baraza hili kwa mujibu wa Muswada umeanzia ngazi ya Taifa mpaka Wilaya. Ukisema ngazi ya Taifa mpaka Wilaya maana yake ni kwamba hujawafikia vijana walioko vijijini na walioko katika kata. Maana tunahitaji tuchukue vijana walioko *level* ya chini kwa sababu ndiyo wana changamoto kubwa. Utawaacha walioko katika Wilaya wajadili masuala ya vijana na kuamua halafu wengi walioko katika vijiji na kata wasipate fursa hii. Tulipendekeza hayo na tulipeleka *schedule of amendment*, tulikaa na Serikali mchana, kuna baadhi ya mambo wameyachukua, tunaamini wataenda kuyaboresha na kuyafanyia kazi ikiwemo suala la Baraza kuanzia ngazi ya Kata, Wilaya, Mkoa na Taifa.

Mheshimiwa Spika, lakini pia suala la Waziri kuteua Mwenyekiti, ni vizuri tuwaache vijana wakafanya maamuzi katika Baraza lao. Unawapa mamlaka ya kisheria kuwepo kwa vijana, halafu Waziri unaenda tena kutaka kuteua Mwenyekiti wa Baraza la Vijana la Taifa, haiwezekani.

Mheshimiwa Spika, Waziri ni Mbunge, Waziri anatokana na chama cha siasa, maana yake anaweza akamteua Mwenyekiti anayetokana na chama chake au anaweza kumchagua Mwenyekiti ambaye anajua mwisho wa siku hawezi kumsumbua, ataweza ku-*maintain* na ku-*control* Baraza. Tuwachie vijana wachague uongozi wao, wasiingiliwe na Waziri, wasiingiliwe na Serikali, tupitishe sheria, wachague wao wenyewe, tuwachie vijana waamue mambo yao kama ambavyo madhumuni ya Muswada huu yanaelekeza.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kwenye suala la Bodi, Muswada unalekeza kwamba Mwenyekiti wa Bodi ya Baraza la Vijana atateuliwa na Rais. Hii siyo taasisi ya umma, taasisi za umma Wenyeviti wao wa Bodi wengi wanachaguliwa na Rais, tuache huu urasimu, lazima tubadilike kimfumo, tubadilike kifikra, tuachane na haya. Tuwaachie vijana kupitia mikutano yao mikuu wenyewe wapendekeze nani awe Mwenyekiti wao wa Bodi ili waweze kusimamia na kushauri Baraza kwa mujibu wa mapendekezo ya Muswada yalivyo.

Mheshimiwa Spika, lakini pia suala la marafiki wa Baraza ama ni ndani ya nchi au nje ya nchi, hivyo hivyo Waziri ujitoe kwenye haya mambo, uwaachie vijana waamue nani awe rafiki yao na nani asiwe rafiki yao, muache kujiingiza, haya masuala ya vijana wafanye wao maamuzi.

Mheshimiwa Spika, nimalizie suala la mwisho la mapato. Mapato ya kuendesha Baraza, kwenye *level* ya Taifa imeonekana ni Wizara mtachangia, lakini tunajua huwa kuna shida ya bajeti, ni lazima hii *commitement* kweli ya kusema Serikali mtachangia kwenye *level* ya Taifa ili Baraza hili liweze kufanya kazi, keshokutwa tukienda kwenye bajeti tunataka tuione, iwepo hapa, maana kupitisha sheria ni jambo moja, kutekeleza ni jambo lingine.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kwenye maeneo ya Wilaya na Kata kama ambavyo tumependekeza ni muhimu sana Halmashauri zetu zikaweka mpangilio wa namna gani ya kusaidia haya mabaraza kwenye nafasi za Wilaya na Kata ili ziweze kufanya kazi kama inavyotakiwa, kwa sababu mabaraza yanaweza yakaundwa kama hayasaidiwi na Serikali kutekeleza majukumu yake, maana yake malengo yatakuwa hayajafikiwa.

Mheshimiwa Spika, kama mbavyo katika Halmashauri zetu wameweza kutenga bajeti na kusaidia Mabaraza ya Kata yanatatua migogoro ya Kata katika maeneo yetu, hivyo hivyo inawezekana pia Mabaraza ya Vijana yakatengewa fedha, yakafanya kazi, yafanya maamuzi, yakawasaidia vijana kujua maoni yao katika maeneo mbalimbali kuanzia ngazi ya Kata, Wilaya mpaka *level* ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Lusinde, atafuatiwa na Mheshimiwa Mtanda.

**MHE. LIVINGSTONE J. LISINDE:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru sana na nimshukuru Mungu kunipa fursa ili na mimi niweze kutoa mchango wangu juu ya uundwaji wa Baraza la Vijana la Taifa.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nishukuru sana kwamba wazo hili ambalo tulianza kulipigania tangu miaka ya 2000, sasa imefika mahali ambapo linazungumzwa katika chombo chenye maamuzi ya kutunga sheria.

Mheshimiwa Spika, kipekee nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, kama alivyosema Mheshimiwa Mangungu kwamba huwezi ukaanzisha kitu kipya, na jambo hili ndivyo lilivyo.

Mheshimiwa Spika, hata ukiichukua Sera yote ya Vijana, Sera yote ya Vijana ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) ni mawazo ya mtu mmoja anaitwa Profesa Kitila Mkumbo, ni mawazo ya mtu mmoja anaitwa Israel Ilunde, ni mawazo ya wale watu ambao walikuja na *document* yao pale Iringa, tulipokuja pale tukashindwana nao, hawa wakaichukua wakaifanya kuwa sera ya chama. Ndiyo maana mnaona hata mazoezi yenyewe ya wanachama ni kareti, maandamano, wanafundishwa namna ya kupigana, miwani myeusi na suti nyeusi, wao ndiyo sera yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapozungumzia Baraza la Vijana, kwanza si suala la umri peke yake. Nashangaa Wabunge tunaacha kujadili vitu vya msingi tunatajana majina, Mzee Mwandosya, sijui mzee nani, inasaidia nini? Halafu mzungumzaji anayewataja hao wazee akiwa anaongea wewe ukiwa nje utafikiri babu ndiyo anaongea, sauti yake ni ya kiutu uzima kuliko umri alionao, mbona sisi hatuhoji hivyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi tukija hapa tunakuja kusikiliza unachosema nini, lakini tukisema tuanze kubaguana kwa umri, ndugu zangu hata katika Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) hakuna Mbunge anayechangia iwe kwa pesa zake na kukiweka kile chama kuliko Mzee Ndesamburo. Pamoja na umri wake mkubwa ndiye anakibeba hicho chama, mbona hawasemi? Hivi kuna kijana gani CHADEMA ana mchango kumpita Ndesamburo? Mnakuja hapa mnatukana wazee wakati mnao wazee ambao wanawasaidieni ninyi wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukifika hapo mimi ndiyo huwa napata shida, napata shida kwa sababu tunasema mwisho wake tunajisema wenyewe bila kujua. Leo tunakataa hapa kwamba katika sheria hii hawa vijana wasiteuliwe. Hatusemi ukweli, sheria inasema vijana watatu watapendekezwa na Baraza. Kwa hiyo, ni ukweli kwamba Baraza ndiyo litakuwa huru kupeleka majina matatu, Waziri hana namna ya kumtoa mtu nje ya yale mapendekezo ya wale vijana.

Mheshimiwa Spika, hivi wote hatujui kwamba jamani anayetunza ngoma ndiye anayechagua wimbo. Eeh! Sasa Serikali itoe pesa za kuendesha Baraza, itoe ruzuku, halafu wale vijana waachiwe, vijana milioni 16 wawe peke yao!

Mheshimiwa Spika, lengo la hii sheria ni kulea vijana, kuwalea, halafu huku tukijua Waheshimiwa Wabunge wote kwamba ujana ni kipindi cha mpito, hakuna mtu atabaki kijana maisha yake yote, haiwezekani. Nani atakuwa kijana maisha yake yote yeye kila siku anabaki na miaka ile ile. Ujana ni kipindi cha mpito tena mpito wenyewe ni wa lazima, sio suala la hiari, ni suala la kuamka asubuhi uko hai, unasonga mbele. Kwa hiyo, hatuwezi tukaweka mambo yote mazuri kwenye umri wa ujana tukawadharau watu wazee ambako ndiko wote tutakwenda kama Mwenyezi Mungu akipenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vitu vya ajabu sana, hivi leo tunakaa hapa tunaanza kujadili na kuonesha ubaya wa watu wazima, tunaanza kuonesha ubaya wa kuteuliwa. Kuna Mbunge gani wa Viti Maalum CHADEMA amepigiwa kura? Wote wameteuliwa hawa na wanafanya kazi nzuri tu, wanafanya kazi nzuri humu ndani, lakini hakuna aliyepigiwa kura hata mmoja. Wazee walikaa kwenye Baraza wakasema ninyi nendeni kuwa Wabunge. Nani anasema hapa, wamepigiwa kura na nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tusidanganyane kwamba demokrasia ni uchaguzi tu, haiwezekani. Ingekuwa demokrasia ni uchaguzi, hawa wangeshatoka? Lakini walikaa watu makini…

Mheshimiwa Spika, lakini vitu vingine mimi bwana navishangaa, nikiendelea kusema sana hawa jamaa wataona kama na nanii, hivi uteuzi gani mbaya? Juzi hapa Rais kamteua Mheshimiwa Mbatia kuwa Mbunge, kuna Mbunge hapa anayesumbua Serikali kama Mheshimiwa Mbatia, mbona anafanya kazi yake vizuri tu pamoja na kuteuliwa? Kuteuliwa kuna dhambi gani kama atateuliwa mtu makini? Kazi yake ataendelea kufanya bila kujali kwamba yeye ameteuliwa au hajateuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi nataka tusipoteze muda kujadili vitu ambavyo huwezi ukawaachia vijana wakajisimamia peke yao, kundi kubwa kama hilo, kundi ambalo lina hamasa kubwa, kundi ambalo tunataka kulilea.

Mheshimiwa Spika, halafu naona Wabunge tunachanganya, tunachanganya kati ya Sheria ya uanzishwaji wa Baraza, tunachanganya na Sera ya Vijana. Tusichanganye mambo hapa, sera itatungwa kulingana na sheria.

Sasa mtu anataja viwanda, makampuni, wewe unazungumzia sera hapa? Sisi hapa tunazungumzia uanzishwaji wa Baraza la Taifa la Vijana. Tunazungumzia sheria tu hapa, kwa hiyo, wakati wa sera Waziri atakaa, vijana wataitwa kwenye makongamano, watachangia watatengeneza sera ambayo inawafaa.

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kuwa kila kitu tunapinga, unajua mtindo tunaotumia huu unanikumbusha mzee mmoja alikuwa ana tabia, watoto wake wanaishi mjini, yeye anaishi kijijini. Sasa ili wale watoto wawahi kuja kumuona, anasingizia amekufa, wale watoto wakija wanamkuta yuko hai. Siku alipokufa kweli, wale watoto hawakwenda, wakajua baba ni tabia yake.

Mheshimiwa Spika, ndiyo hawa mabwana, kila kitu hawataki, hata hawa watakapokuja kushauri cha ukweli tutakuja kuwaacha, tutawapuuza, kumbe wanashauri jambo la ukweli! Maana tabia yao kila kitu ni kupinga tu, kwa miaka mitano hakuna hata moja ambalo wamewahi kusema hili liko sawa. Kila kinachotengenezwa, mme-*copy* mme-*paste*, mme-*copy* mme-*paste*, kama ni kizuri! Yaani wapinzani kwa ujumla wao tunakubaliana kwenye jambo moja tu la mshahara na posho, hapo tuko nao! Hapo tuko nao na hawajawahi kupinga wala hawajawahi kukosoa. Tarehe za posho tuko nao na tunaambizana ee bwana leo zimetoka, leo zimetoka, lakini ikija kwenye masuala ya msingi utaona kila mtu anasimama hapa anakosoa Serikali. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa masuala ya kuwahimiza vijana, vijana kujiunga kwenye *NGO*, hata samaki huwezi kumvua bila kuweka chambo kwenye ndoano. Chambo ya vijana ni lazima wawe kwenye makundi maalum, isipokuwa tusimkataze kijana ambaye yuko peke yake anataka kujiunga, tusimkatalie. Serikali iangalie namna ya kuwaruhusu vijana walioko kwenye *NGO* na vijana na vijana ambao hawako kwenye *NGO* namna ya kushiriki kwenye Baraza hili.

Mheshimiwa Spika, Baraza hili kwa upande mwingine ni pancha kwa vyama vilivyozoea kuwadanganya vijana. Kwa hiyo, wanaona umoja wa vijana wao utakuwa hauna maana tena kama kuna Baraza.

Mheshimiwa Spika, vijana wasiotaka siasa, wasiotaka maandamano, wasiotaka fujo watapata fursa ya kuingia kwenye chombo kwenda kupeleka mawazo yao. Sasa lazima walalamike, lazima walalamike kwa sababu wanaona sasa mnataka kuwanyang'anya vijana kuwatengenezea chombo ambacho wataamua mambo yao kwa hekima, wataamua mambo yao kwa sheria, wataamua mambo yao wakiwa wametulia bila kujazwa jazwa jazba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi nataka niseme, madhumuni yameandikwa humu…

*(Hapa baadhi ya Wabunge walipiga kelele)*

**SPIKA:** Naomba Mheshimiwa Lusinde endelea.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, nashukuru sana. Ukiona hivyo, ujue ndiyo dawa inaingia. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili, ukiingia kwenye Muswada unaona madhumuni ya sheria hii yatakuwa, kuweka jukwaa la utekelezaji wa masuala ya vijana katika ngazi ya Wilaya, Mkoa, Taifa na Kimataifa, kuwahamasisha kujitolea na kujitegemea miongoni mwa vijana, kuishauri Serikali kuhusu masuala yanayohusiana na maendeleo ya vijana.

Mheshimiwa Spika, hivi kweli kuna chama au kuna kiongozi duniani anaweza kuwapa ajira watu milioni 16? Ndiyo maana hapa sheria inasema kuwahamasisha vijana kujitegemea. Eeh, sasa mtu anakuja hapa anasema viwanda, viwanda, vijana gani watapata kazi kwenye viwanda wote hawa au sera hiyo ni sera ipi? Mbona tunatafuta kuungwa mkono kirahisi sana? Lakini mwaka huu tutegemee sarakasi nyingi, Bunge linapofikia mwisho, kila mtu anataka kuonekana ana uchungu na kundi fulani ili uweze kumpa *support*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi nilikuwa naiunga mkono Serikali, suala la nani kawahisha Muswada, nani kachelewesha halina umuhimu hapa, hapa cha muhimu ni kwamba sheria imeletwa Bungeni na Serikali, kazi ya Bunge ni kutunga sheria.

Kwa hiyo, habari ya kukaa hapa kumsifia mtu, Mheshimiwa Mnyika alichokuwa anafanya pale alikuwa anacheza *off-side* tu ili afahamike yupo na amefanikiwa kwa upande mwingine, kwa sababu jamaa zake wamemtaja taja, kiongozi wao wa chama kaonekana na yeye yumo. Lakini ukweli ni kwamba sheria ni hii, Wabunge tuipitishe ili iwe sheria, vijana wetu kwa pamoja wanufaike, tuache longolongo hapa za nani alifanya hiki nani alifanya hiki.

Mheshimiwa Spika, hili la kusema kwamba eti kila mtu mzima, hivi watu wazima wote si ndiyo wazazi, kwa hiyo, watoto wetu na wao waanze kutudharau sisi kwamba tumepitwa na wakati? Ni wakati upi huo ambao watu wazima wamepitwa? Wakati wa kudai uhuru Mzee Sitta ulikuwepo, wakati huu upo, sasa wakati upi ambao wewe umepitwa?

Kwa hiyo, tusidanganyane hapa, watu wazima hawa, sisi vijana ndiyo kuna wakati hatukuwepo, tusitake kudanganya tunaawaambia wazee wamepitwa na wakati, wakati wao wakati wa mkoloni walikuwepo, wakati wa kudai uhuru walikuwepo na sasa hivi hawa hapa wamekaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa sisi vijana ambao kuna wakati umetupita hatukuwepo, wakati huo senti tano ikilipwa mshahara, tukae na wazee watuelimishe, sio kila kitu kujifanya unajua tu, unajua tu, eti kijana azaliwe juzi halafu ajue kuliko baba yake ambaye alikuwa anamkimbiza hospitali

kumpeleka kwenda kutibiwa, aonekane huyo mzee ndiye mshamba, mzuri yeye eti anayejua *facebook*. Tuache masuala ya utani, tuwape heshima wazee wetu.

Mheshimiwa Spika, na kama tunataka sisi kuja kuheshimiwa kwenye uzee wetu, tujiheshimu sisi. Lengo la sheria hii ni kuwafanya vijana wajitegemee, wachape kazi, na hili nalisema kila siku. Tuna vijana wanashinda kutwa nzima anapiga viatu anazungumza badala ya kupiga kiwi viatu. Dunia tumeiona namna inavyokimbia, vijana wetu wakikaa pamoja watakuwa wanajadili mambo ya msingi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mtanda.

**MHE. SAIDI M. MTANDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kupata fursa ya kuchangia mambo machache kwenye hoja ambayo iko mbele yetu.

Kwanza niseme wazi kwamba naunga mkono hoja, na naamini kabisa Serikali inaweza kuya-*accommodate* yale mapendekezo, maoni na ushauri wa kitaalam kabisa kutoka kwenye Kamati ambayo mimi ni Mwenyekiti wake wa Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Lusinde amekwenda mbali, alikuwa akieleza namna suala la wakati lilivyo muhimu katika maisha na mchangiaji mmoja anasema *we are not prisoners of the previous generation.*

Mheshimiwa Spika, lakini mimi ni mwanahistoria kwa taaluma yangu na niliwahi kufundishwa na Profesa Mlahagwa, yeye alikuwa na kauli yake muhimu ya kihistoria inasema *history is about the past, the present and how it determines the future*. Kwa hiyo, umuhimu wa historia, umuhimu wa matukio yaliyopita kwenye kwenda mbele na kuangalia mustakabali wa Taifa kwa siku zijazo ni muhimu sana. Huwezi kufanya maamuzi bila kuangalia tulikotoka ni wapi, tulipo sasa ni wapi na tunakoelekea ni wapi. Kwa hiyo, nilikuwa naomba hili liwe wazi.

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mwenyekiti wa Kamati, nime-*declare interest* na Kamati yangu imewasilisha maoni mengi ambayo kiujumla tunayaunga mkono na hata wale waliotoa maoni ya Kambi ya Upinzani ni Wajumbe wa Kamati yangu, tulishirikiana nao na waliunga mkono ndani ya Kamati akiwemo Waziri Kivuli ambaye alitoa maoni yake pale, na asilimia kubwa ya maoni na ushauri alioutoa ni maoni na ushauri ambao umetolewa na Kamati hii yetu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini katika taarifa ile ya Kambi ya Upinzani asubuhi, yako mambo mawili/matatu naona niyaweke sawa.

La kwanza, msemaji wa Kambi alisema Rais Kikwete amechoka kuongoza nchi. Nataka nimhakikishie kwamba Rais Kikwete bado ni imara na ana uwezo mkubwa wa kuongoza nchi. Na hii inathibitishwa kwa sababu hata jana Rais Kikwete amepewa tuzo ya kiongozi bora ambaye anasimamia amani na utulivu wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimefadhaika kwa sababu asubuhi Mheshimiwa Mnyika na Msemaji wa Upinzani walikuwa wanajaribu kulirubuni Bunge na kuwaeleza uongo Watanzania kwamba Kamati yangu ilikuwa ikifanya mambo kiujanja ujanja na wakituhumu kwamba labda mimi Mwenyekiti nilikuwa nafanya hivyo ili kuwafanya wao wasiwe na taarifa sahihi.

Mheshimiwa Spika, nataka kulithibitishia Bunge hili na Watanzania kwamba kwanza, uwezo wangu wa kuongoza Kamati hauwezi kutiliwa shaka yoyote ile. Nimekuwa Mwenyekiti wa Kamati hii kwa takriban miaka miwili sasa, lakini nimekuwa Makamu kwa mwaka mmoja, kwa miaka mitatu nimekuwa nikiongoza Kamati hii na Kamati hii imekuwa ni mfano bora na taarifa zake zimekuwa ni taarifa makini ndani ya Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho, kwenye hoja zile zilizowasilishwa asubuhi ni kujaribu kueleza dhana potofu juu ya Kituo cha Televisheni cha *Clouds (Clouds TV)*. Msemaji wa Upinzani alikuwa anasema, labda kituo hiki kinatoa upendeleo kwa chama fulani na wangependa maoni ya *Channel Ten* yaletwe ndani ya Bunge hili. Nataka niwahakikishie kwamba mtoa taarifa mwenyewe yeye mwenyewe kama walikuwa na chuki binafsi na migogoro yao ya kimaslahi na watu hao, mambo hayo hayawezi kuchukuliwa na kuingizwa ndani ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, niendelee. Jambo kubwa ambalo tumeliona na ambalo Wabunge wanashauri na Kamati yangu imeshauri ni kuhusu uhuru wa Baraza tunalolizungumzia. Maoni ya Kamati yako wazi juu ya uhuru wa Baraza na wachangiaji wote wameeleza vizuri.

Mheshimiwa Spika, lakini nilitaka niseme mambo mawili, watu ambao wamechangia humu wasiupotoshe umma kwamba Baraza hili kwa muundo, kwa vitendo vyake na kwa namna ambavyo tumejadili halitokuwa huru kwa vijana. Dhana hiyo ni potofu, nataka niwahakikishie kwamba Baraza hili litakuwa huru kwa sababu maeneo yote ambayo tumeona yananyima uhuru na kutotoa haki kwa vijana hawa, Kamati yangu kupitia vikao vyake imetoa ushauri fasaha, ushauri bora na ningeiomba Serikali iyazingatie hayo.

Mheshimiwa Spika, na Serikali imeonesha nia. Wakati tunakaa na Kamati tumejadiliana tumekubaliana kwamba maeneo hayo ni lazima yarekebishwe ili kuweza kutoa dhana ile ya uhuru wa habari.

Mheshimiwa Spika, mimi sielewi inaposemwa kwamba endapo Waziri atatajwa labda katika kuangalia shughuli za Baraza, basi itakuwa imeondoa uhuru wa Baraza, hilo sio kweli, kwa sababu hata Muswada binafsi wa Mheshimiwa John Mnyika amemtambua Waziri kwenye maeneo yasiyopungua kumi akiona umuhimu wa Waziri kushirikishwa kwenye jambo hili, kwenye maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, sasa wanaochangia wengi kwanza hiyo hoja binafsi hawajaisoma, kwa hiyo, wanakuja hapa wakiwa hawaelewi hata mtoa hoja mwenyewe alikuwa na hoja gani juu ya jambo hilo. Kwa hiyo, ukisoma Muswada Binafsi wa Mheshimiwa Mnyika, kifungu cha 1, kuhusu ku-*gazette* anamtambua Waziri na anataka Waziri ndiye afanye kazi hiyo.

Kifungu cha 21, kwamba lazima shughuli hizo Serikali kupitia Waziri ipate taarifa, anamtambua, lakini kifungu cha 36, masuala yote yanayohusu fedha anasema lazima Waziri naye afahamu kwa sababu fedha hizi ni za walipakodi, fedha za Serikali. Unahitaji kwa nini taarifa hizi ziwe za usiri?

Mheshimiwa Spika, pale kwenye kifungu kinachuzungumza uteuzi wa Mwenyekiti wa Bodi, wako watu wanakuja wanasema eti Rais asiteue Mwenyekiti wa Bodi, kwa nini? Wanasema kwa kufanya hivyo utakuwa umeingiza masuala ya siasa.

Mheshimiwa Spika, mimi nawauliza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania sio Jakaya Mrisho Kikwete? Rais huyo sio Amiri Jeshi Mkuu? Rais huyo sio Mwenyekiti wa CCM? Lakini ulisikia lini Wanajeshi wanasema hatuhitaji Rais Kikwete awe Amiri Jeshi kwa sababu siasa itaingia jeshini? Kwa hiyo, hiyo ni dhana potofu, dhana hiyo haiwezi kukubalika, na nilitaka niwatoe hofu Watanzania wanaotusikiliza kwamba kwa kufanya hivyo hakuna lililokosewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho nimalizie kwa kulishauri Bunge lako na kuwaomba Waheshimiwa Wabunge, ukipitia *Hansards* za miaka yote utaona namna ambavyo jambo hili mtoa hoja mwenyewe Mheshimiwa Mnyika na wengine walivyotaka liingie kwa wakati ndani ya Bunge hili. Leo Serikali imeingiza kwa nini linapingwa tena? Walikuwa wakihamasisha Serikali ilete kwa haraka na wanasema tumechelewa, na Kamati yangu ilipobaini kwamba jambo hili limechelewa, tumelileta kwa wakati. Sasa leo unasema jambo hili halijawa tayari, lakini unasema Muswada binafsi uingie ndani ya Bunge, kwani

huyo mtoa hoja binafsi yeye ana sera kuhusu maendeleo ya vijana? Ana *instrument* gani ya ku-*enforce* hili jambo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ndiyo maana Serikali wenye sera yao ya maendeleo ya vijana wameleta Muswada; na sisi tunauboresha Muswada huu utakuwa bora, itakuwa sheria nzuri na Muswada huu ukipita kuwa sheria, nina hakika kabisa vijana watapa *platform*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kwa nini hatutaki Serikali ihusike? Hivi kama tunasema watu hawa, vijana hawa, Baraza hili linapotaka kufanya mikataba ya kimataifa na jumuiya na taasisi nyingine, Serikali isijue, kuna usiri gani kwenye hilo?

Mheshimiwa Spika, sasa hivi dunia imeingia kwenye kipindi kigumu sana na wewe unafahamu. Sasa hivi kuna magaidi duniani kote na mitandao, hivi kwa nini Serikali isijiridhishe kwamba vijana hawa wanapotaka kuingia makubaliano yenye nia njema kwa Taifa letu, watoe taarifa kwa Waziri, kuna ubaya gani? Sasa hivi kuna *ISIS* duniani inasumbua na ugaidi uko wa kimataifa, fedha haramu ziko nyingi, hatuwezi kukubali Baraza hili ligharimiwe na fedha chafu ambazo zitakuwa na nia mbaya kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa nataka niwatoe hofu Wabunge na nataka niwahakikishie kwamba endapo mtapitisha sheria hii, nina hakika kabisa na tumekaa mara nyingi na mtoa hoja mwenyewe Mheshimiwa Mnyika, na tumezungumza naye, tumekubaliana naye, tumempa ushauri wetu, kwa hiyo, nina hakika kabisa jambo hili liko mikono salama, Waheshimiwa Wabunge tufanye maamuzi. Tumechelewa, jambo hili lingekuja siku nyingi zaidi, kwa hiyo, msiwe na wasiwasi na mimi nawatoa wasiwasi kwa sababu Kamati yangu imepata muda wa kupitia jambo hili kwa zaidi ya miezi miwili.

Kwa hiyo, maoni na ushauri na mapendekezo tuliyoyatoa ni maoni ambayo tumejiridhisha tuna hakika kwamba maoni hayo yatasaidia sana endapo Serikali wataweza kuya-*accommodate*.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. DKT. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Na mimi nitazungumza machache kuhusiana na Muswada huu ulioko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kusema kwamba Muswada huu ni muhimu sana katika nchi yetu na hasa ukizingatia idadi ya vijana nchini. Katika nchi yetu takwimu za sensa zilizokuwa zimefanyika hivi karibuni zinaonesha kwamba vijana ni takriban zaidi ya 50% ya idadi ya watu. Vijana hawa katika nchi yetu

wana changamoto nyingi na za aina mbalimbali, hivyo chombo hiki muhimu, *Youth Council* kitasaidia sana kuwaunganisha hao vijana.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tukiulizwa maswali mengi, je, Tanzania mna nia thabiti kuwasadia vijana na tumesaini mikataba mingi sana ya kimataifa. Kwa hiyo, mimi Muswada huu nautafsiri kama ni sehemu mojawapo ya kuridhia Mikataba ya Kimataifa kuhusiana na haki za vijana maana katika nchi yetu baada ya kusaini mikataba ya kimataifa lazima tutunge sheria. Tuna-*sign* zile *international conventions* halafu tuna-*ratify*. Sasa sisi tunapo-*sign* ile mikataba ya kimataifa haiji kuwa sheria moja kwa moja katika nchi yetu, lazima utungie sheria. Kwa hiyo, Muswada huu inaonesha kwamba katika nchi yetu kuna nia njema ya kisiasa kuonesha kwamba kundi hili muhimu la vijana wanapaswa wapewe vipaumbele.

Mheshimiwa Spika, jambo ambalo naomba niseme, chombo hiki muhimu kama jinsi ambavyo imeelezwa kwenye Muswada huu, suala zima la jinsia. Vijana hawa isionekane kwamba ni vijana wa kiume tu, tuna vijana wa kiume na vijana wa kike. Kwa hiyo, vyombo vyote ambavyo tumeviweka humu naunga mkono asilimia 100 na kukumbushia suala zima la jinsia katika vile vyombo ambavyo tumeviunda, kuanzia ngazi ya Wilaya, ngazi za huku juu, suala zima la jinsia, “me” na “ke”, vijana hawa ni muhimu na hususan vijana wa kike.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tukipeleka hela za vijana katika Halmashauri zetu, lakini mara nyingi sana vijana hao wamekuwa hawaelewi ni namna gani wanaweza wakapata fursa ya kuzi-*access* zile fedha katika vyombo hivyo vya Halmashauri zetu. Kwa hiyo *Youth Council* itaweka utaratibu na kuendelea kuwaunganisha vijana na kuonesha kwamba kuna fursa mbalimbali za kuweza kuzi-*access* fedha hizi katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, hivyo naunga mkono asilimia mia moja kwa sababu lengo zima na madhumuni ni kukuza na kuhimiza maadili mema, kuweka mazingira ya ushirikishwaji wa vijana na kutekeleza masuala yanayohusu maendeleo ya vijana.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi vijana wana changamoto nyingi, masuala ya ajira, changamoto za dawa juzi tumejadili, changamoto za UKIMWI, vijana hawa wanahitaji *platform* ya uhakika.

Mheshimiwa Spika, upande wa watoto tumefanikiwa sana kuweka Baraza la Watoto, hivyo Baraza hili la Vijana litakapoanza kazi, litasaidia sana sawa sawa na Baraza la Watoto kuzingatia haki za vijana kama tunavyozingatia haki za watoto katika nchi yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, lakini kikubwa, kama jinsi ambavyo tumesema kwenye Katiba yetu kwamba nchi yetu haina masuala ya udini, haina masuala ya ukabila, Baraza hili kwa kuwa litawaunganisha vijana wote wa dini zote, wa makabila yote, litakuwa ni chombo muhimu sana. Na Baraza hili pia litaweza kuwa sehemu ya kupeleka ajenda ya kutatua matatizo ya aina mbalimbali ili vijana wetu wasiweze kutumika katika ajenda ambazo ni ndivyo sivyo.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengi vijana wanapokuwa hawana kazi, hawana vyombo maalum vya kukutana na kujadiliana masuala yao wenyewe vijana, wanaweza wakatumika ndivyo sivyo.

Mheshimiwa Spika, tumeona kuna nchi zinaingia kwenye migogoro vijana, wanatumia ma-*blog*, wanasema tukutane eneo fulani, *Cramblin Square*. Vijana wa siku hizi wasipokuwa na kazi, badala ya kuuliza ajenda ni nini, ukisema tukutane kwa ajili ya suala fulani, maandamano, hawaulizi ajenda, wanauliza saa ngapi tunaanzia wapi. Lakini kwa kupitia vyombo hivi uelewa wa vijana utaongezeka, wanapoambiwa tukutane kwa jambo fulani watahoji, sawa jambo hilo ni muhimu, ajenda ni nini? Inahusu kitu gani?

Mheshimiwa Spika, nchi nyingi za Tunisia unakuta watu wanakaa kwenye yale maeneo yao ya wazi, wanatumiana tu ma-*blog*, na bila hili chombo kunakuwa na *perpetrators* wa kuwatumia vijana ndivyo sivyo. Lakini chombo hiki kitasaidia haraka sana kupitia Wizara yetu inayoshughulikia masuala ya vijana kupeleka ujumbe.

Mheshimiwa Spika, kuna nchi zimefanya machafuko, nchi ambazo mpaka leo hazija-*stabilize*, unakuta huko nchi kama Tunisia, nchi kama za Syria, vijana wanatumika, wanatumika ndivyo sivyo, maana sasa hivi kuna utandawazi. Lakini kunapokuwa na mabaraza haya ya vijana *well organized*, kunakuwa na uongozi mzuri, basi mambo haya yanazingatiwa.

Mheshimwia Spika, katika umri wa vijana, hata wale wenye miaka 18 ni vijana. Vijana hawa hata wanapokwenda Mahakamani wanaambiwa kwamba lazima uwe na mlezi au mzazi *(guardian)* ndizo sheria zetu, *under 18* wote lazima kuwe na mtu mkubwa *(guardian)*. Sasa leo hii tusipotambua kwamba maeneo yote vijana lazima wawe na watu wazima wanaowaongoza, washauri, pahala pengine wanaita *patron*, pahala pengine wamewapa majina mbalimbali. Wakiwa tu ni vijana wenyewe ni hatari kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, kuna vijana wengine ana miaka 18, hajafikisha hata miaka 21, anasema mimi natamani niendeshe ndege, anatamani sijui afanye vitu… ndiyo maana katika shughuli mbalimbali kuna umri. Tunasema nafasi hii tunaanzia miaka arobaini, nafasi ya kupiga kura miaka 18, kugombea miaka 21.

Wataalam walikaa na kuona uwezo wa kufikiri wa vijana hawa katika umri huu unakuwa bado, lazima wawe chini ya watu ambao wanaweza wakawalea.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana maeneo mengine tunasema kuna jumuiya za umoja wa vijana, wanapokuwa na kamanda, kamanda lazima awe ni mtu mwenye umri mkubwa ndiyo anaitwa kamanda. Sasa jumuiya yenyewe ya vijana, halafu uatafuta kamanda na yeye naye ni mtoto, kwa hiyo ni changamoto. Kwa hiyo, chombo hiki kwa kweli sisi katika nchi yetu kitatusaidia sana.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengine unakuta vitu kama *panya road*, wale ni vijana waliokosa mwelekeo mzuri. Chombo hiki masuala ya *panya road* na nini, wanaweza wakakutana wakashirikiana na kutoa hoja zao.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo jambo hili asilimia mia moja naliunga mkono na naomba niseme kwamba masuala ya jinsia yazingatiwe na chombo hiki kiendelee kufanya kazi sawa sawa na Baraza la Watoto. Tumefanikiwa sana kwenye haki za mtoto, Baraza la Watoto, vivyo hivyo masuala ya vijana, haki za vijana, Baraza la Vijana hili litasaidia kutuunganisha nchi nzima, makabila yote, lugha zote, dini zote, maana haya ni maeneo ambayo Tanzania tumepata *credit* za kutosha. Nchi nyingine za jirani wanajifunza Tanzania, ee! Ninyi mnafanyaje lugha moja? Hamna ukabila, maeneo mengine wakianza kujitambulisha kabla mtu hajataja jina, anataja kabila, mimi ni Mjaluo, mimi ni Myoruba halafu anaweka jina lake pale. Lakini sisi Tanzania na hili Baraza la Vijana, kwa kweli limekuja muda muafaka.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niunge mkono kabisa asilimia mia moja, na hii ni sehemu ya *ratification* ya zile *international conventions* ambazo tumezisaini kuhusiana na haki za vijana kuonesha *political will* masuala ya vijana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa, muda umekwisha. Tulivyopanga ni kwamba zile *amendments* zipo nyingi, kwa hiyo, wote wanaohusika na *amendments* zao wameendelea kufanya kazi na hii inaonesha ndivyo wanavyotunga sheria. Hivyo ndivyo wanavyotunga sheria. Sasa mkisema *rubber stamp,* hizo *amendments* za kazi gani?

Kwa hiyo, sio kweli kwamba tunafanya *rubber stamping*. Ile tu *the fact that* kuna *amendments* kibao ziko kule zinaendelea huko ndiko kutunga sheria. Lakini, inasikitisha ninyi wenyewe mnapojadili hamjadili mambo yanayohusika na sheria mnakwenda mbali. *Anyway*, kwa vyovyote vile tunawashukuru kwa leo mmefanya kazi iliyotosha. Kesho baada ya kipindi cha maswali, Serikali itaanza kujibu hoja, halafu tutaingia Kamati ya Bunge Zima. Kwa hiyo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.40 jioni Bunge liliahirishwa hadi siku ya Jumanne, Tarehe 31 Machi, 2015 Saa Tatu Asubuhi)*